**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Arobaini na Nane - Tarehe 16 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuweka randama hizo na kwa hiyo, wanaotaka kuchangia kuanzia kesho wakumbuke kuanza kuleta leo karatasi zao.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 425

**Ujenzi wa Zahanati kwenye kila Kata**

**MHE. ZAYNABU M. VULLU** aliuliza:-

Ni sera ya Serikali kwamba kila kijiji kiwe na zahanati na kila Kata iwe na Kituo cha Afya:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Vigwaza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa sera ya afya iliyotolewa mwaka 2007 inataka kwamba kila kijiji kiwe na zahanati, kila Kata iwe na Kituo cha Afya na kila Wilaya iwe na hospitali. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imetenga shilingi milioni 100 fedha za MMAM kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha upasuaji katika kituo cha afya cha Miono na shilingi milioni 30 fedha za ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa *(LGCDG)* zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa wodi za wazazi Chalinze na tayari mkandarasi anaendelea na ujenzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Vigwaza ina Zahanati katika vijiji vyote isipokuwa vijiji vya Ruvu Darajani, Buyuni na Vitonga. Katika kijiji cha Ruvu Darajani ujenzi wa zahanati upo katika hatua ya mwisho na katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni nne kukamilisha ujenzi huo.

Aidha, Halmashauri imeweka kipaumbele cha kujenga Kituo cha Afya cha Vigwaza katika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Kwa sasa wananchi katika Kata ya Vigwaza wataendelea kupata huduma za afya katika Vituo vya Afya vya Mlandizi na Chalinze ambavyo vipo karibu na wakazi wa Vigwaza zikiwemo zahanati 43 zilizopo katika mpango wa kujenga kituo cha afya katika Kata ya Vigwaza ukiendelea. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nataka nimfahamishe kwa kuwa mimi natoka katika Jimbo hilo kwamba Kata alizozitaja wananchi wa Vigwaza waende wakahudumiwe ni Kata ambazo zipo mbali sana zaidi ya kilomita 30. Swali je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya hospitali/zahanati ya Kata ya Vigwaza ipandishwe hadhi na iwe Kituo cha Afya kwa sababu mbili zifuatazo:-

Kwanza wananchi wa pale wapate huduma muhimu kwa haraka kitu ambacho sitarajii na hata Wabunge wa humu ndani hawataki kitokee, Kata ile ipo barabarani na barabara ile ni barabara kubwa inayopita magari mengi hiki kituo kikipandishwa hadhi inaweza ikahudumia hata wananchi ambao watapata ajali za gari kitu ambacho hatukitarajii?

Swali la pili kwa kuzingatia kuwa Kata ipo jirani sana na Kata ya Tarawanda na Kata ya Pera na Kata hizo zote hazina zahanati. Je, kwa nini sasa Serikali isiweke mkakati wa kupandisha hadhi moja ya hospitali zilizokuwa pale Vigwaza ili wananchi waweze kupata huduma kwa karibu zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nikubaliane na yeye kwamba *definately* atakuwa anajua mambo ya Kata zake na jimbo lake na Wilaya kuliko mimi, ndiyo maana tupo hapa. *(Makofi)*

Mimi Siha naifahamu kuliko watu wote humu ndani. Kwa hiyo, kabisa anaposema kuhusu suala la umbali ule wala sina tatizo nalo. *Issue* inayozungumzwa hapa ni kuhusu sasa *priority* pale Miono, Kata ya Miono tumeanzisha Shule ya Sekondari ya Kimataifa. Katika Shule ya Sekondari ya Kimataifa pale tunakusudia kuwa na wanafunzi 8,000 Halmashauri ya Bagamoyo ikasema kipaumbele pale ni kupeleka kituo cha afya pale. Tukapaleka pale, *simple and common sense,* kuna Kata ya Kiwangwa kuna barabara ya Msata inayokwenda Bagamoyo ambayo imejengwa vizuri kwa kiwango cha Kimataifa na ajali zimeanza kutokea pale napo tukaweka kautaratibu kanokofanana na kale ka Tumbi, tukaweka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa dada yangu Mheshimiwa Vullu anasema kwamba kuna haa ya kupandisha hadhi zahanati hii iliyopo pale Vigwaza, *no objection*. Sisi tupo tayari, Mheshimiwa Vullu kama anafikiri kwamba kuna haja hiyo zahanati ipo karibu na eneo la Chalinze, ipo karibu na eneo la Mlandizi ambazo huduma hizi zinapatikana, lakini kama Mheshimiwa Vullu anaona kwamba hivi anavyotaka ndiyo anavyoona kwamba itafaa kwa maana ya kipaumbele, sisi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutashirikiana naye kuhakikisha tunapandisha hadhi. Lakini hili jambo ni lazima litokee kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kuhusu hili lingine alilolizungumza, nataka niifahamishe nyumba yako hii, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo katika hela zinazozungumziwa katika eneo la afya imetengwa shilingi bilioni tano na hizo shilingi bilioni tano kwamba zipo pale, ni suala la kipaumbele kama sisi tunafikiri kwamba tupeleke hapa katika hili eneo lingine analolizungumza hapa Tarawanda, *no problem.* Sisi watuletee watuambie wanataka kufanya hivyo, tufanya kesho asubuhi. Mheshimiwa Mkuchika yupo hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa atanielekeza, sisi tutakwenda kufanya kama anavyosema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman Mbunge wa Kishapu. Swali namba 426, hakuna muulizaji, tunaendelea.

Na. 427

**Utekelezaji wa *TASAF* Tanzania Zanzibar**

**MHE. JUMA SURURU JUMA** aliuliza:-

Tangu kuanzishwa kwa mradi wa *TASAF* ni miradi mingapi na aina gani ambayo imeanzishwa Zanzibar?

Je, miradi hiyo imegharimu fedha kiasi gain?

Je, ni kwa kiwango gani imefanikiwa kupunguza umaskini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* mwaka 2001 hadi Mei, 2011 (Awamu ya I na II), jumla ya miradi 750 imetekelezwa katika visima vya Unguja na Pemba. Miradi iliyotekelezwa ni katika sekta zifuatazo:-

Elimu miradi 55, afya miradi 16, maji miradi 52, barabara miradi 20, misitu miradi 25, umwagiliaji miradi 10, kilimo miradi miwili, mifugo miradi 164, uvuvi miradi 179, ujenzi na masoko miradi mitano, mitaro ya maji machafu miradi mitano, biashara na viwanda miradi 13, ukarabati wa magofu ya kale miradi saba na UKIMWI *(ZAC)* miradi 197. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote iliyotekelezwa katika Awamu ya I na II ya *TASAF* katika Visiwa vya Unguja na Pemba imegharimu jumla ya shilingi 12,298,149,385.88. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu miradi inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* inachangia katika juhudi za Serikali za kupunguza umaskini kwa kupitia mkakati wa kupunguza umaskini Zanzibar (MKUZA). Aina ya miradi iliyotekelezwa imechangia katika kupunguza ukosefu wa huduma za jamii, kuongeza kipato cha wananchi na kuongeza ujenzi kwa jamii husika. Aidha, kiwango cha umaskini kilichopunguzwa kwa utekelezaji wa miradi kutoka wadau mbalimbali ikiwemo *TASAF,* kitafahamika wakati wa kupima mafanikio ya MKUZA.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuniona. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu Maendeleo ya *TASAF* ulipoanza ulikuwa na kasi sana, ilikuwa tunausikia kila siku. Lakini kila muda ukienda hatuusikii na wala hausikiki. Je, bado upo mfuko huu?

Swali la pili, wananchi walio wengi wanapenda kusaidiwa na mfuko huu lakini hawajui waanzie wapi au hawajui ni wafanye. Je, ni vigezo gani vya msingi ambavyo vinapaswa kufanywa na wananchi wale ili waweze kupata msaada huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF* bado ipo. Ipo katika awamu yake ya II na kwa kweli awamu ya pili inakaribia kumalizika. Mwaka ujao tutaanza *TASAF* Awamu ya III. Kwa hiyo, bado ipo. Suala la kwamba haisikiki labda iliingia kwa kishindo sasa imezama, lakini ipo na inaendelea. Utaratibu wa kupata miradi ya *TASAF* ni kwa jamii yenyewe. Jamii ndiyo inayoibua mradi halafu inapitia katika Serikali za Mitaa na baadaye fedha inatolewa na *TASAF* Makao Makuu na zinakwenda kwenye akaunti ya jamii na jamii ndiyo inayosimamia utekelezaji wake. Kwa hiyo, ipo na inaendelea na utaanza tena upya katika Awamu ya Tatu mwakani. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *TASAF* inasaidia sana wananchi katika nchi yetu na hususani kule Mbozi Mashariki, lakini tatizo ambalo tumekumbana nalo sana ni urasimu katika *process* yote ya miradi hii inayoibuliwa chini ya *TASAF.* Sasa wakati tunaenda Awamu ya Tatu ya *TASAF* Mheshimiwa Waziri atatuhakikishia kwamba ule urasimu mpaka mradi uje, uwe mradi, ukamilike na uanze kujengwa urasimu huu utakuwa umepungua au utakuwa umekwisha kabisa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, urasimu ni utaratibu sasa, utaratibu unakuwa mbaya kama unakuwa mrefu na haufikii malengo. Lakini ni vigumu sana kuukwepa, ndiyo maana urasimu upo na warasimu wapo. Lakini zinazofanyika ni kwamba wanaomba wadau kutoka kwenye jamii, Halmashauri ya Wilaya ambayo ina wataalam wanakwenda kuangalia kama ule mradi ulioombwa na wananchi kweli upo na unastahili kupewa fedha. Baada ya hapo maombi yale yanapelekwa *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni ilikuwa *TASAF* wapo katika ngazi ya Wilaya hasa Wahasibu katika *TASAF* ile ya kwanza. Baadaye kutokana na kugatua madaraka tukaacha kazi hii yote ifanywe na Halmashauri ya Wilaya. Yapo matatizo yametokea hapo katikati ya kutopata taarifa kwa haraka. Kwa *TASAF* namba tatu itakayoanza mwakani tutaurudisha utaratibu wa *TASAF* namba moja ambapo *TASAF* itakuwa na Mhasibu wake pale ambaye anapeleka taarifa na anahakikisha kwamba fedha zimeenda kwa jamii. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba kwa kufanya hivyo tutapunguza urasimu usiokuwa wa lazima. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Wawi naomba kutoa shukrani kwa *TASAF* kwa miradi kadhaa walioifanya ila nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuna mradi kwa mfano wa Bonde la Mpunga la Dobi. *TASAF* imetoa shilingi milioni 30 lakini imekataa kutoa pesa mpaka kwanza upembuzi yakinifu ufanyike. Sasa hizi pesa zinazotolewa shilingi milioni 30 zinatokaje kama ule upembuzi yakinifu haujafanyika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote inayogharamiwa na *TASAF* huwa haivuki shilingi milioni 30. Hiyo ndiyo kiwango cha juu kabisa. Sasa ikiwa pale miradi imezungumzwa 30 milioni na wanataka kufanya upembuzi yakinifu ni jambo nitahitaji Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anieleze vizuri. Kwa sababu kabla hatujasema ni sh.30 milioni upembuzi yakinifu unatakiwa umefanywa kwanza na umeridhika kwamba mradi ule unastahili kutekelezwa na gharama zake ndizo hizo. Kama hawajafanya upembuzi yakinifu hata 30 milioni siielewi ilivyopatikana. Kwa hiyo nitamwomba Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anieleze ili tuwasiliane na *TASAF* waende wajue tatizo liko wapi. *(Makofi)*

Na. 428

**Mafuta kwa Magari ya Polisi**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Micheweni kina magari mawili, moja linahudumia Kituo na lingine linamhudumia *OCD.* Lakini magari haya muda mwingi yanashindwa kufanya kazi wakati wote kutokana na tatizo la mafuta:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kupeleka mafuta kwenye vituo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta kwa ajili ya magari yote ya polisi yaliyopo katika mikoa, vikosi na wilaya hununuliwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa/Kikosi au kugawiwa katika Kamandi

husika baada ya kasma ya matumizi ya fedha ya mwezi *(warrant of fund)* kutumwa kutoka Makao Makuu ya Polisi. Magari anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge hupokea mgao wake wa mafuta kutoka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba imekuwa inatokea magari ya polisi yanashindwa kufanya kazi kutokana na ukosefu wa mafuta. Tunalo tatizo la uhaba wa rasilimali fedha. *(Makofi)*

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa polisi wana majukumu ya kulinda usalama wa wananchi na mali zao na kwa kuwa askari wa kituo hiki kunapotokea tukio lolote wanakosa ufuatiliaji wa mara moja na wa kina kutokana na uhaba wa mafuta. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba mgao huu uliopo haufai na ipo haja ya kufanyiwa marekebisho ili askari wa kituo hiki wapate mafuta kulingana na utaratibu uliopangiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa hii ni wiki ya pili magari ya kituo hiki cha polisi hayatembei kulingana na uhaba huu wa mafuta na hadi jana washitakiwa walipelekwa Mahakamani kwa kuombewa *lift* ya gari. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba mafuta kulingana na mgao uliopo na kwa vile hayafiki kulingana na utaratibu ambao haufai, ipo haja ya utaratibu huu uwekwe na askari hawa washiriki katika mgao huo wa utaratibu ambao utapangwa katika ugawaji wa mafuta haya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Haji Khatib Kai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sio mgawo, mgawo utaendelea kuwepo kwa sababu baada ya Bajeti kupita inabidi vituo husika ama Kamandi husika zipate pesa za mafuta. Tatizo la msingi hapa ni uhaba wa rasilimali fedha. Lakini nishukuru kusema kwamba baada ya Bajeti yetu kupita, tutatizama ni jinsi gani tutaweza kujipanga inagwa bado nitakiri kwamba haijatosheleza katika kiwango ambacho tulikuwa tunakitarajia lakini hata hivyo jitihada zitafanyika kuona kwamba mafuta yanaweza kufika na niweze kusema kwamba tatizo sio mgawo, isipokuwa tatizo ni zile fedha za kuweza kununulia mafuta na kuhakikisha kwamba mafuta yanakuwepo ndio tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake la pili ambalo nimelipokea kwa mara ya kwanza la kusema kwamba kwa wiki mbili sasa katika kituo hiki kumekuwa magari hayaendi kwa sababu hakuna mafuta na hiyo imesababisha kwamba wahalifu wapelekwe katika Mahakama kwa kutumia lifti za watu, hili ni jambo jipya. Lakini niseme kwamba hairuhusiwi kisheria na kiutaratibu kupeleka watu kwa kutumia *lift* za watu. Nadhani kama hiyo imetokea itakuwa ni kosa, lakini nimeichukua kutoka kwako na tutaitizama ni kwa nini imetokea namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kwamba tatizo kubwa tulilonalo ni hilo la rasilimali fedha na tunajitahidi kufanya kila jitihada na nisitumie muda mrefu wa Bunge lako Tukufu kujibu swali hili, lakini nishukuru kusema kwamba Kamati ya *NUU* ambayo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge, inalitizama hili suala kuona vipi itaweza kuishauri Serikali, tuweze kwenda mbele katika hili. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, Kituo cha Polisi Kwimba kinahitaji gari, tutumie njia gani ili tupate gari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali ama ombi ama dai la Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala kweli amelisema hapa lakini pia aliwahi kutudokezea kwamba katika Kituo chake wanahitaji gari. Nimuombe tu na ninajua kwamba atatuelewa kwamba avute subira kwa sababu sasa hivi hali ya fedha kwa kweli haituruhusu na katika Bajeti yetu ambayo tunashukuru kwamba Bunge hili liliipitisha hatuna mahali ambapo tumeomba

kununua gari katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, lakini endapo itatokea basi tutafanya kila jitihada kuona kwamba ombi la Mheshimiwa Ndassa, linafikiriwa. *(Makofi)*

Na. 429

**Kituo cha Polisi Konde**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Konde kilijengwa mwaka 1950 na kinahudumia vijiji karibu nusu ya Wilaya ya Micheweni vikiwemo vya Msuka, Mkangale, Mgogoni, Tumbe na Matangatuani. Lakini kwa sasa kituo hicho kimechakaa sana na hadhi yake ni mbaya kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo kipya au kukifanyia ukarabati mkubwa kituo kilichopo ili kiweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi na kufanya askari na familia zao wanaoishi pale wawe katika hali ya usalama?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Saidi Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mpango wa kukarabati majengo ya zamani pamoja na kujenga majengo mapya kwa ajili ya askari polisi nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha. Matarajio yetu ni kwamba mpaka kufikia mwaka 2015 tutakuwa tumekarabati majengo yote likiwemo jengo la Kituo cha Polisi Konde pamoja na jengo la kuishi askari lililopo eneo hilo. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na makazi bora, wakiwemo askari wetu. Je, Serikali kupitia Wizara hii, haioni haja kuchukua dhamana kwa mashirika makubwa ya kifedha ili askari wetu waweze kupatiwa vifaa vya ujenzi kwa njia ya mkopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa majengo ambayo wanaishi askari wa pale yapo katika hali ya uchakavu mkubwa unaotishia usalama wao, je, Mheshimiwa Waziri, upo tayari kufanya ziara katika Jimbo langu na kukagua majengo yale ili askari wale wajenge imani kwamba Serikali itachukua hatua za kuweza kuyakarabati katika muda stahiki, badala ya kusubiri mpaka mwaka 2015? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatib Saidi Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara ninapokuja hapa kujibu maswali yanayohusu stahiki na hali za askari wetu, kwa kweli nimekuwa ninasema kwamba ni hali ambayo hata sisi wenyewe haituridhishi. Lakini jitihada kwa kweli zinafanyika na ninaomba Bunge lako Tukufu, lituelewe hivyo kwamba, jitihada zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza la nyongeza, kuhusu mikopo, niseme kwamba mpaka sasa hivi kwa kweli hakuna kitu kama hicho kwa maana ya kusema kuna utaratibu katika nchi nzima. Lakini niseme kwamba hili ni suala ambalo limo katika utaratibu mzima wa maboresho. Tutakapotizama kuboresha zile Sheria na Kanuni zote za Jeshi la Polisi, ni kuona ni vipi maeneo kama haya tunaweza tukafanya ili kuhakikisha kwamba askari wetu wanakuwa katika ile dhana nzima ya maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, vilevile kwamba hata mimi mwenyewe inanitia simanzi kutizama hali halisi ilivyo ya majengo ambayo wanaishi askari wetu na niseme tu kwamba mimi nipo radhi na tayari tutapanga mimi na yeye na sio kwamba tu nitakwenda katika Jimbo lake, lakini nina azma ya kufanya ziara Zanzibar,

nitakwenda Pemba na nitakwenda Zanzibar kutizama hali halisi ilivyo katika vituo vyetu vya polisi, tuweze kuona ni mambo gani ambayo tunaweza tukayafanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kabla ya kuendelea Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuwaandaa watakaokuwa wachangiaji wetu mara baada ya kipindi hiki cha maswali ambapo watatu wa kwanza watakuwa ni Mheshimiwa Ezekia Wenje, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumter Mshama na Mchungaji Israel Natse, aendelee kujiandaa. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Fedha. Namuita Mheshimiwa Juma Nkamia.

Na. 430

**Shirika la Hifadhi ya Jamii – *NSSF* na Ujenzi wa *UDOM***

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ni muhimili muhimu katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma; na kwa sababu Shirika hilo linaendeshwa na michango ya wanachama wake na vitega uchumi walivyonavyo:-

Je, Serikali imekwishalipatia Shirika hilo kiasi gani cha fedha tangu lianze na kumaliza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya WazirI wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia sasa Serikali haijalipa *NSSF* kiasi chochote cha fedha katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Kinachosubiriwa ni kwa *NSSF* kutekeleza matakwa ya mkataba uliosainiwa tarehe 23 Mei, 2008 kati ya Wizara ya Fedha na *NSSF.* Kifungu cha 3(vi) ambapo pamoja na mambo mengine, kinaelekeza kwamba *NSSF* inapaswa kutayarisha na kuwasilisha taarifa ya kukamilika kwa mradi inayothibitisha hali ya ukamilifu wa mradi kiufundi na kifedha ikiambatanisha hesabu za mwisho *(final accounts).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 5(ii) cha mkataba huu, taarifa iliyowasilishwa na *NSSF* inapaswa kukubalika na pande husika ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambayo itaingia mkataba wa pango na *NSSF*. Mkataba huu wa pango utaonyesha kiasi halisi cha gharama za mradi pamoja na riba kinachotakiwa kulipwa kwa *NSSF* kila mwezi na malipo haya yanatakiwa kuanza kulipwa mwezi mmoja baada ya mkataba wa pango kuingiwa. Malipo haya yatalipwa kwa kipindi kisichozidi miaka kumi. *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Fedha ndio Mhusika Mkuu wa kushughulikia malipo haya ya *NSSF* kutokana na ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Je, Wizara haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kukutana yenyewe na *NSSF* kupitia Msajili wa Hazina, ili kumaliza tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Chuo Kikuu kwa sasa hivi sio nzuri sana. Kuna harufu mbaya inatoka katika maeneo ya mabweni ya wanafunzi na *NSSF* walikuwa wapo tayari kutengeneza *sewage system* ili kuondoa tatizo hili na huenda baada ya mwezi wa 10, wanafunzi watakapoingia hali inaweza kuwa mbaya zaidi. Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu sasa wa kumalizia malipo haya ya *NSSF* ili *NSSF* waweze kujenga *sewage system* ambayo wapo tayari?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nkamia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Wizara ya Fedha haina tatizo kukutana na *NSSF* ili kuendelea kulizungumza suala hili na kulikamilisha kwa mujibu wa mkataba uliowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu harufu mbaya, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba malipo ya *NSSF* kwenye ujenzi wa *UDOM* hayalipwi kwa kitita, yanalipwa kama malipo ya pango kwa mwezi. Kwa hiyo, bila ya mkataba wa pango kuingiwa, msaada wetu katika kufanya kazi zinazotakiwa ni mdogo, isipokuwa suala la harufu tutalifuatilia pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili tuone nini tunaweza kufanya kulimaliza. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa *NSSF* imekuwa ikifanya kazi kubwa nchini na hivi sasa ina mipango ya kuendelea kusaidia kuweka vitega uchumi katika mikoa mingine mingi nchini ikiwemo ujenzi wa nyumba za polisi, lakini na vitu vingine vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa tatizo hili la Kimkataba katika kujenga Chuo Kikuu cha *UDOM* mpaka sasa inaonekana kuna utata mkubwa sana wa makubaliano kati ya Wizara ya Fedha, kwa maana ya Serikali na *NSSF* yenyewe ili kuweza kukamilisha ujenzi wa Chuo hicho na kuendelea na miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yupo tayari sasa basi *NSSF,* Wizara ya Fedha, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, tukae pamoja na kuona nini kifanyike ili kuweza kulisaidia Shirika hili kuendelea kutoa huduma hizo muhimu sana katika nchi yetu ya Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba na mimi niipongeze sana *NSSF* kwa kazi kubwa inayoifanya kwa maendeleo ya nchi hii. Pia niseme kwamba Wizara ya Fedha haitakuwa kikwazo cha maendeleo ambayo yanaletwa na *NSSF* katika Taifa hili katika kutatua matatizo ya sekta tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha ipo tayari kukaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge pamoja na *NSSF* na wadau wengine ili kuona kama kuna utata unapatiwa ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Na. 431

**Uanzishwaji wa Hifadhi ya Msitu wa Minyughe**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU** aliuliza:-

Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 imeweka utaratibu mzima wa jinsi ya kuanzisha hifadhi ya misitu za aina mbalimbali na sheria imesisitiza ushirikishwaji wa wananchi wa maeneo husika katika mchakato mzima; hifadhi ya msitu wa Minyughe katika wilaya mpya ya Ikungi imeanzishwa bila kuzingatia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria husika na kuwaadhiri wananchi wa kata za Ighombwe, Iglanson, Issuna, Iyumbu, Mgungira, Minyughe, Muhintiri, Mwaru na Sepuka kutolipwa fidia:-

Je, wananchi wangapi katika vijiji mbalimbali kwenye kata zilizotajwa wameathirika na uanzishwaji wa hifadhi ya msitu huo katika maeneo yao?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafidia wananchi walioathirika na kuanzishwa kwa hifadhi hiyo?

Kama Serikali haina mpango wowote wa kuwafidia wananchi hao, je, itawarudisha wananchi hao katika maeneo yao waliyokuwa nayo kabla ya kuanzishwa hifadhi hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), na naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, msitu wa Minyughe una ukubwa wa hekta 264,600 na unamilikiwa na vijiji 19 vya Mtunduru, Masweya, Ighombwe, Mwaru, Mtugizi, Mlandala, Msosa, Misake, Mgungira, Mhintiri, Kinyamtembee, Mnyange, Iglansoni, Issuna, Mkiwa, Nkoiree, Nduru, Iyumbu na Ufuna. Vijiji hivi kwa pamoja mwaka 2003/2004 viliamua kuanzisha msitu wa Minyughe, chini ya usimamizi shirikishi wa misitu *(Community Based Forest Management – CBFM),* vikiwezeshwa na mradi wa *Land and Agriculture Management Project (LAMP)* chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa msitu huu ulianzishwa na vijiji chini ya usimamizi shirikishi wa misitu, msitu huu kwa 100% ni mali ya vijiji husika. Usimamizi na matumizi ya rasimali za msitu huu zipo chini ya Serikali za vijiji husika. Matumizi ya rasilimali za msitu huu yanaongozwa na sheria ndogo na mpango wa usimamizi endelevu waliojiwekea wakati wanaanzisha msitu huo. Kwa aina hii ya msitu Serikali Kuu au Halmashauri za Wilaya ni watoa ushauri tu wa kitaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hakuna fidia yoyote itakayolipwa na Serikali Kuu kwa wananchi waliohamishwa kwa kuwa uanzishwaji wake na usimamizi wake ni wa wananchi wa eneo lenyewe husika. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali langu halijajibiwa kwa utimilifu na baadaye nitaomba Mwongozo wako. Lakini hata hivyo, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Misitu inataka kila Hifadhi ya Msitu inayoanzishwa kwanza itangazwe katika Gazeti la Serikali, swali langu la kwanza ni je, Hifadhi ya Msitu wa Miyughe ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali namba ngapi? La Tarehe ngapi na la mwaka gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, na swali la pili, kwa vile kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu huu kumesababisha watu kunyang'anywa mali zao, na Katiba yetu inasema ni marufuku kwa mwananchi kunyang'anywa mali yake bila utaratibu wa sheria unaoweka fidia. Je, hilo jibu kwamba wananchi hawatakiwi kulipwa fidia wamelitioa kutoka sheria ipi ya nchi hii? Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza anauliza kwamba ni tangazo lipi la Serikali lililotumika. Ni kwamba mchakato wa kutangaza msitu huu haujakamilika. Kwa mujibu wa taratibu tunazozijua sisi ni kwamba taratibu zote za awali hadi kufikia makubaliano kwa vijiji husika ulifanyika na wakawa wamekubaliana. Kwa hiyo, ndio maana uendeshaji wake na usimamizi wake unazingatia makubaliano ambayo wananchi wenyewe wamejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la fidia kama nilivyosema, ni kwamba wananchi kwenye maeneo yao mbalimbali wanakubaliana namna gani watumie ardhi yao. Wapo wanaokubaliana eneo hili walitumie kwa ufugaji, eneo hili walitumie kwa shughuli nyingine zozote. Katika mazingira kama haya ambayo wananchi wenyewe wanakuwa wamekubaliana, ukiacha hii *element* ya wananchi kunyang'anywa mali zao ambayo sisi kama Wizara hatuna taarifa nazo ni kwamba wanapokuwa wamekubaliana kwamba wananchi wahamie eneo fulani, wanakuwa wamekubaliana na kupewa eneo la ardhi mbadala, na kama hiyo ilikamilika kama ambavyo

tuliambiwa, basi tunategemea kwamba haya mengine yote yalizingatiwa kwa jinsi walivyokuwa wamekubaliana wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Na. 432

**Ahadi ya Umeme - Namanyere**

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Serikali kupitia Waziri wa Nishati na Madini aliahidi kuwa ifikapo mwezi wa Machi, 2011 umeme utawaka katika Mji wa Namanyere ukitokea Sumbawanga:-

Je, Serikali ina maelezo gani juu ya utekelezaji wa ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ratiba ya utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Mji wa Namanyere kutokea Sumbawanga ulikuwa umebainisha kuwa barua za malipo *(letters of credit)* zifunguliwe mwezi Machi, 2010 ili hatua zingine stahili zifuatwe. Kwa mujibu wa ratiba hiyo ya awali mradi huo ungemalizika Machi, 2011 kama ilivyoelezwa na Waziri wa Nishati na Madini. Hata hivyo, barua hizo za *LC* kwa ajili ya mradi huo zilichelewa na zilifunguliwa mwezi Novemba, 2010, utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Desemba, 2010 na unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo unatekelezwa na mkandarasi kampuni ya Ro*usant International* ya Afrika ya Kusini. Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo *KV 33* wenye urefu wa kilomita 90 kutoka Sumbawanga na unasafirishwa kwenda Namanyere. Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *KV 0.4* kilomita 25 za usambazaji wa umeme utakapofika kwa wateja pale Namanyere, *transfoma* 18 njia nzima na uzalishaji wa umeme kwenye wateja kama 890 kwa tathmini iliyofanywa mwaka jana, nadhani kwa sasa hivi Mheshimiwa Kessy watakuwa wameongeza kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizokwishafanyika hadi sasa ni pamoja na upimaji na usanifu wa njia za umeme. Uchimbaji wa mashimo ya kusimika nguzo za nyaya za umeme pamoja na usimikaji nguzo unaoendelea. Hadi jana tarehe 15 Agosti, 2011 mashimo 818 kati ya 989 yalikuwa yameshachimbwa na nguzo 307 kati ya nguzo ya 898 zilishasimikwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Natumaini nguzo safari hii na asilimia ziko sahihi, Mheshimiwa Keissy swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kwa niaba ya wana Nkasi kusema kweli nawashukuru sana Waziri na Naibu Waziri baada ya siku 30 tu mradi umeshapunguzwa umefikia asilimia 34 ni kweli na leo asubuhi nimezungumza na Diwani amenihakikishia kabisa nguzo zilikuwa tayari, lakini namuomba Naibu Waziri kama yupo tayari kwenda kuangalia maana yake mradi utasuasua baadaye naona wananchi kule wanataka Naibu Waziri akaangalie au Waziri akaangalie mradi unavyokwenda. Je, yupo tayari kwenda kuangalia mradi jinsi unavyofanyika kule Namanyele? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa kifupi sana Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kupokea pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na wakandarasi waliopo hapo, lakini naomba nimuahidi Mheshimiwa Keissy na wakazi wa Nkasi Kaskazini kwamba Waziri wa Nishati na Madini ama mimi Naibu Waziri wake tutafika kwenye eneo hilo tukague utekelezaji wa mradi na kuangalia pia maeneo mengine ya karibu katika mradi huo ili mradi upate utekelezaji wa haraka. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, katika jibu lako la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameonyesha kwamba mradi huu umechelewa kwa takribani miezi nane, na imekuwa kawaida ya miradi mingi ya umeme kuchelewa hali ambayo inaongeza gharama za miradi na imekuwa kawaida vilevile ya kauli ambazo zinakuwa zikitolewa Bungeni kutokutelezwa ipasavyo ikiwemo kauli ya kabla ya Bajeti tulielezwa kwamba mgao utapungua lakini mara baada ya Bajeti kupitishwa mgao umeongezeka sana maeneo mbalimbali ya nchi.

Sasa ningeomba tu kauli ya Serikali, kwa hizi ahadi zinazotolewa Bungeni, Serikali inasimamiaje hizi ahadi zinazotolewa ili kuhakikisha kwamba hazicheleweshwi wala hazibadiliki badiliki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimsaidie tu Mheshimiwa John Mnyika, miradi hii inafanywa kwa utaratibu wa mikataba ambayo ama mkandarasi anaingia na *TANESCO* ama anainga na *REA,* kutokana na makubaliano yao ya *funding.* Na hakuna lengo la kuchelewesha miradi, hakuna mtu ambaye kwa makusudi anachelewesha miradi kwa sababu haifai mkandarasi kuchelewesha mradi wala na sisi haitufai kuchelewesha miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweka ratiba ambayo tunakusudia ndiyo itapata utekelezaji muafaka wa miradi na kulingana na ratiba hizo sisi tutasimamia mikataba hiyo ili mikataba na miradi hiyo ipate utekelezaji kwa wakati unaostahili. *(Makofi)*

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwa kuwa Wilaya ya Kilombero ina vyanzo viwili vya kuzalisha umeme vya Kihansi na Kidatu; na kwa kuwa kwenye mradi wa mpango kabambe wa kusambaza umeme vijijini kwenye mwaka huu Wilaya ya Kilombero, hatujapelekewa hata kijiji kimoja. Je, Waziri atukubaliana nami ya kwamba Wilaya ya Kilombero wana haki kabisa ya msingi ya kuingizwa kwenye mradi huu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Regia Mtema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Regia Mtema na hili si suala la kwa vijiji vilivyopo Kihansi na Kidatu tu, pia lipo kwa Mtera na kadhalika na tumesema na hata kwa yale maeneo ambayo yatazalisha gesi kwa mfano Mtwara, kuja kwenye Gridi ya Taifa, Lindi kuja kwenye Gridi ya Taifa Somanga, kuanzia sasa pale kwenye vyanzo vikuu vya umeme badala ya kutoka *transmission lines* ile kubwa kilowati 132 zinakwenda kuunganishwa kwenye ma-*transmission line,* pale pale pawe na uzalishaji mdogo wa kuingia kwenye nyaya za *KV 33* mpaka 11, ili maeneo yanayozunguka yafaidike na ule mradi kuwa pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa utaratibu huo Kidatu inatazamwa, Kihansi inatazamwa, Mtera inatazamwa, na maeneo yale mengine yote ambayo yatakuwa uzalishaji ambao unaingia kwenye gridi ndiyo utaratibu uliopangwa kwenye mpango. *(Makofi)*

Na. 433

**Nyakahura Kupatiwa Umeme**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA** aliuliza:-

Wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kupatiwa umeme eneo la Nyakahura:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais tarehe 26 Agosti, 2010 alitoa ahadi ya kupatiwa umeme eneo la Nyakahura. Upembuzi yakinifu ulifanywa kufuatia ahadi hiyo ya kupeleka umeme Nyakahura kutokea Biharamulo umbali wa kilomita kama 67 na gharama za mradi zilibainika kuwa shilingi bilioni 4.34. Sasa makadirio ya gharama za mradi yalishapelekwa *TANESCO* Makao Mkuu kwa ajili ya kutafutiwa fedha za utekelezaji. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kufanyika baada ya kupatikana hizo fedha yaani ufumbuzi wa tatizo la fedha. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru, naomba kwanza nisikubaliane na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, kulingana na ahadi iliyotolewa na Rais. Kwa kuwa katika majibu mengi tumekuwa tukiambiwa kwamba ahadi ya Rais utekelezaji na kwa kuwa kuna mradi wa umeme ambao unategemewa kupita eneo hilo kutokea Masaka, kupita jimbo la Karagwe kwenda Lusumo, Nyakahura, Lisaunga mpaka Nyakanazi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba ni wakati muafaka wa kutoa jibu ni lini wananchi hawa watapatiwa umeme hususan ikiwemo Shule ya Sekondari Nyakahura na zahanati iliyojengwa pale Kalalambe?

Pili, kwa kuwa imekuwa ni taabu, Biharamulo tuna jenereta ambayo tuna *share* na Wilaya ya Chato, ni lini nguzo zitandandazwa ili kusudi wananchi wetu waweze kupata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Ni lini? Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbassa kwamba katika utekelezaji wa ahadi za Rais, ni utekelezaji ambao tunatarajia ufanyike ndani ya kipindi cha miaka mitano na siyo blabla, ni kwamba hatua ya kwanza kwenye mradi wa umeme ni kwamba lazima ufanyie tathmini na tathmini iliyofanyiwa umebaini kwamba una shilingi bilioni 4.34 kwa hiyo katika jumla ya miradi yote ambayo tulikuwa tunaanza nayo ipo katika utekelezaji pamoja na hizi ahadi za Rais. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutaitafutia ufumbuzi na tutaitafutia pesa ili ipate utekelezaji kwa hiyo, hili limo na hatua ya kwanza ya kufanya tathmini ya mradi tayari kwa hiyo, hatua ya pili ni hiyo ambayo tutapitia *TANESCO* kwa maana ya Serikali Kuu ama tutapitia *REA* lakini jinsi tutakavyokuwa tunapata ufumbuzi wa ku-*financing* hii kitu tutakuambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la nguzo sikuelewa kwa sababu pale umekwenda mpaka Nyakanazi ambako kuna mradi wa *transmission line* kubwa inayotoka inazunguka huku, sasa sikuelewa kama ulikuwa unazungumza kwa sababu umetaja Chato na Biharamulo. Lakini nina imani kwamba kama anazungumzia nguzo, nguzo za kusambaza umeme katika maeneo yale nimelipokea na tutalifanyia kazi, kwa sababu kama kuna tatizo la usambazi basi ni jambo la kwenda kulifanyia kazi na kuona kiwango cha tatizo. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo pia Serikali iliahidi kutupatia umeme wa kuanzia wa jenereta na mwaka jana Serikali iliweka Bajeti ya kununua jenereta na mwezi Disemba walikuja wataalam na tukawapa eneo la kuweka jenereta hiyo na wakatuambia mwezi Julai, umeme huo ungewaka na katika kauli ya Serikali Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni alisema umeme huo utaanza kuwaka mwezi Disemba. Lakini mpaka sasa hivi nazungumza hata dalili hakuna *site clearance* wala dalili

zozote zinazoonyesha kwamba mwezi Disemba utapatikana umeme huo, je, Serikali inaweza kutueleza, ni kweli mwezi Disemba umeme huo utawaka?

**NAIBU SPIKA:** Umeme wa Namtumbo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vita Kawawa anajua tumekwenda wote Namtumbo na baada ya kufanya ziara ile pale tuligundua kwamba Namtumbo pana mahitaji ya umeme ambayo baada ya ile 2009, tukapeleka watu wamefanya tathmini na wamebaini kwamba kwanza tulifikiria kwamba jenereta kama Megawati moja lingefika pale lingetosheleza kwa mahitaji mapana yaliyoko pale baina ya ofisi ya wilaya na hospitali na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameniwasilishia malalamiko ya kwamba katika jenereta yenyewe kwanza kabla ya hata hizi kazi za *ground clearance* na nini, jenereta iliyopelekwa pale ni ya megawati 0.4 ambayo ni jenereta ndogo, na mahitaji ya pale yanakisiwa kufikia karibu megawati moja. Sasa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Vita Kawawa, kwanza kuna lile tatizo la jenereta lenyewe kwamba ni dogo, umeliwasilisha na mimi nimewapelekea *TANESCO* wanasema kwa sababu ni jenereta la mpito likisubiri umeme wa Makambako - Songea, bado nakubaliana na wewe kwamba umeme huo upo mbali, tulitizame. *(Makofi)*

Lakini hili la pili, ni kwamba nadhani hii kazi ya kufanya *ground clearance* ya pale na kujenga kitako kimesimama kidogo kwa sababu tuna utata wa hilo jenereta. Ukisema jenereta la *0.4 KV* maana yake kitako kidogo, ukisema kubwa zaidi maana yake kitako kikubwa, kwa hiyo nadhani kwanza tupate ufumbuzi wa hilo jenereta halafu hizo kazi nakuhakikishia kwamba tutasimamia kwa pamoja ili zipate utekelezaji wa haraka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nishati ya umeme ni kero ya wananchi, maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Nishati na Madini kupitia *REA,* Bwawa la Nyumba ya Mungu kuna sekondari inayoitwa sekondari ya Nyumba ya Mungu kilomita tano tu kutoka kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu ambayo haina umeme na ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa miaka karibu mitano iliyopita sasa.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kukamilisha ahadi hiyo ya Rais kwa kupeleka umeme katika shule ya sekondari ya Nyumba ya Mungu, iliyopo kilomita tatu tu kutoka mahali umeme unapozalishwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ole-Sendeka kama ifuatavyo:-

Ni kweli pana ahadi pale katika orodha ya ahadi ipo ni kilomita tatu, nne hivi ambazo ni kama kwa gharama za sasa hivi ukiweka na *transfoma* labda kwenye shilingi milioni 130 kiasi kama hapo sasa na mimi namuomba Mheshimiwa Ole-Sendeka tuendelee kufuatilia na *REA,* tuone kwa sababu kama nilivyosema mwaka jana palikuwa na tatizo la upatikanaji wa fedha ndiyo haikutekelezwa. Tuone kama mwaka huu tunaweza tukaichomeka kwa sababu ni ahadi na kusema kweli pana umuhimu wa kupeleka umeme kwenye shule ya sekondari. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuwa tangu mwaka 2007 Serikali ilipeleka nguzo katika maeneo ya Kayanga, Ndama, Nyabwegira hadi Runyaga na nguzo hizo zingine zimesimama na zingine zimelala chini na wananchi wa kule wamekasirika wanatishia hata kuzichoma moto. Lakini pia kwa kuwa ahadi ya Rais ya kupeleka umeme vijiji vya Busheshe, Nyakayanja, Nyaishozi hadi Ihende, sioni dalili yoyote ambayo Serikali

inatekeleza na pia umeme wa Bugene, Kiruruma hadi Nyakaiga, je, Serikali inasema nini kuhusiana na ahadi za Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi aliyoitaja Mheshimiwa Blandes hapa tayari pana miradi kama mitatu hivi, pana huu wa Nyabwegire huu, pana huu Nyakayanja na ameutaja Nyaishozi na ambao Mheshimiwa Mama Ishengoma amekuwa anausemea sana na kuna huu mradi wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pana miradi ambayo inatekelezwa na *REA* na kama alivyosema kuna nguzo ambazo zimekaa pale chini hiyo sasa ni miradi ya *TANESCO,* zile ambazo nguzo zimelala, naomba msizichome moto mpaka zikafanyiwe tathmini zionekane hali ya nguzo zenyewe. Kuna kazi za *TANESCO* na kazi za *REA,* naomba nimhakikishie kwamba pana mikakati, pana miradi mingi kidogo pale mkoani Kagera pamoja na ule mradi wa kule Nkege kwa Mheshimiwa Assumpter na kadhalika, pana miradi mingi kidogo. *(Makofi)*

Naomba nikusanye miradi yote ya Kagera ili kwa miradi yote iliyozunguka eneo lile kuanzia Karagwe, Muleba, Bukoba Vijijini na wapi nikupeni utekelezaji na hatua tulizofikia kwa yote lakini ni kweli kwamba hii miradi mingine iliyotolewa ahadi kwenye kipindi kile kile nilipokuwa najibu swali la Biharamulo ahadi ni wakati ule ule wa mwezi wa nane, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nipate utekelezaji wa miradi hii ili niwapatie Wabunge wote wa Kagera kwa pamoja. *(Makofi)*

Na, 434

**Tatizo la Maji- Mji wa Geita**

**MHE. VICK P. KAMATA** aliuliza:-

Mji wa Geita unakua haraka sana kutokana na ongezeko la shughuli za kibiashara, kijamii na idadi ya watu hali inayosababisha upatikanaji wa maji ya uhakika kuwa mgumu.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuupatia Mji wa Geita maji ya kutosha hasa kwa kuwa mji huo unatarajiwa kuwa makao makuu ya mkoa wa Geita?

Je, ni lini Serikali itatekeleza mpango wa kuupatia Mji wa Geita maji kutoka Ziwa Victoria na vyanzo vingine ili kukidhi mahitaji kwa muda wa kati na mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vick Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatekeleza miradi miwili ya muda mfupi kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Geita, miradi hiyo ni *Lake Victoria Water and Sanitation Initiatives Phase II* unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Na mradi wa maji ya kunywa *Geita Potable Water Supply* unaogharamiwa na kampuni ya Mgodi wa Geita. *(Makofi)*

Mradi wa *Lake Victoria sanitation Phase II,* utakuwa na awamu mbili, mpango wa dharura na mpango wa kati. Katika mpango wa dharura, kazi zifuatazo zitafanyika:-

Kupanua na kukarabati miundombinu ya maji, kufunga *pump* mpya Tambukareli, kufunga mita za maji, kununua vifaa vya kupima ubora wa maji, kujenga matanki kumi madogo ya maji na kununua gari moja na pikipiki tatu. Mpango wa kati utahusisha usanifu wa miradi mbalimbali ya maji Geita ikiwa ni pamoja na matumizi ya maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mwanza kwa kushirikiana na *UN Habitat* inakamilisha utaratibu za kumwajiri mtaalam mshauri atakayesimamia mpango wa dharura na kusanifu mradi. Mtaalam huyo ataajiriwa mwezi Oktoba, 2011 na utekelezaji wa mpango wa dharura utaanza mwezi Desemba, 2011 baada ya mkandarasi kuajiriwa. Usanifu wa mpango wa muda wa kati utaanza mwezi Novemba, 2011 na kukamilika mwezi Desemba, 2013 na ujenzi wa miradi utaanza Januari, 2014. Jumla ya shilingi bilioni 6.4 zimetolewa kupitia *Lake Victoria Initiatives Phase II* kwa ajili ya miradi mbalimbali Geita ikiwa ni pamoja na miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji ya kunywa Geita unaofadhiliwa na mgodi utagharimu shilingi bilioni 6.99. Chanzo cha maji ni Bwawa la Nyankanga linalopata maji kutoka bomba kuu linalopeleka maji kwenye Mgodi kutoka Ziwa Victoria. Kazi zitakazofanyika ni ununuzi wa pampu ya kusukuma maji, ulazaji wa bomba kuu hadi kwenye matanki na ujenzi wa nyumba ya mtambo, chujio la maji na matanki mawili yenye mita za ujazo 600 kila moja. Ujenzi wa mradi huo utaanza mwezi Septemba, 2011 na kukamilika mwezi Februari, 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mrefu Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imeanza usanifu wa Mradi wa Majisafi na Majitaka katika Mji wa Geita kupitia mtaalamu mshauri *Don Consult Ltd.* aliyeajiriwa mwezi Septemba, 2009. Mpango huo utaangalia mahitaji ya maji Geita hadi kufikia mwaka 2032. Usanifu utakamilika mwezi Septemba, 2011 na ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2012/2013. Matokeo ya usanifu huo yataelekeza aina ya teknolojia ya muda mrefu itakayofaa kuboresha huduma ya maji Geita. *(Makofi)*

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwanza kabisa namshukuru Naibu Waziri wa Maji kwa majibu mazuri ambayo naamini kabisa yamekonga nyoyo za wananchi wote wa Geita. Naipongeza sana Serikali, naipongeza sana Benki ya Maendeleo ya Afrika, nawapongeza sana *GGM* na ninaamini kabisa sasa tatizo la maji Mkoa wetu mpya wa Geita litakuwa ni historia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba niipongeze Serikali kwa jitihada hizi lakini ninaomba kama Naibu Waziri atakuwa na nafasi tuongozane hadi Geita kwa sababu takwimu anazozitoa hapa sisi tumekaa na Mgodi wa *GGM,* programu hii ni ya muda mrefu sasa hivi tukianza kuzungumzia mwaka 2012/2013 hatukubaliani na hilo.

Ninachosema mimi ni kwamba upande wa Serikali kidogo tunachelewa kiutekelezaji, *GGM* imeshaanza kazi hiyo, bomba zimeshaingia, tunaona gari la maji linazunguka Geita saa 24. Katika hizo saa 24 hata ule usanifu mitaa gani bomba zitapita ili tusianze haya mambo ya fidia kwa nyumba za watu, ile ramani toka mwaka jana tunaipigia kelele hadi sasa. Kwa hiyo, ninaomba kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri naomba twende wote Geita na mimi nikiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Donald Max pamoja na kushukuru pongezi za Mheshimiwa Vick Kamata kwa swali lake la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kweli Geita tatizo la maji ni kubwa na kitu ambacho kimeleta matatizo kuchelewesha mradi huu wa pili wa *Geita Gold Mine* ni kile chanzo ambacho walikuwa wameainisha kutoa maji, Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Geita walikuwa wanakipinga kwa kuhofia kwamba labda kuna uchafuzi wa kile chanzo. Sasa kwa sasa hivi baada ya kupima vipimo vyote vimeonyesha kwamba yale maji ni safi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba ndugu yangu Mheshimiwa Donald Max pamoja na kwamba mimi nitakuja kuangalia lakini washawishi Madiwani wakubali utaalamu unaoelekeza kwamba yale maji ni safi ili ule mradi wa pili tuanze kuchukua maji pale na wananchi wa Geita waanze kupata maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Najua kabisa suala la maji ni kero ya wananchi, Wizara hii inakuja Waheshimiwa Wabunge naomba tuvumiliane. *(Makofi)*

Swali la mwisho kwa leo ni ni swail namba 426 naomba Mheshimiwa James Lembeli aulize.

Na. 426

**Kukamilika kwa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kishapu**

**MHE. JAMES D. LEMBELI (K.N.Y. MHE. SULEIMAN NCHAMBI SULEIMAN)** aliuliza:-

Wilaya ya Kishapu haina Hospitali ya Wilaya tangu mwaka 2003 na Hospitali iliyoanzishwa kujengwa bado haijakamilika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa kipaumbele katika kumaliza ujenzi wa Hospitali hiyo ili kuondokana na aibu ya wananchi kuendelea kuteseka kwa kukosa matibabu kwa ngazi ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Nchambi, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu haina Hospitali ya Wilaya. Ni kweli kwamba Serikali imeanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya hiyo kwa lengo la kuwaondolea adha ya matibabu wananchi wa Wilaya hii. Katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 Halmashauri ilitenga shilingi milioni 101 fedha za Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa *(LGCG)* kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* ambapo ujenzi umefanyika na jengo limefikia hatua ya kuezekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo, Halmashauri katika mwaka 2011/2012 Halmashauri imepanga kutumia shilingi bilioni 219.9 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 189.9 ni fedha za Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa *(LGCG)* na shilingi milioni 29.96 ni vyanzo vya ndani ya Halmashauri. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa Wodi mbili za Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo, Halmashauri katika mwaka 2011/2012 imewasilisha maombi maalum shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hiyo. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa jengo la *OPD,* ujenzi wa chumba cha upasuaji, chumba za maabara na chumba cha kuhifadhia maiti. Fedha hizi zitatarajiwa kukamilisha ujenzi wa Hopitali ya Wilaya ya Kishapu hadi kutumika. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Kishapu ilianzishwa muda mrefu; na kwa kuwa Serikali kila mwaka imeendelea kutoa ahadi za kutenga pesa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo na ukilinganisha na Kishapu kuwa ni Wilaya yenye utajiri mkubwa wa almasi na pamba. Serikali haioni kwamba kuendelea kutoa ahadi kama hizi kwa muda mrefu na ukilinganisha na utajiri uliopo pale haiwatendei haki ya msingi wananchi wa Wilaya ya Kishapu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema hapa ni kweli, ukiwa na *economic base* ita-*determine the super structure,* itakuonyesha na kukuambia kwamba hapa hali inakwenda hivi. Sasa kinachosemwa hapa yeye Mheshimiwa Lembeli haoni *coloration* kati ya utajiri uliopo pale Kishapu na hali halisi inayojitokeza pale. *(Makofi)*

Mimi nimekwenda Kishapu na hiki kinachozungumzwa hapa ninakifahamu, hao wananchi wa Kishapu wanaozungumzwa ukijibu hapa kwamba hujali hilo jambo utakuwa mtu wa ajabu sana. Kilichotokea hapa ni hii changamoto kwetu sisi maana yake Halmashauri ndizo zinazojenga hospitali, haijengwi na Serikali Kuu kwani Serikali Kuu haijengi hospitali kuu, kinachojenga Hospitali, Zahanati na Vituo vya Afya ni Halmashauri na Halmashauri ikiona kwamba kujenga hospitali ni kipaumbele hakuna mtu atakayebisha katika jambo hili, *it is unfortunately* sasa kwamba tunachoambiwa hapa ni kwamba kuna hilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzetu ameomba sasa hivi shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kufanya kazi hii inayozungumzwa hapa; na Mheshimiwa Lembeli Kahama nimekwenda mara tatu pale anafahamu, nimefika pale! Sasa tufanyaje? Tusema hapa hapa leo itajengwa hospitali au lah! Leo leo itakamilika! Haitawezekana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kumuahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba *concern* yake tumeiona na tutahakikisha kwamba tunasimamia jambo hili ili wananchi wa Kishapu waweze kupata hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mimi napenda nimuulize Waziri kwamba kwa kuwa hospitali nyingi za Wilaya zimekuwa zikijengwa lakini hospitali hizi hazina madaktari wa kutosha wala vipimo vya kutosha vya kupima magonjwa ya Watanzania yaani maradhi mbalimbali. Je, Waziri atanihakikishiaje hizi hospitali zinazojengwa zinapata madaktari na vipimo vya kutosha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Msabaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mawili anayozungumza ni kweli na Mheshimiwa Waziri wa Afya alipokuwa anapitisha hapa Bajeti yake tulikuwa tunazungumza hapa kwamba sasa hivi utaratibu tuliouweka ni kwamba madaktari badala ya kupita katikati humu waende moja kwa moja wapelekwe katika Halmashauri zinazohusika. Kwa hiyo, nina uhakikika kabisa kwamba hili tatizo litakuwa limemalizika. *(Makofi)*

Hili la madawa tuliambiwa kwamba ni dawa na siyo madawa, kuna kitu kinachoitwa *Integrated Logistical System* ambacho kimekuwa *introduced,* hii Bohari ya Dawa imehama kutoka Makao Makuu sasa hivi tumezipeleka katika Kanda na katika hiyo *Integrated Logistic System* tulichosema pale ni kwamba twende tukatambue hali halisi ya pale panapohusika, dawa za aina gani zinatakiwa pale, matatizo yaliyopo katika lile eneo ni ya aina gani na kwa hiyo, tuweze kubaini kwamba ni kiasi gani cha dawa kiweze kupelekwa pale. Kwa hiyo, utaratibu huu niliousema hapa mimi nina hakika kwamba hii ni hatua kubwa ambayo itatusaidia kuondokana na matatizo ya dawa katika vituo vya afya na katika hospitali zetu. *(Makofi)*

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mji wa Bahi sasa ni Makao Wakuu ya Wilaya ya Bahi na kwa kuwa wahamiaji sasa kutoka  watumishi, wafanyabiashara na wawekezaji wengine wamekuwa na nafasi kubwa na hivyo Kituo cha Afya cha Kijiji cha Bahi kimeelemewa kwa maana ya idadi ya wagonjwa na tayari Halmashauri imeomba mara tatu Serikalini kupata fedha kuanza kujenga Hospitali ya Wilaya katika Mji wa Bahi na haijafanikiwa. Je, Serikali ni lini sasa itaanza kutoa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Mji wa Bahi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omary Badwel, Mbunge wa Bahi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Halmashauri inayozungumzwa hapa ni Halmashauri mpya na katika hizi Halmashauri mpya sisi kama Serikali tunaona kwamba kuna haja ya kuzipa kipaumbele. Sina takwimu hapa sasa hivi nitakwenda kumtafutia Mheshimiwa Badwel kujua kwamba tumeweka kiasi gani katika *Local Government Capital Grant* kwa sababu hiyo ndiyo tunaikimbilia mara moja 50% ya hiyo fedha ni lazima ibaki katika Halmashauri na 50% ndiyo inayokwenda kwenye Kata, Vijiji na Vitongoji. Kwa hiyo, nitakwenda kuiangalia *figure* hii ili niweze kujua vizuri lakini *the Member of Parliament is making a very valid point* hapa kuzungumzia habari ya Hospitali ya Wilaya kwa sababu Bahi ni Halmashauri mpya na ni Wilaya mpya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Maswali yamekwisha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, matangazo ni kama ifuatavyo:-

Naomba niwatambulishe wageni tulionao hapa Bungeni nikianza na wale ambao wapo kwenye jukwaa la Spika, naomba kuwatambua wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge Mheshimiwa William Lukuvi na mgeni wake ni Ndugu Fadhil Nyomolelo. *(Makofi)*

Pia naomba kutambua wageni 16 ambao ni viongozi wa Makanisa mbalimbali nao ni wageni wa Mheshimiwa William Lukuvi, hawajafika kutoka Isimani. *(Makofi)*

Pia wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 70 wa *Club* ya Wapinga Rushwa kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri na Shule ya Sekondari ya *Central* zote za Dodoma mjini. Karibuni sana nafikiri Bungeni mmeweze kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. *(Makofi)*

Naomba kumtambulisha mgeni wa Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye ni *CO* wa *Dar es Salaam Community Bank* Ndugu Edmund Mkwawa. Karibu sana! *(Makofi)*

Naomba kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Naibu Waziri wa Ujenzi ambao ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela Ndugu Mwasasumbe pamoja na Afisa Utumishi wa Mamlaka ya Mji huo mdogo wa Kyela Ndugu Sanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mhandisi Gerson Lwenge, Naibu Waziri wa Maji anawatambulisha Madiwani wake watano kutoka Jimbo la Njombe Magharibi. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani muone mambo yanavyoendelea hapa na mlinganishe tofauti ya Baraza la Madiwani na Bunge, kule kwenye Baraza la Madiwani wote mnavaa majoho lakini hapa navaa mimi tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Richard Ndassa, anaomba kumtambulisha mgeni wake ambaye ni Mheshimiwa Balozi John Paul Rupia, huyo ni mmoja wa wazee wetu na alishafanya kazi mpaka Ofisi ya Rais wakati huo akiwa Katibu Mkuu na Mkuu wa Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Matangazo ya vikao mbalimbali, kikao cha kwanza Katibu wa Wabunge wote wa CCM Mheshimiwa Jenista Mhagama anawaomba Wabunge wa CCM saa 7.15 mchana baada ya kutoka hapa kama kawaida nadhani tumeelewana, kule kule. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge wa Kupiga Vita UKIMWI Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o *(TAPAC),* maana hapa kuna Kamati ya UKIMWI na Chama cha Kupiga Vita UKIMWI na Mwenyekiti wake wa vyama vyote viwili nafikiri ni yeye mwenyewe Mheshimiwa Mng'ong'o kwa hiyo, hili linahusu *TAPAC. (Makofi)*

Wanachama wote wa *TAPAC* na wale wapya wanaotaka kujiandikisha kuna kikao leo kuanzia saa 7.15 mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Sasa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o itabidi mtafute ukumbi mwingine kwa sababu CCM watakuwa huko. *(Makofi)*

Mama Kippa, Kaimu Afisa Utumishi Ofisi ya Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye viwanja vya maonyesho ya Bunge kuna maonyesho ya magari yanayotumia gesi pamoja na majiko yanayotumia gesi, tunaombwa kufika na kuyaona. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho ni la Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa anaomba Kamati yake wakutane leo baada ya saa 7.15 mchana katika ukumbi namba 227. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea na shughuli nyingine, Katibu!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Wale wanaotaka Mwongozo wote wasimame Mheshimiwa Zambi usiwashe *microphone* kwanza, ni wawili na ninafunga daftari langu. *(Makofi)*

Tunaanza na Mheshimiwa Tundu Lissu !

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo lililotokea wakati wa kipindi cha maswali na Mwongozo ninaoomba unahusu swali langu namba 431 pamoja na swali moja la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo kidogo kwa nini naomba Mwongozo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali langu la msingi niliuliza maswali matatu ya msingi, niliuliza ni wananchi wangapi ambao wameathiriwa na uanzishwaji wa hifadhi ya msitu wa Minyughe, (b) niliuliza Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia kwa wananchi walioathirika kutokana na uanzishwaji wa hifadhi hiyo na (c) niliuliza kama Serikali haina mpango wowote wa kuwalipa wananchi fidia, je, ipo tayari kuwarudisha katika maeneo waliyokuwamo kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi ?

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri katika maswali yote matatu amejibu swali (b) kwamba Serikali haina mpango wowote wa kulipa fidia. Swali la kwanza wananchi wangapi wameathiriwa na uanzishaji wa hifadhi, halijajibiwa kabisa. Swali (c) kama kuna mpango wa kuwarudisha kwa sababu hawajalipwa fidia halijajibiwa kabisa na swali la nyongeza kwamba ni tangazo gani la Serikali lililoanzisha hifadhi ya msitu wa Minyughe vilevile halijajibiwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili inawawajibisha Mawaziri kujibu maswali kikamilifu kama yanavyoulizwa, na Kanuni ya 45(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inasema kwamba; "Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika Kikao kingine cha Bunge."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa vile mimi sijaridhika na majibu ya maswali yangu naomba utoe Mwongozo, kama huu si muda muafaka kwa Mheshimiwa Naibu Spika, kumwelekeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ajibu haya maswali kwa ufasaha katika Kikao kijacho cha Bunge. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mmwongozo wako kwa kuzingatia Kkanuni ya 68(7), lakini pia na ile ya Kkanuni ya 46(1) ambayo inazungumzia Mawaziri kujibu maswali kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati wa kipindi cha maswali na majibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja alipokuwa anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Kiwanga kuhusiana na kupanda bei ya mafuta ambayo ilikuwa imetangazwa juzi na Mamlaka ya Maji na Nishati *(EWURA).* Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua hivi kwa nini bei ya mafuta inapanda kwa mafuta ambayo tayari yalikuwepo nchini na wakati huo Wizara ilishatuhakikishia kwamba yalikuwepo mafuta ya kutosha ya kuweza kutumika kwa zaidi ya siku 60.

Mwisho Waziri akasema anafikiri *EWURA* inaweza ikawa imefanya makosa kwa kuamua bei ya mafuta yaliyokuwepo nchini yaanze kutumia bei mpya jana. Lakini pia jana usiku nikamsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa *EWURA* akisema kwamba sheria za kodi inataka mkipandisha mafuta bei inaanza kutumika *immediately* hapo hapo. *(Makofi)*

Sasa nataka kujua Mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amelieleza Bunge hili na nikiamini kwamba yeye ndio Serikali na yule ni Mkurugenzi ambaye anawajibika kwake wametoa majibu mawili ya kuwakanganya wananchi. Lakini pia haiingia akilini kwa viongozi wawili wakitofautiana, Mkurugenzi wa *EWURA* amemsikia Waziri wake akisema na yeye anaenda kusema vinginevyo kwenye vyombo vya habari. Katika hili Serikali inatueleza nini, naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nianze na Mwongozo wa Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lissu alikuwa na hoja mbili. Moja hajaridhika na majibu yaliyotolewa, lakini ya pili, yapo majibu ambayo hayakupatikana kabisa kwa maswali aliyoyauliza. Sasa nitaanza na ile ya kwanza ya kutokuridhika na majibu. *(Makofi)*

Kama tunavyofahamu Waheshimiwa Wabunge, Bunge linaendeshwa kwa Kanuni, taratibu, miongozo mbalimbali, maamuzi ya Maspika. Sasa kwa wale ambao tulikuwepo hapa tarehe 15 Agosti, jana tu hapa Mheshimiwa Lucy Owenya aliuliza swali linalofanana kabisa na swali la Mheshimiwa Tundu Lissu akataka Mwongozo kwa Spika Mheshimiwa Anne Makinda akiwa hapa kwenye kiti, kufuatia swali lake kutokujibiwa vizuri na akatumia vifungu vilevile ambavyo Mheshimiwa Tundu Lissu amevitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika akajibu ifuatavyo na hapa nanukuu; “Ni mimi tu ambaye nina mamlaka ya kumwambia Waziri jibu lako sijaridhika, ukarudie tena. Sasa hilo unaweza kulileta kwa utaratibu mwingine.” Kwa jinsi hiyo Wabunge ambao majibu yao hawaridhiki nao wanapaswa kuyaleta maswali yao kwa utaratibu mwingine. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, Mheshimiwa Tundu Lissu amesema kwamba maswali yake ameyaeleza kama matatu hivi hayakujibiwa kabisa. Sasa kwa yale maswali ambayo hayakujibiwa kabisa Mwongozo wangu ni kwamba Makatibu hakikisheni kwamba swali hilo linapangiwa katika siku za karibuni ili liweze kupata majibu muafaka kwa maeneo ambayo hayakujibiwa kabisa. *(Makofi)*

Hili la pili la Mheshimiwa Zambi la ufafanuzi wa migongano ya kauli kati ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Taasisi ya *EWURA* ambayo ndiyo inahusika na masuala haya tutawasiliana na Serikali kwa wakati muafaka nitatoa Mwongozo wangu. *(Makofi)*

**Hoja za Serikali**

**Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mheshimiwa Ezekia Wenje na Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Mshama ajiandae.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyamagana naomba sasa nianze kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimezaliwa miaka kama 18 baada ya Uhuru na historia inasema kwamba kipindi Wakoloni walipokuwepo kwenye Taifa hili, kipindi wanauchumi wa Kikoloni *(The so called colonial economy)* ardhi ya wakulima ile ardhi nzuri ambayo tunaita *fertile land* ilikuwa inachukuliwa na Wazungu. Walichukua maeneo makubwa na hili lilipelekea kutengeneza matabaka makubwa kati ya wenye ardhi na Waafrika wengi wasiokuwa na ardhi. Sasa leo miaka 50 baadaye, baada ya sasa kupigana tukapata Uhuru utaratibu huu unarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii kuna Watanzania wasomi wachache waliopata imani ya Watanzania wengi na wakawaunga mkono kudai Uhuru wa nchi hii na ahadi ya wale Watanzania waliopigania Uhuru walikuwa na lengo na maono ya kutengeneza nchi isiyokuwepo na matabaka ya wenye ardhi na wasiokuwa na ardhi au wenye nacho na wasiokuwa nacho. *(Makofi)*

Sasa leo miaka 50 baada ya Uhuru ukija Mwanza ninakotoka naanzia sehemu moja panaitwa Luchelele kuna matatizo makubwa ya ardhi. Hapa ni sehemu ambapo kuna *beach* tunasema ufukwe wa Ziwa kwenye Kanda ya Ziwa, Ziwa Victoria. Ni sehemu nzuri lakini kuna watu waliozaliwa pale miaka nenda rudi. Kuna wazee wa Kisukuma wanaishi pale toka babu na babu na ndio ardhi yao wamezaliwa hapo. Leo kuna watu wachache wanaoamini kwamba wao ndio wana haki ya kuishi kwenye *beach,* wengine hawana haki ya kuishi kwenye *beach* ile, ardhi ya Luchelele ilichukuliwa na hata leo tunapozungumza Mkurugenzi wa Jiji wa Mwanza amejenga hoteli kubwa hapo ninaposema Luchelele na wananchi waliokuwa wanaishi yale maeneo ile ardhi iliyochukuliwa wakapewa *compensation* ya ajabu kweli na hakuna, walipewa fidia ya fedha kidogo, lakini hakuna ardhi mbadala waliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu ulikuwa na ardhi kwa mfano heka nane wanakuja wanapima, wakishapima mwananchi anaachia kiwanja cha *plot* moja halafu yeye anapewa fidia kwenye viwanja nane anapewa fidia ya shilingi milioni sita halafu kile kimoja anachopewa anaambiwa pia alipie labda shilingi milioni tatu ndani ya wiki moja, inafikia wakati ardhi inapimwa, wananchi wanatakiwa wahame na hata fidia hawajapewa ardhi yao imeshauziwa watu wengine na wale watu wanatakiwa waje waanze kujenga na huyu mtu anatakiwa ahame na fidia hajapewa hivi hawa watu waende wapi? Kwa hiyo, fidia inayotolewa ni ndogo sana katika hili eneo la ardhi.

Naomba hili mtusaidie Mwanza kuna matatizo makubwa, eneo panaitwa Luchelele Ziwani wananchi waliporwa ardhi, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mheshimiwa Amanzi amejitahidi sana kufanya vikao vingi na akatoa hata maelekezo Jiji kwamba hawa watu walipewa fidia kidogo waongezeni fidia hapa mpaka leo wale watu hawajapewa fidia yao. Hata Mkuu wa Wilaya amejitahidi, jitihada zake zimefikia hapo, ni matatizo makubwa wananchi wanalalamika kila siku. Sasa hili ni tatizo naomba mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na lile eneo la Luchelele Mwanza kuna eneo lingine linaitwa *Capri Point* lina tatizo kubwa kati ya wananchi na Kanisa. Imekuwa *deal dull* miaka mingi. Kila wakati watu wa Jiji wanaenda wanapima, mtu anayetakiwa kutoa fidia haijulikani, ni tatizo la miaka na miaka na miaka. Wananchi wanaoishi pale hawaruhusiwi tena ku-*develop* nyumba zao kwa sababu haieleweki nani anamiliki ile ardhi. Tunaomba mtusaidie. Sio hapo tu kuna eneo lingine sehemu ya Isamilo, watu wa Jiji walienda wanapima mpaka leo wananchi hawapewi fidia. Sasa mtu hajapewa fidia hawezi aka-*develop* nyumba yake na anatakiwa ahame na fidia hajapewa, sasa atahama ataenda wapi? *(Makofi)*

Sasa mimi nilikuwa napendekeza sio hapo tu kuna hiyo Isamilo, kuna Bugarika, Maina, Butimba Jiji la Mwanza kila kona kuna matatizo ya ardhi kwa sababu ule mji unakuwa kwa kasi kubwa sana. Sasa unapokuwa kwa kasi kubwa na thamani ya ardhi pia inaongezeka, kwa hiyo matatizo ya ardhi yanaongezeka kila kukicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri kwa nini Serikali isione kwamba kwa sasa ni muda muafaka wa maeneo kama Majiji haya kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha ambapo kuna matatizo makubwa ya ardhi kwa nini Maafisa Ardhi wao wanaoitwa Mipango Miji kwenye hayo maeneo, kwa nini wasiripoti moja kwa moja Wizarani? Kwa sababu hapa itampa Waziri rungu moja kwa moja la kwenda ku-*inspect* na kuwawajibisha moja kwa moja panapokuwepo na matatizo. Hili suala kwamba wanaripoti ndani ya Halmashauri mle mle linafanya hata Waziri akienda kutumia rungu lake kwa *discipline* itakuwa ni ngumu. *(Makofi)*

Mimi napendekeza kwamba kwenye maeneo ambayo ni *strategic* kama hii miji, hao Maafisa Mipango waripoti moja kwa moja Wizarani au iwepo na *direct link* ya *supervision* kati ya Wizara ya Ardhi na Halmashauri ili Waziri wa Ardhi awe na uwezo wa kuwawajibisha. Kama hiyo inawezekana Mheshimiwa Waziri nafikiri hii itakusaidia katika kuwa-*discipline* hawa watumishi wa ardhi ambao wanakiuka taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine nilichokuwa nataka kuzungumza ni kwamba fidia wanayopewa kwa sababu dhana ya kumfidia kwa Kiingereza ni kwamba mtu anakuwa *compensated* ili asiwe *what's off* lakini pia asiwe *better off,* aendelee katika ile *level* aliyokuwa nayo. Sasa leo unakuta mtu alikuwa na nyumba hata kama nyumba labda ina vyumba viwili lakini pia kiwanja anacho anatakiwa ahame halafu anapewa fidia ya shilingi milioni mbilii. Shilingi milioni mbili labda anaweza akajenga kioski cha chumba kimoja tu ni fedha ndogo kweli. Bei ya mabati yamepanda, bei ya misumari na kila kitu gharama zote za ujenzi zimepanda.

Sasa shilingi milioni mbili ni fedha kidogo kweli, haiwezi ikasaidia kitu chochote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kama inawezekana hebu tufanye *review* upya kwenye *guidelines* zinazofanya mtu awe *compensated* ili *in resents* ya *meaning of compensation* mtu asiwe *worse off* na asiwe *better off,* lakini aendelee katika ile *level* aliyokuwa nayo. Kwa hiyo, fidia zimekuwa ndogo sana naomba mtusaidie kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sehemu kama Jiji la Mwanza yawezekana maeneo yanapimwa leo halafu inachukua miaka hata mitano kuja kumfidia na wakati huo huo kama nilivyotangulia kusema haruhusiwi kuendeleza makazi yake.

Mimi nafikiri yawezekana yana changamoto ya fedha, kwa nini Serikali isione kwamba sasa ni muda muafaka wa maeneo kama Majiji kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha Serikali *inject* fedha kidogo ili iwasaidie kuwalipa wananchi fidia ili baada ya kupima mtu asikae pale ili miaka mitano aendelee kuishi pale, fidia hajapewa na hawezi akaendeleza makazi yake. Naomba Serikali iliangalie pia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji la Mwanza naomba niwe muwazi kwa sababu nikishasema ukweli nitabaki kuwa *free,* kuna mtu mmoja anaitwa Otieno. Huyu Otieno anafanya kazi kwenye Idara ya Ardhi, huyu Otieno ameota mapembe. Katika kila kundi la watu kumi Mwanza ambao wana tatizo la ardhi angalau watu saba watamtaja Otieno kwamba adui wa ardhi ya watu wa Mwanza, ni mtu anaitwa Otieno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemtaja kwa sababu Otieni huyu ni kero kubwa kwa wananchi wa Mwanza naomba achukuliwe hatua na sio hatua ya kuhamishwa tu kwa sababu ninyi Serikali mna tabia kwamba mtu akishavuruga, wananchi wanalalamika, mnamtoa Mwanza mnampeleka Nachingwea, nani kasema hapo Nachingwea ndio wanataka mtu mjanja mjanja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kipindi kilichopita pale Jiji Mwanza Mheshimiwa Kandoro, Mkuu wa Mkoa aliwahi kuvunja kuna majamaa walikuwepo pale walikuwa ni *big brothers* wametengeneza Jiji, walikuwa watemi, ardhi wao ndio wanaamua nani apewe nini, nani asipewe na nani anyang'anywe, waliondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kuondolewa kwao hata hawakuchukuliwa hatua, walihamishwa nasikia wameanza kurudi taratibu. Wengine walipelekwa mbali sasa hivi mmoja

amesharudi yupo Sengerema, amejihifadhi pale anataka kuja tena kwenye Jiji la Mwanza, hatutaki watu wa *style* hii na wakirudi tutawafukuza…

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu Otieno naomba Serikali ichunguze, mimi mpaka nimekuja nikataja jina lake hapa mjue ni jinamizi kubwa kweli kwenye Jiji la Mwanza, anasumbua wananchi wetu. Naomba Serikali ilichunguze hili ili huyu Otieno achukuliwe hatua na sio kuhamishwa. Yupo mwingine anaitwa Frank Joseph Kilawe yeye pia ni Afisa Mipango Miji Mkoa, hao ni adui wa watu wa Mwanza kwenye ardhi yao. Huyu pia…

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje tulia kidogo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Blandes ningekupa nafasi, lakini kwa vile umeongea kwa kuwasha hicho chombo kabla sijakupa nafasi kaa chini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Wenje endelea na natoa ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge tufuate ule utaratibu wetu wa kawaida. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Hawa niliowataja naomba Serikali ijitahidi kuwachunguza na ikiwezekana kwa kweli wachukuliwe hatua sio kuhamishwa tu, kwa sababu hawa watu ndio wanaosaidia wengine kupora ardhi huko Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hali halisi katika Jiji la Mwanza tuna matatizo makubwa ya ardhi. Watu wanyonge wazawa wanaporwa ardhi na wanachofanya wanafika nyumbani kwa mtu wanamuangalia alivyo wanajua huyu mama au huyu mzee hana mtoto mwenye digrii kwa hiyo hana mtu wa kumtetea. Wanakuja pale wanamdanganya unaambiwa imefikia wakati Mwanza unaambiwa wanakuja wanakuletea karatasi unaambiwa wewe saini, unasaini kwa huku hujui hata fidia yako inakwenda kuwa ni shilingi ngapi? *(Makofi)*

Ukisha saini, mwananchi anasainishwa huku hajui fidia anakwenda kulipwa shilingi ngapi. Anasainishwa huku hajui hata taratibu zilizofanyika kutathmini ardhi yake, hajui hata ardhi yake ina thamani kiasi gani. Yeye anasainishwa, akifika kule kuna wengine wamelipwa mpaka shilingi laki nne, kuna wengine wamelipwa fidia mpaka shilingi elfu thelathini, tuna takwimu zote. Barua za malalamiko yao na mtu alilipwa nini mpaka *photocopy* ya *cheque* walizolipwa ninazo kwenye ofisi yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nimwombe Mheshimiwa Waziri, tuna imani kubwa na yeye na leo kwangu mimi kama Wenje siwezi nikasema hawezi, *you have less than a year* kwenye Wizara, kwa hiyo, *we believe you can stand perform, you can stand and change this Ministry.* Mimi naomba nikuhakikishie pamoja na kwamba sitaunga mkono bajeti yako lakini nina imani kubwa sana na wewe na mimi naomba Mheshimiwa Waziri kama inawezekana upange safari uje Mwanza. Uje nikupeleke kwenye maeneo ambapo wananchi wangu wamedhulumiwa ardhi na wewe uende ushuhudie, isije ikabaki tunazungumza hapa halafu hakuna kinachotokea. Mimi nina imani kubwa na wewe Mheshimiwa Waziri, naamini utanisaidia, naomba uje Mwanza, twende nikupeleke hapo Lichelele uone kinachotokea, nikupeleke kwenye haya maeneo niliyotaja na uone wananchi wangu jinsi walivyodhulumiwa ardhi. Mheshimiwa Waziri ukija, nitakushukuru sana hata imani yangu kwangu itaongezeka mara dufu, naomba uje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie. Katika kutafuta takwimu hapa na pale, nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Mjini, ni dhahiri hii *concept* niliyokuwa naisema kwamba nchi hii tunarudisha Wakoloni ni kweli, *Settlers* wanarudi, Mugabe imemshinda sera hii, *Settlers* amewafukuza na sisi ndiyo tunawarudisha. Leo kama Kasulu kuna *square kilometer* 606 kwenye vijiji vya Kagerekanda, Mgombe, *this is too big,* amepewa mwekezaji anaitwa

*Tanzania Game Tracking Safaris Limited*. Sasa huyu mtu amechukua maeneo makubwa na ni maeneo watu walikuwa wanalima, *no wonder* siku hizi hata chakula hakuna, kwa sababu maeneo ambako watu walikuwa wanalima leo yamechukuliwa, wamepewa watu *in the name of* uwekezaji. Hapa tunarudisha Wakoloni, tunarudisha *Settlers* na kitu watakachofanya hawa watu ni kuendelea ku-*create* matabaka kati ya wenye ardhi na wasiokuwa na ardhi. Kwa hiyo, *we are bringing back the old colonial concept,* tunafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, siungi mkono hoja na Mheshimiwa Prof. Tibaijuka nakuomba ukaribie Mwanza. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninazo shukrani mbele ya Mungu na mbele ya Bunge lako Tukufu, kupata nafasi hii hata kuwa mzima na kuwepo kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda niwashukuru wananchi wa Nkenge kwa namna tofauti na ya pekee kwa ushirikiano wanaonipa katika kuliendeleza Jimbo letu la Nkenge, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nitoe pole nyingi kwa Wanakakunyu, kwa matatizo makubwa wanayoyapata kutokana na tatizo la ardhi, wengine wamepoteza mashamba yao, wengine wamechomewa nyumba zao, wengine wamepoteza hata ndugu zao katika kupambana na wawekezaji katika eneo la Nkenge. Hivyo ninataka kuwatia moyo kwamba nitasimama kidete kuwatetea na kuhakikisha kwamba ardhi yao iliyoporwa inarudi katika mikono yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo letu la Nkenge, tunalo tatizo kubwa la ardhi hasa katika Kata ya Kakanyu. Kata ya Kakunyu, ni Kata nzuri iliyo na maeneo ya kufuga, iliyo na maeneo ya kulima lakini kwa namna ya pekee na kwa ukiritimba mkubwa watu wa *NARCO*, waliamua kugawana maeneo hayo kuwapa watu wachache ardhi nyingi na wenye ardhi wakibaki bila matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipotembelea katika Jimbo letu la Nkenge alikuwa na mambo aliyoyaona na akaagiza kwamba migogoro ya ardhi iishe mara moja na tena akatoa usemi ya kwamba msigawe ardhi kana kwamba ninyi ndiyo kizazi cha mwisho. Maana tunagawa vinaishia halafu wanaokuja hawana kitu kingine. Kwa hiyo, mimi nataka niseme hivi na mimi ndiye Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Kagera, tumekubaliana katika mambo mengi hasa yanayohusu ardhi na hatutakubali watu wachache wachukue ardhi watawale walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze tatizo lililopo. Jambo la kwanza, *NARCO* iliamua kugawa lile eneo bila kushirikisha wananchi. Sasa naomba nitaje walivyojigawia maeneo katika sehemu hizo na naomba uniruhusu nisome na nikutajie mmojammoja amechukua sehemu gani na anafanya nini. Kwanza kabisa, ninaanza na *block* ya kwanza, alichukua Gen. Marwa, amefariki na hakuna kinachoendelea katika *block* hilo. Katika *block* namba mbili, ni wananchi wa Kakunyu. *Block* namba tatu, kuna kiini macho eti cha Ng'ombe *Women Group* lakini hati imeandikwa Charles Rwabulongolongo hakuna lolote linaloendelea na hajafanya kitu chochote bado wananchi wanapigana kuingia katika eneo hilo na hawawezi kuchukua. *Block* namba nne, ni wananchi wa kijiji cha Kakunyu. *Block* namba tano, wananchi wa Kakunyu lakini unaweza ukaangalia ni namna gani mbele na nyuma wamezungukwa na hawa matajiri ambao hawaonekani. Ukiangalia *block* namba sita, kuna Rweyemamu, hakuna lolote alilolifanya, ardhi ipo pale na wananchi hawana mahali pa kulishia hata wanyama wao. Katika *block* namba saba, wamekipa kijiji cha Bugango na katika kijiji hicho wamekata kipande wanataka kuipa JKT. Katika *block* namba nane, kuna kijiji Bugango na *block* namba tisa, ni kijiji cha Bugango pia lakini miaka yote hawa watu wa Bugango walikuwepo pale, ghafla mtu anawakatia kipande kama watu wa kuja. Katika *block* namba kumi, kuna Mheshimiwa Katagira, yeye kidogo ng'ombe wapo anaonyesha dalili ya kwamba anatekeleza lakini hebu tuangalie *block* namba kumi na moja kuna kikundi kinaitwa Chomzungu, yaani wafanyakazi wa *Ranch* ya Kakunyu wameamua kujipa nafasi wakajichukulia na wao kipande, tayari wameweka mahali pale kama ardhi yao. Sasa sielewi Chomzungu ni Wazungu au Waafrika?

Mheshimiwa Naibu Spika, *block* namba kumi na mbili, kuna *NARCO* yenyewe nayo ikajikatia kipande, namba kumi na tatu ni Kagera Sugar, namba kumi na nne, ni Mr. Mahava. Huyu Mr. Mahava hayupo amekimbia na yeye alikuwa Meneja wa Ranchi ya Kongwa kwa hiyo ameingilia na kule ana kipande na Kongwa ana kipande ili mradi tu ana uwezo wa kuchukua ardhi kama anavyotaka. Ukiangalia *block* namba 15, kuna Mr. Kanati, katika watu wote *block* zote ishirini na mbili ni Mr. Kanati aliye na ng'ombe 2500 na ameajiri watu lakini hapa ndipo kuna moto na hapa mahali watu wamepigana na mtu mmoja amekufa waking'ang'ania kuingia katika hiyo *block* na kwa sababu huyo Mwenyekiti wa Kata ya Kakunyu ameshachukua *block* namba kumi na nne na sasa anapambana kuchukua namba kumi na tano. *Block* namba kumi na sita, kuna Mr. Kagene yeye hana ng'ombe hata mmoja alikuwa anakodisha ng'ombe kutoka Uganda wanakula na wanaondoka na namba kumi na saba Mr. Lona Charles, huyu yeye anaingiza ng'ombe kutoka Uganda mpaka juzi *DC* wetu alipochachamaa ndiyo ameacha na *block* haina mtu iko pale lakini watu wanapigana waweze kuingia mahali pale. *Block* namba kumi na nane, hii inagombaniwa na Mr. Kazola na Samson na kesi iko Mahakamani na haijulikani mwenye nayo ni nani na nani anatakiwa apewe. *Block* namba kumi na tisa, Mr. Laizer, ana ng'ombe 200 tu lakini ana hekta 1,000 hakuna lolote analolifanya, wananchi wanahangaika hawana mahali pa kulishia wanyama wao. *Block* namba ishirini na ishirini na moja ni *blocks* ambazo zina wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaangalia sehemu kubwa namna hiyo kuchukuliwa na watu watano na wananchi wengine wakazungukwa mbele na nyuma hawana sehemu za kulisha wanyama, hawana sehemu za kunyweshea wanyama wao, hawawezi kupita kwenye *block* hizi na wakipita wanapigwa na kuuawa. Mimi ninaitaka Serikali katika jambo hili ifute kabisa hizi hati sanasana watu wawili wanaoonekana wanaweza kufanya tunaweza kuwafikilia, Mr. Kanati anastahili kupongezwa kwa sababu amefuata masharti yanayotakiwa.

Ngoja niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu kama watatokea watu wakagawana vipangevipande sijui tutafanya nini. Ni kwa nini miaka yote watu walikuwa na ardhi yao, ghafla unazuka mfumo wa kwamba tunaleta maendeleo na maendeleo yenyewe hatujayaona, mtu ana ng'ombe 200 anachukua hekta 1000. Mimi nina ng'ombe 250 lakini hata robo heka sina lakini watu wengine wana uamuzi na hawaambiwi lolote. Mahangaiko haya tuna zaidi ya miaka sita tunaongea habari za *blocks* lakini hakuna uamuzi unaotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zimeletwa Tume na Tume mpaka Makatibu Wakuu wamekuja kwetu lakini hatujui kuna mzimu gani, hakuna majibu. Sasa nina *document* hii hapa nitawakabidhi Mheshimiwa Waziri na Naibu wake waangalie. Tumeeleza kila kitu, tatizo ni nini, kwani hawa watu wakinyang'anywa maeneo watakufa? Wananchi wanakufa wao wanaendelea kuchukua sehemu. Mimi kama Mbunge wa watu wa Kakunyu, sitakubali watu waendelee kufa, hati juu ya hati haijaweza kutokea. Hati ya *NARCO* juu yake kuna hati za watu, watu wenyewe wameingia mitini, kazi hawafanyi, Taifa haliingizi kitu, wananchi hawaingizi kitu. Mimi naomba kusema hivi unapokuwa umechukua ardhi na umesema unakwenda kutuletea mazao ya wanyama, ina maana tunakwenda ku-*export* nyama, kuna wanyama watakuwepo na kuna watu wataajiriwa lakini unachukua ardhi, unakwenda kuleta Waganda kutoka Uganda kulishia wanyama wao pale huku unalipwa na wananchi wenye sehemu zao hawawezi kulisha wanyama pale, mimi naona biashara hii ya kuweka wawekezaji kwenye maeneo ya ardhi imetushinda. Hebu tufikirie kitu kingine cha kufanya katika maeneo hayo na wananchi warudishiwe maeneo yao na waishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya ziara katika Kata ya Kakunyu. Kwanza wameniuliza mara ya kwanza wakati tunanadi sera na Mheshimiwa Rais ananadi sera ya ardhi katika kampeni alieleza kabisa kwamba nina uhakika huyu mama tatizo la Kakunyu la viwanja limekwisha. Juzi nimekwenda wakaniuliza yale maneno tuliyoambiwa pale Bunazi na Rais kuwa tatizo la *Block* halitakuwepo tena sasa yako wapi? Usirudi tena kama huna jibu la kutueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, unanipenda nirudi kule au nibakie hapa Dodoma au niende kule nikiwa na majibu. Naomba nipewe majibu ili niweze kwenda kuwahudumia watu wa Kakunyu. Wilaya ya Misenyi ni Wilaya mpya, nadhani katika hili tumeelewana na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri tumeongea na akasema hawezi kututupa, atakuja aliangalie na sioni kwa nini linachukua muda mrefu. Watu watatu Nkenge wamepoteza maisha na bado mtu ana *block* moja

yeye anaishi vizuri na hayupo ametelekeza eneo hilo, anakaa sehemu nyingine watu wapigana na kuuana. Kwa nini tusichukue hiyo ardhi na tukarudishia wananchi? Makatibu Wakuu zaidi ya watano wamekuja Nkenge kuangalia na hakuna majibu. Mimi nadhani leo majibu nitapewa uzuri ndiyo huo na Wanankenge nawatia moyo jawabu lipo, eneo lenu lazima mrudishiwe au Serikali ikae na wananchi iwaulize mnataka kufikia wapi na wapi mnataka mchukue na wapi tuwaachie Serikali. Kwa hiyo, nadhani wananchi wapewe nafasi ya wao kusema wanatosheka na ardhi kiwango gani na inayobaki Serikali ichukue kama watakavyokuwa wamekubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misenyi ni Wilaya mpya tunashukuru kupata Wilaya mpya lakini kuna tatizo la watu kuchukuliwa ardhi ya sehemu zao kama walivyosema wenzangu. Sisi tunajenga Wilaya mpya lakini si haki kumchukulia mtu sehemu yake labda umepata viwanja vitano ukampatia kiwanja kimoja, ana watoto wake watatu wapo karibu kuoa, ukampatia kiwanja kimoja, ana wajukuu wako pale, ukamkatia kakipande na chenyewe unapomkatia vile vingine unaviuza kwa bei kubwa. Akitaka kununua mwenyewe bado anunue kwa gharama kubwa. Mimi nilikuwa najiuliza hizo pesa zinakwenda wapi? Kama una m-*compensate,* kwa nini humpi hela inayolingana na wewe unavyouza? Wewe unauza milioni tano, yeye unampa fidia ya shilingi milioni moja. Hivi kweli ni haki mtu anatendewa? Mimi naomba Wizara ya Ardhi irudie tena kufikiria kwa nini inafanya mambo hayo. Mimi nilidhani kwetu tu kumbe ni Tanzania nzima. Kwa hiyo, mimi naomba watu wapewe maeneo kama ambavyo wanauza kwenye Serikali au kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee jambo lingine la kesi za ardhi. Kwa kweli kesi za ardhi zinatisha. Siku moja nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri nikimlilia hali ilivyo na yeye mwenyeye pia anasema nashangaa inakuaje kesi ambayo inahusu ardhi apelekewe mtu ambaye hata mambo ya ardhi hayajui. Huyohuyo Hakimu anakuwa Tabora, anakuwa Mwanza, anakuwa Kagera, Kagera kesi ikaisha anahairisha, Tabora anaacha ameahirisha, Dar es Salaam anaacha ameahirisha kesi zote zimeahirishwa. Mtu mmoja huyo na akirudi mara ya pili anakwambia nilikuwa Kigoma na ukiuliza Kigoma kesi haijahukumiwa. Hivi ni namna gani tunaweza kuendesha nchi kwa namna hiyo? Mimi naomba sana kama Hakimu umetaja tarehe hebu maliza kesi hiyo. Miaka sita, miaka saba kesi haijaisha. Mimi niseme kama una *project* yako miaka sita ni kesi mtaji bado upo? Si mtaji utakuwa umeenda na ardhi ile hata huihitaji tena maana uwezo utakuwa huna? Kwa hiyo, mimi naomba kesi zitafutiwe nafasi na ziishe kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kuongelea upangaji wa nyumba. Upangaji wa nyumba nchi nyingine kama Kenya wameweka muda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa kuwa umesema una *document,* nakupa nafasi uilete Meza Kuu na kuikabidhi hapa kwa Makatibu wangu na sisi tutahakikisha Mheshimiwa Waziri anaipata kwa utaratibu wetu wa kawaida kuhusiana na matatizo ya wananchi wako wa Kakunyu, kule Nkenge katika Wilaya ya Misenyi. Makatibu naomba muipokee *document* hiyo.

*(Hapa nyaraka husika iliwasilishwa Mezani)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana na Waheshimiwa Wabunge wengine kama mmejiandaa na umeandika kitu chako kwa uhakika, utaratibu wa namna ya kukabidhi ni huu.

Namwita Mheshimiwa Mchungaji Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili name niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa niaba ya wananchi wa Karatu, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza najiuliza kwa nchi yetu nzima kila mahali kilio cha ardhi kimekuwa kikubwa na migogoro ya ardhi kwa nchi nzima. Swali ambalo tunapaswa kujiuliza Watanzania ni kwa nini ardhi yetu ya Tanzania na Watanzania wana migogoro nayo, tatizo liko wapi? Ukiangalia tatizo lipo katika mfumo au mamlaka inayohusika na ardhi hii. Kumekuwa na

tabia ya ardhi kunyakuliwa bila wananchi wa Tanzania kushirikishwa na hili ni tatizo kubwa kwa nchi yetu. Mamlaka ambayo imepewa dhamana ya kutunza ardhi haitendi inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani nilisema juu ya mamlaka yote yatiiwe, yaheshimiwe, Ustaadh Mheshimiwa Nkamia akatoa tafakuri nyingine ni sawa lakini alisahau kusema mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Mamlaka adilifu iliyowekwa. Naomba hili neno adilifu pigia mstari na kama Mamlaka si adilifu ni vigumu sana kutiiwa na ndiyo maana kuna migogoro, kuna migongano na matatizo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema machache kwa ujumla na baadaye nihamie katika Jimbo langu la Karatu. Ardhi ni mali na ardhi ni mtaji wa Mtanzania. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe kila kipande cha ardhi kinapimwa, kinamilikishwa na kinapangiwa matumizi yake ili huyu Mtanzania aweze kutumia ardhi yake kwenda katika vyombo vya fedha na kutumia kama mtaji wake kupata mikopo na kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la ardhi yetu, ninawaza na kufikiri kwamba katika mchakato wa Katiba Mpya ambayo Watanzania tunataka, basi suala la ardhi liwekwe Kikatiba, lielezwe moja kwa moja ndani ya Katiba na Watanzania wajue kwamba wanamiliki ardhi Kikatiba. Ardhi ile ambayo udhamini wake uko chini ya Rais, basi ardhi ile pia iridhiwe na Wabunge kabla ya maamuzi yoyote kutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linaloleta migogoro ya ardhi kwetu Tanzania, ni mikataba mibovu inayowekwa pasipo wananchi kushirikishwa. Katika Sheria ya Ardhi, wananchi ndiyo wenye dhamana ya ardhi lakini, imetokea katika maeneo mengi, mikataba inafanywa na viongozi wa maeneo husika bila wananchi wenye dhamana ya ardhi kushirikishwa. Baada ya mikataba hiyo kusainiwa, wananchi wanashangaa tu maeneo yao yanachukuliwa. Wakihoji, wanaambiwa tayari tuna mikataba. Hii ni kwa sababu ya kuwa na viongozi wasio waadilifu labda pengine niseme wasio wazalendo ndani ya nchi yao wenyewe. Wametanguliza maslahi yao binafsi na kuuza ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ukanda wa Kaskazini ambako kweli ardhi haitoshi, haipo, ukiongeza kieneo kidogo tu katika kihamba chako, hatua moja, mbili, ni mgogoro wa ajabu! Sembuse watu wanamilikisha maelfu ya eka kwa wageni. Hawa Watanzania wataenda wapi? Hili Serikali iliangalie sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya tatizo kubwa la mikataba mibovu, nataka kusema *a case study* ya Kijiji cha Chemchem kule Karatu. Mwaka wa 1988 – 1989, mwekezaji mmoja aliingia mkataba na uongozi wa kijiji, mwekezaji anayejiita *Leisure Holdings Tanzania Limited* na mkataba wenyewe ulikuwa wa ekari 80. Kwa sababu mkataba umefanywa baina ya mwekezaji na viongozi, baadaye mkataba huo umebadilishwa na ukasomeka hekta 80.9 na wananchi walichoona ni kwamba maeneo mengine mapya yamechukuliwa, wakaanza kuhoji imekuwaje sasa maeneo haya yanachukuliwa na mkataba ulikuwa ekari 80 na sasa unasomeka hekta 80.9? *It is more than two times* ya eneo hilo. Wananchi wamekuja kushtuka kwa sababu maeneo yao ya maji, matenki ya maji, wanakopeleka mifugo yao, sasa mwekezaji anaweka uzio na hii imeleta mgogoro. Jambo hili wakati Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri, lilitunzwa na likaachwa hivyohivyo linaendelea mpaka leo, ni mgogoro mkubwa. Namwomba Waziri afike Karatu ajionee mwenyewe, atakuta mikataba inayohusika katika ofisi za Vijiji hivyo, angalie ukweli na mwekezaji huyo ili kutatua migogoro hiyo maana wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kusema ili nikubaliane na hoja ya Wizara hii, ni mahusiano kati ya Hifadhi za Taifa na Vijiji vinavyopakana na Hifadhi hizo. Hapa pengine ningeshauri Wizara tatu zinazohusika, zinazofanana, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii, Kilimo, Chakula na Ushirika, wakae kwa pamoja, waone jinsi gani matatizo haya ya kudumu ya ardhi kati ya Hifadhi, Vijiji, wakulima, wafugaji yatatuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye ukanda wa Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, Vijiji vya Lositete, Mbulumbulu, Tloma, Makhoromba, Endamaghang, kuna matatizo makubwa

sana ya mipaka ya ardhi. Naomba Waziri au Mawaziri wanaohusika, kwa pamoja waweze kufika na kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TANAPA*, Manyara, Vijiji vya Chemchem**,** Endallah, Kansay, Buger, Marang**,** matatizo ya mipaka ya Vijiji ni makubwa sana. Naomba Waziri afike aone hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi, naomba Waziri, Serikali, kwanza Mabaraza haya ya Ardhi yaimarishwe. Hayapo kwenye bajeti, hayawezi kutenda kazi yake sawasawa na zaidi sana tunao wahitimu wa Chuo Ardhi, hao waajiriwe, wawe Makatibu wa Mabaraza hayo maana wana ufahamu wa Sheria ya Ardhi. Tunapata matatizo ya kesi nyingi za ardhi zinaahirishwa, hazishughulikiwi, wale Wazee wa Baraza kwa kweli ufahamu wao ni mdogo na tunao vijana wale wahitimu, hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye makazi, moja ya shida kubwa ya miji yetu, kwanza miji mingi haina *master plan* na ndiyo maana unakuta kuna majengo ya ajabuajabu katika miji yetu. Kwa hiyo, Serikali iwe na mpango mkakati wa kuwa na *master plan* kwa miji yetu. Moja ya shida kubwa ni uadilifu kwa Watedaji wa Idara ya Ardhi Mheshimiwa Waziri. Uaminifu hakuna, utakuta kiwanja kinauzwa mara mbili, tatu, wananchi wanagombana, wahusika wamekaa pembeni, wameshapata chao. Hili linawezekana kwa ajili ya maendeleo ya sasa ya sayansi na teknolojia kujua nchi nzima viwanja viko vingapi, katika miji ipi na ikoje, inawezekana. Kwa hiyo, wahusika ni rahisi sana kuwajibishwa na kuchukuliwa hatua inavyopasa. Katika miji yetu kama utaratibu wa *master plan* utafuatwa na watumishi wakawa waadilifu kusimamia, ni imani yangu kwamba migogoro ya viwanja katika miji yetu itaisha na ni hakika kwamba watu watafanya kazi inayopasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize na kuzungumzia migogoro ya wafugaji na maeneo ya wafugaji. Naomba Wizara hizi zikae haraka. Eneo moja la Olieren kule Lositeti la wafugaji, wanapata mahangaiko makubwa sana, hawana eneo la kulishia mifugo yao maana limechukuliwa. Kwa hiyo, naomba maeneo yote ambayo yana matatizo, Waziri na uongozi wanayashughulikia. Kuahirisha kutatua tatizo si kupata *solution* ya tatizo. Nafikiri hata kama ni mambo magumu, naomba Wizara, Serikali mtoe maamuzi. Mtoe maamuzi hata kama ni magumu ili kuleta amani katika nchi hii. Inasikitisha kuona kama Watanzania ndani ya nchi yao wawe watumwa, wawe walinzi katika nchi yao kwa sababu ya watu wachache wasio wazalendo kwa kupenda nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine Serikali itoe tamko, tangazo rasmi kwa nchi nzima, suala la kuuza ardhi, mwisho. Hapana! Watanzania wasiuze ardhi, hata wageni wasimilikishwe ardhi, badala yake wageni wapewe *lease* ya ardhi. Ardhi ni yetu, atakapoondoka, atuachie ardhi yetu. Tena nafikiri katika Katiba Mpya, *lease* ya miaka 33, 66, 99, ifikiriwe kwa upya. Mimi sidhani kama tunahitaji kumpa mwekezaji *lease* ya miaka 99, halafu haiendelezi, badala yake anawakodishia Watanzania, ni aibu! Ni aibu mgeni kuja kuchukua ardhi yetu, halafu Watanzania tuanze kukodisha ardhi yetu. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali ifikiri kwa upya juu ya *lease* na umilikishaji wa ardhi yetu. Watanzania wamilikishwe ardhi, wageni wapewe *lease* na *lease* ningependekeza baadaye kwenye Katiba huko isizidi miaka 50 na iwe *renewable* kama anaendeleza kwa faida ya Taifa na kama haendelezi, *lease* hiyo ifutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kupigiwa kengele. Siungi mkono hoja hii mpaka ufumbuzi wa matatizo ya ardhi Waziri alete majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima hapa katika ardhi nchini Tanzania ni migogoro ya ardhi. Wachangiaji wengi wanachangia kuhusu migogoro ya ardhi na nisingependa kurudia lakini ninapenda tu kutoa jinsi nilivyoona na nilivyopitia na kuishuhudia hiyo migogoro. Nimeona kabisa migogoro mingi ya ardhi inatokana na kukosekana kwa upimaji wa ardhi katika Vijiji nchini Tanzania na rushwa kwa Watendaji katika ngazi za Vijiji, Kata, huko ndiko kwenyewe. Kwa hiyo, ndiyo maana migogoro mingi inazuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina ardhi kubwa sana, lakini najiuliza, yaani tangu uhuru mpaka leo, eti asilimia moja ya ardhi nchini Tanzania ndiyo iliyopimwa! Hivi tunaenda wapi? Miaka 50, asilimia moja! Wizara inasema kabisa kazi yetu ni hii, wameorodhesha pale kwenye kile kitabu, sitaki kusema kwa sababu kila mmoja anacho na anajua kazi ya Wizara, kwa nini hawawajibiki? Kwa nini hawafanyi kazi zao? Kwa nini miaka 50 ya uhuru wamepima ardhi asilimia moja ya nchi yetu? Tunakwenda wapi? Kupima asilimia 100 ya ardhi yetu inatakiwa miaka mingapi? Hebu tufanye mahesabu! Miaka 100,000, haiwezekani! Haiwezekani! Siungi mkono hoja! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kwa nchi yetu, aibu kwa Taifa na ndio maana wawekezaji wanapokuja wanaona kabisa hawa wamepima asilimia moja, kwa hiyo mimi nikija nikibeba hii ardhi, haijapimwa, ni mali yangu, wenyewe hawana habari nayo. Tunapangaje mipango yetu na ongezeko la watu kwa kigezo kwamba tumepima asilimia moja? Haiwezekani! Haiwezekani! Mmeshindwa, kaeni pembeni, wapishe wenzenu wanaoweza kupima ardhi, kuwakabidhi Watanzania ardhi yao kila mmoja ajue anamiliki wapi, Serikali ya kwake ipi, mwekezaji akija apelekwe wapi, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matatizo haya ya ardhi, katika Halmashauri zetu, kuna Maafisa Ardhi, cha kushangaza, mimi nilienda pale Kilombero kwa Afisa Ardhi kwenda kulipia kijumba changu (*plot* yangu) ambapo jengo langu mpaka leo halijamalizika. Nimeenda, nimekuta ile ofisi iko shaghala baghala. Nikamuuliza wewe vipi, hii ndiyo Ofisi ya Ardhi? Akasema eeh! Nikalipia pale, nikamwambia hizo hela kwa nini sasa hamwendi kupima ardhi za watu? Akasema hizi hela zote zinaenda Makao Makuu. Inakuwaje? Kwa nini Maafisa Ardhi wako pale, wamekaa ofisini, ardhi hazipimwi, miji mipya inazaliwa, wananchi wanaongezeka, miji haipangwi, halafu baadaye mnasema hapa inapita barabara mnabomolea watu! Serikali ipo kama haipo! Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, ni vyema hizo hela wanazolipia watu majengo huko chini kabla hamjawapelekea bajeti nyingine, muwaelekeze watumie hizo hela kwa kwenda kupima ardhi za wanavijiji. Lazima muwe na takwimu. Kila Wilaya lazima ipime, hawa Maafisa Ardhi wamefanya kazi gani kwa mwaka mzima, wamepima ardhi kiasi gani. Leo Wilaya ya Kilombero, eti wanasema mwaka 2009/2010 walipima tu Vijiji viwili. Tunaenda wapi? Kwa nini tuna Maafisa wa Ardhi? Wanafanya kazi gani? Kwa hiyo, lazima tubadilike! Kwa hiyo, migogoro ya ardhi inatokana na rushwa na kutopima hiyo ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi, kipi kianze, kuwapeleka wawekezaji ama wafugaji? Kwa mfano, Wilaya ya Kilombero kabla hamjaandaa maeneo na kupima kwamba hawa wafugaji tunawahamishia huku, tutawapeleka sehemu fulani au mnawapeleka kwanza ili wagombane na wakulima, wapigane, wauane, halafu ndipo sasa Wizara inaenda kutatua mgogoro. Nyie vipi? Kwa nini hamuendi kwanza kufanya ile kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mnavyowahamisha watu, mnavyowapeleka katika haya maeneo, ile ardhi imeshapimwa kwa hiyo unajua kabisa ninampeleka hapa, mwisho wako hapa, unamwonyesha kabisa na mipaka yake. Kwa hiyo, lazima mjirekebishe, muone kwamba migogoro, mauaji na misongamano inasababishwa na Serikali yenyewe iliyoko madarakani, inashindwa kujipanga, kufanya kazi zake kiufasaha. Mnakuja hapa, maneno mengi, vitendo hamna. Sasa tufanye kwa vitendo, maneno tuache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukulia mfano Kilombero ambako nakujua sana na Mkoa mzima wa Morogoro. Leo, Mkoa wa Morogoro kuna migogoro mingi katika kila Wilaya. Watu wamejitwalia maeneo. Kwingine wametwaa maeneo, wamemiliki, halafu wanawakodisha tena wakulima, hekari shilingi 40,000/=, inakuwaje? Kwa nini hamuwamilikishi watu hizo ardhi? Mnammilikisha mtu mmoja, halimi, yeye kazi yake kukodisha watu, anachukua hela, amekaa mguu juu anakula bia yake tu! Haiwezekani! Lazima tujirekebishe, tujisahihishe, tuone tumekosea wapi, tujisahihishe, tuanze upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero, nimeona hapa mmeweka katika kitabu hiki, ukurasa wa 56 kuhusu orodha ya Vijiji vilivyokaguliwa kubaini maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Sasa, katika Wilaya hii ya Kilombero, unakuta kuna Vijiji vingapi hapa mmeorozesha, Idete, Miwangani, Kisegese, Igima, Ikwambi, Njagi, Lungongole (kwa mama yangu huko), Lukolongo, Udagaji, Chisano, Chiwachiwa hamkuiweka lakini maeneo haya yote kama Chisano, juzi tu wiki iliyopita, ameuwawa Mtendaji wa Kijiji na Wafugaji. Kwanza, kachomwa sindano ya sumu, anapelekwa hospitalini, amekufa kwa sababu ya mgogoro wa ardhi lakini, mnasema mmeweka maeneo hayo kwa ajili ya uwekezaji, wawekezaji gani! Nasikia wawekezaji hao ni *SUDECO*. Sasa kwa taarifa yenu, jana watu wametoka na mapanga, *K-1* na *K-2* wanaandama, wanahangaika kwa wawekezaji hawa wa Kiwanda cha Sukari, hawaangalii maslahi ya wafanyakazi, wanawapunja. Huyu Kaburu aliyewekeza Wilaya ya Kilombero, amempiga mfanyakazi mpaka amelazwa hospitali, juzi tu! Taarifa hizi zipo na leo Mkuu wa Wilaya ya Kilombero na Kilosa wanasema wanaenda kufanya mazungumzo na hawa wafanyakazi kwa sababu waliwaahidi terehe 15 wangeenda kutatua mgogoro, hawakwenda, matokeo yake wale wameandamana kwa mapanga jana usiku wameamua kwamba hawawataki hawa wawekezaji, wanawanyanyasa. Nani asiyejua wawekezaji wa Viwanda vya Sukari Mkoani Morogoro, iwe Mvomero, iwe Kilombero, wanavyowanyanyasa wafanyakaz? Leo wawekezaji wanawanyanyasa wafanyakazi na wananchi kwa ujumla, lakini leo mmefanya tathmini hivyo Vijiji mlivyotaja ndiyo kuna mgogoro mkubwa Wilaya ya Kilombero, naomba mliangalie na wananchi hivi wako njiani wanakuja, wawakilishi wao wawili wanakuja leo kuja kuonana na Waziri mwenye dhamana kujua hatma ya mgogoro wa Wilaya ya Kilombero kuhusu ardhi. Ni vema mkashirikisha wananchi katika ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, hao wanaokuja hawana mapanga kwa Waziri?

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hawana mapanga hao, ila wana visu tu. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Endelea!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema mnapoangalia suala zima la mgogoro wa ardhi na matatizo ya wananchi, hata Mwalimu Nyerere alisema kwamba, ardhi itakuwa mikononi mwa wananchi na wananchi ndiyo wenye haki ya mwisho katika kutoa ardhi yao washirikishwe lakini leo hawashirikishwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana usiku nilipigiwa simu Morogoro Vijijini, Kata ya Mvua, kuna Mbunge mmoja wa Kisesa ameenda hapo juzi Morogoro Vijijini, Kata ya Mvua, Kijiji cha Dala eti ametwaa hekari mia tatu. Kijiji chenyewe kidogo, anabeba heka mia tatu eti anawadanganya wale kwamba ameshaongea na viongozi wa Kijiji na Diwani eti yeye ndiye atakuwa Mbunge tena pale, kwa hiyo lile Jimbo litakuwa na Wabunge wawili, ina maana Jimbo la Kisesa ameliacha? Kwani yeye ni Viti Maalum? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Morogoro mnatuonea? Eti ameongozana na wenzake anasema tupate heka hamsini hamsini, wapo sita jumla hekari 300. Wananchi wamelalamika, wamenipigia simu usiku wa manane, wanasema amewadanganya wale wajingawajinga pale, anasema anaahidi atatoa laki tano, amegawa na mpira na jezi na kuwapa na shilingi elfu mojamoja waliohudhuria katika kile kikao, aibu! Leo tupo Bungeni tunawatetea watu, sisi bado tupo humu badala ya kutetea migogoro mtu anapiga chenga anaenda huko anaenda kubeba ardhi, haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaenda kupeleka malalamiko yao kwa Mkurugenzi, Mbunge wa Kisesa namuambia aache hiyo habari, aende akamiliki ardhi huko huko Shinyanga-Kisesa, Wasukuma tulionao Mkoa wa Morogoro wanatutosha na kama mtu anakuja kumiliki ardhi afuate taratibu, aache kurubuni wananchi, haiwezekani Mbunge anaenda unatoa shilingi elfu mojamoja ili watu wakupitishie hoja yako, haiwezekani hiyo ni rushwa, habari ndiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la makazi, nawapongeza sana *National Housing*, lakini utakuta makazi yenyewe wanayoyasema, mimi niliendа kuangalia vipeperushi ni milioni mia moja, eeh! Hata mimi Mbunge siwezi, nikasema hii balaa! Wananchi wa kawaida wataweza milioni mia moja, kuchukua *compound* ya ghorofa kule juu, haiwezekani. Ni lazima tujiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najiuliza wananchi wa Kilombero watafaidika nini na huu mpango, hamna kitu! Kwa nini *National Housing* sasa? Pamoja na mipango ya watu wakubwa hebu wekeni na mipango ya watu wadogo, nendeni vijijini. Muwashirikishe vijana kwa akina mama, wanaweza kufyatua matofali muwape mikopo ya bei nafuu, piteni katika kila kijiji sema kila kijiji labda utajenga nyumba mia moja, watu watafyatua matofali, mtatoa gharama zenu na watu watalipa kidogokidogo kama enzi ya Mwalimu jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani zile nyumba za Magomeni Mwalimu mwenye si alikuwa anashika tofali anajenga na wananchi wakamilikishwa nyumba, uwongo au kweli? Nyumba za Magomeni, hebu igeni enzi ya Mwalimu ilikuwaje, nendeni vijijini mkawafaidishe na watu Vijijini, lakini kubwa zaidi ombeni vifaa vya ujenzi vipunguzwe gharama. Serikali itoe kodi katika vifaa vya ujenzi kama kweli inataka kumsaidia Mtanzania na mtu anapolala kwenye nyumba nzuri ya bati, ya simenti, yenye madirisha makubwa, afya itaongezeka, itaimarika, Watanzania watapata nguvu watafanya kazi, Taifa litaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kuongelea mambo mengi kwa sababu nilitaka nijue zaidi kwamba Wilaya ya Kilombero na mgogoro wa ardhi katika zile Kata na vijiji, wawakilishi wanakuja, wataongea na Naibu Waziri ili wapate jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu Manispaa ya Bukoba, jamani wananchi wana ekari zao labda nane wanakuja wanapimiwa, anapewa kiwanja kimoja anauziwa, halafu vile vinane hata watoto wake hawapewi, akitaka kupewa anaambiwa anunue kwa shilingi milioni nane, hivi vipi nyie! Ni kwa nini? Serikali ijirekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wapimiwe ardhi yao, wapewe hela ambayo wanaweza wakailipa kidogokidogo na ikiwezekana basi kuwepo na mpango maalum wa waliomilikishwa wajengewe nyumba alipe kidogokidogo hawezi kuondoka. Acheni kuwaona watu kama wakimbizi ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, simalizi dakika, naomba nitulie, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia katika suala la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kuwapa pole wananchi wa familia tatu Mpanda, Kata ya Nsemulwa, ambao nyumba zao usiku wa kuamkia jana zilichomwa moto. Naliomba Jeshi la Polisi Wilayani Mpanda wajitahidi kwa kadri wanavyoweza kuwapata watuhumiwa na kuwachukulia hatua kali ili liwe fundisho kwa watu ambao wanakuwa na tabia kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi limekuwa ni suala zito sana kwa nchi yetu. Pamoja na kwamba ni suala zito, ardhi ni suala mtambuka. Ina maana kwamba karibu sekta zote ni lazima zinaguswa na ardhi. Kutokana na bajeti finyu mliyoipatia Wizara mwaka huu, naiomba Serikali iweze kuiongezea Wizara hii bajeti ya kutosha ili iweze kufanya kazi zake sawasawa. Kwa maana ya upimaji na kuweza kupanga matumizi ya ardhi ili kuweza kuepukana na migogoro inayotokea mara kwa mara katika masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameongelewa na nisingependa kuyarudia lakini jambo la msingi napenda kuwapongeza pia *National Housing* kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya kuhakikisha wananchi wanakuwa na makazi bora lakini nawaomba gharama kama wachangiaji wengine waliotangulia kusema, wananchi tupo wa aina mbalimbali, wenye vipato mbalimbali na mahitaji tofauti. Kwa maana hiyo basi, *National Housing* iweze kujenga

nyumba kuanzia zile za kima cha chini mpaka kima cha juu. Unaweza kujenga nyumba za vyumba viwili, nyumba za mabachela na vyumba vitatu na kuendelea kwa kadri ya vipato vya wananchi wa Tanzania vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala la uwekezaji, naliongelea suala hili kwa sababu limeongelewa na linanigusa, mimi ni Mwanampanda, sasa tumepata fursa ya uwekezaji katika maeneo ya Katumba na Mishamo na watu wamekuwa wakihoji bila kutafuta kwa nini Wanampanda wameamua kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, naongea suala hili kwa uchungu sana, wakati bajeti ya Wizara ya Ujenzi inapitishwa tulitengewa kiasi cha fedha kwa ajili ya barabara zetu, siyo kwamba barabara hizo hazipitiki, hizi barabara zinapitika na wenzangu wa CHADEMA wamekuwa wakipita na kuzitumia na kuja kututukana matusi Wanampanda. Wanampanda tumechoka kutukanwa, tunahitaji maendeleo, tumechoka kudharauliwa, tunachotaka ni maendeleo. Tumepata fursa ya uwekezaji na taratibu zinaendelea na zimefuatwa kiutaratibu na kisheria. Nashangaa limetamkwa kusema Madiwani wamepelekwa Marekani kuzibwa midomo. Naomba Mheshimiwa aliyetamka hivyo awataje hao Madiwani waliopelekwa Marekani kuzibwa midomo. Ninachofahamu Halmashauri kwa kushirikiana na Madiwani ambao ni wawakilishi wa wananchi kwa maana kwamba wananchi wamewakilishwa, wakaingia mazungumzo, na kwanza hata mkataba wenyewe bado, ndiyo kwanza tupo kwenye utafiti kwa kushirikiana na Chuo cha Kilimo *SUA*, huyo mtu bado hajapewa. Labda jambo la msingi hapa liongelewe, kama ni wawekezaji waliomo wa ndani ambao ni wazawa kama kuna walakini labda waangaliwe upya, je, wana maslahi na wananchi au wana maslahi yao binafsi? Lakini siyo suala la kusema kwamba tusiwekeze, hii ni fursa tumeipata Wanampanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa yetu ipo nyuma siyo sawa na Mikoa ya Kaskazini, leo wanakuja kuanza kutuingilia kwenye maendeleo yetu ambayo sisi Wanampanda tumeamua, uwekezaji huu siyo wa Wanampanda tu, ni kwa ajili ya kilimo. Tunaelewa kabisa dunia sasa hivi ina tatizo la njaa, hata kama tunataka tuwape wawekezaji, Mpanda ni kubwa na kuna maeneo makubwa sana ya mapori, bado wafugaji kule tunao hata sisi wanatutosha kama Mheshimiwa Kiwanga alivyosema kwamba Morogoro wafugaji wanawatosha na sisi kwetu wanatutosha, tuacheni tulime. Sisi tumekuwa ni wakulima toka zamani na tunataka tulime na tuwekeze tuweze kuzalisha chakula ili tupate fursa za ajira, tupate fursa za ku-*interact* na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Ujenzi wamepigia kelele, hatuna barabara za lami ni ukweli, mmekuja kwetu ninyi, mkaingia mpaka vijijini hamkuona lami, leo tumepewa fedha za barabara imekuwa nongwa, leo ni nongwa kwa wawekezaji kuja Mpanda, haiwezekani na sisi tunataka maendeleo. Wananchi wa Mpanda wanataka maendeleo hawataki maneno, hawataki blabla! Kwanza ni wachapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa Mbunge mmoja alitamka watu wa Mpanda kazi yao ni kulewa, ni matusi ya aina gani hayo? Hapa Dodoma hamna vilabu vya pombe, Dar es Salaam hamna baa, Mbeya hakuna baa, Kilimanjaro hakuna pombe? Kwa nini Mpanda? Tumechoka kutukanwa, tunataka maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea jambo hili kwa uchungu sana, nimezaliwa Mpanda, nimekulia pale, ninajua matatizo ya Wanampanda na nikifa nitazikwa pale na siyo wao, ninyi Kaskazini ni kwenu tuacheni na sisi tupate maendeleo ninyi mmeshapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya kazi Nronga, kuna lami mpaka kule juu mbona sijasema? Kwa nini kila kitu nongwa Mpanda, Mikoa ya Kusini imekuwa nyuma kwa maendeleo toka zamani, sasa tunapata hizo fursa mnatuzuia, kwa nini mzuie fursa zetu? Madiwani ni wawakilishi halali wa wananchi, labda hapa kitu cha kusema labda Serikali iweke sheria sasa kwamba zile hisa asilimia 25 apewe mzawa na kwa sababu Madiwani na Halmashauri zilishirikiana kufanya hivyo, kwa maana kwamba labda hiyo hisa iende Halmashauri asilimia 25 na hilo gawio basi Madiwani na kupitia Halamashauri zao waamue labda mwaka huu wataweka madawati, mwaka kesho watafanya hiki, lakini siyo kusema kwamba tusifanye hilo tunalotaka kulifanya. Hilo ni

jambo jema kabisa na lina manufaa kwa Taifa na ni jambo la maendeleo kwa wananchi wa Mpanda na siyo tu wananchi wa Mpanda ni Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa wakulima muda mrefu mpaka Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi ameamua kupeleka na mabehewa kwa ajili ya kubeba mahindi, mimi leo nashangaa mnasema wananchi wa Mpanda wanalewa, jamani naomba niwatoe hiyo *concept* kichwani, wananchi wa Mpanda ni wachapakazi, ni wazuri wanapendeza, ni wakarimu wala hawana matatizo, ni wachapakazi kweli. Sasa tunaomba tuachiwe hiyo fursa kwa niaba ya Wanampanda tuweze nasi kuona tunasonga mbele kwa namna ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala lingine, katika Halmashauri ya Mpanda Mjini katika suala la kuanza kufanya makazi, kuna eneo la Kasimba, hili eneo lilitengewa makazi kwa ajili ya wananchi lakini kwa bahati nzuri au mbaya, inaweza ikawa nzuri kwa upande wa Serikali na inaweza ikawa mbaya kwa upande wa mlalamikaji, hilo eneo lilichukuliwa likajengwa Ofisi za Serikali ambazo ni Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi zingine, wananchi wa lile eneo ni zaidi ya mwaka sasa wamekuwa wakidai fidia zao, lakini mpaka sasa hawajapata fidia zao, wakienda Halmashauri wanasumbuliwa, Wizarani nafikiri wameshapeleka barua na bado hawajapata majibu yao. Naomba leo Waziri nipate majibu nini hatma ya wananchi wa Mpanda waliokuwa wamepewa maeneo kwa ajili ya makazi eneo la Kasimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kengele ya pili ipigwe kwa sababu nimeongea kwa uchungu sana, naomba niishie hapa ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pudenciana, ni imani yangu kwamba wamesikia. Mheshimiwa Jitu Soni atafuatiwa Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wote wa Jimbo la Babati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ardhi. Mimi naomba kwanza kabisa Wizara hii ingeongezewa bajeti hata ikibidi mara mbili au mara tatu. Bajeti ni ndogo kutokana na matatizo ya ardhi ndani ya nchi yetu ambayo tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa niaba ya wananchi wa Babati Vijijini, naomba Wizara na Serikali leo hii itupe tamko kuhusiana na matatizo ambayo tunayo ndani ya Jimbo la Babati Vijijini. Ni matatizo ambayo yamedumu sasa kwa takribani miaka 25 katika Bonde la Kiru, viongozi wa Kitaifa kuanzia Waziri Mkuu, Jaji Mkuu, Tume mbalimbali zimeundwa ndani ya miaka 25 kipindi hicho mimi nilikuwa bado niko shuleni, lakini hadi leo hii hayo matatizo hayajatatuliwa, imefika mahali sasa kila mmoja anajiamulia kuchukua sheria mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanafanya hivyo kutokana na wao kukosa imani, wamekaa pale kwa muda mrefu, wanahitaji kutatuliwa matatizo yao. Kila Tume ikiundwa majibu hayapatikani. Mbali na hilo huko nyuma inapofikia muda wa muafaka, muafaka haufuatwi, kuna mashamba ambayo yalikuwa ya Serikali na Serikali ilitoa kwamba wananchi wa Babati wenye mgogoro wapewe, baadhi ya maeneo yale walipewa watu kutoka nje, yaani wawekezaji kutoka nje, mtu ametoka Arusha ametoka wapi wakati sisi tuna shida ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Serikali iangalie kwamba katika Bonde lile watu wapatiwe muafaka, watu wapatiwe maeneo ili kila mmoja aweze kuishi vizuri na aweze kujijenga, kila mmoja ana haki ya kuwa na eneo lake, kila mmoja ana haki ya kujijenga ili aweze kuishi. Kijana aliyezaliwa kabla ya miaka ishirini na tano leo yeye anafamilia na hiyo familia pia inahitaji kuwa na usalama. Usalama ambao Mtanzania anaweza kupata ni ardhi pekee, hana kitu kingine. Watanzania wengi ni maskini hasa huko vijijini. Mimi naomba Serikali iangalie namna ya kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maeneo ambayo bado Serikali ina mashamba kule, mashamba ambayo Serikali inamiliki kwa hisa fulani, yangeangaliwa yale mashamba ya Rivacu, wananchi wangepewa yale maeneo ili migogoro hii iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningeomba suala la Sheria, wananchi wengi sasa hivi kwa sababu ardhi imekuwa na thamani wanauza maeneo yao, ingeangaliwa Sheria mtu asiweze kuuza ardhi yake kwa urahisi. Leo hii akishauza ile ardhi baada ya muda kidogo hana pa kwenda, familia inateseka akina mama wanateseka, watoto wanateseka na baadaye tutakuwa na tabaka la watu ambao hawana ardhi na wachache wenye uwezo watakuwa na hiyo ardhi. Nchi nyingi hicho kitu hakiruhusiwi, ukitaka kuuza ardhi itakuwa na mlolongo mzuri, haki ya kila mtu ipatikane na tulinde maslahi ya hivi vizazi vinavyofuata ili kila Mtanzania apate haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi ni suala la ardhi ya kilimo, maeneo mengi ya kilimo sasa hivi ndiyo yanajengewa makazi. Serikali ingeangalia namna maeneo ambayo hayafai kwa kilimo ndiyo yangejengwe makazi. Serikali ipeleke huduma kwa mfano barabara, ipeleke maji, ipeleke umeme ili watu wakajenge katika maeneo hayo na maeneo ya ardhi ya kilimo yabaki, tuendelee kuzalisha chakula. Itafika mahali milima na maeneo ambayo hayafai kulima yatakuwa yamebaki wazi na maeneo ya kulima yatakuwa hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba wananchi wa Babati tujulishwe kuna maeneo mengi Tanzania ambapo tunasema hakuna watu na wanahitaji watu kuwekeza. Tuna vijana wengi, wananchi wanendelea kuongezeka siku hadi siku, wale ambao hawana migogoro, wale ambao wenye migogoro Serikali ije itusaidie kutatua lakini wale ambao wanataka maeneo basi mtuoneshe ni wapi ili sisi pia tuwahamasishe watu wetu wahamie katika hayo maeneo na huduma muhimu zipelekwe ili migongano isiendelee kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Wilaya ya Babati Vijijini, kuna suala la Hifadhi ya Tarangire, kuna vijiji vya Gedamara, Ayamango, Gidejabong, wale wananchi wanateseka, leo ni miaka karibu sita hawaruhusiwa kujenga, hawarusiwi kufanya chochote na fidia ambayo wanategemea kupewa ni ndogo na maeneo mbadala hawajaonyeshwa mpaka leo. Mimi naomba Serikali iangalie hilo tatizo liishe ili wale wananchi wapate maeneo mbadala na wapewe fidia stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna maeneo kwa mfano ya mijini ambapo maeneo ya watu wanachukuliwa fidia wanapewa shilingi 300,000 au shilingi 400,000 wakati ekari moja sasa hivi ni zaidi shilingi milioni tano au milioni saba katika eneo lile. Mimi naomba mahali ambapo Halmashauri inaamua kuchukua eneo kwa ajili ya kugawa *plot,* wangeangalia namna ya kuuza ile ardhi kwa mnada, yule mtu anapewa fidia ya shilingi 300,000 lakini ileile ardhi baada ya kupewa anauziwa mwekezaji au mwingine ambaye anataka kuwekeza pale kwa shilingi milioni kumi, milioni 15 ile eka moja inaweza kutoa mpaka shilingi milioni ishirini. Kwa nini ile haki asipate yule mtu ambaye alikuwa na ile ardhi kuanzia enzi ya babu zake? Halmashauri isubiri ipate hiyo kodi ambayo ingepata kila mwaka kodi ya ardhi au na mapato mengine ambayo itategemea kupata ili kila mtu apate stahiki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanja vingi kwa mfano maeneo ya Pwani wananchi wanaondolewa pale wanalipwa milioni moja, milioni mbili lakini *beach plots* zinakuja kuuzwa milioni 100, hivi huyu mwananchi ungempa hiyo milioni 100 kungekuwa kuna migogoro?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Komoto pale Babati wamechukuliwa maeneo yao wamelipwa fidia ndogo na tulishazungumza mpaka kwenye *RCC* kwamba maeneo kama yale wangelipwa watu kwa bei ya soko ili wale wananchi wasilalamike. Mtu angepewa fidia ya bei ya soko hawezi kulalamika hata siku moja. Leo fidia hapewi, eneo mbadala hapewi, tungeangalia namna nzuri ili mtu utakapomkuta umlipe kwa bei ya soko. Walikuwa wanalamika kwamba yale maeneo mengine wananchi wa kawaida wasingeweza kujenga, yaani mtu maskini hataweza kujenga. Hivi maskini mmoja ndio unataka umuongezee na kumsaidia na yule mwingine ndio umfanye awe maskini kabisa? Sheria iangaliwe ili yule ambaye anakutwa ana haki ya kuwepo pale ukitaka kumwondoa umfidie vizuri, kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine kwenye Wizara hii ninaomba yaangaliwe. Naomba Baraza la Ardhi, lingeangaliwa upya kabisa. Kwanza wapewe mafungu ya kutosha, lakini wapewe na nyenzo, wapewe usafiri, wapewe na vitendea kazi. Wana matatizo

mengi sana, wanyonge katika Baraza la Ardhi, hata siku moja hawapati haki. Mtu anapigwa tarehe 1, 2, 3, huna uwezo wa kusafiri, haki yako imepotea. Mimi naomba wangeangalia namna ya kutatua matatizo haya. Baraza la Ardhi halishirikishi Idara ya Ardhi ambayo iko ndani ya Wilaya hiyo, wanajiamulia pale wakati wako Wizara moja, ingekuwa wako Wizara mbili tofauti tungejua. Kama wanaona hawawezi kuwa katika Wizara hiyo basi mngeamua kuirudisha katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu hapa hawawatendei haki wananchi wengi ambao ni wanyonge. Kila siku unapigwa tarehe mpaka unachoka ardhi yako unaporwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba tuangalie upya suala la upimaji wa ardhi ya vijiji. Leo hii mimi nashukuru Babati Vijijini maeneo yetu mengi yamepimwa na hati zinaendelea kutolewa, naipongeza Serikali kwa hilo. Mradi sasa umeshaisha, sasa itabidi Halmashauri ndio zianze kubeba mzigo huo, hivi ni kweli Halmashauri zitaweza kazi hiyo? Kwanza, vifaa vya kupima Halmashauri zetu nyingi ndani ya nchi hii hawana. Mimi naomba vifaa vingenunuliwa vya kutosha na pia gharama za kupima wangeangalia mfumo mwingine ili wananchi wetu wapimiwe hizo ardhi. Ardhi ndio njia peke ambayo itamkomboa huyo mwananchi wa kawaida ambapo ataweza kutumia ile ardhi kwa kukopa, ataweza kuwekeza. Mbali na hiyo, wengi zile mila na desturi ambazo tunazo, akina mama na watoto watakosa haki kama wasipokuwa na hizo hati. Leo hizo hati zikiwa zina jina la familia, mama na baba na watoto ni vigumu hata ndugu wa wale marehemu kama mmoja akitangulia mbele ya haki kuja kudai ile ardhi, akina mama na watoto watapata haki yao. Kwa hiyo, naomba tungeangalia suala hili na Serikali iangalie namna ya kutafuta fedha ili sekta hiyo ifanyiwe kazi na watu wapate hizo hati miliki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika maeneo ya wazi mengi, wakati sisi tunasoma shule maeneo ya wazi yalikuwa mengi, leo maeneo ya shule, maeneo ya zahanati, maeneo ya hospitali yote yamechukuliwa. Mimi naomba tusiwahurumie watu ambao amevamia ndani ya eneo la huduma za jamii, wanyang'anywe na wafikishwe katika mkono wa sheria bila huruma yoyote. Siyo kubomolewa tu bali alipe na hiyo fidia kwa miaka yote hiyo ambapo yupo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala la mpaka kati ya Kiteto na Kondoa liangaliwe upya, sehemu za Simanjiro ambapo wanapakana na Hifadhi ya Tarangire, sehemu ya Kimotoroka, pia maeneo ambayo ni ya wafugaji wetu, wengi hawana maeneo na pia maeneo ambayo ni ya wafugaji yapimwe. Leo hii wafugaji wengi hawana maeneo, hawapimiwi ardhi yao, watakwenda wapi, maeneo yatachukuliwa na wajanja, baadaye hiyo mifugo itakwenda wapi? Wengi wao hawajasoma na elimu juu ya hizi Sheria za Ardhi hawajui, mimi naomba itolewe na watu waendelee kuelimishwa. Wenye kupata hiyo elimu ndio wanakuwa wajanja na ndio wanapora ardhi huko vijijini. Leo hii sehemu nyingi ardhi imekuwa ndio siasa. Leo hii mtu akitaka uongozi anasema nikipata haya maeneo mimi nitahakikisha mtapewa iwe hifadhi, iwe ni mashamba, ndio siasa. Mimi naomba, hii Sheria wananchi wengi wangeendelea kuelimishwa, mwananchi anadanganywa, ukiwa ndani ya eneo la hifadhi, ukiwa eneo lolote, ukikaa miaka 12 itakuwa ni haki yako, inatumika kama siasa. Sasa mimi naomba wale wanaobainika kuchochea migogoro kwa ajili ya siasa pia wachukuliwe hatua za kisheria ili watu waendelee kupata elimu na watu wapate haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Wizara ya Ardhi iangalie masuala ya kupeleka na kuboresha huduma mbalimbali, ishirikiane na Wizara nyingine kwa mfano ya Mindombinu, Wizara ya Uchukuzi na Nishati na Madini wapeleke huduma vijijini. Maeneo ya mjini ambapo watu wanaendelea kujazana ambao hawana kazi, wangeboresha hizo huduma kule vijijini na watu wakapata hati zao za ardhi, mimi naamini watu wasingekimbilia mijini na huko vijijini pia pangekuwa kuna maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuige mifano katika nchi mbalimbali, nchi zingine mwekezaji masharti ambayo anapewa wakati anakuja kuwekeza huwa wanayafuata. Hapa kwetu mtu anaweza kushika maeneo, mimi naamini kwa mfano kule Kigoma watu walipewa maeneo makubwa kuja kupanda Michikichi lakini hadi leo hii siamini kama kuna hata hekta 1000 ambayo mwekezaji wa nje ya Kigoma amekuja kupanda lakini maeneo tayari wamekwishamilikishwa. Mtu ambaye hatumii ardhi, wapewe ambao wana uwezo wa kutumia na ambao wana nia ya kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama India, juzi tulijaribu kufanya *research* wanasema huwezi kwa mtu wa kawaida ambaye si mkulima ambaye babu au baba yake hakumiliki ardhi ya kilimo ambaye ni raia wa pale haruhusiwi kumiliki ardhi ya kilimo, ina maana inawalinda wale watu wa kilimo (wakulima). Wewe kama hujawahi kuwa mkulima basi hutakuwa mkulima hata siku moja. Hapa leo wakulima wengi katika maeneo ambayo watu wamewekeza mtu mwenye uwezo anakuja ananunua ile ardhi, yule mtu anabaki kuwa kibarua kwa yule ambaye amenunua. Itafika mahali ambapo *ratio* kati ya wale ambao wana uwezo na wasiokuwa na uwezo itakuwa kubwa na tutafikia mahali ambapo hii nchi haitatawalika tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala la ardhi tuangalie kwa upya, tuangalie namna ya kuboresha ili kila Mtanzania hata yule mnyonge apate haki yake. Mimi naomba suala la Babati Vijijini, nasisitiza tena ni mgogoro wa miaka 25, nimeukuta, tumekuwa nao huko nyuma, watu walikuwa hawajafikia hatua ya kupigana na leo hii watu imefika mahali ambapo wanauana kwa ajili ya hiyo ardhi. Nchi ya Tanzania pia ilipigana vita kwa ajili ya hiyo ardhi na Idd Amin huko Uganda. Mimi naamini kila mmoja pia ana haki ya kufanya hivyo. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iangalie, ili amani isitoweke iweze kuangalia namna ya kumwezesha kila mmoja na ilinde kila upande, mwenye haki apate na wale ambao wanastahili kupata ardhi wapewe na tuonyeshwe maeneo mbadala ili tuweze kuhamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kushukuru lakini naomba suala la Babati Vijijini, Serikali ije iangalie kwa uwezo wake wote na safari hii mgogoro uwe umeisha, iwe ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata majibu ndio nitafikiria kwamba naunga mkono hoja au siungi mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi adimu niweze kuchangia katika Wizara ya Ardhi. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu siku ya leo kuweza kunipa afya njema na kuweza kusimama na kusema kilio cha wananchi wa Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposikia Randama ya Wizara ya Ardhi imewekwa Mezani ilinikumbusha mbali sana wakati niko kwenye kampeni katika Jimbo la Babati Mjini nikigombea Jimbo, nikiomba kura wananchi wanichague niwawakilishe katika Jimbo lile. Nilikumbuka huko mbali kwa sababu katika safari yangu hiyo ya kuomba kura katika Jimbo la Babati Mjini asilimia 90 za kero zao ni migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, siku ya leo nilivyoona Randama hii imewekwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakichangia migogoro hii, mwanzoni nilidhani kwamba tatizo la migogoro ya ardhi liko Babati, liko Mkoa wa Manyara lakini nasikitika kwamba migogoro hii iko Tanzania yote, iko katika Majimbo yote, iko katika Mikoa yote, iko karibu Kata nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba nchi yetu imekua, *population* imeongezeka, idadi ya wananchi imeongezeka lakini bado sisi tuna ekari zilezile, kilomita za mraba laki tisa karibia na nusu, ardhi tuliyonayo haiongezeki. Kinachotakiwa Serikali iwe na mipango mizuri ya kupanga rasilimali hii ya ardhi kwa wananchi na idadi ya watu inayozidi kuongezeka kila mwaka. Masikitiko ni kwamba Serikali imefanya migogoro ya ardhi au vilio vya Watanzania kwa ujumla kama kelele za mlango hazizuii wenye nchi kulala, ni kweli mtapuuza lakini migogoro hii ni mikubwa sana, akisimama Mbunge wa Mwanza atasema kule Mwanza kuna migogoro, akisimama wa Dar es Salaam, Ubungo ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika anasema na wananchi wake wa Kwembe hawajalipwa, kila Mbunge akasimama atasema migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifikie hatua Serikali iwe sikivu, miongoni mwa kesi nyingi kwenye Mahakama ni migogoro ya ardhi. Kwa nini Serikali imepuuza Wizara hii ikaipa bajeti kwa upungufu zaidi ya mwaka jana? Mwaka jana walipewa *almost* shilingi bilioni 53 lakini mwaka huu wamepunguziwa hiyo bajeti wamepewa shilingi bilioni 47, kwa nini? Imepuuza Wizara hii, imeona kwamba migogoro imekwisha? Kama migogoro imekwisha watuambie ni ya wapi imetatuliwa kwa sababu kila Mbunge anayesimama anazungumza kuhusu migogoro ya maeneo yake. Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuzungumza sasa hivi Jitu Soni, amezungumzia migogoro ya Babati Vijijini maeneo ya Kiru ina miaka 25 lakini Serikali je, imechukua hatua gani, mtuambie, hakuna! Katika Bunge hili Tukufu nilisema Mawaziri watano wakiwemo wa Wilaya hiyo walikwenda Kiru,

lakini baada ya hapo tuliona wananchi walizidi kuuana hata wale wananchi waliowekwa mahabusu zaidi ya 80, wao baada ya kutoka na mmoja akapoteza maisha, Polisi walimpiga kwa sababu waliambiwa waseme nani aliyemchinja yule msimamizi wa mashamba, tukisema Polisi wanaua Serikali inasema CHADEMA mnadanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi, hizi siyo kelele za mlango hata mkifunga masikio yenu wananchi wataendelea kuteseka. Wizara hii kutengewa bajeti ndogo kiasi hicho wakati migogoro inazidi kuongezeka, mimi naona ni aibu, ni kupuuza kero za Watanzania. Mimi nilikuwa na imani na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Naibu Waziri wake, walianza vizuri sana lakini nashangaa ule moto umezimwa kwa nini? Mheshimiwa Waziri hatuuoni tena moto wako, migogoro imekwisha, haijaisha! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie haya machache, kwanza, *lease* katika Mkoa wa Manyara. Mkoa wa Manyara tumezungukwa na *lease* nyingi sana. Nyingi zime-*expire* lakini cha kusikitisha maeneo haya hayarudishwi kwa wananchi. Ni hivi juzi wananchi wa maeneo ya Singu, Endasago, Alizaayo walikuwa wananipigia simu wakisema Mheshimiwa Pauline Gekul, tusaidie kuuliza kuhusu mashamba ya Rivacu, Mheshimiwa Naibu Waziri anayafahamu, wanauliza kwa nini sisi Watanzania hatupewi, sisi wananchi wa maeneo hayo tunaona mashamba haya *breweries* hawayaendelezi tena lakini wananchi tumekuwa manamba kwenye maeneo hayo, tunakodishiwa mashamba hayo, kwa nini tusigawiwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atakapokuwa ana-*windup* anipatie majibu kwa nini mashamba haya, kama hizi *lease* zime-*expire* wasiwagawie Watanzania? Kwa nini Watanzania wanaendelea kuwa manamba katika nchi yao, wanabaki kuwa ombaomba wa maeneo kutokana na ardhi zao walizopewa na Mungu kupewa wawekezaji. Wao ndio wawagawie kwa vipimo wanavyovijua wao. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja na majibu, anisaidie shamba la Rivacu kama lime-*expire* Watanzania wa Singu, wa Ari, wa Endasago wagawiwe haya mashamba na wenyewe waweze kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Silatoni, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu. Shamba la Silatoni takribani miaka 10 sasa Watanzania wa Babati tulilipa fedha Halmashauri wakasema watatugawia hayo mashamba lakini wakati nazunguka kwenye kampeni wakanisisii sana Mheshimiwa ndugu yetu Pauline Gekul tusaidie ukifanikiwa tuambie fedha zetu ziko wapi miaka 10 tangu mwaka 2002 watu wamelipa, Halmashauri haigawi hilo shamba lakini pia wanasema kuna kesi. Nakumbuka mwaka 2004 wakati wa Utawala wa Mheshimiwa Rais Mkapa alisema kwamba hili shamba lirudi kwa wananchi, alifuta ile *lease,* kama kesi inaendelea kwa nini msiwaambie Watanzania hatma ya fedha zao, wananchi wa Babati waliolipa fedha zao siyo wa kurudishiwa fedha zao, siyo wa kupewa mashamba. Naomba niambiwe kuhusu hilo Shamba Silatoni lakini pia Shamba Nila, Shamba la Hanadeko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba wananchi wanaokaa maeneo ya Misuna, maeneo ya Kiongozi wanavyonyanyasika. Kaya 74 wanatakiwa waondoke kwenye eneo hilo, wanaitwa ni wavamizi katika maeneo hayo. Katika hizo kaya 74 ni *almost* wananchi wengi sana, ukiweka na watoto ni wengi sana. Wanatakiwa waondoke, waende wapi wananchi wa Misuna, wananchi wa Kiongozi? Hili shamba amepatiwa mwekezaji lakini mwekezaji huyu anaungana na Halmashauri, wananchi hawana mahali pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hivi, namshukuru Mwenyezi Mungu leo nimesisima na nimepata nafasi kusema haya, kweli simu ni nyingi ninazopigiwa kuhusu migogoro ya ardhi Babati, wananchi wananyanyasika sana. Niwape mfano wananchi wa Wemairo juzi waliwekewa karamu na mwekezaji, wakapikiwa pilau, wakapewa na soda wakasainishwa kwamba wasifuatilie hilo shamba la ekari 111, mwekezaji wa shamba hilo anaitwa Babu Hatia. Wananchi, ng'ombe wakiingia kwenye mashamba hayo wanapelekwa Mahakamani, ni mahabusu lakini wananchi hao 15 cha kusikitisha wameapishwa mpaka wakalambishwa na asali wasifuatilie maeneo yao. Mnataka tufanye nini? Tulie? Hatuwezi! CHADEMA sisi tutaandamana maana kulia siyo *style* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa kweli mambo haya yanadhalilisha, yanasikitisha, kama hii nchi ina utawala bora, inakuaje mwekezaji anawaapisha Watanzania kwamba mkifuatilia mtalala mahabusu. Wanalambishwa asali, wamelambishwa watu tisa kati ya 15 lakini sita wamekataa lakini wanatafutwa. Serikali iko wapi? Babati tunateseka na migogoro ya ardhi na tumeshazungumza mara nyingi sana. Naongea kwa masikitiko kwa kweli Mheshimiwa Waziri, naomba unapokuja jioni na majibu niambie hatima ya Babati, hatma ya wananchi wa Mkoa wa Manyara na *lease* hizi ambazo zime-*expire* ambazo kwa kweli zimemilikiwa na watu wachache ambao ni vigogo katika nchi hii, ndio wanaowekeza Babati wananchi wanasogezwa pembeni. Mtupatie maeneo ya hao wazawa wa Babati na Mkoa wa Manyara wakakae wapi ili ninyi muendelee kukodisha kwa hawa ambao wana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naamini Mawaziri wamenisikia na wanafahamu Babati ilivyo. Nihamie kwenye upimaji wa ardhi. Tatizo la upimaji wa ardhi pale Babati, Halmashauri imetoa hiyo tenda kwa kampuni binafsi inaitwa *Geo Information and Engineering* tangu mwaka 2008. Wananchi wa Babati wanalipishwa shilingi 90,000 kupiwa maeneo yao. Nauliza jamani mniambie kwa nini wananchi wanalipa shilingi 90,000 siyo wote, Halmashauri imetangaza kuwa ni Halmashauri ya Mji, lakini Watanzania wa Babati wana mashamba yao unamwambia alipe shilingi 90,000, akauze magunia ya mbaazi yote, auze ya mahindi, alale njaa, alipe shilingi 90,000 kwa ajili ya Serikali kumpimia maeneo yake? Siyo haki. Cha kushangaza, Halmashauri hiyo ina watalaam, ina ma-*Surveyer* wazuri sana lakini hawana vifaa. Mheshimiwa Waziri nimeshakueleza sana kwamba Halmashauri ipatiwe vifaa. Watalaam hawa wamejitahidi wamekwenda kuazima vifaa Mkoani pale, Mkoa umewapatia vifaa Halmashauri pale hawataki kuwapatia hiyo kazi ya kupima wanaendelea na huyu mwenye kampuni binafsi anawalipisha Watanzania wa Babati shilingi 90,000, sitaki kumtaja. Naomba sana mtuambie wananchi wa Babati watapumzika lini na hii adha ya kulipa elfu tisini na kunyang'anywa maeneo yao pale ambapo wanashindwa kulipa hizo elfu tisini kwa ajili ya kupimiwa maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihamie kwenye fidia. Fidia mnazotoa kwa Watanzania hawa ni ndogo sana. Mheshimiwa Jitu Soni alizungumzia Komoto, mimi niseme tatizo la Komoto ni kubwa, kesi iko Mahakamani, viwanja vimegawanywa mia sita karibia na thelathini, waliotaka viwanja wamelipa pesa, wale wenye mashamba yao hawajalipwa fidia, hizo pesa ziko wapi? Tangu mwaka 2006 hizo pesa ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wale ambao wamenunua viwanja wanashindwa kuviendeleza, hizo pesa zimepotelea wapi, Halmashauri? Kibaya zaidi wananchi wa Bagara wamepisha ujenzi wa Kituo cha Polisi, *Field Force*, Polisi wametoa shilingi milioni 76 lakini zimepotelea Halmashauri. Hizo pesa wananchi wa Bagara hawajalipwa, wananchi 12 kila siku nyumbani wananibishia hodi, nawaambia karibuni tuzungumze, wanasema Mheshimiwa tusaidie pesa zetu, ukienda Halmashauri hakuna majibu. Wananchi wa Bagara wamepoteza imani na Serikali, wananchi wa Komoto wamepoteza imani na Serikali, wananchi wa Babati kwa ujumla wamepoteza imani na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe kama Serikali hii ni sikivu, mje na majibu yanayotosheleza maana pale Bagara Sekondari, watoto juzi wametinga Halmashauri, kwa Mkurugenzi, Mkurugenzi tuambie hatuna viwanja, mpaka eneo la sekondari viwanja vya wanafunzi, magoli yameng'olewa, viwanja vinauzwa. Mnataka tufanyeje? Migogoro ya ardhi ni mikubwa, lakini pia ni aibu kutenga shilingi bilioni 47, ilikuwa shilingi bilioni 53 mnazidi kupunguza *as if* migogoro ya ardhi imekwisha, ni aibu kwa Serikali, ni kupuuza kilio cha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mapendekezo kwa kumalizia. Kwanza, mnapopima kwenye Miji wale wazawa mnapowakuta pale Mheshimiwa Waziri muwatengee basi maeneo yao. Hiki kilio kinafanana na wananchi wa Dodoma, wanalalamika na *CDA*, wanasema jamani tunasogezwa pembeni, unalipwa fidia kiwanja kimoja unaenda kuishi wapi? Hilo shamba lilikuwa linasomesha watoto, hilo shamba analima mahindi na mbaazi na mazao mengine, analipa ada za watoto wake, leo unampa fidia kiwanja kimoja huyu Mtanzania anaishije katika nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango Miji watenge maeneo ya wazawa kwa Mikoa yote, wasiwakaribishe tu watu wenye fedha zao wale wa pale wanaokutwa wanasogezwa pembeni, muwatengee maeneo yao na wenyewe waone kwamba wako katika Tanzania hii ambayo inasemekana ina amani. Pendekezo la pili, mzipatie Halmashauri vifaa vya kupima ardhi, acheni kuwabebesha Watanzania mzigo wa kupimiwa maeneo yao. Kama asilimia moja mpaka leo ndiyo imepimwa ni aibu kwa Serikali miaka hamsini ya uhuru. Mkapime, muwapatie Watanzania hati miliki *(title deed)*, wakakope benki, wajiendeleze hata kwenye biashara zao, Halmashauri mziwezeshe. Mheshimimiwa Waziri mtusikilize vilio vyetu, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba mimi siungi mkono hoja kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Manyara watanishangaa sana. Migogoro yao haijapatiwa utatuzi na naomba majibu ya kina sana. Babati sio wabaya kiasi kwamba tunauana, ni mikataba mibovu mnayowapa wawekezaji bila kuwashirikisha Watanzania. Sio watu wabaya mpaka wauane kiasi hicho. Mkoa wa Manyara mtoe *treatment* ya tofauti, kuna migogoro mikubwa, kuna *lease* hazina watu zimekaa tu. Tena wananchi wa Magugu nisisahau kusema, ukitaka kulima pale shamba la Magugu unakodishiwa shamba mwisho wa siku unapeleka magunia ya mpunga, *almost* laki na themanini, mwekezaji amekaa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja kwa asilimia mia moja*. (Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA**: Jamani, sasa kama kila mtu haungi mkono, mnataka hoja hii iende wapi?

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia tukawa wazima na hai na nikaweza kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia katika Wizara hii.

La pili, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mtizamo wangu, Wizara hii nimeona ina changamoto mbili kubwa. Ya kwanza, ni ya utekelezaji ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho katika Wizara yenyewe lakini changamoto ya pili ni ya kibajeti ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyekaa sasa hivi kaizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii kwa kweli ina urasimu mkubwa katika shughuli mbalimbali ambazo wanazifanya matokeo yake wananchi wanapata usumbufu mkubwa katika suala zima la ardhi ikiwa katika kupata hati au kupimiwa au vinginevyo. Ili nieleweke, nina mfano hai hapa. Yuko mwananchi mmoja aliomba kiwanja na akaenda Ofisi ya Ardhi maarufu wanaita Ardhi, Dar es Salaam pale na mwananchi huyu alifika pale tarehe 25 Julai, 2008 na akapewa fomu yenye maombi ya kiwanja. Kuanzia pale, mwananchi yule alianza kupanda na kushuka kwenye *lift* katika Wizara ile. Kiwanja bahati nzuri alikipata lakini kiwanja alikipata tarehe 11 Januari, 2010, hii ni karibu miezi kumi na nane. Sasa mwananchi kama huyu, karibu mwaka na nusu anaenda Wizara ya Ardhi kufuatilia maombi yake yamefikia wapi. Kwa hiyo, katika hali kama hii ndiyo hapo mazingira ya rushwa yanapopatikana na vilevile huo ujenzi holela ambapo Serikali inasema inataka irekebishe yale maeneo mengine ambayo tayari ujenzi holela umefanyika, basi itakuwa si rahisi mwananchi miezi kumi nane anahangaikia kiwanja wakati vimeshapimwa lazima atajenga holela. Kwa hiyo, nadhani hii ni changamoto ya kwanza ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, ni suala zima la bajeti. Ni kweli Wizara hii kama alivyozungumza mwenzangu, bajeti ya Wizara hii kwa kipindi kilichopita ilikuwa ni shilingi bilioni 53.8 na mwaka huu ni shilingi 47.8 kuna upungufu wa shilingi bilioni sita. Kwa hivyo, ni dhahiri Serikali haiendi sambamba na mwamko wa wananchi, kwa sababu wananchi wanahitaji viwanja vilivyopimwa, wanahitaji mashamba yaliyopimwa, wanahitaji vijiji vilivyopimwa, lakini Serikali kwa kupunguza hizi shilingi bilioni sita ni kuashiria kuwa wao hawako pamoja na wananchi katika suala zima la kupata hati na kupimiwa maeneo yao. Kwa hiyo, suala hili kwa kweli linavunja moyo na linasikitisha. Hata kama ingekuwa shilingi bilioni 53 bado kwa Wizara hii ingekuwa ni fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi ni kuwa ukiangalia bajeti iliyopita ambayo Wizara ilitegemea ipate shilingi karibu bilioni 20 kwa ajili ya maendeleo mpaka Mei, 2011, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilipata shilingi bilioni 4,673,383,000 kutoka bilioni 20. Sasa kusema kweli haieleweki. Kutoka shilingi bilioni 20 unawapa shilingi bilioni nne, kwa hiyo kwa vyovyote vile utendaji wa Wizara hii kwa kweli utakuwa na dosari kubwa hata kibajeti kama ambavyo nimeshazungumza hapo mwanzo. Matokeo yake ni jambo la aibu, miaka hamsini ya uhuru, nchi haina hazina ya ardhi kwa maana ya *land bank*. Wawekezaji wanakwenda kubanana kulekule na wanavijiji matokeo yake kama ambavyo Wabunge wengi wameshazungumza migogoro inatokea na hili linasababishwa na suala la bajeti finyu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza, kwa kweli kwa maana ya wawekezaji wakubwa kama ni wa ndani ya nchi au nje ya nchi, kwa kweli haina maana kwa sababu Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* hawana ardhi ambayo mwekezaji akitoka nje au hata ndani ya nchi anayetaka akapewa. Kwa hivyo imekuwa ni maneno tu, Kilimo Kwanza kwa maana hiyo kilimo kitabakia kwanza kwa wakulima wadogowadogo lakini wawekezaji wakubwa kwa kweli hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ardhi zina migogoro na ili migogoro itatuliwe ni wahusika kupeleka kwenye vyombo vinavyohusika. Ukiangalia Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 yako Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Ni jambo la kusikitisha uundwaji wa Mabaraza haya kwa kweli unakwenda kwa kasi ndogo kweli. Kuna Wilaya ambazo hivi sasa zina migogoro ya ardhi lakini hawana pahali pa kupeleka malalamiko yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka mwaka 2009/2010 kulikuwa na Mabaraza 39 ya Ardhi ya Wilaya. Mwaka 2010/2011, wakaongeza matatu tu, katika bajeti hii ambayo Mheshimiwa Waziri jana kaiwasilisha, wana Mabaraza sita. Kwa hivyo, jumla itakuwa ni Mabaraza 48. Sasa zile Wilaya ambazo hazina Mabaraza, kesi zao ziende wapi kwa sababu kazi moja ya Mabaraza haya ni kushughulikia migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, inaonekana kwa kweli Wizara hii ina mashaka makubwa kwa kweli. Kwa hivyo, nadhani hili pia nalo linasababishwa na suala zima la kibajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wabunge wengi ambavyo wamezungumza, kwa kweli ardhi zina migogoro mingi mfano katika maeneo ya Kilombero, Kilwa, Babati na kadhalika. Nadhani umefika wakati kutafuta njia ya kupunguza migogoro hii. Nadhani umefika wakati sasa kuletwa Sheria tena haraka hapa Bungeni ili wawekezaji walazimishwe na Sheria kuwa lazima waingie ubia na wanavijiji vinginevyo migogoro hii kwa kweli itandelea. Hilo litaondoa mfarakano au mgongano baina ya wanavijiji na wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la ardhi kwa kweli lina mgogoro baina ya wafugaji na wakulima. Navyoona suluhisho la suala hili ni kufanya kazi kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 2010, Sheria ya Mifugo inayohusiana na Usajili na Utambuzi wa Mifugo. Sheria hii itakapofanya kazi labda inawezekana Kanuni bado na kawaida huwa zinachukua hata miaka mitatu katika utendaji wetu huu, basi nadhani hii inaweza ikasaidia sana kwa sababu Sheria hii inataka wafugaji wawe katika maeneo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitahadharishe kitu kimoja, Tanzania tunayo kawaida ya kutunga Sheria lakini hatuangalii gharama za Sheria zile kwa sababu kila Sheria unayoitunga, nia yake ni kurekebisha upungufu ambao umetokea. Kwa hiyo, kila Sheria ina gharama yake ukikosa kujua gharama ya Sheria basi matokeo yake Sheria ile inabakia katika makabati. Kwa hiyo, Sheria hii ninayoisema Na. 12 ya mwaka 2010, kama haikuwekewa bajeti yake katika utekelezaji, basi Sheria hii haitafanya kazi lakini kama itafikiriwa bajeti yake, basi naamini tatizo la wafugaji na wakulima kwa asilimia kubwa litapata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo Watanzania kwa kweli nasema tumelala, suala la mpaka baina ya Tanzania na Malawi. Mimi kwa kweli katika kufuatilia kwangu siridhiki na Wizara inavyolifuatilia suala hili na inawezekana kwa sababu hivi sasa ni shwari lakini mara tu baada ya uhuru wa Malawi vurugu zilianza, ikaonekana kuna haja ya kulitatua lakini mpaka leo kwa kweli suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Badala yake inashughulikiwa mipaka ya Msumbiji-Tanzania ambayo kwa kiasi kikubwa hakuna matatizo, Kenya na Tanzania kwa kiasi kikubwa

hakuna matatizo, lakini Malawi na Tanzania ambako kila Mtanzania anajua kuwa kuna ramani nyingine zinaonesha Ziwa Nyasa liko wapi, Ziwa lote linaonekana kuwa liko nchi ya Malawi. Hili ni tatizo na kutolishughulikia suala hilo, iko siku moja Mwenyezi Mungu anaweza akajalia pale pakaonekana mafuta pengine, hapo ndipo tutakapoona tatizo lakini leo linaonekana ni suala la kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwaka 2008 katika kushughulikia suala hili, kwa sababu mpaka wa Malawi na Tanzania una sehemu mbili, kuna sehemu ya Mto Songwe na sehemu ya Ziwa lenyewe Nyasa. Kwa hiyo, kilichofanyika katika mwaka 2008, kulifanyika mambo mawili. Kwanza kuanzisha mradi uliodhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ya kujenga vizuizi ya kufanya Mto Songwe usihame lakini mwaka huo huo wa 2008 likafanyika suala zima la kuunda Kamati, Wizara iliunda Kamati ya kutafuta, kukusanya nyaraka za kihistoria na za kisheria na kidiplomasia, hiyo ndiyo iliyokuwa kazi ya mwaka 2009/2010, sikuona kilichofanyika kwa kweli. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri, mwaka 2010/2011, mazungumzo yatafanyika na hao watendaji. Sasa mwaka huu, Wizara inawasubiri Wamalawi waitikie mwaliko waje Tanzania. Mimi nadhani sisi tutoke kwa sababu wao hawana tatizo, tatizo la mpaka wa Tanzania na Malawi liko kwetu sisi. Linapotokea lolote basi wao watarudi hata kama ni makosa kwa sababu inaeleweka pengine katika mipaka ya maji basi inapita baina ya nchi na nchi, lakini wao hawako hivyo, hawaamini hivyo. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya Wizara kwa kweli wakalifuatilia suala hili na wakaweza kulitatua, vingenevyo patakapokuja kutokea lolote la maana pale katika maji ukiachana na samaki, basi panaweza pakatokea vurugu, halafu tutakaja tukaona kuwa tunaingia katika jambo ambalo hatukulitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Shirika la Nyumba la Taifa. Kwa kweli kwa maelezo yao na mtizamo wao kwa kweli tuseme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa, napenda Waziri na Naibu Waziri watuombe radhi Wabunge na Watanzania. Nasema hivyo kwa sababu wametudanganya. Wametuonesha miradi mingi, changamoto wanazijua na fedha walizotengewa au walizotenga hazitoshi, tusingependa kudanganywa. Naomba tu nimwombe Waziri akamwambie Rais hii kazi imemshinda, atafute mtu mwingine kwa sababu fedha alizonazo na changamoto zilizopo, hazifanani. Kama anaona aibu, anitume mimi nitakwenda kumwambia nikionana naye. Kwa kweli Watanzania sio wakudanganywa tena, fedha hazitoshi, kazi ngumu. Tusijitahidi kuishi kwa matumaini kwamba tutafanikiwa wakati hatuwezi! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli ambayo inatumika kwamba ardhi ni mali ya Serikali, mimi nilikuwa nadhani sasa ardhi iwe mali ya mtu mmojammoja anayemiliki kisheria. Hii ardhi kuwa mali ya Serikali inawafanya Watanzania wafikirie kwamba kuishi kwenye ardhi ya Tanzania ni msaada.

Watu wachache wanatumia kauli hii kwa kuwapa wawekezaji wenye fedha kwa kutumia mbinu za kifisadi. Wanamilikisha ardhi wale wakienda kugoma wanaambiwa kuwa kumbuka ardhi ni mali ya Serikali, mtu anakuwa mpole. Naomba tunapokwenda kuandika Katiba mpya sasa ardhi iwe mali ya mtu mmoja mmoja anayemiliki kisheria. Tukiwamilikisha Watanzania ardhi, kwanza asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini, tukawamilikisha ardhi ya vijijini wakaiongeza thamani, wakakopa benki, wanaweza kuendelea na tutakuwa tumewaendeleza Watanzania kwa asilimia 80 kuliko kuangalia mijini peke yake. Miradi mingi ya maendeleo ya makazi inafanyika mijini, wakati sehemu kubwa ya Watanzania iko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tufikirie sana pia watu wa vijijini ambao ni wengi. Tuwamilikishe ardhi, wakakope benki, wafanye biashara wanazodhani au kama wanaweza kufanya shughuli za kilimo waendelee kwa kiasi kikubwa kwa sababu wanaishi kule. Kuna changamoto nyingi sana kwenye Halmashauri zetu. Vifaa vya kupimia ardhi sehemu nyingine ni

vya kizamani au havipo. Magari hawana. Wanapofikia muda wanataka kwenda kupima ardhi mtu anatakiwa kupimiwa, anaambiwa atafute usafiri, wakati hapa tunatenga fedha kwa ajili ya Wizara. Sasa najua fedha hizi hazitoshi, ndiyo maana mwanzo nilimwambia Mheshimiwa Waziri atuombe radhi kwamba ametudanganya. Hii miradi anayosema itatekelezeka, haitatekelezeka kwa fedha alizotengewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutumie utaratibu ule ule uliofanyika kwenye Wizara ya Ujenzi, zipunguzwe fedha aongezewe kama kweli hataki kutuomba radhi na anataka kazi hii isionekane imemshinda. Yeye ni Profesa, nimeziona kazi zake nyingi nje na nimesoma kazi zake nyingi sana alipokuwa Nairobi. Lakini sijui kama ameomba dola za Kimarekani au ni fedha za Kitanzania. Profesa mimi najua kabisa hata yeye anajua hizi hazitoshi. Kama anadhani zinatosha, basi huko mbele hatafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi imefikia katika hatua mbaya sana. Mpaka sasa kuna migogoro kati ya Jeshi na raia ni mbaya. Huko tunakoelekea ni mbaya, wengi wanaogopa kusema. Lakini bora niseme kwamba, tumefikia muda kuna wananchi wana migogoro ya ardhi na jeshi. Hili nina uhakika kabisa, Serikali sijui itatumia burasa zipi. Lakini wananchi sasa wanapoteza imani na jeshi lao wanapoteza imani na Serikali kwa sababu ya migogoro. Tumefikia hatua watu kama alivyosema mwenzangu wanashika mipaka kwa ajili ya ardhi na halafu Sekali hiyo hiyo inawatangazia watu Kilimo Kwanza hapa.

Nadhani habari ya Kilimo Kwanza mkawatangazie Uingereza, Marekani na South Afrika mnaowapa ardhi ya kilimo. Kwa sababu Watanzania mnawaambia Kilimo Kwanza wakati mnachukua ardhi yao, mnawadanganya. *(Makafi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sihitaji kuchukua muda mwingi sana. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri, katika majibu yake asihangaike kuomba tu tuendelee kupitisha. Yeye amwambie Mheshimiwa Rais kwamba, hii ngoma ni nzito. Nimechemsha, tafuta mtu mwingine afanye kazi hii kama fedha anazotengewa ni hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vicent hizo ndogo tena huziungi mkono. Baada ya Mheshimiwa Vicent Nyerere kama nilivyosema ni Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Shekifu Henry ajiandae na Mheshimiwa Siylvestry Koka atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho wa mchana huu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nukushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii. Lakini vile vile siungi mkono hoja si kwa sababu sina imani na Waziri wala Naibu Waziri, hapana. Ni kwa sababu licha ya wao kuwa na nia njema ya kufanya kazi mbali ya kuwa na fedha finyu. Lakini nadhani hapati ushirikiano wa kutosha kutoka Serikalini kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mzungumzaji mmoja nadhani ni mama Kikwembe *if I am not mistaken* wakati nimetoka akapiga mawe kidogo. Lakini nimhakikishie kwamba siwezi kuzungumza kitu ambacho sina ushahidi nacho. Aliniambia nimtajie majina ya Madiwani waliokwenda Marekani siku nne. Nitamtajia Kata, majina itakuwa kazi yake yeye kutafuta. Kuna Diwani wa Kata ya Magamba, kuna Diwani wa Kata ya Sitalike, kuna Diwani Viti Maalum Karema na kuna Diwani Viti Maalum Uruwira. Sasa majina akayatafute yeye. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inasikitisha. Unapoona Mbunge mnajaribu kutetea eneo lake yeye, anakuja ana-*crash down* pasipo hoja za msingi na kwa sababu ya uvuvi wa kusoma. Juzi kwenye *SADC Forum* iliyokwisha tu majuzi. Moja ya ajenda ilikuwa ni *Land Crabbing Africa.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazungu huko walishamaliza kwao, wanakuja kurudisha ukoloni. Kibaya zaidi mtaalam wa Canada, mzungu huyo huyo akaenda na mikataba mizito hivi na

mkataba uliotolewa mfano, kama *West Case Scenario* ni mkataba wa *Agrisoil Tanzania.* Nasikitika jana namsikia Mbunge mmoja kutoka Kigoma, anasema eti wenzake wa Kigoma wameshindwa kutumia ardhi, wakati kuna hekta 80,000 wameshindwa kutumia ardhi, kwa hiyo walete wawekezaji. Tena msomi mzuri, inasikitisha. Kwa hiyo, niseme hili la suala la *Agrisoil* mbali na upungufu wake wote na upuuzi wake wote umekiuka Sheria ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zetu ziko wazi kabisa na hii namwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu asipoli-*handle* vizuri anaweza akaanguka nalo. Ataanguka nalo kabisa. Kwa sababu kuna ushahidi wa moja kwa moja unaoonyesha kwamba Ofisi yake ilihusika. Kwa hiyo tutumie busara tuokoe nchi. Sheria ya Ardhi iko wazi. Muwasaidie Mawaziri, mumsaidie Naibu Waziri. Sheria ya Ardhi iko wazi kabisa. Mgeni ama mwekezaji anapotaka kuja kumiliki ardhi ya nchi imeeleza wazi, kifungu cha 19, Kifungu cha 20(i) hadi 20(iv) mabadiliko ya 2004. *Very clear* na imesema wazi kabisa kama kuna *joint venture* inamhusu raia na Sheria ya Uraia haijatambua kampuni, haijatambua Halmashauri, haijatambua kitu kingine chochote raia mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtuambie huko Rukwa ni raia gani anamiliki hekta laki mbili na kitu. Huko Lugufu Kigoma kuna raia gani anamiliki hekta 80,000 ambaye anaingia ubia sasa ili ule mchakato wa kufuata *TAC* usifuatwe. Naomba tuache ushabiki. Hii ni *crisis*...

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ili niweze kumpa taarifa Mheshimiwa Halima Mbunge wa Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hakuna mwekezaji aliyepewa Hati Miliki kule Rukwa. Ninachojua na ninachofahamu ni kwamba kuna makubaliano ya awali ili watu wazungumze namna bora ya kuweza kuwafanya wawekezaji kutoka nje washirikiane na wananchi wa Rukwa na Kigoma. Kwa hiyo, anavyosema Sheria imevunjwa naomba nimweleze kwamba hakuna Sheria iliyovunjwa na hakuna umiliki uliotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Halima.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza taarifa yake siitaki. Lakini pili, mimi mwenyewe hivi kiwanja changu sina Hati Miliki. Hati Miliki siyo *issue.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatu, kuna kitabu cha makubaliano waliyoingia baina ya Halmashauri na *Agrisoil* na mkitaka nitaleta kwenye Meza yako. Wao wenyewe hapa wamekiri, kuna hivyo vitu vinavyoendelea Bungeni. Kwa hiyo, kama nyinyi ambao ndiyo mnatakiwa mtekeleze Sheria mnakuja hapa mnatetea wahalifu, tunakoelekea kama nchi kunatisha. Hatutafuti umaarufu wa kisiasa, umaarufu upo tayari, tunataka kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nirudi Jimboni maana nilisimama kwa ajili ya Jimbo. Lakini alinivurugua *system* Mama Kikwembe ikabidi nirudi kule ambacho sikutaka kurudi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Suala la kwanza...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba umewasha *microphone* jambo ambalo nilishalikataza. Kwa hiyo Mheshimiwa Halima endelea. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunilinda. Katika Jimbo langu na nadhani katika Majimbo ya Dar es Salaam ndiyo yanaongoza katika migogoro ya ardhi. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri suala la Mabwepande. Miaka

minne iliyopita mlikwenda pale, mkawaambia wananchi wasiendeleze maeneo yao. Mkawalipa wengine kama 160.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa. Mzungumzaji anayeendelea amesema kwa mafumbo kwamba aliyeongea wa Kigoma jana ni mimi. Niliongea kuhusu Lugufu. Nataka kumpa taarifa ni vizuri jamani tukiwa hapa Bungeni angalau tuseme ukweli. Lugufu kuna hekta 23,000 na siyo 80,000. Lugufu hao *Agrisoil* wamepewa hekta 10,000 na siyo 80,000. Nawaombeni, tusitafute umaarufu kwa kusema uwongo. Ninachosema watu wa Kigoma sisi ndiyo tunajua. Tusigeuzane watu wengine maendeleo yenu ni ya maana zaidi kuliko maendeleo yetu. Sisi tuna hakika wale watu wakianza kazi ya kulima katika ule mji, watu wote watakuwa wanakwenda ku-*supply* mazao pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwenye Bunge lako huu uzalendo unaoletwa, uzalendo uchwara hatuutaki Kigoma, tunataka maendeleo. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwonea huruma sana kwa sababu 2015 sijui kama atarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mabwepande. Naomba na muda wangu huu pia uzingatiwe. Miaka minne iliyopita Serikali ilikwenda kufanya tathmini na ninavyozungumza hivi pia na katika mfumo huo huo nazungumzia eneo la Kwembe kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mnyika. Nilikwenda kufanya tathmini, wananchi wakaambiwa wasiendeleze maeneo yao na kwamba Serikali ina mipango ya kuja kulichukua lile eneo kwa ajili ya matumizi mapya. Jimbo la Ubungo lilikuwa ni kwa ajili ya kujenga Chuo cha Muhimbili kwa mantiki ya *Campus* nyingine. Lakini vile vile Mabwepande kulikuwa kuna chuo cha *IFM* na miradi mingine 20,000 ya viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, imepita zaidi ya miaka minne. Wananchi hawajui mustakabali wao. Waliolipwa ni wananchi 160 tu kwa kipindi hicho zaidi ya wananchi 600, hawajui mustakabali wao ukoje. Lakini vile vile kwa upande wa Kwembe Serikali iliwaahidi wananchi kuwalipa pamoja na thamani ya ardhi na siyo mimea, kwa sababu pia Sheria zinasema hivyo na wananchi wa Kwembe hawana tatizo la kuhama. Tatizo lao la msingi ni ile haki yao waliyokubaliana kimsingi walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mabwepande tunavyozungumza leo hii na nakumbuka wakati wa Kamati, nilivyokuja kwenye Kamati yao, nilimwambia kuna uvamizi wa hali ya juu unaendelea. Wananchi ambao waliiamini Serikali yao hawakulima, hawakujenga kwa sababu waliambiwa kwamba kuna mipango ya maendeleo, wakaa pembeni leo wamegeuka wakimbizi kwenye ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimeshapiga kelele katika Halmashauri, nimekwenda kwake kwa njia ya barua. Lakini hali kule ni mbovu. Naomba Serikali ichukue hatua. Mimi kama Mbunge wa Kawe silindi mvamizi hata mmoja. Wasije watu wakawa huko kwa maslahi yao, wanasema Mheshimiwa Halima Mdee anatuunga mkono. Sijatuma mvamizi yoyote akavamie eneo,nataka haki itendeke. Kwa hiyo, naomba suala la Mabwepande na suala la Kwembe naomba myafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine Mheshimiwa Waziri kuna hili suala la Boko Dovya katika Shamba la Bwana Somji. Kuna taarifa hapa kwa vyombo vya habari kutoka kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kipindi kile alipokuwepo Mheshimiwa Chiligati, alikiri kwamba hili tatizo limekwisha. Serikali itachukua lile eneo kwa ajili ya kugawiwa kwa wananchi. Mpaka leo hakuna kinachoeleweka Somji anaendelea kuwasumbua wananchi ambao wako kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, naomba tafadhali tafadhali niweze kupata ufafanuzi kwa haya masuala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni suala la Chasimba. Hili suala siyo dogo kama watu ambavyo wanataka walifikirie. Ni suala ambalo linahusisha wananchi zaidi ya 10,000. Ni

suala ambalo ushahidi wake uko wazi na nimeeleza kwa kina sana kwenye hotuba yangu. Lakini nitalizungumza hapa. Inawezekana Serikali mkaja na *scenario* kwamba hili suala ni la zamani, liliendа Mahakamani na limeamualiwa Mahakamani. Kwa hiyo, wananchi waondoke, naomba mtumie busara. Nina hukumu ya Mahakama hapa. Nina *documents* hapa nitamletea Mheshimiwa Waziri zinazoonesha jinsi kijiji kilivyosajiliwa zinazoonesha kwamba mmiliki wa kiwanda hamiliki viwanja vyote vitatu kwa mantiki ya moja, nne na saba. Lakini nimesoma hukumu hapa, inasema naomba ninukuu kidogo: *"It is the respondent case from a total twelve witnesses that the village officials of Boko".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu kidogo, kengele ya kwanza? *It is the respondent case from a total of twelve witnesses that the village officials of Boko and Tegeta were contacted with the view of securing more land by organizing meetings with the villages. At the end of the day the respondent managed to buy a number of villages by wealth composition.* Hukumu sababu katika hii kesi *respondent* alikuwa ni *TUGHE*. Kwa sababu ilikuwa ni Mahakama ya juu kabisa. Wanakiri kwamba walioweza ku-*manage* ni *a number of villages* sio *all of the villages.* Ndiyo maana nashukuru tu kwa maana ya Mheshimiwa Ole-Medeye*.* Nashukuru sana. Wananchi waliokuwepo pale ni watu wazima, tofauti na maeneo mengine ya uvamizi, unaona ni vijana vijana tu wamekuja juzi. Naomba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini kesi ambayo ilikuwa inahusu watu takriban 1,000 ikaamuliwa *on technical grounds* kwamba linapokuja suala la ardhi, hatuangalii suala la *representative's suit* hairuhusiwi. Ikiwa ni Mahakama ya Rufaa *Court of Appeal,* haki za maelfu za wananchi zikaminywa *simply because* kwa uelewa wao labda mdogo waliamua wenzao 13 wakawakilishe Mahakamani na kati ya wenzao 13 waliokwenda kuwakilisha Mahakamani *still* walishindwa kuthibitisha wanne kati yao kwamba walilipwa fidia. Kwa hiyo, naomba Waziri asiwe mkali, naomba mtumie busara. Nawaombea wapiga kura wangu. Najua kuna haki imeminywa sehemu. Najua kuna *interest* za watu zinataka kuwaumiza watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia wanataka kuhamishiwa Mabwepande. Sisi hili hatuliafiki. Tunajua eneo la kiwanda ni kubwa. Wakitaka kujipanua wataacha chenji. Tunaomba muwasaidie wananchi na niwaambie kwa hili, maana Madiwani wa Kata hizo mbili ni wa CCM. Moja, tumesema iwe jua, iwe mvua, sisi tutakufa na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatufanyi uchochezi. Lakini nadhani natumia lugha laini sana. Ukienda Chasimba mwenyewe, sijui! Ole Medeye, tulikwendanae na anajua zaidi, naomba tuwasaidie wananchi wetu. Kuna siasa hapa, kuna vyama vyote viko kule, tuweke utu kwanza; eneo lipo la kutosha, la msingi ni kwenda kufanya vikao na wananchi, kujua eneo la kiwanda liko wapi, wananchi wanaweza wakakaa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, hivi viwanja 20,000. Kunakuwa kuna tatizo kwamba, Wizara kwa nia njema kabisa mnaandaa miradi mbalimbali. Lakini tatizo ni kwamba, miradi hiyo haimilikishwi kwa wananchi ili waweze kujua viwanja vya wazi ni vipi? Viwanja vya shule ni vipi? Viwanja vya huduma za jamii ni vipi? Matokeo yake viwanja hivi vimegeuka kuwa sehemu ya Wenyeviti wa Mitaa kupata kula yao! Kwa hiyo, naomba katika miradi yoyote ambayo mliifanya, mwende mkai-*review,* muangalie maeneo ya wazi, maeneo ya umma ni yapi? Myafanye yawe wazi, ili wananchi kwenye maeneo hayo wawe walinzi wa ile rasilimali. Bila kufanya hivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sheria haitambui kama Mwenyekiti wa Mtaa, anaweza akagawa eneo, lakini nitakwambia huko Dar-es-Salaam, wanagawa kwa kwenda mbele! Wakati nyie mnatoa maagizo huku, Wenyeviti wa Mitaa na baadhi ya Madiwani ambao sio waaminifu wanaendelea kuuza maeneo kwa kushirikiana na watu wa Manispaa ambao sio waaminifu. Kwa hiyo, naomba haya myaangalie kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa na ambalo pia sio la muhimu, ni viwanja vya wazi Mkoa wa Dar-es-Salaam. Tunajua mna changamoto kubwa kwa sababu, wengi ambao wamewahi kupewa hayo maeneo ya wazi, hususan katika maeneo *strategic,* ni wakubwa! Wengine wamejenga ma-*bungalow* yao! Sasa naomba leo mtuhakikishie wakati mnahitimisha, ile

taarifa iliyotolewa na Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Lukuvi, mtaitekeleza kwa ukamilifu wake na ndani ya kipindi gani? Nakuhakikishia Mheshimiwa Tibaijuka, ukiniahidi hilo nitakuona kweli wewe ule moto wako unaendelea. Ukiwa unasitasita nitajua yale ambayo yanasemwa, ulianza kwa *speed* wenzio wakakuminya! Tunakuamini mama, namwamini Mheshimiwa Naibu Waziri sana kama ambavyo namwamini yeye sana, hii sekta ndio uhai wa nchi. Hii sekta tukiipuuza na naiambia Serikali, tukiipuuza watoto wetu, wajukuu zetu watakuja kuchinjana na hatutaki tutengeneze Tanzania ya kuchinjana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii. Lakini pengine nianze tu kwa wasiwasi wangu na niombe hasa Kiti, Naibu Spika na Wenyeviti, kulinda Kanuni Namba 64, ambayo inatamka: “Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli; lakini Kifungu cha (g) kinasema, Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine”. Inawezekana ukawa na hasira kweli, jambo limekuudhi, lakini mstahi mwenzako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Mary Nagu, ni mtu mzima kwa mwanangu pale, Mdee! Lakini anapoamka akamwambia, sikukubali na yeye ni Waziri, haipendezi! Nafikiri twende kwa nia hiyo, tujenge kwa pamoja, kila mmoja ana nia nzuri ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu kubwa moja, kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu, aliniwezesha kutumikia mihimili hii mikuu miwili. Nimekuwa Mbunge kwa miaka 10, nikaondoka kwenye Ubunge nikaenda kutumikia mhimili unaoitwa Serikali. Leo wananchi wa Lushoto, wameona wanirudishe Bungeni. Napenda kusema kweli kweli kwamba, naunga mkono hoja kwa sababu, mengi tunayoyazungumza hapa ni kwa sababu hatuko katika huo mhimili wa pili, mhimili wa Serikali, rahisi kusema lakini kutenda sio rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze ninavyoona matatizo na migogoro iliyopo kutokana na uzoefu wangu, kwa kifupi sana, baadaye nitazungumzia Jimbo, maana nina hiyo migogoro. Ni ukweli kwamba, tunalo tatizo sasa hivi katika suala hili la ardhi, migogoro mingi ambayo ni ya zamani, inatokana na utaratibu uliokuwepo hapo nyuma wakati mashamba yalipotaifishwa na zikaundwa taasisi za Kiserikali zikashindwa, baadaye mashamba yale yakauzwa au yakabinafsishwa. Haya kuyabadilisha kwa hati zile ni lazima utumie Sheria Namba 4 ya 1999. Sheria ile inataka Kanuni na haki itendeke na inahitajika kulipa kitu kinachoitwa *compensation* na kinaleta migogoro mikubwa kwa upande wa Serikali! Hapa nashauri, busara zitumike sana, kushauriana na walionunua mashamba, kukaa vizuri na kuona ni wapi wameshindwa kutekeleza, maeneo yale ambayo wameshindwa kuyadhibiti basi yatwaliwe ili yapelekwe kwa wananchi, hiyo itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili ndio huo ninaokuja nao, ni utaratibu wa mfumo uliopo sasa katika Wizara yetu ya Ardhi. Ni ukweli kwamba, Wizara hii ni Wizara mtambuka, lakini watumishi walioko katika eneo hili, wanawajibika katika maeneo mengi, wanawajibika *TAMISEMI,* wanawajibika Wizarani! Sasa imekuwa mfano wa mtoto anayelelewa na babu. Mama ni Wizara au aliyezaa mtoto ni Wizara ya Ardhi, lakini analelewa na babu ambaye ni *TAMISEMI.* Kwa hiyo, matokeo mtoto huyu akifanya madudu kule huyu mama anashindwa kumdhibiti! Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili kwa undani wake. Jinsi gani katika hizi Wizara ambazo ni *technical,* Wizara ya ardhi, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, itakavyoweza iweze kuwa Wizara yenyewe inayohusika na sekta, iwajibike katika kuwadhibiti watumishi wasiotii taratibu. Na *TAMISEMI* itumike katika kupeleka mapendekezo au kuwapeleka wale wasiohusika katika maeneo, ili watu wasionewe na watumishi wasifanye madudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wangu, najua kabisa kama Mkuu wa Mkoa, malalamiko yaliyosemwa Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Mtwara na nilikuwa ni sehemu muhimu sana ya kutatua matatizo hayo. Namshukuru Mungu kwamba, hakuna mtu ambaye amefariki katika utawala wangu, niliweza kudhibiti, tukakaa tukazungumza tukaelewana, naomba Serikali iwe na busara ya kuelewesha wamiliki na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika maeneo yanayonihusu kwa kifupi tu. Mabaraza ya Ardhi, kwa kweli yadhibitiwe na naomba Lushoto, lianzishwe Baraza la Ardhi. Kama unataka ujue ukoloni wa Ardhi ulianzia wapi, ni Lushoto. Sisi wakati wa uhuru hatukuwa na eneo! Watu waliondolewa katika maeneo yao, Wazungu wakachukua maeneo yote mazuri kwa kulima kahawa, kulima chai, sisi tukatupwa huko nje. Bahati nzuri, marehemu Mheshimiwa Kawawa, kwa mara ya kwanza utaifishaji wa ardhi ulianza 1961 Lushoto. Mashamba yale yalitwaliwa wakapewa wananchi, ndio tukawa kidogo tuna nafuu. Kwa hiyo, Baraza la Ardhi haliko Lushoto na tunalo tatizo la ardhi! Tunaomba sana suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mikataba. Nashauri ili tusipate matatizo, wale wote waliopewa ardhi na wakashindwa kuitumia, kipindi kikifika wanyang'anywe ardhi ile kwa sababu wameshindwa. Kwa sababu, watu wengine wanahodhi ardhi kwa manufaa yao, ili waje wauze baadaye. Sasa nafikiri Sheria ni lazima idhibitiwe, nashukuru kwamba sasa mnaunda hawa *Land Rangers,* lakini *Land rangers* hawa wapewe mamlaka ya kisheria kutoa taarifa na wanaoshindwa kuendeleza ardhi itwaliwe ili iendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kabla muda haujakwisha. Najua nina mengi ya kuzungumza, nije Lushoto. Kama nilivyosema, Mji wa Lushoto na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla wakati wa uhuru ilikuwa imevamiwa na mabepari wa ardhi, lakini kwa bahati nzuri Serikali ikaliona hili kama hatari na ardhi ikarejeshwa kwa wananchi. Sasa nije katika tatizo ambalo ninaliona dogo, Mheshimiwa nimekuandikia barua, nakala nimemwandikia Waziri Mkuu, nimekuandikia wewe nakala, ni tatizo dogo lakini lina historia ngumu ambayo itawachefusha moyo wananchi wa Lushoto. Hawajawahi kujitokeza kuandamana kudai haki zao, lakini sasa wanatishia kufanya hivyo na nisingependa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lushoto ni mji mdogo, hatuna ardhi! Mwaka 1999/2000, mimi nikiwa Mbunge wa Lushoto, nilisimamisha ugawaji wa viwanja kwa kushirikiana na Serikali katika eneo la Hospitali. Baada ya kusimamisha ukaja mgogoro mkubwa, ilibidi Naibu Waziri wakati huo ndugu Mudhihir, aje Lushoto; akashindwa, akaja Waziri mwenyewe Cheyo, alipofika Lushoto kweli akaona umuhimu wa kuhifadhi ardhi ile kwa ajili ya Hospitali, upanuzi wa Hospitali! Ardhi ile ikahifadhiwa, lakini kwa busara zetu tukaona ni vizuri wananchi wale ambao wamenyang'anywa ardhi tuwape eneo lingine. Mimi kama Mbunge, nikaenda kwa Waziri wa Maliasili, Mama Zakhia Meghji, nikamwomba akakubali kuachia msitu ulioko pale karibu na Mjini Lushoto, ili upimwe wananchi wale wapewe fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya kipindi changu kikaisha. Sasa sielewi ni kwa sababu gani, maana walinifuata wenyewe, baba rudi kwa sababu tunaamini utatusaidia. Kipindi kile kilipokwisha, viwanja vile vilipimwa; mwaka jana viwanja vimeanza kugawanywa. Wananchi wale walionyang'anywa maeneo yale ambayo kwa kweli Serikali kwa uchungu ilibidi watoe msitu ule tuupime, wakanyimwa ardhi! Sasa hapa niseme nini? Kupata eneo lenyewe Lushoto kulipima ni kazi kubwa! Kwa sababu, maeneo yote yamemilikiwa na watu na maeneo mengi ni misitu ya Serikali! Unapima wapi? Wananchi wale wamenyimwa! Kwa bahati mbaya sana Mkuu wa Wilaya, ambaye ndiye anayesimamia haki za watu hawa, ndiye anayekwenda kuungana kusema kwamba, ataunda Tume! Wakati na yeye amepewa kiwanja pale! Wananchi hawa watatendewa haki vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge mzoefu, Mbunge wa zamani na Mzee pia, wananchi walipoomba waandamane, nimewaambia hapana! Ngojeni nitafanya jitihada mpewe haki zenu! Sasa naomba kwanza tutengue ugawaji ule wa viwanja. Najua Wilaya na Halmashauri zinapaswa kufanya, lakini mimi naweza kusimamia. Wale wananchi walionyimwa haki yao, wapewe tuepushe migogoro hii ya kuichukia Serikali yetu kwa sababu zisizo za msingi. Mimi ni mmoja wa watetezi wakubwa wa Serikali ya *CCM,* uwezo tulionao ni mkubwa sana, dhamana na heshima tuliyopewa ni kubwa sana, Watendaji wasipoangaliwa, watatupeleka pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuangalie utendaji. Matatizo mengi yanayotokea leo ni yale ambayo yanafanywa na watendaji. Tunaposema hatua za haraka hazichukuliwi kwa watendaji hawa! Matokeo yake wananchi wanakosa matumaini, wananchi wanaamua

kujichukulia sheria, tusifike huko, wana imani na sisi, tuwatendee mema, tuwafanyie yale wanayotaka kwa uangalifu, busara zitumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatusemi watu wasiwe na mamlaka ya kugawa ardhi, lakini haki itumike. Aliyenyimwa aangaliwe, aliyenyang'anywa aangaliwe kwanza! Na Kanuni na Sheria ndivyo zinavyosema. Lakini unakwenda unamnyang'anya, unampa mtu mwingine, tena kwa kumtafuta! Kwa nini mwananchi asiamini umepewa hongo na ni kwa nini tufike huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Maafisa Ardhi, Wakuu wa Wilaya, naomba sana, mambo haya yametendeka katika maeneo yao, wayaone na watende haki. Migogoro mingi tunayoipata leo ni kutokana na kutoangalia misingi ya tatizo. Mara nyingi tatizo linaanza pale ambapo wananchi wanaona wanaonewa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na jazba zote tulizonazo, naomba Bunge hili tuwe kitu kimoja. Ni ukweli kwamba, bajeti ya Waziri ni ndogo, nashauri kwa mfano, ili tuwe na *Land Bank,* wakati nikiwa Mkuu wa Mkoa, tuliomba tutenge maeneo. Lakini kwa Sheria ile Namba 5, huwezi kwa sababu kwanza hujajua maeneo yapi, hayana watu! Maeneo ya wapi ni ziada! Utatengaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwanza Wizara hii ipewe hela za kutosha. Vijiji vipimiwe maeneo yao, wapewe ardhi ya kutisha, maeneo ya ziada yaliyozidi yageuzwe yawe ni *Land Bank!* Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wizara, wakishirikiana na Wizara, wasimamie hiyo *Land Bank* na wao wasije wakaingia huu ugonjwa wa kuiuza wakishirikiana na Wizara. Ili Mwekezaji anapokuja anaelekezwa kwenye maeneo tuliyo na hakika yasiyo na migogoro. Hivi sasa tunampa tatizo kubwa sana Waziri wa Uwekezaji, huwezi ukawekeza bila ardhi! Huyu Waziri, kazi yake itakuwa ni nini sasa? Maana watu watakuja watatafuta, kinyume chake tunakuja kutukanana hapa! Wewe una hekari 24,000, hatuna uhakika, mwingine anasema nina hekari 80! Sasa ipi ni ipi? Lakini tungekuwa tunaitambua ardhi, hata kama mwekezaji akija ataelezwa na atapewa bila migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi duniani Waheshimiwa Wabunge, inaweza kuendelea bila uwekezaji! Haiwezekani jamani, tusidanganye! Duniani kote *experience* imeonesha kwamba, unapokuwa na uwekezaji unajenga tabaka la kati. Unapokuwa na tabaka la kati, ndio unalipandisha liweze kulipa kodi. Tabaka hili ndio litakaloendesha uchumi wa nchi. Sasa hawa hawatakuja kuwekeza kama ninyi hamuwapi mazingira ya ukarimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda pale Kiru, wale waliyapata mashamba yale kwa utaratibu waliopewa na Serikali yetu. Lakini leo hawawezi kuwekeza kwa sababu, wana wasiwasi! Lakini tunashindwa nini kuzungumza nao? Tukawaambia wale walioshindwa, nimeweza kugawa karibu hekta 1,600 kwenye mashamba kule walikoshindwa! Basi juhudi zile ziendelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nikushukuru sana na naunga mkono hoja, mpeni hela Waziri, akafanye kazi. *(Makofi)*

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Nichukue fursa hii kuipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla, kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kidogo kushangaa kwamba, Wizara hii imepewa bajeti kidogo kulingana na majukumu, Wizara hii iliyonayo. Wote tunakubaliana kwamba ni Wizara mtambuka ambayo inaingiliana na Wizara zote. Sasa kama mambo hayajakaa vizuri katika Wizara hii, hata hiyo, Wizara ya Ujenzi, itapitisha wapi barabara kama upimaji na shughuli muhimu zinazohusiana na kuelekeza maeneo hazitafanyika. Ni wazi na ningeomba kwamba, Serikali iangalie upya ni namna gani itaboresha bajeti ya Wizara hii ili na Wizara nyingine zinazoshabihiana katika utendaji na zenyewe zikae katika mstari unaokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie migogoro mbalimbali ambayo inatokana na utendaji katika Wizara hii. Tunafahamu kabisa kwamba, ardhi ndio rasilimali pekee Mungu

aliyowapa wananchi wote na ndio rasilimali pekee ambayo kila mwananchi ana uwezo wa kujivunia. Wakati tunaiangalia *National Cake,* cha msingi kabisa ambacho kila Mtanzania amepewa ni ardhi, *regardless* iko wapi na ina thamani kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migongano mingi kuhusu ardhi. Ndio maana hata tukiwa hapa Bungeni, maswali ya ardhi pamoja na kulipa fidia hayatakwisha. Hata kama tutatumia Sheria ya mwaka 1974, anayoizungumzia sana Mheshimiwa Magufuli, bado migogoro na madai ya ardhi hayatakwisha baina ya wananchi na Serikali yao. Hili linaelekea kuwafanya wananchi kuichukia Serikali yao pasipo na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwamba, tuangalie upya utaratibu mzima wa ardhi. Tunapokwenda katika miradi tunatumia pesa nyingi sana kulipa fidia. Mradi bilioni 10 utasikia bilioni tatu mpaka nne, zimetumika kulipa fidia. Kwa nini fedha tusizitumie kupima maeneo ya nchi yetu kwa ujumla wake. Kukawa na *master plan* ya nchi inayo-*take care* vijiji, inayo-*take care* miji ili hata mwananchi wa kawaida hata kama anajenga nyumba yake ya nyasi anajua barabara itakuja kupita pale, ataigeuzia barabarani na siku ya mwisho hata mwekezaji akija atafaidika kwa sababu atauza shamba au kiwanja ambacho kiko katika mpangilio. Tuachane na kulipa fidia, kulipa fidia leo na kesho na keshokutwa, tukiwa na *master plan* wananchi watajifiti katika *master plan* hiyo na ndiyo maana tunapoteza maeneo muhimu ambayo yangekuwa ni madhali kubwa ya Mji wa Dar es Salaam kama vile Kimara na Mbezi, hakika kungekuwa na *master plan* ya barabara leo hii ule ungekuwa ni mji ambao kila mtu angekimbilia kwenda kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika Jimbo langu, Jimbo la Kibaha Mjini ni mji unaopanuka lakini pembezoni bado kuna watu waliohodhi mashamba makubwa na wamekuwa wakiacha mashamba haya, sasa yamekuwa ni mashamba pori, yaani mashamba yasiyohudumiwa na matokeo yake yamekuwa yakileta athari kubwa kwa wananchi. Mwananchi aliye na eka yake moja analima mhogo wanyamapori ikiwa ni pamoja na ngedere na nguruwe mwitu watakula nusu ya eka watamwachia angalau hiyo eka moja ndiyo atakayoambulia katika eka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara ichukue hatua madhubuti kuhusu hawa watu wanaohodhi mashamba haya makubwa lakini hawataki kuyahudumia. Naamini katika uwekezaji wa mashamba kwa maana ya *microeconomy* ili wakulima wadogo wadogo waweze kufaidi huu uwekezaji mkubwa katika mashamba. Lakini nadhani kuweka mashamba makubwa kuanzia ekari 20 mpaka 200/300 bila kuzihudumia na kufuga wanyamapori. Niiombe Wizara itumie sheria na mkono wa Serikali kuwalazimisha watu hawa aidha, wahudumie mashamba haya au wayarudishe ili wananchi waweze kugawiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu mwaka huu peke yake watu wawili wamekwishauawa na chatu kwa ajili ya haya mashamba pori. Kwa hiyo, tufike mahali tukubaliane kwamba na Serikali itilie mkazo jambo hili ili wananchi wangu waweze kufanya kazi kwa amani na nina imani si kwa Kibaha pekee bali kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Kibaha Mjini hususan Kata ya Tumbi, Mtaa wa Mwanalugali, wananchi walichukuliwa ardhi yao ikapimwa na wakasimamishwa kufanya shughuli yoyote kwa ajili ya maendeleo. Hii ni takriban miaka 12 iliyopita nazungumzia mwaka 1999 kabla hata ya Mji wa Kibaha, hadi leo ni wachache waliopata fidia na wenyewe wanadai mapunjo. Lakini walio wengi hadi leo hawajalipwa fidia na hawawezi kuendeleza yale mashamba kwa takriban miaka 12 na sasa ule unakuwa ni mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara husika ichukue hatua za makusudi kukutana na kumaliza tatizo hili ambalo limekuwepo kwa zaidi ya miaka 12. Nimwombe Waziri husika aniahidi katika ku-*wind up* bajeti yake hii kwamba ni lini atakuja kukutana na hao wananchi wanaolalamika kwa takriban miaka 12 na kuona ni namna gani atatusaidia ku-*solve* matatizo haya niliyoyazungumza ikiwa ni pamoja na mashamba pori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Wilaya ya Kibaha Mjini na Bagamoyo, kuna mgogoro wa mpaka katika maeneo ya vikawe, kibao cha mpaka kimekuwa kikisogezwa kila mara na kila

upande unamlaumu mwenzake. Sasa nimeona niliseme hili ili Wizara husika iweze kulichukua na kulifanyia kazi maana usipoziba ufa mwishoni utajenga ukuta. Sasa tufike mahali tukubaliane kwamba mipaka hii ya Mikoa na Wilaya inafanyika katika utaratibu gani wa kudumu ili kuondoa matatizo haya madogo madogo yanayoweza kutuletea migogoro ndani ya Wilaya zetu. Nimwombe sana Waziri mwenye dhamana ahakikishe analipa kipaumbele hili la kuhakikisha kwamba siku moja ataitembelea Kibaha Mjini ili tushirikiane kuondoa migogoro hii na matatizo haya yamekuwa yakijitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba shirika letu la *National Housing* limeanza kupata mafanikio makubwa chini ya *management* mpya. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi Mkuu pamoja na timu yake kwamba wameanza kufanya kazi nzuri. Mimi ni mfanyabiashara na nina imani kama unataka kazi ifanyike mpe nafasi meneja wako afanye kazi lakini umpe malengo na wewe uwe na kazi ya kumhoji kulingana na yale malengo uliyompa. Lakini kama bado unamkamata shati bado utakuwa unamshika katika utendaji siku ya mwisho utakapomuuliza mbona hukufanikiwa atakwambia lakini si ulinishika shati, ningewezaje kushinda mbio hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba, Shirika la Nyumba lipewe nafasi, ila lipewe sera inayokubalika na inayokidhi matakwa ya Watanzania wenye uwezo na wasio na uwezo. Lakini wapewe nafasi watumie rasilimali walizonazo za nyumba hizi walizonazo ili kuendeleza matarajio ya wananchi wa Tanzania katika nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikubaliani kabisa na mchangiaji wa jana aliyekuwa anasema nyumba za Dar es Salaam zilizokaliwa kwa muda mrefu basi ziuzwe kwa bei rahisi kwa wale wakazi wa hizi nyumba. Nakataa kwa sababu nafahamu nyumba hizi zimejengwa kwa kahawa, nyumba hizi zimejengwa kwa pamba, zimejengwa kwa chai enzi ya Mwalimu. Sasa iweje leo watu wachache wapewe kwa bei rahisi iliyo chini ya soko na kama basi unataka kuwauzia nyumba hizi, tuwafikirie wale wanyonge ambao hawana hizi nyumba za *National Housing*, ziuzwe kwa bei ya soko na pesa zitakazopatikana zikajenge nyumba za bei nafuu kwa ajili ya wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo namna pekee ya ku-*distribute wealth* kutoka kwa wale walionacho kwenda kwa wale wasionacho katika ujenzi wa nyumba kupitia Shirika letu la *National Housing*. Hizi nyumba hata wakiuziwa kwa bei rahisi tayari ziko kwenye *prime area*, hata wakiuziwa kwa bei rahisi haitapita mwezi wao watakuwa wameshauza kwa mamilioni ya pesa. Kwa hiyo, hatuoni ni namna gani itakuwa ni *distribution* ya keki kwa ajili ya Watanzania wote. Kwa hiyo, naliomba hili liangaliwe na naomba sasa hata matumizi ya kuuza kwa kiasi kikubwa yatoke kwenye shirika, menejimenti ya shirika ili siku ya mwisho wakikosea tuwaulize. Siku moja ndugu yetu Mchechu tumwite, tumwambie ulituahidi *a, b, c, d* lakini mbona umefanya vingine. Lakini ikiwezekana hata kama amefanya makosa yaliyo wazi kupita kiasi hatua zichukuliwe, lakini kama tutaendelea kumshika mkono tutaishia kwenye mashirika mengi ambayo yameendelea kuitia Serikali yetu aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuizungumzia sasa Wizara ya Ardhi katika suala muhimu la uwekezaji wa mashamba makubwa, naunga mkono uwekezaji mkubwa, tunapinga u-*settler* lakini sijui tunapinga wapi u-*settler* huu, kwa maana sasa tuko katika *capitalism economy* kama tunasema watu wawekeze kwenye viwanda vikubwa vya mabilioni ya pesa, kwanini tusiwekeze katika kilimo katika mabilioni ya pesa na maelfu ya ekari. Lakini ninachokiomba mkulima mdogo aliyekutwa katika eneo hilo alindwe na wale wawekezaji katika mashamba watuambie ni namna gani wale wakulima wanaozunguka mashamba watafaidika na uwekezaji huo. *Outgrowing* ni njia nzuri kwa sababu yule mwekezaji ataweka kiwanda kwa ajili ya ku-*process* na ku-*add value* katika mazao na wale wadogo wadogo hawana uwezo huo, sasa uhakikishe kuna utaratibu ambao unamlazimisha mwekezaji yule, kuchukua mazao kutoka kwa wakulima wadogo kwa bei ya kuridhisha na kuendelea kuya-*process* ku-*add value* na kwa faida ya wale wakulima, kwa faida yake kama mwekezaji na kwa faida ya Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hivi kama kweli tunataka kilimo cha kisasa hatuwezi kukwepa u-*settler*, hatuwezi kukwepa u-*settler*, lakini u-*settler* huu sasa siyo kama ule wa kikoloni ni u-*settler* kati ya mwekezaji na mwananchi mzalendo Mtanzania hilo ndilo jambo muhimu

ambalo nataka Serikali kuhakikisha si kwa wale wawekezaji peke yao ni pamoja na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja *provided* Waziri atatoa majibu sahihi ya haya yote niliyoyaomba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha, utupelekee salaam Kibaha Tumbi, Kibaha Mwalugayi..

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Zimefika Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Kibaha Mkoani, Kibaha Maili Moja, Kibaha Picha ya Ndege, Kibaha Boko, Kibaha Mkuza, Kibaha kwa Matias… *(Kicheko)*

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Inaelekea Mheshimiwa na wewe una mashamba pori nitakuangalia vizuri. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, nilisoma shirika la elimu Kibaha. Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa ambao walitaka kuchangia hoja hii ambayo bado hawajapata nafasi mpaka sasa hivi ni 38. Kwa hiyo kwa vyovyote vile kama hujapata nafasi usiione kama meza hii ina sababu na wewe au vipi, hapana, kwa sababu muda wenyewe hautoshi jambo la ardhi ni jambo linalowahusu wananchi wetu ambao tunawawakilisha, linaonesha uzito na unyeti wa jambo lenyewe kwa maisha ya watu wetu.

Katika kumalizia niseme neno dogo tu, Sheria yetu ya Ardhi ya Vijiji kwa nia njema kabisa ilitoa mamlaka na inatoa mpaka sasa kwa Serikali zetu za vijiji na wananchi katika vijiji kumiliki ardhi yao na kuigawa kwa matumizi mbalimbali kadri wanavyoona inafaa. Lakini kwa kweli sheria hii katika baadhi ya maeneo imetumika vibaya kwa kweli, mtendaji wa kijiji anagawa maeneo anavyotaka, wale wajumbe wa Serikali ya Kijiji wale 25 wanagawa maeneo kuliko hata ile *limit* waliyopewa, wanagawa eka mia moja, mia mbili au mia tatu hata mia tano. *(Makofi)*

Ni jambo ambalo kwa kweli tunapigia kelele wageni wanaokuja katika nchi yetu, lakini hatuangalii wenyewe huku ndani, jinsi ambavyo baadhi ya watu wanavyokwenda kurubuni hizi Serikali za Vijiji kwa kutumia mamlaka waliyopewa Serikali za Vijiji ya kugawa ardhi yao kwa kweli Wilaya hata kama ya kwangu Kongwa, Kilindi, Kiteto sasa hivi ni Simanjiro ni ufyekaji ambao haujapata kuonekana katika nchi yetu, mkubwa sana na uharibifu mkubwa wa mazingira kutokana na *loop* hii, Mtendaji wa Kijiji tu anachukua madaraka anafanya anavyotaka au Serikali ya Kijiji, sasa mtawafunga wote 25, haiwezekani haya madaraka tuliyowapa tuweke *checks and balances.*

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru tutakaporudi saa kumi kamili jioni tutaanza na majibu ya upande wa Serikali kwa kuanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu tutaendelea na utaratibu wetu kama kawaida. Kwa jinsi hiyo kadri tulivyojipangia kwamba shughuli zetu zinakwisha saa saba na robo. Sasa naomba kuchukua fursa hii kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni ya leo, CCM mkutane pale mnapotakiwa kukutana.

*(Saa 07.13 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa10:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi yao nzuri kwa kujenga nyumba na kuweza kuwapunguzia wananchi wetu upungufu wa makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali kwamba sisi Wabunge tuliopo hapa Dodoma, basi tupewe kipaumbele cha kukopeshwa nyumba kwa ajili ya makazi yetu. Tunapata shida, wengi wetu tunaishi uraiani ambapo hata usalama wetu ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuishauri Serikali kwamba wananchi wapewe kipaumbele katika kumilikishwa ardhi kwa ajili ya kilimo na makazi. Inasikitisha sana kuona Mtanzania anakodi ardhi ya nchi yake kwa Mwekezaji ili apate kulima na kuendesha maisha yake. Naiomba Serikali kwamba hali hii ikomeshwe mara moja, na pia kama kuna viongozi ambao wamemilikishwa ardhi kubwa, basi hata kama wanaitumia kwa kilimo, basi igawiwe kwa wananchi ili nao wafaidike na ardhi ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali kwamba watu wote waliokodishiwa nyumba na Serikali au kuuziwa na Serikali, basi iwe ni mara moja tu na isiwe zaidi ya moja. Hili litapelekea kuzuia matajiri wasizihodhi hizi nyumba peke yao ili wafaidike Watanzania wote ambao wanataka kukodi au kununua nyumba hizi za Serikali.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yake kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango iliyoelezwa yote inatekelezeka. Ninaamini chini ya usimamizi wake, malengo yatafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la ardhi katika Jimbo la Mlalo. Lipo shamba la Katani la Mnazi katika Tarafa ya Umba. Shamba hilo liliuzwa kwa raia wa Kenya. Mpaka sasa wananchi wanauliza, ilikuwaje shamba hilo likauzwa kwa raia wa nchi ya kigeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo yako kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mbozi Magharibi eneo la Mji mdogo wa Tunduma pamekuwepo na mgogoro wa wananchi kunyang'anywa maeneo yao (ardhi) pamoja na maeneo ya biashara na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na kuwapa watu binafsi wenye pesa kwa ajili ya makazi. Hivyo, hali hii imesababisha sintofahamu kati ya wananchi na Halmashauri yao na hivyo, kutishia kuvunjika kwa hali ya usalama kwa eneo hilo na Taifa kwa ujumla, kwani ni eneo la mpakani kati ya Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipindi vya hivi karibuni, eneo la Tunduma kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari yaliyokosa maeneo ya kuegesha. Hivyo kwa wakati huu tunaiomba Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mbozi itupatie eneo kwa ajili ya uwekezaji hususan sisi kujenga bandari ya nchi kavu, itakayosaidia magari makubwa kupaki, hivyo kuipatia Halmashauri mapato pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka aliyowasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu yenye wakazi wapatao milioni 40 imejaliwa kuwa na hekta milioni 44 za ardhi inayofaa kwa kilimo, lakini ni asilimia 23 tu ndiyo inayotumika. Kuna hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo ni asilimia moja tu ndiyo iliyo chini ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iharakishe mpango wa kilimo cha umwagiliaji ili watumiaji wengi wa ardhi waweze kufaidika na kuondokana na adha ya umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina raslimali za kutosha zinazoweza kusaidia kuleta mabadiliko endelevu ya uchumi wa Tanzania na kuinua hali za maisha za wananchi. Pamoja na hayo, asilimia 34 ya Watanzania wengi wakiwa wale wanaotegemea Ardhi/Kilimo wanaishi katika hali ya umasikini. Asilimia 80 ya Watanzania hutegemea kilimo/ardhi kwa ajili ya kujiendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, bado migogoro mingi ya ardhi haitatuliwi kwa wakati. Nashauri Serikali iharakishe utatuzi wa migogoro ya ardhi. Migogoro mingi imekuwa mtaji kwa baadhi ya Maafisa wa ardhi wasio na uadilifu. Pia Serikali ipitie upya gharama za upimaji ardhi kwa ajili ya utoaji wa hati za usajili. Watumiaji wengi wa ardhi hawakopesheki na mabenki kwa ukosefu wa hati miliki ya ardhi ambazo wengine wamezaliwa katika maeneo hayo ya ardhi. Serikali ichunguze na viongozi, Maafisa wa Ardhi wasio na uadilifu wasimamishwe kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Seikali iandae hatua na taratibu za kisheria zitakazowezesha vijiji na wanakiji kutumia ardhi kama hisa kwa shughuli za ubia na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wa ardhi ya *KIA* hadi Kambi ya Makaa Wilayani Meru ambao kwa zaidi ya miaka 40 wametumia ardhi hiyo kwa ajili ya kilimo. Serikali imetoa taarifa kwao kuhamisha watumiaji wa ardhi zaidi ya wakulima 200 ili kutumia ardhi hiyo kama eneo la viwanda na hivyo kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wa ardhi ya *(KIA) Kilimanjaro International Airport* na Kambi ya Makaa Wilayani Meru wangependelea Serikali itoe utaratibu wa wao kutumia ardhi ambayo wameitumia zaidi ya miaka 40, waitumie kama hisa kwa shughuli ya ubia na wawekezaji watakaojenga viwanda katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia watakayopewa ya fedha itawaletea matatizo makubwa. Wapo watakaotapanya fedha hizo na hivyo badala ya kujinufaisha wao na familia zao; watakuwa wamerudi nyuma kimaendeleo; badala ya kuondoa umasikini na kupata maisha bora; itakuwa kinyume na umasikini utaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia Serikali iwafikirie wananchi wake, iweke utaratibu mzuri, ardhi waliyonayo itumike kama hisa ili watumiaji wa ardhi ya *KIA* na Kambi ya Makaa wafaidike na viwanda vitakavyojengwa katika maeneo hayo ambayo wameyatumia kwa kilimo kwa miaka mingi, kwa kufanya ubia na wawekezaji wa viwanda katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wa Wizara kwa utendaji mzuri wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kuwa katika Mkoa wa Mtwara kuna shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta ambao umeshaanza kutoa matumaini makubwa hasa Sekta ya Gesi, naiomba Wizara iisaidie Manispaa ya Mtwara na Halmashauri ya Mtwara katika kupanga Mji wa Mtwara na Vitongoji vya Mtwara/Mikindani na Halmashauri ya Wilaya ili kupokea uwekezaji mkubwa wa viwanda vinavyoendana na upatikanaji wa raslimali ya gesi, bandari asilia na malighafi nyingi muhimu kwa uendelezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Wizara ya Ardhi kujenga Ofisi ya kisasa ya Kanda ya Kusini Mtwara ili kumwezesha Msajili wa Hati Kanda ya Kusini Mtwara kuwa na eneo la kisasa na hadhi ya kuweza kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Shirika la Nyumba la Taifa kuwekeza katika ujenzi wa nyumba katika Mkoa wa Mtwara kutokana na mahitaji makubwa sana ya nyumba katika Mkoa huo hasa kutokana na wingi wa vyuo vilivyopo na vinavyojengwa kwenye Mkoa huo, kasi ya uwekezaji hasa katika Sekta ya Gesi na utafutaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa dhati kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri inayoonyesha maboresho katika sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naomba kutoa maoni, ushauri, na kupewa maelezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la tafsiri ya Sheria ya Ardhi Vijijini kwa lugha ya Kiswahili, natoa pongezi kubwa kwa utekelezaji huo wa mfano kwa Wizara nyingine za ziada katika ngazi ya Mabaraza ya Kata ambayo hayana kipato cha kutosha na kuendelea kutafsiri sheria na marekebisho yote ya Sheria ya Ardhi kwa Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migongano kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika juu ya kufutwa kwa hati za mashamba yasiyoendelezwa, napenda kusema kwamba Sheria ya Ardhi inatoa fursa na hatua za kutekelezwa ili kuwezesha kufutwa kwa Hati Miliki za Mashamba yasiyoendelezwa kwa muda mrefu. Wilaya ya Muheza imefuata utaratibu huo kikamilifu kwa mashamba ya *Kibaranga Sisal Estate, Mlingoti Sisal Estate, Lewa Sisal Estate Bwembwera Sisal Estate, Kihuhuri Sisal Estate, Kwafungo Sisal Estate, Songa Sisal Estate*, Kilapula na Azimio Ranchi Tanga Mwaka 2005/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, yafuatayo pia yamefanyika:-

(1) Aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alitembelea mashamba hayo na kuona hali halisi na kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuahidi kuwasaidia mara baada ya kufuata utaratibu wa kufutwa hati ili nao wapate ardhi;

(2) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Julai/Agosti, 2010 aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Muheza kwamba: “Ninafahamu malalamiko ya wananchi wa Wilaya ya Muheza kuhusu mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa na uhaba wa ardhi unaowakabili kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imetekeleza utaratibu wa kisheria kutaka hati za mashamba yasiyoendelezwa, zifutwe. Naahidi nitatekeleza hivyo kwa mujibu wa sheria na nitaanza na Shamba la Kibaranga na mengine kufuatia. Lile la Bwembwera tutalazimika kuangalia utaratibu wa kisheria kwa kuwa liliuzwa kupitia chombo cha Serikali.”

(3) Chombo cha Serikali *CHC (Consolidated Holdings Corporation)* ilipita katika mashamba hayo kuona hali halisi ya mashamba hayo katika Wilaya ya Muheza wakiwa pamoja na viongozi wa Bodi ya Mkonge, Viongozi wa Mkoa na Wilaya ya Muheza ili kusaidia Serikali kujua hali halisi ya kutoendelezwa kwa mashamba hayo na bila shaka wametoa taarifa yao.

(4) Kutokana na wamiliki halisi waliopewa hati halisi kutelekeza mashamba hayo kwa zaidi ya miaka 40 sasa, wananchi wanaoishi pembezoni mwa mapori ya mashamba hayo wameingia na kupanda mazao ya kudumu, kujenga na kuvuna kwa mahitaji ya maisha yao kwa zaidi ya miaka 40 sasa.

(a) Kwa kuwa wamiliki halisi wenye hati walitoroka na kuacha kuendeleza ardhi ya mashamba hayo na hata kutolipia kodi ya ardhi kwa mashamba hayo kwa muda wote huo (zaidi ya miaka 40): Je, bado wana haki ya kumiliki maeneo hayo licha ya ucheleweshwaji wa hatua za ufutaji wa hati zao?

(b) Je, hao wanaodaiwa kuwa wakulima wadogo waliojigawia ardhi ya mashamba hayo bila hata kushirikisha Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wameweza kupata hati mpya kabla ya hati halisi kufutwa na Mheshimiwa Rais kisheria?

(c) Je, kuna haki gani kuwapa ardhi wageni kwa jina la Wawekezaji wadogo na kuwaacha wananchi wazalendo na wazaliwa wanaoishi karibu na mashamba hayo ya mababu zao ambao sasa kutokana na ongezeko la watu, wana shida ya Ardhi?

(d) Wananchi 1,028 walioondolewa katika eneo la Hifadhi ya Msitu wa Derema - Amani Muheza, idadi hiyo ya wananchi ilikubali kuondoka katika eneo la hifadhi kwa ahadi ya kulipwa fidia kupitia Benki ya Dunia na Wizara ya Maliasili na Utalii. Ahadi ya fidia imekamilika, ahadi ambayo bado ni "Kupewa Ardhi". Ardhi iliyokusudiwa ni hekta 980 kutoka eneo la Shamba la *Mlingoti/Kibaranga Sisal Estate*. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilikwishatoa pendekezo hilo na kusubiri utekelezaji wake baada ya hati miliki ya ardhi kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuelewe kwamba Serikali inashiriki kukwamisha utekelezaji wa ahadi kwa wananchi hao. Lini sasa hati zitafutwa ili wananchi wenye shida ya ardhi wapate maeneo ya kujiendeleza? Wale wenye nia nzuri ya kuendeleza kilimo waweze kupata hati mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hotuba ya Mheshimiwa Waziri ingawa kiasi cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo alama ya Utaifa. Hakuna Taifa lisilokuwa na ardhi duniani. Kwa mantiki hiyo, Seirkali katika mikakati yake, ni vyema kuwa na sheria ambazo zitakidhi mahitaji na matarajio ya wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo chanzo cha vita duniani na migogoro pia ndani ya nchi yetu. Migogoro inakuja kutokana na umuhimu na uthamani wa ardhi yenyewe. Ardhi ni sehemu ambapo mtu anazaliwa, anakulia, anajenga nyumba, analima na kuwekeza na kupata chakula. Kwa mantiki hiyo ardhi ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mazuri Serikali imeyaandaa ikiwemo mipango ya kuyapima na kuyamilikisha kwa Watanzania. Tanzania ni nchi nzuri, hata hivyo tunapata shida kidogo kutokana na ongezeko kubwa la watu na shughuli za kibinadamu za kilimo na ufugaji, na matokeo yake tumekuwa tukishuhudia mapigano ya wakulima na wafugaji. Ili kukabiliana na hali hii, ni vyema kukawa na mipango maalum ya kuyapima na kuyatenda mahsusi kwa ajili ya kilimo na yale ya malisho kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la Hati miliki za kimila ni jambo la msingi sana hasa kwa wananchi walioko maeneo ya vijijini ambao kimsingi wanayo ardhi ya kutosha ambayo ikipimwa itakuwa inatambuliwa kisheria kwa maana ya Hati miliki za kimila. Sula hili lipewe kipaumbele na Wizara iendelee kusukuma kwa haraka kuzitaka Halmashauri za Wilaya kutenga fungu kwa ajili ya kujenga ofisi kwa ajili ya kuhifadhi majalada kwa ajili ya Masijala ili hatimaye mpango mahsusi wa Serikali wa Hati miliki za kimila na upimaji wa mashamba waweze kuyamiliki kisheria na kuwawezesha kupata mikopo benki kwa ajili ya kuweza kuwekeza katika kilimo na kupata maendeleo na kuifanya kauli mbiu ya Serikali ya Kilimo Kwanza ilete maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iwaangalie kwa makini watumishi walioko chini ya Wizara hii, na Mipango Miji iwaangalie na kuwapa miongozo waepukanae na tabia ya kuendekeza rushwa na hatimaye kusababisha migogoro isiyokwisha na hatimaye inaweza kusababisha maafa kwa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linafanya kazi nzuri, tunalipatia ushirikiano na kuitaka Serikali ifanye juu chini kuyalipa madeni inayodaiwa ili kulipa uwezo shirika kujenga nyumba zaidi na ikiwezekana kujenga nyumba za gharama nafuu na kuwauzia wananchi ili wawe na makazi nadhifu kwa gharama nafuu.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo inafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya pongezi hizo, ninalo ombi dogo, lakini la msingi sana. Naomba Serikali iweke utaratibu mzuri wa kutoa elimu kwa wananchi, waelewe umuhimu wa kuwa na Hati miliki ya maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Serikali ipunguze gharama za ushughulikiaji wa Hati hizo, kwani ni kubwa mno, mwananchi wa kawaida hawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Anna Tibaijuka - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu Waziri - Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye kwa kazi nzuri na kuisimamia vizuri Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kuwa uwazi katika uendeshaji wa Wizara hii umeongezeka na hata faili lako unaweza kuliona popote lilipo. Kwa namna ya pekee, nawapongeza jinsi ambavyo mnashirikiana. Kuna Wizara inasemekana Mawaziri hawapatani mpaka wa chini yao wanapata *chance* ya kuwasengenya na hata kuachiana majukumu inakuwa taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa na tatizo juu ya viwanja vya Jumuiya ya wazazi, tulifuatilia Wizarani na tulipomkuta Mheshimiwa G.J. Ole-Medeye, Waziri akiwa safarini Bukoba, alitusaidia sana kwa uwazi bila kusubiri kesho na tulipata majibu yote mara moja na kutuondolea usumbufu. Huu ndio utendaji unaotakiwa ili Wizara kuwa kiungo cha maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kutokuwepo wakati Wizara hii ikiwasilisha kwa mdomo. Wizara hii ni muhimu sana katika nchi, na ndiyo mhimili mkuu wa uchumi wa Watanzania. Bila ardhi, ni bure. Bila Watanzania kupimiwa ardhi zao, ni bure. Bila kuwa na upimaji mzuri wa maeneo yetu na kupanga miji kadri ya matumizi sahihi, ni bure, na ndio maana kero za makazi na kunyang'anyana viwanja, uchafuzi hauishi.

Swali langu ni kwamba: Kwanini Wizara hii bajeti yake hailingani wa kazi zake? Tunasema mtu ukiwa na nyumba unaweza kukopa, ukiwa na hati unakopesheka, mbona Wizara hii ina hivyo vyote lakini bado haikopesheki? Tatizo ni nini? Lakini siyo hivyo tu, tumegundua pia Serikali inachukua sehemu kubwa ya pato la Wizara hii na hivyo kuinyong'onyesha kwa kupewa bajeti kidogo. Je, kwanini Serikali isiwaachie pato leo ili wajitegemee angalau hata kwa miaka 10 tu ya kuanzia?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wizara zinawanyonya wenzao. Wao kazi yao ni kutumia na kuzalisha hasara na kutegemea kudai Serikali iwapatie hela zaidi. Hii haifai hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wizara zimepewa kuendesha raslimali nzito za nchi hii lakini zinatengeneza hasara tu kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili nimewaeleza mara nyingi katika michango yangu kuhusu kuwaacha watu kuishi katika maeneo maalum na mapito ya maji na hatarishi. Ni kitu gani kinawafanya mnaangalia ujenzi unaoendelea maeneo kama Jangwani, miaka ya 1980 maeneo yale hayakuwa na nyumba hata moja. Leo Bonde la Msimbazi lote limejaa nyumba, kesho yakitokea mafuriko, watu wakafa mtaunda Tume? Au itakuwa geresha tu? *Dumping sites* zipo wapi? Lakini pia katika upimaji wenu, kunakuwa hakuna *condition* za ujenzi *versus* aina ya majengo mfano tu, mwingine ghorofa, mwingine hoteli, mwingine kijumba kidogo jambo ambalo linatoa kero kwa *planners* wa huduma nyingine kama maji na umeme. Ni vyema kushirikisha wadau ili kuwa na mipango mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu, Waheshimiwa Mawaziri, nyie mbona hamtaki kutembelea Ruvuma? Sisi tuna taabu kuu ya mpaka wetu na Malawi.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kushukuru kuchangia kwenye Wizara hii. Mchango wangu unaingia katika hati za wamiliki wa mashamba ya Mkonge. Mashamba mengi yamekuwa misitu, hayaendelezwi. Kwa nini hati miliki ya hawa wenye mashamba yasifutwe ili wananchi wagaiwe mashamba haya? Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ugawaji viwanja kwa wananchi lakini Halmashauri hugawa viwanja mara mbili kwa wananchi na kuleta mgongano mkubwa sana kwa wananchi. Naomba Serikali kupitia Wizara hii, nipate majibu imechukua hatua gani kwa Watendaji hao ambao wanagonganisha wananchi. Kumekuwepo na shida ya baadhi ya wananchi kupewa maeneo na Serikali, baadaye wenye maeneo yao hurudi na kuwadhalilisha wananchi kwa kuwatoa sehemu walizopewa na Serikali. Ni kwanini wananchi wanaomiliki ardhi baadaye anapokonywa na kupewa watu wengine bila wenye ardhi kupewa malipo yoyote? Ni kwanini wanaomiliki nyumba za Serikali wakipewa muda wa kutoka ndani huwa hawataki kutoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba mengi ya Mkonge huwa hayalimwi na wamezuia mashamba mengi, naomba hati zake zifutwe mara moja ili wananchi wapewe sehemu za kulima.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni moja katika hazina kubwa, si kwa nchi tu, bali na raia wake (Watanzania).

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri kwa sasa wajikite zaidi kwa kutenganisha maeneo ya wakulima na wafugaji, hili ni bomu, na endapo tutaendelea kwenda kienyeji, basi siyo muda mrefu panaweza kutokeza tatizo na mapambano baina ya wafugaji na wakulima. Haya tunayashuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja na maeneo ya wazi, ni tatizo. Maeneo mengi mijini na vijijini yanavamiwa na ama wajenzi (matajiri) au Mawakala wa viwanja kuwauzia wafanyabiashara. Nawapongeza kwa kuweka utaratibu wa kutaka kuanzisha ulinzi wa maeneo na hili tunalishuhudia. Ninachotaka kutahadharisha kwenye utaratibu, ni lazima elimu ya kutosha itolewe, la sivyo, tutaunda mtafaruku baina ya walinzi ama Manispaa au Sungusungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, pawe na mpango mahususi utakaooanisha taratibu au uendeshaji, kama utakuwa wa moja kwa moja au utakuwa chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tunaiomba iendeleze taratibu zake za mipango miji na wazuie ujenzi holela na wajitahidi kwa sasa wahusika wapime viwanja katika miji inayokua kwa haraka kama vile Arusha, Moshi, Mbeya, Tanga, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haya yatafanyika, itaondoa mikusanyiko ya ujenzi holela mijini.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Tibaijuka, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole – Medeye, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina mambo mengi ambayo inabidi kufuatilia, hivyo fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hiyo ni ndogo sana. Migogoro ya ardhi, nyumba na hata Sheria ni mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro iliyopo ni mingi na pia tutarajie itaongezeka sana endapo hatutabadilisha baadhi ya sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wawekezaji katika ardhi linawapa wageni kuhodhi maeneo makubwa na kuacha wananchi (vijiji/Wazawa) kuuza na wao kuwa waajiriwa kwenye ardhi yao. Je, ni lini Serikali italeta sheria ambayo itamwelekeza Mwekezaji aingie ubia na wananchi (Wazawa/Vijiji)? Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata hofu baada ya kupitia hotuba ya Wizara ambayo imeonyesha zaidi ya vijiji 30 vilivyopo katika Wilaya ya Kisarawe na Rufiji Mkoa wa Pwani, vilivyoorodheshwa kwamba kuna maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Je, wananchi wanaoendesha shughuli zao katika vijiji tajwa watafaidika na nini au wamepewa kipaumbele gani? Je, walishirikishwa katika maandalizi ya kujua aina ya uwekezaji? Naomba nipatiwe majibu. Narudia Sheria ya Uwekezaji (ardhi) iletwe hapa ikiwa na maslahi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali itupatie ufumbuzi wa mgogoro wa mipaka ya msitu wa Kazimzumbwi na Kijiji cha Kimwani – Chanika. Kwanini Serikali ina tabia ya kuacha wananchi wajenge/kulima kwa muda mrefu bila ya kuwaondoa kwa taratibu stahili hatimaye kuwadhalilisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya maswali yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji makini. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kufuatilia kwa karibu ujenzi wa masjala za ardhi katika Wilaya. Lakini katika Jimbo la Bagamoyo tuna tatizo kubwa sana la mashamba pori na uvamizi wa ardhi. Katika Kata za Kerege, Zinga, Magomeni na Vigwaza kuna wananchi waliohodhi ardhi kubwa sana na kuacha ardhi hiyo bila kuiendeleza kwa miaka zaidi ya 15, na kusababisha malalamiko makubwa kwa wananchi ambao hawana ardhi ya kulima. Baadhi yao wanalima katika mashamba hayo kama Manamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Wizara isimamie mabadiliko ya umiliki wa ardhi ili ardhi isiyoendelezwa itwaliwe bila mlolongo mrefu sana. Kero za mashamba pori ni kubwa sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa tathmini ya ardhi na mali kwa ajili ya fidia pindi Serikali inapotwaa ardhi, haiko wazi/bayana. Wakati wa ujenzi wa barabara ya Bagamoyo - Msata, wananchi walilipwa fidia ndogo sana na wala hawakuelezwa wanalipwa nini. Hapakuwa na mchanganuo wa malipo kwa wananchi. Usiri ni wa nini? Mheshimiwa Waziri aagize tathmini ziwe wazi na wanaolipwa wajulishwe mapema au wakati wa malipo. Pia Mthamini Mkuu wa Serikali afuatilie kwa karibu taratibu za uthamini wa miradi yote mikubwa mikubwa. Inaelekea uonevu unatokea sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN. O. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Naibu Waziri. *Big-up*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwamba Wizara itatue haraka mgogoro wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la akiba la Liparambauko lina mgogoro mkubwa kati ya utawala wa pori hilo na vijiji vinavyozunguka pori hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Upimaji Ardhi wa Wilaya ya Mbinga anayeitwa Chipakapaka, hana uwezo, lawama pande zote. Hakuna hata nyumba moja kwenye Wilaya ya Nyasa yenye hati. Mtoeni haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iongeze juhudi. Naunga mkono hoja kwa waraka huu.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa kuanza kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika zoezi la ujenzi

wa awali wa nyumba 290 katika eneo la Medeli Mkoani Dodoma. Ni imani yangu kwamba ifikapo 2015 lengo la ujenzi wa jumla ya nyumba 15,000 litakuwa limekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ione haja ya kuondoa kodi katika vifaa vya ujenzi ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba hizo. Lakini pia Serikali iondoe kodi kwenye uuzwaji wa nyumba zinazotarajiwa kuuzwa na Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mantiki wala tija ya kuweka kodi ya asilimia 18 kwenye bei ya nyumba hizo. Hii ni kwa sababu vifaa vyote vya ujenzi wa nyumba vinatozwa kodi. Lakini pia kutakuwa na ongezeko kubwa la bei ya nyumba hizo. Hii haiwezi kumsaidia Mtanzania mwenye kipato cha kawaida kumudu kununua nyumba hizo. Nchi nyingi duniani hazitozi kodi kwenye vifaa vya ujenzi, lengo kuu ni kuleta unafuu wa gharama za ujenzi wa majengo mbalimbali, lakini pia kuweza kujenga nyumba bora na imara zaidi. Hivyo, ni lazima Serikali ijifunze kutoka kwa nchi zinazofuata utaratibu huo ili kulisaidia Shirika letu la Nyumba, lakini pia kuwasaidia Watanzania kupunguza gharama za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie suala la ardhi. Duniani kote, ardhi ndiyo raslimali namba moja katika kukuza uchumi, lakini pia kuendeleza nchi. Endapo ardhi itatumika vizuri na kwa mpangilio mzuri uliowekwa na Serikali itaondoa tatizo la umasikini wa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima, wapo wafugaji pia. Hawa wote wanatumia ardhi kama mtaji wao wa kuwapatia ajira ya kudumu, kujipatia kipato, kusomesha watoto, kujenga nyumba, kujipatia chakula na kadhalika. Idadi hii ya watumiaji wa ardhi inaongezeka kadri ambavyo idadi ya Watanzania inavyokua. Tumeshuhudia migogoro mingi sana baina ya wakulima na wafugaji wanaogombea ardhi. Hata migogoro ya mtu na mtu wanaogombea mipaka ya ardhi, migogoro hii itakwisha endapo Serikali itachukua hatua za makusudi na za haraka. Serikali sasa ni lazima ichukue hatua za kitaalamu kwa kupima ardhi yote nchini, kuipangia mipango ya matumizi bora, lakini pia kuimilikisha kwa wananchi. Ninaisihi Serikali kupitia Wizara husika iharakishe zoezi la upimaji wa ardhi ili kuweka bayana matumizi yaliyo sahihi ya ardhi kwa wananchi na kuondoa tatizo la migogoro ya ardhi. Watu wakipimiwa ardhi yao na wakamilikishwa itapunguza pia tatizo la umasikini kwa vile wataweza kuitumia kama dhamana ya kupata mikopo kwenye taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba Wizara itimize wajibu wake ili kuleta tija na maendeleo kwa nchi na Watanzania.

**MHE. AMINA A. CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itangulize huduma muhimu kama maji, barabara na umeme kabla Wizara haijaanza kutoa viwanja. Hii itasaidia pia kuwarahisishia sana wananchi wakati wa ujenzi na pia baada ya kutolewa viwanja wananchi waliopewa wataharakia kujenga kwa sababu huduma muhimu zipo na siyo kuhangaikiwa na wananchi au Wabunge wa sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara yako iwahimize Maofisa wasimamizi ardhi wasimamie vizuri na waangalie maeneo yaliyo wazi mara kwa mara ili yasivamiwe na pia ikiwezekana yawekewe mabango. Hii itasaidia pia ujenzi holela na kuvunjiwa wananchi nyumba zao kutokana na uzembe wa pande zote mbili upande wa wananchi na upande wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara iwapatie wamiliki nyumba hati miliki zao bila usumbufu kwa sababu wananchi wengi ni waathirika waliokosa hati za nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ramani iliyopo ya miaka ya 1990 ifuatiliwe upya hasa Jiji la Dar es Salaam kwa sababu maeneo mengi tayari yamevamiwa na wananchi wameshajiimarisha, na kuvunja ni kumtia hasara mwananchi pia na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. Ahsante.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutambua jitihada zinazofanywa na Wizara za kurekebisha matatizo ya muda mrefu na hasa migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kwa muda mrefu Maofisa wengi wa Wizara wamekuwa *very corrupt.* Hiyo ni changamoto kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumzia matatizo ya ardhi yanayohusu Wilaya ya Ngara, naomba ninyi kama Mawaziri mseme ukweli kuhusu Katibu Mkuu – Ndugu Patrick Rutabanzibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Katibu Mkuu mstaafu wa Utumishi, siku zote namwona Ndugu Patrick Rutabanzibwa kama the *best Permanent Secretary in terms of intergrity, intelligence, hard working and patriotism*. Binafsi nimefuatilia sana *performance* ya Ndugu Patrick katika Wizara mbalimbali na hasa katika Wizara ya Nishati na Madini ambako alionyesha uadilifu mkubwa sana katika vishawishi vingi. Nilisikitika sana jana wakati Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyojaribu kumsema vibaya. Naomba mumsaidie katika jitihada zake za *"to put the house in order."* Wizara ya Ardhi imeoza, kuna wezi wengi. Huo ni ukweli mtupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa nije kwenye upande wa Ngara. Nianze kwa kuishukuru Wizara kwa upimaji wa vijiji 68 kati ya vijiji 73. Naomba sasa tupatiwe Hati miliki za vijiji hivyo ikiwa ni pamoja na kukamilisha matumizi bora ya ardhi ili tuweze kufaidika na mradi wa Mkurabita. Wananchi wapate Hati miliki ya mashamba yao ili waweze kutumia hati hizo kama *Colateral* ya kupitia mikopo ya Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ngara iko pembezoni mwa nchi hii na inapakana na nchi za Rwanda na Burundi, nchi ambazo zina uhaba mkubwa wa ardhi. Kutokana na uhaba wa ardhi katika nchi hizo mbili, Wilaya ya Ngara ina matatizo makubwa ya kuingiliwa na wahamiaji haramu wakiwa na ng'ombe wengi na kuanza kuingilia ardhi ya wakulima. Wananchi wanapokonywa ardhi yao na wahamiaji kutoka nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iharakishe utoaji wa hati miliki kwa mashamba ya wanavijiji ili wasibugudhiwe na wahamiaji haramu. Tutakapoanza kutekeleza sera ya *"Common Market"* ya *East African Community* ya *"Free Movement of people and goods",* itakuwa mbaya zaidi kama ardhi ya wananchi katika vijiji vyao itakuwa haijapimwa. Juzi juzi wakulima sita wa Ngara wameuawa na wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawaruhusu wahamiaji haramu kuchunga ng'ombe kwenye ardhi yetu bila kuwahusisha wananchi (wakulima).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inunue darubini za upimaji wa ardhi na *Computer* za uchoraji ramani ili kuzigawa Wilayani hasa Ngara ambako maeneo mengi yanatakiwa kupimwa kwa ajili ya mpango wa *EPZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Migogoro ya Ardhi ya Ngara na Kagera kwa ujumla inatokana na uhaba wa ardhi kutokana na *high density ya population* pamoja na wingi wa uhamiaji haramu kutoka nchi za jirani. Naomba nimkumbushie Mheshimiwa Waziri ombi letu la kupewa Baraza la Ardhi ili wananchi wa Ngara wasiendelee kusumbuka kusafiri kwenda Wilaya ya Chato kuhudhuria kesi za ardhi. Katika hotuba ya Waziri, naona Karagwe watapewa Baraza la Ardhi la Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iweke *land use plan* katika Kata zifuatazo, Nyakisasa, Keza, Rusumo, Murusagamba, Muganza, Bugarama, Bukiriro, Rulenge, Kabanga na Kirushya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la heri.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watalaam kwa hotuba nzuri waliyoitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikazanie kujenga na kuweka masjala ya ardhi kwenye kila Wilaya ili kuweza kurahisisha zoezi la kupima ardhi ya vijiji na hatimaye kumpatia kila mwanakijiji hati miliki ya mila.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo yatolewe kila kijiji ili kijenge masjala ya ardhi na mafunzo ya kutosha yatolewe kwa Watendaji wa Kijiji ambao ndio Maofisa Ardhi ya Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikishirikiana na TAMISEMI ihakiki na kubaini mipaka kati ya Wizara ya Kiteto na Kondoa ili kumaliza mgogoro uliodumu kwa muda mrefu sasa.

**MHE. RAYA IBRHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ardhi ni mali, ardhi ni thamani pia ni msingi wa maendeleo, vilevile ni mtaji. Hivyo basi, thamani ya ardhi ipandishwe na wananchi wapewe hati ili wakope na wafanye biashara na kusomesha watoto, vilevile kujikwamua kutokana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Serikali itoe elimu kwa Maafisa ardhi kwenye Halmashauri ili kuongeza ufanisi katika kazi na kuepuka *"Double allocation."* Vilevile kuna *Graduates* wengi toka Chuo cha Ardhi hawana ajira na wana ujuzi wa kutosha, ni vyema sasa kwa Serikali kuwaajiri watu wenye ujuzi na elimu ya kutosha na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba nyingi zinazouzwa na mashirika huwa na bei kubwa/ghali na hazilingani bei na ubora, ni ghali ukilinganisha na ubora. Mfano mzuri ni nyumba za Shirika zilizopo Medeli Dodoma na nyinginezo. Nyumba hizo ni ghali hasa ukiangalia ni ghorofa. Bei hailingani kabisa na nyumba/*apartment* hiyo inayouzwa. Hivyo basi, kuondoa dhana nzima ya kutaka kuwasaidia wananchi kupata makazi na badala yake kuona ni mzigo zaidi na kushindwa kununa au kumudu gharama za nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa nyumba za Shirika ambazo zinakodishwa, hazifanyiwi ukarabati na kuonekana mbovu zaidi. Hivyo basi, napendekeza kuwe na bajeti maalum kwa ajili ya kufanya ukarabati nyumba hizo za mashirika na kuwa kivutio zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi siyo suala la Muungano, lakini kiungo cha ardhi yetu ni Katiba ya Taifa letu. Ardhi ni urithi wa wananchi na mtaji wa uchumi na nchi yetu. Raslimali zote nyingine iwe ni bahari, mashamba, misitu, madini, mafuta yote yapo chini au juu ya ardhi. Bara kwa kushirikiana na Visiwani waweke kipaumbele suala la ardhi wakati huu tunapoingiza kwenye mjadala wa Katiba mpya ya Muungano.

Katiba ya sasa ina ubovu wa kutoweka bayana masuala ya umiliki wa ardhi. Hivyo Katiba mpya ihakikishe watu hawanyang'anywi ardhi ovyo ovyo. Pia Katiba mpya ipunguze madaraka ya Rais kutoa ardhi. Katiba mpya iongeze nguvu zilizopo za kisheria kuhakikisha wananchi wanalipwa fidia stahili na kwa wakati. Katiba mpya ihakikishe wananchi wanahusishwa kwenye umiliki kama wabia wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa ardhi siyo suala la Muungano, lakini hata kwa upande za Zanzibar nako kuna matatizo ya udhaifu na migogoro katika Sekta ya Ardhi. Yapo sawa kabisa, na huku Bara kuna malalamiko ya ardhi kuporwa na wageni kwa ajili ya kilimo cha mashamba makubwa, uchimbaji wa madini na uwindaji na pia Unguja na Pemba kuna wimbi la uporaji wa ardhi kwa kisingizio cha uwekezaji kwenye Sekta ya Utalii, hasa kupisha ujenzi wa mahoteli bila wananchi kulipwa fidia inayostahili, mfano, Nunguri, Kwengwa, Matamwe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni mtandao wa *wiki leaks* ulivujisha taarifa za harufu ya rushwa katika uporaji wa ardhi zikihusisha vigogo wa SMZ. Serikali hizi mbili zishirikiane kuondoa hali hiyo na kuingia katika Katiba mpya ambapo itawatetea wananchi wanaonyang'anywa ardhi kiholela pia kuwalinda wazawa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kuainisha migogoro ya ardhi katika sehemu/Mikoa mbalimbali katika hotuba yake. Kwa uchambuzi wake wa kuonyesha migogoro ya ardhi iliyopo Dar es Salaam, Mbeya, Mara, Rukwa na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali kushirikiana na Wizara itoe kauli kuhusiana na migogoro ya ardhi na kuitafutia ufumbuzi na hatimaye kuwafanya wananchi kuwa na imani na viongozi wao na pia kufurahia uwekezaji bila ya kunyang'anywa ardhi yao.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iongeze kasi ya urasimishaji wa makazi holela na kuwawezesha kupata mikopo ili kuzuia wasiuze ovyo ardhi kutokana na umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bomoabomoa, ni vyema Serikali ikawa na wakaguzi ambao watakuwa wakiangalia ujenzi katika maeneo yasiyoruhusiwa ili kusitisha ujenzi katika hatua za awali na hivyo kupunguza bomoa bomoa ambazo zinaweza kuzuilika. Ikumbukwe kwamba bomoa bomoa ni kuongeza umaskini kwa wananchi na kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ishirikiane na Wizara za Maji na Nishati ili huduma za maji na umeme ziwahishwe katika maeneo yote yaliyopimwa jambo ambalo litawawezesha wananchi kuanza ujenzi kwa haraka katika maeneo hayo na kupunguza msongamano mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Wizara ya Ardhi iliahidi kuharakisha utoaji hati miliki kupitia ofisi za kanda, iharakishe sasa kuwapeleka Makamishna katika kanda zilizoanzishwa ili wananchi wapate hati miliki kwa haraka na waweze kuzitumia kwa shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kupewa dhamana kuiongoza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwa kuwa Waziri Profesa Tibaijuka ni mtaalam aliyebobea katika fani ya Makazi na Maendeleo yake, ataisimamia vizuri Wizara ili Tanzania ipite katika hali tuliyonayo ya watu wengi wasio na makazi mazuri wanayostahili binadamu wa karne ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Namtumbo, kuna mambo mawili ambayo Wizara ya Ardhi ilianzisha kwanza miji midogo, pili zoezi la hati za kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitangaza miji midogo katika Wilaya ya Namtumbo na kwa mujibu wa Sheria, eneo hilo lilitakiwa kuendelezwa kwa kujenga majengo ya kudumu mpaka zoezi la kupima na kuupanga mji huo likamilike. Sasa ni miaka zaidi ya kumi wananchi wa maeneo hayo wanashindwa kujenga kuendeleza makazi yao kwa sababu kuzuiwa kwa mujibu wa sheria ambayo Serikali haitimizi wajibu wake wa kuja kupanga miji midogo hiyo na kuipima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Serikali ilianzisha zoezi la hati za kimila katika Wilaya ya Namtumbo na lilifanyika katika Kata ya Msindo, lakini zoezi hilo limesimama kuendelea katika Kata na vijiji vingine, hivyo imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa vijiji na Kata nyingine kuwa, mbona zoezi hilo haliendelei na wanasema Serikali imebagua sababu wanahitaji zoezi hilo likamilike eneo lote la Namtumbo, wamefikia kusema au kwa sababu eneo hilo anakaa aliyekuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara na alitumia nafasi yake kuulazimisha mradi wakati akiwa kazini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ili Serikali isieleweke hivyo, unafanya kazi kwa kushinikizwa na Mkuu wa Wizara ndiyo ifanye kazi kwa *Interest* binafsi, zoezi la hati za kimila liendelee Wilayani Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile jiji la Dar es Salaam hivi sasa linabadilishwa kwa haraka sana kupitia ujenzi wa maghorofa na kuondoa nyumba ndogo ndogo za zamani, lakini katika ujenzi huo kila anayejenga anachimba kisima chake kwa sababu Serikali imeshindwa kukabiliana na tatizo la maji na kwa bahati mbaya sana Mji wa Dar es Salaam uko karibu na bahari na hivyo kupelekea visima vinavyochimbwa kutoa zaidi maji ya chumvi; kutokana na hali hiyo, mabomba baada ya muda yanafanya kutu na kuoza. Je, Serikali haioni kwamba hii inaweza kuleta athari kubwa kwa majumba hayo na pia ukizingatia maji hayo siyo safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Dar es Salaam umejengwa holela sasa, kwani maghorofa yamegandana kiasi ambacho hata hewa safi inakosekana. Ni hatari sana. Je, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Drainage system* inayotumika hadi leo ni ile ile ya miaka ya nyuma na ndiyo maana mara kwa mara mitaro ya maji machafu inaziba kwani uwezo wake ni mdogo, sasa imezidiwa mno. Wakazi waliopo leo Dar es Salaam ni wengi mno ukilinganisha na zamani na miundombinu ni ile ile. Je, Serikali itachukua hatua gani kurekebisha hali hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maghorofa yanayojengwa hayana viwango na hupelekea kusababisha maafa wakati mwingine. Je, Serikali ya jiji huwa imekwenda likizo mpaka kuachia nyumba inajengwa mpaka inafikia kuleta maafa?

**MHE. ABUU HAMOUD JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi ya mwaka 2011/2012. Pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa bajeti ambayo imetayarishwa kwa umahiri na utaalamu na inalenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayosisitiza kukuza uchumi madhubuti na endelevu katika matumizi bora ya ardhi. Kuendeleza mpango wa kurasimisha ardhi na nyumba kwa kutoa hati miliki za ardhi vijijini pamoja na leseni za makazi katika maeneo ambayo hayakupimwa na hayapimiki *(squatters)*, Mpango huu unalenga kupunguza umasikini kwa kuwezesha wananchi kutumia leseni hizo kuweza kukopesheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa ardhi yenye rutuba, mabonde, mito, maziwa na milima. Ardhi hii inatumika kwa shughuli za kilimo cha mazao mbalimbali na mifugo. Ardhi hii ni raslimali ya kwanza ya nchi yetu ambayo inapatikana hapa nchini pekee, dhahabu, almasi na vito vya aina mbalimbali kama *ruby, granite, suffire, marble* na kadhalika. Watafiti wa Sekta ya Madini na Nishati wametoa taarifa kwamba, katika baadhi ya maeneo kuna dalili ya kupatikana nishati ukiwepo mkaa wa mawe na gesi asilia. Kwa maana hiyo, ardhi ya nchi yetu ni mhimili wa uzalishaji unaotegemewa na wananchi katika kujenga uchumi wetu. Pamoja na umuhimu wa ardhi hii, kama Serikali haitapanga mipango mizuri itakayoelekeza namna ardhi hii itakavyotumika na kugawanywa kwa shughuli za maendeleo, inaweza ikasababisha malalamiko na migogoro mingi isiyo na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za karibuni wananchi wamekuwa na mwamko wa kutambua thamani ya ardhi na wamekuwa wakilalamika sana ardhi kugawiwa kwa wageni kutoka nje ya nchi kwa kisingizio cha uwekezaji na baadaye wanaiohodhi na kuiacha ardhi hii iwe mapori. Aidha, wanalalamikia vitendo vya viongozi wao wa Halmashauri au Serikali za Mitaa/vijiji kuuza ardhi bila kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika. Hili limekuwa tatizo sugu na tumesikia malalamiko mengi kutoka Wilaya mbalimbali, mfano Wilaya ya Kilosa, Handeni, Mvomero, Kilindi, Rorya na kadhalika. Matatizo haya yameambukiza hata mijini ambako yamezuka makundi ya watu ambao wanavamia maeneo ambayo yamekwishagawiwa watu na watu hawa wameshayaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeshuhudia migogoro ya ardhi katika maeneo ya Mivumoni na Goba katika Wilaya ya Kinondoni ambako wananchi wamefikia hatua ya kushikiana mapanga na kuchinjana kama kuku wakigombea ardhi. Serikali inashauriwa kuweka wazi

maeneo ambayo yamepimwa na wananchi wanazo hati ili kuondokana na migogoro hii inayopelekea umwagaji wa damu katika nchi yetu ambayo ina sifa ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze hatua za Serikali kuhakikisha mipaka ya vijiji inapimwa ili kuweka kumbukumbu sawa za maeneo ya vijiji vyote hapa nchini. Mpango huu ni mzuri, kwani vijiji sasa vinaweza kuweka mipango yake ya matumizi ya ardhi na kwa kujua ukubwa wake na mipaka yake. Jambo hili litaharakisha maendeleo vijijini kwani vijiji vitaweza kutenga maeneo ya kilimo, ufugaji, utalii, bustani za asili, maeneo ya majengo ya huduma za jamii kama shule, mahospitali, hoteli, maeneo ya michezo mbalimbali, migodi na kutunza mazingira hasa katika vyanzo vya maji.

Ningependa kushauri Serikali kwamba katika kupanga na kupima mipaka ya vijiji hivi, wataalam wa upimaji wahakikishe wamewashirikisha wananchi wa vijiji husika kikamilifu, na wakati wa kuweka mipaka, basi wananchi wanaozunguka maeneo hayo wawepo kuhakiki na kujua mipaka ya vijiji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu katika utekelezaji wa zoezi hili, tayari kumekuwepo na migogoro mingi katika vijiji vilivyopimwa na kuwekewa mipaka. Mimi binafsi nimekutana na tatizo hilo katika Jimbo langu la Kibaha Vijijini ambapo zoezi lilifanyika na kuwekewa mipaka ya Kata ya Ruvu na Kwala. Wananchi na hasa wazee wa Kata ya Ruvu hawakubaliani kabisa na mipka iliyowekwa na mpango huu kwa sababu eneo kubwa la kijiji cha Ruvu imemegwa na kuingizwa katika eneo la Kwala. Isitoshe, eneo lililochukuliwa ni eneo lenye rutuba na pia lina historia ya jadi na mila. Tatizo hili lipo na nimekwishamwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kibaha kumshauri ama zoezi la kupima lifanyie upya au aje kuongea na wazee kufafanua sababu za mipaka ile kuzidisha ardhi upande wa Kwala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa mingi ina maeneo ambayo ardhi yake bado haijakaliwa na wananchi wengi na kwa hiyo, yapo maeneo ambayo yakipimwa na kuwekewa mipango mizuri yatakuwa na mwonekano na mandhari nzuri. Nasikitika kutoa mfano na kusema kwamba Mji wa Dar es Salaam kwa kweli umejengwa kiholela sana, hata maeneo ya mpango miji yaliyopimwa miaka ya karibuni, kuanzia mwaka (1980) kama Mikocheni, *Mbezi Beach*, Kijitonyama na Sinza majengo yanaonekana kusongamana sana na hata ujenzi wa nyumba zake hauko katika mpangilio unaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kwenda kwa mkazi wa maeneo hayo, unapata shida sana ya kufuata maelekezo, kwani hakuna barabara za kueleweka, mitaa haina majina na hii pia inafanya huduma za jamii kama barabara, mabomba ya maji safi na maji taka, nguzo za umeme na njia za mawasiliano ya simu kuwafikia kwa shida sana. Katika kupima maeneo haya, haikuzingatiwa kuwepo kwa maeneo ya huduma kama Vituo vya Usalama/Polisi, zahanati, shule na maeneo ya michezo, na kama yalikuwepo, basi yaliuzwa au yalivamiwa. Maeneo kama Tandale na Manzese ndiyo usisema kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo yanasikitisha sana katika ujenzi holela ni maeneo yanayozunguka kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere. Hasa ukiwa angani, ndege inapoanza kupaa au inapotua na kama ni mgeni na unaingia hapa nchini kwa mara ya kwanza kinasikitisha *(eye sore)*. Wananchi wengi wanajiuliza kwamba hivi wataalamu wa upimaji wamesomea kazi yao? Kama wamesomea: Je, wana ujuzi kama wapimaji wa nchi nyingine zilizoendelea katika mipango miji? Jibu ni kwamba wengi wao wamesoma katika nchi za nje, pia tunacho Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam kinachozalisha wataalam wa taaluma za mipango miji na usanifu majengo kila mwaka.

Naishauri Serikali kuwa makini katika maeneo mengine ambayo hayajajengwa kiholela ili kuweka mipango miji itakayokuwa na mvuto kwa maana ya kuweka masharti ya ramani za majengo, kuweka huduma za jamii kabla ya kugawa viwanja wa maana ya kwamba, mtu anayetaka kiwanja anunue pamoja na ramani ya nyumba inayoelekeza ujenzi na upande itakayoelekea, alipie huduma zitakazokuwa zimejengwa kama miundombinu ya barabara, maji, umeme na kadhalika. Ningeomba kama kutakuwa na uwezekano, Serikali ifanye majaribio ya ujenzi wa mji wa mfano utakaokuwa unaonyesha mipangilio ya barabara, mitaa, huduma na

kadhalika katika mji mdogo wa Mlandizi katika Jimbo la Kibaha Vijijini ambako ardhi bado ni kubwa na kuna haja ya kusukuma maendeleo ya Jimbo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitembea katika baadhi ya Vijiji, utakuta Mikoa mingi imeezeka nyumba kwa makuti au tembe. Nyumba hizo zilikidhi hali ya maisha ya zamani, lakini kwa wakati huu pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokea duniani, inatakiwa kuweka tahadhari katika kila kitu ikiwa ni pamoja na tahadhari ya ujenzi wa nyumba kuepuka majanga ya moto, mafuriko, kuezuliwa kwa upepo na mengineyo mengi yanayosababisha familia kukosa makazi na kupoteza mali. Nashauri kituo cha utafiti wa vifaa vya ujenzi na nyumba bora kwa gharama nafuu *(NHBRA),* vifaa hivi visambazwe vijijini ili kuwawezesha wananchi kujenga nyumba zao kwa kutumia vifaa hivi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu anakuwa na heshima katika jamii kama ana nyumba na mji wake. Kipato cha kila siku cha mwananchi hakitoshelezi mahitaji yake na kumwezesha kujenga nyumba bora. Mabenki yaliyohamasishwa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, yana masharti magumu sana ambayo hayampi nafasi mwananchi wa kijijini kuyamudu. Mabenki haya yanahitaji dhamana na yanatoza riba kubwa sana. Wakati mwingine hata kama una dhamana, urasimu wa kupata mkopo ili uweze kujenga au kununua nyumba ni ndoto. Kama uko Dar es Salaam au katika Mikoa mikubwa kama Mwanza, Arusha, Mbeya, Kilimanjaro, Dodoma na kadhalika bei ya viwanja ni kubwa sana. Bei ya kiwanja cha kawaida kinaweza kikauzwa kuanzia Sh.5,000,000/= hadi Sh.10,000,000/=. Inategemea na eneo, ukubwa na maeneo ya kiwanja kilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za nyumba nazo ni kubwa sana, na mara nyingi utakuta nyumba zinauzwa kwa bei ya pesa za kigeni ambazo mwananchi wa kawaida kama mkulima, mfugaji au mfanyakazi hawezi kuzimudu. Kutokana na hali hii, nashauri Serikali iendeleze na kulipa uwezo Shirika la Nyumba Tanzania *(NHC),* pamoja na Wakala wa ujenzi wa Nyumba za Serikali *(TBA)* ili Taasisi hizi ziweze kuwa na dhamana ya kujenga nyumba na kuuza kwa wananchi kwa njia ya mkopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni roho ya nchi na makazi ya wananchi, hivyo bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inapaswa kuongezwa na ufanisi wa Wizara, Halmashauri na ngazi nyingine katika sekta husika unapaswa kuimarisha. Kwa upande wa bajeti ya matumizi ya kawaida, mkazo wa nyongeza ya bajeti unapaswa kuwekwa kwa kifungu 1001 (kasma 270300), kifungu 1003 (kasma 271100), kifungu 3001 (kasma 27700), kifungu 3002 (kasma 270600), kifungu 3003 (kasma 260500). Kwa upande wa bajeti ya maendeleo fedha za ndani zinapaswa kuongezwa kwenye kifungu 1003, 2001, 2002 na 3001.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Julai, 2011 wakati wa majumuisho ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lilipokaa kama Kamati nilihoji kuhusu fidia ya wananchi wa eneo la Kwembe Mlonganzila wanaopaswa kuhama kupisha ujenzi wa majengo ya Chuo cha Afya Muhimbili *(MUHAS).* Hata hivyo, jibu lililotolewa lilihusu wananchi ambao walibaki baada ya wananchi 1919 kupewa fidia ya maendeleo na mimea. Aya ya 25 ya hotuba ya Waziri ya tarehe 15 Agosti, 2011 ukurasa wa 13 imetaja tathmini ya fidia bila kueleza iwapo wananchi watalipwa fidia ya ardhi kama ambavyo Wizara iliahidi. Wizara izingatie kwamba Rais Jakaya Kikwete aliahidi Julai, 2008 kuwa wananchi wa eneo hilo wangelipwa fidia stahiki pamoja na kupewa viwanja mbadala (rejea *Daily News* – 22 Julai, 2008). Waziri Mkuu ameelekeza kwa baina ya tarehe 21 Aprili, 2010 yenye Kumb. Na. PM/P/1/569/29 ya kuelekeza mgogoro wa fidia ya ardhi umalizwe.

Tarehe 22 Novemba, 2010 katika kikao na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Serikali iliahidi kulipa fidia zote stahiki ikiwemo fidia ya ardhi. Maelezo ya barua ya tarehe 17 Desemba, 2009 yenye Kumb. LO/246321 hayakuwa sahihi kwa kutozingatia historia ya eneo husika tangu wakati wa uhuru, uwepo wa hati ya kijiji cha Kwembe kilichosajiliwa na kupewa hati No.DSM VC 40 ya tarehe 22 Februari, 1980. Maeneo mengine yote yanayozunguka eneo hili yamelipwa fidia ya ardhi: viwanja 600 Kwembe, Dampo Kisopwa, ekari 200 za wasioona, na mji wa mgano Luguruni. (Rejea pia barua yangu ya 13 Mei, 2011 – OMU/AR/005/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iongeze kasi ya kushughulikia migogoro ya ardhi, kuweka kuongeza ujenzi wa nyumba, kuongeza kasi ya kutoa hati za kumiliki ardhi na kusimamia mipango miji ikiwemo katika Jimbo la Ubungo. Lengo la kutoa hati 21,000 kwa mwaka ni dogo sana Kitaifa. Hata kwa Jiji la Dar es Salaam pekee, Ofisi ya Kanda ya Mashariki iwekewe lengo kubwa zaidi. Mikutano ya mipaka ifanyike pia Manispaa ya Kinondoni ili kuepusha migogoro na Manispaa za Ilala na Kisarawe katika maeneo mbalimbali. Katika kuhamasisha maendeleo ya nyumba, naunga mkono uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika, naikaribisha Wizara kufanya uhamasishaji na mafunzo kwa vitendo kwa kuwa Manispaa ya Kinondoni haikufikiwa katika mwaka 2010/2011. Pia Wizara ishirikiane na Manispaa kutenga maeneo maalum ya ujenzi wa nyumba Kata za pembezoni za Goba, Kibamba kwa kushirikiana na Mashirika ya Hifadhi ya Jamii na *NHC*. Aidha, Serikali itoe kauli kuhusu uendelezwaji wa mji wa Luguruni *(Satellite town).*

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai na afya njema. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa utendaji wake na nimpe pole kwa mzigo mzito sana aliobebeshwa, "Wizara ngumu"

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii akubali kuwa ardhi ni raslimali kubwa na tegemeo la Watanzania wote. Hivyo, wajibu wa kuthamini na kupanga matumizi bora ya ardhi iwe ni kauli mbiu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema tutenge eneo la makazi ya watu kimkoa, eneo la kilimo na eneo la viwanda bila kusahauliwa eneo la malisho kwa wafugaji wa nchi hii ambao nao wana haki sawa na kufaidika na raslimali ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawahitaji sana wawekezaji kuja kuwekeza nchini, ila hata siku moja Watanzania kugeuzwa wanyapara/wakimbizi ndani ya ardhi yao, haikubaliki. Utaratibu uwepo wa kuwahamisha wananchi pale itakapokuwa kuna haja ya kufanya hivyo kwa faida na maslahi ya watu na Taifa lao. Vijiji ambavyo wananchi wamezaliana hapo kwa karne nyingi, siyo busara hata kidogo kuwahamisha wananchi kinyama! Hii ni nchi yao, haiwezekani iwe mgeni anapapatikiwa, mzalendo anafedheheshwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya viwanja ni makubwa na kuwe na utaratibu wa viwanja vya wenye uwezo mkubwa, uwezo wa kati na uwezo wa chini, ili kila mmoja wetu awe na fursa ya kufaidika na matunda ya nchi hii na hili litaondoa kinyang'anyiro cha maeneo ya ujenzi kwa walionacho na wale wasiokuwanacho. Kwa kuwa Serikali haijalisimamia ipasavyo suala hili, ndiyo maana Watendaji wa Ardhi ndio wanaoisababishia Wizara lawama kama sio aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi yamekuwa ni balaa/vurugu kwa kukosa usimamizi. Jiji la Dar es Salaam badala ya kuwa mahali pa kuvutia wageni, leo ni jiji la kero, usafiri taabu, msongamano wa watu na magari ni vurugu tupu, uchafu uliokithiri wa pembeni mwa nyumba, barabara chafu, michirizi na mifereji ya maji machafu iliyojazwa takataka, chupa za maji na mengi mengine yanasababishwa taswira mbaya ndani ya jiji, siyo tu kwa wakazi wa Dar es Salaam, lakini pia kwa wageni ambao hupenda kuitembelea nchi na hususan Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze hivi ni kwanini Halmashauri za Miji zinavuruga mipango ya mipango miji na kuweka viduka na vitu visivyotarajiwa kwenye chochoro za majumba na maduka ya miji na hasa Jiji la Dar es Salaam na kusababisha uchafu, harufu mbaya inayokera na kuudhi na siyo ajabu hata kuhatarisha afya zao!

Mheshimiwa Naibu Spika, kila msimu wa mvua ufikapo, miji mingi huwa ni balaa badala ya faraja na wananchi kukumbwa na maafa makubwa ya kukosa makazi na kupoteza mali. Hili siyo jambo la kulitazama kwa jicho la mzaha. Ni jambo kubwa, zito, kwani linagusa maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuona wawekezaji wa kigeni ndio watakaotuondoa hapa tulipo na kupiga hatua ya kimaendeleo kwa kuwadhalilisha wananchi wazawa, bila ya kuwasikiliza, bila ya kuwashirikisha wananchi wenye eneo husika, jambo hili Serikali inabeba bomu

kubwa! Siku likilipuka, sijui nani aje ajibu lawama au dhima ya maafa yatakayotokea, pale wenye ardhi yao, haki yao, na hapa ndipo pao! Kujitetea dhidi ya "Wageni."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana mamlaka ya nchi hii ni ya Wazalendo wenyewe. Iheshimiwe, ilindwe na itunzwe kwa faida ya Watanzania wa sasa na wale wajao.

Mheshimiwa Spika Spika, tujipange kuzitumia raslimali zetu zilizopo kwa umakini mkubwa na tuweze kuwaletea maendeleo endelevu kwa raslimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila Mheshimiwa Waziri ili aweze kuendeleza heshima na matumaini makubwa ya Watanzania kwake yeye binafsi Mheshimiwa Waziri, tafadhali asafishe mara moja Watendaji wachafu! La sivyo watamchafua. Namtakia kila la kheri!

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vyote vya Tarafa ya Loliondo na Sale katika Wilaya ya Ngorongoro havijapimwa isipokuwa vijiji viwili vya Engaresero na Ololosokwan.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya hali hiyo ni migogoro isiyokwisha kati ya wakulima na wafugaji kwa upande mmoja na mapigano ya kikabila kati ya Wamasai na Wasonjo au Wabatemi wakigombea mipaka ya mashamba na maeneo ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, ipime mipaka ya Vijiji vyenye migogoro ili kuwezesha uongozi wa Wilaya ya Ngorongoro kusimamia mipaka hiyo kisheria. Vijiji vyenye migogoro sugu ya mipaka/mashamba ni Maaloni – Yasi Mdito, Sale – Malambo (Olchoro), Naan – Kisangiro na Oloivien – Mageri – Mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya Vijiji nane vinavyozunguka kitalu cha uwindaji cha kampuni ya *OBC*, bado kupatiwa ufumbuzi kutokana na wananchi kukataa mpango wa ushuroba *(Corridor)* uliopendekezwa na Serikali kwa kuwa haukuwa shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Mkoa wa Arusha na Shinyanga katika vijiji vya Kakesio (Ngorongoro) na Makao (Meatu) vina mgogoro!

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi ni ajira kwa wananchi wa nchi yetu, kila mtu ana haki ya kumiliki ardhi kisheria bila kunyanyaswa na wawekezaji. Nchi yetu ya Tanzania ni njia huru na tunapata mapato kutokana na ardhi kwa mfano, madini, mafuta, gesi, maji, mazao, misitu na mifugo inategemea ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni muhimu kwa watu wote Vijijini na Mijini, kila mtu ana haki ya kutumia ardhi kwa sababu ni zawadi tuliyopewa na Mungu. Sasa hivi kuna tatizo kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania ya kutojiamini na matumizi ya ardhi ndiyo maana tunaona kuwa wawekezaji kutoka nje wanaweza kutumia vizuri ardhi yetu kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi bado inaruhusu mtu kupewa ardhi na kumiliki kwa muda wa miaka 99 ambapo maisha na muda wa kuishi kwa binadamu ni miaka 70: Je, kwanini Serikali inatoa kwa wawekezaji kumiliki miaka 99?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo katika Jimbo la Mufindi Kusini yamechukuliwa na wawekezaji bila ya kuhusishwa wanakijiji kwa mfano, kijiji cha Isaula kilichopo Kata ya Kiyowela kuna tatizo kubwa la ugomvi kati ya wanakijiji na *MPM* ambaye ni mwekezaji. Je, Serikali imejipanga vipi kuwasaidia wananchi hawa ambao wanachukuliwa ardhi yao na huyu mwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kabisa kuwa Watanzania hatuwezi kugeuka na kuwa Wakimbizi ndani ya nchi yetu, Wakoloni tulishawatoa wala hatutegemei ukoloni mamboleo kurudi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Sheria ya wanakijiji kutoa maamuzi katika ardhi yao washirikishwe kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika swali langu ambalo niliwahi kuuliza hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kuwa atakwenda kutatua mgogoro wa ardhi katika kijiji cha Isaula, naomba anithibitishie lini atakuja katika Jimbo la Mufindi Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nakupongeza wewe, Naibu Spika na wenyeviti wote watatu, jinsi mnavyoendesha vikao vya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Naibu Waziri wake - Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Katibu Mkuu - Bwana Patrick Rutabanzibwa, Naibu Katibu Mkuu - Bibi Maria Bilia na wafanyakazi wote chini ya Wizara hii, kwa kazi nzito na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni chanzo cha maisha ya binadamu. Maisha ya binadamu yeyote yule yanategemea ardhi, chakula tunachokula, maji tunayokunywa, hewa tunayovuta, nyumba tunayolala vyote bila ya ardhi havingekuwepo. Kwa hiyo, ndiyo sababu ninasema ardhi ni maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi aliyoanza nayo Waziri wa Ardhi na Naibu wake, naomba wasirudi nyuma. Waziri anafanya kazi nzuri sana, kwa hiyo, azidi kusonga mbele. Mpango unaoendeleza ujenzi wa nyumba na kuziuza kwa wahitaji Watanzania, ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo kubwa kwa mpango huu, ni kuwa nyumba ziwe na bei nafuu ambayo mtu wa kati na kawaida atamudu kulipa kwa muda wa miaka hiyo iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa kwa Watanzania wafanyakazi ni makazi. Tatizo hili la nyumba ni kubwa kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la bei liangaliwe, tusije tukawajengea tabaka ya hali ya juu ya watu (ambao siyo wahitaji sana wa nyumba hizi) badala ya kuwasaidia tabaka mbalimbali za Watanzania. Nyumba zinaweza kujengwa za aina tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni nzuri, itakusaidia, utanufaika nayo kama imetunzwa vizuri. Wizara hii ya Ardhi kwa jambo hili, inabidi ishirikiane na Wizara nyingine kama Mifugo na Uvuvi, Mazingira, Biashara na Viwanda, Nishati na Madini, Maliasili na Utalii. Wizara ikishirikiana na Wizara hizo, nilizozitaja, ardhi itakuwa nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi bora ya ardhi ni jambo zuri sana, kwani kwanza inasaidia kupunguza migongano na migogoro ya ardhi kati ya wananchi. Mpango wa hati miliki ni mzuri kwani mwananchi anapata na kujua ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikoa, hati miliki za kimila zinatolewa. Ingekuwa nzuri kuenea Mikoa, Vvijiji vyote vya Tanzania, kila Mtanzania afahamu ardhi yake na matumizi yake. Mradi huu unaendeshwa na inabidi uendelee kuendeshwa. Tatizo linakuwa katika upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji unahitaji fedha, wataalam, vyombo. Kwa hiyo, Halmashauri nyingi kama siyo zote, inakuwa vigumu kupima ardhi zao na kupata hati miliki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa ardhi, tuzidi kuwa nao karibu, kuangalia mwenendo wao kikazi, ili Wizara iwe na sura nzuri yenye wafanyakazi waadilifu, waungwana, waaminifu na wachapakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mpango wake wa kuanza kupanga Mji. Viwanja vya Kigamboni, ushauri ni kuwa ndiyo viwanja viwe vinapimwa lakini mara tu vinapojitokeza viwanja vilivyopakana ni zaidi ya viwili, kwenye *plot* moja ni vizuri yule mmiliki wa *plot* hiyo apewe kiwanja kimoja bila ya kutozwa fedha. Hivyo, wananchi watafurahia zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kampuni/Mashirika yasiyo ya Serikali *(NGOs)* yanayojishughulisha na upimaji wa ardhi, ningependa kujua kama: Je, mashirika haya yanayo maelewano/wanapashana habari na Wizara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hizi, ingekuwa vizuri wajitambulishe au watambuliwe na Wizara husika ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kabla ya kuanza kazi za upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi nzuri, na kusema kuwa, Mheshimiwa Waziri azidi kusonga mbele daima na milele, ila wananchi wapate mikopo kwa kutumia ardhi zao za hati miliki kwa urahisi bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote walioko katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na watendaji wengine wote, kwanza kwa hotuba ya Waziri, lakini pia kwa kazi nzuri tunayoiona inafanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara imetoa kipaumbele katika kuboresha mfumo wa kumbukumbu za ardhi na kuimarisha mawasiliano kati yake na ofisi za kanda, naomba basi nipatiwe majibu ya maswali yafuatayo:-

(a) Serikali ilitoa viwanja karibu kila Mkoa na zikajengwa nyumba kwa ajili ya utamaduni *(Community Centre)* lakini mpaka sasa sielewi nyumba hizo baadhi zimebadilishwa matumizi au umiliki: Je, habari hizo ni za kweli? Kwanini? Je, Wizara inachukua hatua gani ili kushirikiana na Wizara husika ziweze kurudi mikononi mwa Sekta ya utamaduni?

(b) Serikali ilitoa eneo pia Mkoani Dar es Salaam kwa wasanii wa Tingatinga, sehemu hiyo inajulikana kama *Morogoro store*, na Serikali ya Uswisi ndiyo iliyosaidia kuendeleza shughuliza wasanii wale. Lakini cha ajabu Wizara ya Ardhi ilimpa mtu mwingine kinyume na awali sehemu ya ardhi akajenga na sasa hivi ameanzisha zogo kuwataka wasanii wale waondoke, pale anadai eti ni eneo lake la *Parking*, na inasemekana anashirikiana na baadhi ya Maafisa Ardhi, na suala hili linatambulika Wizarani. Je, Serikali au Wizara, wako tayari kulitolea maelezo ya kina uhalali wa kufanya hivyo? Kama kweli Wizara imeweka kipaumbele ili kutunza nyaraka, kwanini waligawa haki ya wasanii wale? Je, kwanini Wizara huchelewa kutoa hati? Naomba nipatiwe maelezo ya hatima ya *(Morogoro Store Tingatinga)* Wasanii wale na eneo lao.

(c) Jengo la Anatoglo lilijengwa na Waingereza/*Green* kwa lengo la kusaidia wasanii wa fani zote, ilikuwa Ofisi ya utamaduni ya Mkoa wa Dar es Salaam, lakini sasa hivi naona Wizara ya Viwanda wameweka ofisi zao. Sasa naomba kujua, jengo hilo bado linatambulika kuwa mali ya nani? Naomba jibu na Wizara isaidie jengo hilo pia kurudi kama ilivyokusudiwa.

(d) Kuna eneo lipo *opposite* na *Avallon* palipotolewa na *plan* yake ilikuwa ni jengo la Sanaa chini ya Fatma Said Ally akiwa Waziri mwaka 1986 na mchoro (ramani) ilikuwa tayari, lakini

nashangaa kuna *parking* tu. Je, tutafanyaje? Mbona haki za wasanii hata kwenye ardhi zinakiukwa tu? Naomba jibu.

(e) Mwaka 1988 wasanii wachongaji waliokuwa *Oysterbay* walipewa kiwanja Mwenge baada ya kuhamishwa toka *Oysterbay* ili kupisha upanuzi wa barabara maeneo ya *Best Bite* karibu na iliyokuwa *Gogo Hotel*. Kiwanja walichopewa Mwenge ni No.1 na 13 *Block 46 Business Area* Kijitonyama, Mwenge, *Offer* imetolewa kwa Chama cha Wasanii wachongaji Tanzania (CHA WAWATA) lakini baadhi ya Watendaji wa Serikali (ardhi) wakishirikiana na wafanyabiashara wanataka kuwapora. Naomba Wizara ikazie macho pale ili kulinda na kutenda haki na wasanii wale.

(f) Naomba Wizara inipe maelezo suala la nyumba ya Sanaa Dar es Salaam ni mali ya nani kwani jengo lile lilijengwa kwa msaada wa Nordish na kilitokea na Mwalimu Nyerere kwa wasanii, lakini sasa hivi naona watu wanafikia kulia tu, mara niambiwe ilikuwa maliasili, mara utamaduni kwa kuwa ardhi ndiyo mtoa viwanja, hati na kadhalika. Naomba kujua ni mali ya nani na imekuwaje kutoka mikononi mwa wasanii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza Shirika la Nyumba Tanzania, nikianza na Mkurugenzi Mkuu (Mr. Mchedu). Kazi inayoonekana sasa, inapelekea Tanzania kwenye ulimwengu wa nchi za kisasa, miji iliyopangika. Kweli itatia moyo na inavutia. Mimi nikutie moyo tu na Mungu akupe hekima zaidi na awape ushirikiano mzuri wewe na Watendaji wote walio chini yako. Ila naomba *NHC* waje pia Singida tukianza na Wilaya mpya ya Mkalama ambayo nitapata fursa ya kuipanga miji vizuri, pia kule wakulima wana hela, wasidhani watakosa wanunuzi na wapangaji, watakuwepo tena wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naona ugumu kuunga mkono hoja nikikumbuka mali za Wasanii, lakini kwa kuwa nina imani na Waziri na Naibu Waziri, najua watanijibu na kulishughulikia. Hivyo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa migogoro mingi ya viwanja vinatokana na Maafisa ardhi wa Mikoa na Wilaya kutokuwa chini ya Wizara ya Ardhi: Je, Serikali iko tayari sasa kubadilisha mfumo huu mbovu ili Maafisa Ardhi wote wawe chini ya Wizara ya Ardhi ili kuwepo na utaratibu mzuri na uhakika wa upimaji, ugawaji na umilikishaji wa Ardhi/Viwanja kwa maendeleo ya Taifa na ustawi wa jamii?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Sheria mpya ya Ardhi itakayoletwa hapa Bungeni, imtambue mwanamke katika masuala ya kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa ingawaje katika suala la Ardhi, migogoro haiishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi nchini wanahamishwa katika maeneo yao bila malipo halali na kwa wakati. Je, sheria inasema ni muda gani anafaa kulipwa mwananchi kabla hajahama toka eneo moja hadi lingine? Naomba jibu kwa manufaa ya wananchi wasiojua sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara kwa kuanzisha mradi huu wa kuzikopesha Halmashauri mbalimbali pesa za kupima viwanja katika Halmashauri zao. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni urejeshaji wa hizo fedha kwa uzembe wa watumishi waliomo katika Wizara hii ikiwemo na Mwanza, kuna tatizo gani kwa Mheshimiwa Waziri kuwaita Wakurugenzi wote na kuwahoji kuhusu urejeshaji wa kizembe wa fedha hizi? Ninaamini viwanja vyote vimeuzwa ila Halmashauri hawataki kuzirejesha hizo pesa. Je, iweje sasa kama Halmashauri zote hazitarudisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunawahitjai wawekezaji. Tatizo, wawekezaji wengine hupewa ardhi ambapo hushindwa kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Tanzania husema ardhi ni mali ya umma. Kama ardhi iko wazi ambapo wananchi wengine wanaihitaji, Serikali ipo: Je, Serikali ipo kazini kweli? Naiomba Serikali ichukue hatua za makusudi za kupima ardhi yote nchini ili ardhi hii iweze kutumika kulingana na mahitaji mbalimbali ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina taratibu nzuri tu za kutoa fedha kwa kuwathamini waathirika mbalimbali wanaoathiriwa, aidha, na miradi au huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iende au ibadilike kutokana na hali ya thamani ya fedha kwa wakati wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam yameonekana maendeleo ya kukua kwa Jiji hilo kwa kujenga maghorofa marefu, na kwa vile Jiji hilo lilipata aina ya Mji wa nyumba ndogo ambazo zilizingatia mitaro ya maji taka inayokwenda sambamba na ukubwa na idadii ya kaya hizo zinazoishi katika jiji hilo: Je Serikali ina mpango gani wa kupanua *"drainage system"* ambayo itakwenda sambamba na ukuaji wa mji huo kwa kujenga maghorofa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile majengo hayo yanayojengwa jijini humo ni kuanzia ghorofa tano hadi 15. Je, huduma ya magari ya Zimamoto yaliyo na uwezo wa kuuzima moto iwapo hali hiyo kwa bahati mbaya itakapotokea yapo? Je, magari hayo yapo kwa ukubwa unaolingana na barabara nyembamba zinazopitia katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, nyumba hizo zimejengwa kwa vigezo vinavyotakiwa au kukubali hasa baada ya kubainika kuwa majengo mengi hayapo katika usimamizi mzuri unaotakiwa. Je, nyumba zilizobainika kuwa hazina viwango vinavyotakiwa, hatua gani za kisheria zilizochukuliwa dhidi yao ili iwe fundisho kwa wengine watakaoamua kujenga na vile vile kuepusha ajali ya kuporomoka kama ilivyotokea kwa baadhi ya majengo jijini Dar es Salaam.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi za wananchi wanyonge na wazalendo wa nchi hii za ardhi zimekuwa zinazungushwa bila sababu hasa Kanda ya Mahakama kuu Tabora zaidi ya miaka 16 sasa. Je, Waziri haoni huu ni wakati maalum wa kuweka kikomo cha muda wa kesi kusikilizwa ukizingatia hakuna ushahidi wowote wanaosubiri. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko dhidi ya Wazee hawa wanyonge ambao wana umri zaidi ya miaka sabini bado wanapelekwa Mahakamani bila sababu na kucheleweshwa kulipiwa haki zao licha ya kwamba umri wao umekwenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kumekuwa na wimbi la utapeli wa viwanja na nyumba hasa mjini Dar es Salaam, madalali wanauza nyumba kwa bei ya juu zaidi ili na wao wapate chochote. Lakini hali hii imekithiri, inafikia nyumba kama inauzwa Shilingi milioni 100, basi inauzwa kwa shilingi milioni 200 na wakati mwingine wanauziwa hata watu watatu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka Wizara ya Ardhi iweze kuchukua jukumu hili la kuhakikisha kila mnunuzi wa nyumba na muuzaji wanauziana Mahakamani hasa Mahakama ya Ardhi au kwa Mawakili eneo ambalo linaonekana ni salama zaidi na kwakuwa *documents* zitakuwa *verified* itakuwa ni salama kwa wananchi na kuepusha migogoro isiyo na tija?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, Manispaa ya Kigoma Ujiji hasa maeneo ya Mlole hili licha ya Serikali kutoa tamko kuwa kina cha Ziwa Tanganyika kinapungua kwa sababu ya kujenga milimani na kusababisha maporomoko ya udongo na kuhatarisha usalama wa Ziwa: Je,

nani ambaye anaendelea kutoa fursa hiyo ya kujenga? Je, ni jitihada gani Wizara yako imechukua juu ya suala hili? Ni lini wananchi wataacha kujenga?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana na ndio suluhu ya maendeleo na kupunguza umasikini. Lakini cha ajabu, Wizara hii imetengewa fedha kidogo wakati ina majukumu makubwa sana hususan ya kutoa hati miliki (*Tittle deed).* Ni wazi kuwa bila hati hizi mwananchi hawezi bila kupata mkopo wala eneo lake haliwezi kupata thamani stahili. Ni hati hizi tu zitakazowawezesha wananchi, siyo tu kupatana thamani halisi ya ardhi yao, bali pia kuweza kujiendeleza katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba/makazi ni muhimu sana na ndicho kitu pekee kinachomtofoutisha binadamu na mnyama. Wakati mnyama anaishi porini na kupigwa na jua na mvua na adha zote, lakini binadamu wana makazi au maeneo, dhidi ya kujisitiri. Ni jambo la kusikitisha kuona nyumba za *NHC* ambazo lengo lake ni kwa ajili ya wananchi wenye pato la chini, lakini cha ajabu nyumba hizi zimekuwa kwa ajili ya wenye fedha. Matokeo yake, watu hawa huwa wanapangisha nyumba hizo *(subletting).* Hili ni tatizo kubwa, kwani huu ni ulanguzi kwa kuwa mpangishwaji na *NHC* anakuwa anapata faida kubwa sana. Mfano, nyumba ya Sh. 100,000/= kwa mwezi, mpangaji huyu anadai Sh. 200,000/= mpaka Sh. 300,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hawa watu wanapewa nyumba na Serikali, nao wanatoa kwa wengine, ina maana hawazihitaji. Naomba *NHC* ifuatilie kwa makini na wale wote watakaogundulika wanyang'anywe na kulipa *fine* pamoja na juhudi kubwa ya Shirika la Nyumba la Ujenzi bado nasisitiza ni vyema Shirika hili lijenge nyumba za aina tatu: nyumba za watu wa kipato cha chini, cha kati na cha juu. Kwa mantiki hii naamini kila mwananchi mhitaji atapata nyumba kwa stahiki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi imekithiri nchi nzima kila mtu analalamika. Pamoja na kwamba ardhi ni mali ya Serikali huku Rais akiwa ni mwamana wa ardhi hii. Tatizo la migogoro ya ardhi hapa nchini linaletwa na Serikali yenyewe. Haiingii akilini kuwa Serikali inakaa kimya mwananchi anajenga hadi anamaliza ndiyo Serikali inakuja kuvunja. Hivi Serikali inategemea nini? Yaani mtu anajenga kwa taabu na kibaya zaidi anakuwa amepewa ardhi hii na Watendaji wa Serikali. Haiwezekani eneo moja wagawiwe watu wawili au watatu. Hii ni fujo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ndio yenye ardhi na ndio wenye kutunga sheria ni lazima sheria hizi zieleweke vizuri kwa wananchi kwani ni wazi wengi hawajui Sheria za Ardhi na Mabaraza ya Ardhi yaboreshwe ili yafanye kazi ipasavyo.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Wizara inakabiliwa na matatizo ya kurithi yaliyosababishwa na mabadiliko ya Sera ya Ardhi. Mambo yaliharibika zaidi wakati wa madaraka Mikoani. Matatizo yanayojitokeza sasa yanahitaji ujasiri mkubwa kuyatatua. Baadhi ya Maafisa na viongozi wa Serikali ni sehemu kubwa ya tatizo, naomba Wizara isimame imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ziwa Nyasa, Serikali iseme mpaka hasa kati ya Malawi na Tanzania ni wapi? Hizo alama ambazo zimeimarishwa huko Ziwa Nyasa zinasaidia kupata suluhu ya mpaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jina, tutaendelea kuliita Ziwa Nyasa na Malawi wanaliita Ziwa Malawi hadi lini? Je, mataifa yanayotuzunguka wanasema nini juu ya utata huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo la wahalifu kung'oa alama za mipaka ya nchi. Tatizo liko kati ya Uganda na Tanzania, Kenya na Tanzania, Burundi na Tanzania na kadhalika. Je, ni lini tutamaliza tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya kusimamia ardhi yamegawanyika mno katika maeneo mbali mbali Wizara mbalimbali, Wilaya hata Vijiji? Je, Wizara ya Ardhi itafanya nini katika hili? Je, mmeishauri Serikali namna ya kulitatua tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaopiga kelele humu ndani wanasumbuliwa na mwangwi *(echo)* ya matendo yao. Baadhi yao ndio wanakuwa wakala wa kuuza ardhi katika maeneo yao.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi ngumu na nzuri wanayoifanya. Nawapongeza kwa hotuba nzuri ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa yafuatayo:-

Kamati za Serikali za vijiji wapewe *limit* ya ukubwa wa ardhi wanavyoweza kumpa Mwekezaji. Inakuwaje kijiji kinatoa *association* ya hekta 2,000 kwa mwekezaji mgeni, tena bila hata Halmashauri kuipa taarifa yoyote?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini, TAMISEMI na Maliasili na Utalii ili kuondoa kabisa migogoro ya wananchi na wawekezaji wa kuchimba madini pamoja na vitalu vya uwindaji katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, migogoro kati ya wawindaji na wachimba madini na wananchi ni mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wa madini na wawindaji wasipewe vitalu kwenye vijiji na mashamba ya wananchi, mfano ni Mzungu aliyechukua eneo kubwa katika Kijiji cha Nyambogo katika Kata ya Tomunguo bila uongozi wa Kijiji na Halmashauri kupewa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini waangaliwe kwa makini, ikiwezekana wasogezwe kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara iangalie na itafute suluhu mgogoro wa wananchi wa Gezaulole Kata ya Gwasa, kati ya wananchi na ndugu Shuma ambaye amehodhi ardhi zaidi ya miaka 20 na sasa anataka Kitongoji kizima kihame kwa sababu anayo hati miliki tangu enzi ya Mwalimu. Mgogoro unaweza kusababisha maafa, kwani amebomoa nyumba za wananchi bila sababu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nikiamini kwamba rai zangu zitatafutiwa suluhu ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia utekelezaji wenye mafanikio katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kutuletea hotuba nzuri yenye mipango kabambe, ila tatizo la viongozi wetu siyo kuandika mipango mizuri kwenye maandishi, bali ni kutekeleza yale wanayoyawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na ongezeko la migogoro ya ardhi katika vijiji vyetu, miji yetu kwa sababu ya tamaa ya kujitapia fedha kinyume na taratibu zetu hasa kwa Maafisa Ardhi waliopo katika Halmashauri zetu za Wilaya, Miji na Manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mfano wa mgogoro wa ardhi uliopo katika Wilaya yangu ya Rufiji kati ya Kijiji cha Ikwiriri Kusini na Kijiji cha Nyamwage ambao kwa makusudi umesababishwa na tamaa ya Afisa Ardhi Ndugu Wambura kwa kutoa maelezo mapya kuhusu

mpaka wa Vijiji hivi viwili kuwa ni Mto Rufiji wakati mpaka halisi wa asili ulikuwa ni eneo la miembe miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasababisha kujenga chuki baina ya wazawa wa kabila moja katika Wilaya moja kwa sababu ya Mtendaji ambaye yeye baada ya muda atakuwa ameondoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, Wizara ihakikishe inawasimamia vizuri Watendaji wake kufuata sera, sheria na kanuni za uendelezaji ardhi ili kuepusha au kupunguza migogoro ya ardhi inayoongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la ardhi kutolewa kwa wawekezaji kiholela. Ardhi ni raslimali muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi. Lakini kumekuwepo na tatizo kubwa la ongezeko la wawekezaji hewa ambao wanapewa ardhi na hatimaye wanashindwa kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa tatizo la migogoro ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji haiwezi kumalizwa na Wizara hii peke yake kwa sababu kumekuwepo na mkanganyiko wa jinsi ardhi hii inavyotolewa kwa wawezekezaji hasa ambao siyo raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji wa Idara ya Ardhi wamekuwa wakitumika wakati wa kufanya tathmini ya mazao. Wakati ambapo ardhi inataka kutwaliwa, hivyo basi, inakuwa vigumu sana kwa wananchi kukubali kuwa baadhi ya wawekezaji wanapewa kibali toka juu, namaanisha ngazi za juu na siyo kutoka katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, ni mgogoro kati ya wawekezaji wenye asili ya Uturuki waliopewa ardhi katika Bonde la Mto Rufiji, na walifanya tathmini ya mazao, miti ya miembe, Miyombo iliyokuwepo kwenye mashamba ya wananchi na kuwaahidi kuwalipa, lakini hatimaye hadi leo hii kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa, hivyo kusababisha mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kinachosikitisha ni kwamba wawekezaji hawa kwa sasa wameshindwa kuiendeleza ardhi hii ya Warufiji na wazawa wanakosa ardhi kwa ajili ya kulima hali ya kuwa ardhi yao inaendelea kumilikiwa na wawekezaji bila ya kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Wizara, natambua kuwa Wizara hii ni mtambuka. Naomba ihakikishe kuwa inafanya kazi sambamba na Wizara nyingine kama vile Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuhakikisha kuwa migogoro mingi ya ardhi hususan vijini inasuluhishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo ya kina kuhusu vigogo sita waliotajwa na Kambi ya Upinzani kuwa wanamiliki ardhi kubwa katika Kijiji cha Wami Dakawa wakati wananchi wa eneo hilo wanashindwa kupata ardhi ili wajikwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inashindwa nini kuwa na masjala Wilayani kote ili wananchi wapate *Tittle Deeds*? Vile vile Serikali inaweza kabisa kuruhusu hati za kimila vijijini ili wananchi wa vijijini wapate hati miliki za ardhi pamoja na nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya *CAG* ya mwaka 2010 inaonyesha kuwa *CV/CL* kuna tatizo la umiliki wa ardhi na majengo kwenye Balozi za Maputo na Uingereza. Je, mpaka sasa Serikali imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero ina mgogoro mkubwa wa ardhi, tunaomba Wizara iliangalie suala hili kwa jicho la tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba nyingi za *NHC* ni chakavu na chafu sana. Hivi Wizara haioni aibu? Napendekeza nyumba hizi zikarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa viwanja ufanyike mapema ili kuboresha mipango Miji.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji 18 katika Wilaya ya Lindi Vijijini vimechukuliwa na Mwekezaji zaidi ya ekari 1,600. Vijiji vya asili hivyo ni Mvuleni, Ruvu, Mandawa, Kushungu, Kiswele, Kibanje, Kange, Mtaliodi, Rushungi, Mandawa, Hoteli Tatu. Hadaa kubwa imefanywa na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya na Serikali za vijiji kwa kuwatilia saini na mikataba mibovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya fidia hayakidhi haja na kwa jumla wananchi hawashirikishwi kikamilifu katika mikataba hiyo. Kampuni ya Gulnet ndiyo iliyonunua ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa barabara ya Kibiti - Lindi umeathiri sehemu kubwa ya Mji wa Lindi ambayo sehemu iliyojengwa barabara hiyo ni makazi ya watu zaidi ya miaka mitano iliyopita. Fidia hizo zimewafanya leo wasiwe na sehemu za kukaa na baadhi ya nyumba zina hati miliki lakini hazithaminiwi hati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa mwenye mamlaka ya kufuta hati hizo ni Rais, lakini hatudhani kama Rais atazijua hati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria, taratibu na kanuni za fidia imekuwa siri, leo hazifahamiki kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Serikali irudie tena kuangalia kama malipo yale ya fidia yalikuwa sahihi. Nahitaji kauli ya Serikali juu ya hili.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na pia na mimi kunipa uwezo wa kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasikitishwa sana na migogoro ya ardhi hasa migogoro inayohusisha wafugaji na wakulima, kwa kweli hili ni tatizo sugu hapa nchini kwetu na kwa ujumla wake ni jambo ambalo ufumbuzi wake umekuwa ni kitendawili ambacho Serikali imeshindwa kukitegua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakulima wangapi katika sehemu mbalimbali katika nchi hii ambao wamepoteza makazi na ardhi yao kwa njia ya dhuluma tu kutoka kwa wenye uwezo aidha, wa kimamlaka au kwa njia ya udanganyifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sitaki niamini kuwa Serikali imeshindwa kutatua tatizo la ardhi katika nchi yetu, bali kinachoonekana ni kukosekana kwa umakini katika kushughulikia jambo hili zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naiomba Serikali kuanzisha Kamisheni maalumu ya kushughulikia migogoro ya ardhi hususan ile ya wakulima na wafugaji ili watu wetu kila mmoja aishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa juu ya upatikanaji wa upangishaji kwa nyumba za *NHC* hasa katika Jiji la Dar es Salaam, hasa yakihusisha upendeleo unaofanyika kwa Watanzania wenye asili ya Kiasia kuwa asilimia 90 ya nyumba hizo, wanazimiliki wao. Ningependa kuona nyumba hizo zinamilikiwa kiupangaji na Watanzania wenye asili zote. Lengo la Serikali kujenga na kutaifisha nyumba hizo ni Watanzania kuishi katika makazi bora. Je, lengo hilo limewekwa upande? Ahsante.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote waliopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopita 2010/2011 Waziri aliyekuwepo aliahidi kuanzisha Ofisi ya Kanda ya Usajili wa Hati pale Mtwara, lakini hadi sasa mpango huo haujaanza na wala hakuna *confirmed* Msajili wa Ardhi wala Kamishna. Ningependa kupata maelezo, kwa nini hili halijakamilishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, daftari la kusajili hati za Vijiji na vyeti lisiuzwe kama linavyofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa Halmashauri. Ni vyema Wizara au Serikali igharamie yenyewe, kwani jambo hili linakuwa mzigo kwa Halmashauri zenye Vijiji vingi. Aidha, Serikali igharimie mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji wakati wa maandalizi ya hatimiliki za kimila. Inakuwa vigumu sana Halmashauri kumudu gharama hizo, kwani Vijiji ni vingi kuliko uwezo wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi kwa ajili ya wawekezaji Vijijini ni tatizo linalohitaji utatuzi wa haraka sana, kwani Vijiji vyetu havijatenga na wala mipango hiyo haipo na Serikali ya Vijiji havijui utaratibu wa kufikia mpango bora wa ardhi hizo. Lakini wawekezaji wanapofika Vijijini hupewa maeneo yasiyopimwa na Serikali za Wilaya au Mkoa na wakati mwingine hata Wizara. Matokeo yake ni vurugu na migogoro isiyokwisha, utaratibu wa elimu na msaada kwa Serikali ya Vijiji wa namna ya mpango na matumizi endelevu ya maeneo hayo uandaliwe na iwe wa kudumu kwa kila Kijiji kinapoanzishwa na kusajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wafanyakazi wenye dhamana na ugawaji wa viwanja ni tatizo kubwa, waangaliwe kwa ukaribu na usimamizi mkubwa kwani ndio chanzo cha *double allocation* na migogoro isiyokwisha.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia hotuba ya Wizara hii mwaka jana, nilitoa ushauri kuhusu kazi za Shirika la Nyumba la Taifa, nilitoa ushauri kuhusu wajibu wake katika kukidhi makusudio ya uanzishwaji wa Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa kuchukua hatua za kusimamia uboreshaji wa Shirika katika muundo wake na utendaji wake. Shirika sasa limepata Mkurugenzi Mkuu mwenye dira, anaona mbali na ni mchapakazi. Watendaji wenzake pia wanafanya kazi kwa nguvu moja tangu uongozi mpya uanze kazi kuna mabadiliko makubwa yanayoonekana hasa katika ujenzi wa nyumba mpya za kuuzia wananchi na baadhi kuzipangisha pia. Nchi nyingi za Kimataifa kama Malysia, Singapore, Indonesia na kadhalika wamefanikiwa sana katika zoezi kama hili. Wananchi wengi wanaishi katika zoezi kama hili. Wananchi wengi wanaishi katika nyumba za kisasa. Tatizo kubwa ninaloliona kwa nchi yetu ni kwamba pamoja na dhamira hiyo nzuri, ukweli ni kwamba gharama za kuuzia nyumba hizo ni kubwa mno na sioni uwezekano wa wananchi wa kawaida wa kipato cha chini kumudu gharama hizo.

Ninashauri Serikali kwa pamoja na Shirika la Nyumba waziangalie upya gharama za kuuzia nyumba hizo. Nashauri pia sasa Shirika lijielekeze pia katika Mikoa mikubwa kwa mfano Mbeya na Iringa kama ilivyofanya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uendelezaji wa mji, ni kweli kwamba jukumu la kusimamia na uendelezaji wa miji ni jukumu la Serikali za Mitaa, lakini Wizara hii kutokana na ujuzi wao wa kisera, wataalamu wasijitoe katika jukumu hili la kufuatilia utekelezaji. Wizara iendelee kushirikiana na Serikali za Mitaa. Washirikiane pia katika suala la kutoa elimu kwa viongozi wa mitaa, kata na wilaya kwani wengi hawana uelewa mkubwa wa mipango ya miji kwa mfano, ujenzi wa nyumba na mpangilio hasa katika Jiji la Dar es Salaam linatisha. Majengo marefu yanayojengwa hayana *parking* hasa Kariakoo, *system* za maji taka ni mbovu au hakuna kabisa.

Hakuna maeneo ya wazi kwa michezo, kupumzika na kadhalika. Tunatembea kwenye nchi za wenzetu tunaona miji yao inavyopendeza na kuvutia lakini miji yetu haivutii kabisa.

Naomba kupongeza hatua ya Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na kuanzisha *central city parks* Jijini Dar es Salaam. Naupongeza sana mpango huo hasa kwa eneo la Jangwani na naunga mkono. Mpango huo uendelezwe pia katika miji mingine hapa nchini. Jambo muhimu ni kuhakikisha kuwa wananchi na viongozi wa maeneo hayo wanaelimishwa vizuri na iwapo maeneo hayo yalikuwa ni makazi ya watu, basi utaratibu wa kuwatafutia maeneo mengine ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kazi njema na mafanikio katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda kuchukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ujenzi holela wa maghorofa ya Kariakoo. Majengo haya hayapo katika ramani nzuri na hata mingine kujengwa bila ubora na hata kuhatarisha maisha ya watu. Majengo haya yamejengwa kwa msongamano usio wa kawaida bila hata kuacha nafasi. Na cha kushangaza maghorofa haya yamejengwa bila hata kuachwa miundombinu kama mitaro ya kupitishia maji taka, hata ajali ya moto ikitokea kwa msongamano huu wa maghorofa haya ni rahisi kuteketea kwa nyumba nyingi kwa sababu nyumba moja ikashika moto ni rahisi na nyingine kuwaka kwa sababu ya huu msongamano. Hata mvua zikinyesha pana kuwa hapapitiki. Nataka nijue watu hawa wanaojenga haya maghorofa Kariakoo vibali wanavipata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uvamizi wa maeneo ya wazi katika Mkoa wa Dar es Salaam kuvamiwa na matajiri na watu wenye umaarufu Serikalini. Na wengine kujenga katika maeneo ya *parking.* Kutokana na uvamizi huo wa maeneo ya wazi ya umma katika Mkoa wa Dar es Salaam na kutokana na malalamiko ya wananchi kuhusu uvamizi huo wa maeneo ya wazi ya umma. Ningependa kumuuliza Waziri ni viwanja vingapi vimerudishwa na ni vingapi bado vipo katika mikono ya wavamizi? Na ni hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika Wizarani na kwenye Halmashauri walioshiriki kusababisha hali kama hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la matatizo na tathmini ya malipo ya fidia. Wananchi wengi wamekuwa wakibomolewa nyumba zao na kuhamishwa katika makazi yao ya kudumu. Na kibaya zaidi hawalipwi fidia zao kwa wakati muafaka. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa wananchi kulalamika kupunjwa ama kutolipwa kabisa fidia pale ambapo wanatakiwa na Serikali kuhama maeneo yao ili kupisha matumizi mapya ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zetu zinatamka bayana kwamba pale ambapo mwananchi anapochukuliwa eneo lake na Serikali kwa matumizi mengine na hivyo kutakiwa kuhama anatakiwa kulipwa fidia inayojumuisha thamani ya ardhi, usumbufu, usafiri na hasara ambayo muathirika ataipata kutokana na kuchukuliwa eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, kumekuwa na migogoro mikubwa baina ya hawa wakulima na wafugaji na kusababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe na hata wengine kupoteza maisha yao. Kutokana na hali hii wanaume wengi wamekuwa wakikimbia wake zao wakati wa matukio na wanawake zao kubaki katika mazingira magumu na hili linakuwa ni janga la Kitaifa. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa nchi yetu kutokea kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji na chanzo cha migogoro hiyo ni kutokana na kutokuwa na mipango thabiti ya Serikali ili kubainisha kutengenisha maeneo maalum kwa ajili ya wakulima na halikadhalika wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo na ufugaji ni sekta zinazoongoza kwa kutoa mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa. Halikadhalika ndizo zinazotoa ajira, kwa zaidi 80% ya

Watanzania wamejiajiri katika sekta hii na hasa vijijini. Hivyo basi kuboresha hizi sekta mbili maana yake tutakuwa tumeboresha 80% ya Watanzania kwa kuwa na uhakika wa kipato, usalama wa chakula na kuongezeka kwa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la wazee wasiojiweza, wanaohangaika, kuombaomba na kulala kwenye mitaro, vituo vya mabasi na katika mabaraza ya maduka ya mjini, wazee hawa wamekuwa wakizagaa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na mingineyo na hata wageni wanaokuja hapa Tanzania wamekuwa wakikumbana na hali kama hii na wazee hawa kuombaomba, hii ni aibu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani na Wizara kuhakikisha inawajengea wazee hawa nyumba za makazi katika mikoa yao wanayotoka ili kupunguza wimbi hili la wazee kuzurura mijini na kuombaomba?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja endapo nitapatiwa majibu kwa haya niliyoyachangia kwa maandishi hapo juu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru na nimpongeze Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa tangu Mheshimiwa Anna Tibaijuka awe Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo pamoja na kutunga sheria nyingi za ardhi bado Tanzania inakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukodishaji wa ardhi kwa wageni, nchi nyingi zinaingia katika vurugu za kisiasa kutokana na kuwaachia wageni sehemu kubwa ya ardhi na yenye rutuba nyingi. Migogoro ya ardhi nchini Kenya, Zimbabwe na hata Afrika Kusini ni baadhi ya mifano michache.

Tutambue kuwa binadamu (watu) wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki, kwa hivyo Tanzania tunahitaji kuwa makini kwa maeneo wanayopewa wageni kwa jina la wawekezaji. Kwa kipindi kirefu hivyo kuwanyima Watanzania fursa ya kuwa na ardhi ya kutosha. Lakini pia kuna hisia kuwa miradi mikubwa ya kilimo inayoanzishwa kwa mfano *SAGCOT* itawafanywa wawekezaji wakubwa kumiliki maeneo makubwa ya kilimo na kuwaacha wakulima wadogo walio pembezoni kuwa wanaomba katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki wa ardhi kubwa kwa wazawa, wapo Watanzania matajiri au wanasiasa wakubwa wanaomilikishwa maeneo makubwa lakini hawayatumii. Lakini cha kushangaza pamoja na maeneo hayo kumilikishwa wenye uwezo kwa miaka mingi kodi *(land rent)* ni ndogo sana. Serikali inafaa ifuatilie mashamba yote waliopewa wakubwa na ambayo hawayatumii ili yarejeshwe kwa wananchi waweze kutumia ardhi hiyo ama kwa ufugaji au kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuzaji wa nyumba za *NHC.* Madhumuni ya Serikali kujenga nyumba kupitia Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ni kuwasaidia wananchi hasa wasio na uwezo. Azma hiyo inaonesha imeachwa na nyumba sasa zinauzwa kwa bei ya kutupwa, hili ni kosa kubwa, inatia wasiwasi na huenda halikufanywa kwa nia njema. Naomba Serikali isiendelee kuuza nyumba; sababu ya nyumba kutia hasara Shirika la Nyumba la Taifa haina msingi kwa sababu ni wao wenyewe walioziacha nyumba kufikia hali zilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuzaji wa viwanja, Serikali inajitahidi kupima viwanja ili vigawiwe kwa wananchi. Jambo la msingi ni kupunguza bei ya viwanja hivyo na kuzidisha kasi ya upimaji ili Watanzania wengi na hasa wale wenye kipato cha chini waweze kupata viwanja.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kupongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, ningependa kupata ufafanuzi katika hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Wizara ime-*allocate* hekta 25,000 kwa mwekezaji *Arkadie Ltd.* katika Wilaya ya Mkinga? Wilaya haina hekta hizo, tunahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa Wizara bia kushauriana na uongozi wa Mkoa wa Tanga na uongozi wa Wilaya ya Mkinga ime-*approve allocation* ya hekta 25,000 katika vijiji vya Mavovo, Makikonge, Mwakijembe, Mbuta, Magodi na Mwanyumba Wilayani Mkinga, Mkoa wa Tanga ili aweze kutekeleza mradi wa kilimo cha Jatropha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hekta 25,000 ni nyingi mno kupewa mwekezaji mmoja wakati eneo la Wilaya nzima yote ni kama hekta 250,000 licha ya kuwa Wilaya haina ardhi ya kutosha kumpa mwekezaji mmoja karibu asilimia 10 ya ardhi ya Wilaya inawaweka wananchi wa Wilaya ya Mkinga hasa vijiji husika katika hali ya mashaka ya kutokuwa na ardhi ya kutosha kwa shughuli zao za maendeleo na hivyo kuzidi kuwaweka katika hali ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini mwekezaji huyu apewe hekta 25,000, wakati tayari wapo wawekezaji wengine (mashamba) 10 yenye jumla ya hekta 25,000 tu. Wilaya ya Mkinga na viongozi wa Mkoa wa Tanga hatukubaliani na uamuzi huu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Wizara ya Ardhi kulirejesha suala hili katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ili lishughulikiwe kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na TAMISEMI. Sisi kama viongozi wa wananchi katika Wilaya ya Mkinga na Mkoa wa Tanga tunapendekeza kuwa mwekezaji huyu apewe ardhi kwa jinsi itakavyopatikana vijijini na wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia kwa Wizara kuangalia suala hili kwa mapana zaidi, eneo husika lipo mpakani na Kenya. Ni hatari maeneo ya mpakani ardhi yake kutolewa kwa mwekezaji wa nje. Tunahitaji majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Wizara itakamilisha uundwaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya, Kata na Vijiji? Sheria za Ardhi (Namba 4 na 5) za mwaka 1999 zikisomwa pamoja na Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya 2002 zinaanzisha na kuweka utaratibu wa kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya hadi Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa karibia miaka kumi tangu sheria hizi zipitishwe na Bunge bado Mabaraza ya Ardhi hayajaundwa katika baadhi ya Vijiji, Kata na Wilaya na pale ambapo yameundwa basi utendaji wake si wa kuridhisha kabisa kinyume na malengo yake yaliyokusudiwa ya kupunguza kero kubwa za ardhi kwa wananchi hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara ina mikakati gani ya makusudi na ya haraka ya kuanzisha na kuimarisha mabaraza haya katika ngazi husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia Wizara ikazijengea uwezo Halmashauri ili zisimamie uundwaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iharakishe kutatua kero ya muda mrefu ya wananchi wa Kitongoji cha Kwamkembe, Kijiji cha Marungu Wilaya ya Tanga. Kumekuwa na kero ya muda mrefu ya wananchi wa kitongoji cha Kwamkembe, Kijiji cha Marungu Wilaya ya Tanga kuhusu kumilikishwa shamba lenye ukubwa wa hekta 820 lililokuwa linamilikiwa na ma-*settler* wa kizungu waliokuwa wakilima mkonge tangu mwaka 1952 hadi mwaka 1963.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumejitokeza wawekezaji bandia ambao nia yao ni kumilikisna hati miliki ya shamba hili kwa lengo la kujichotea mikopo benki bila kuwa na nia ya dhati ya kuendeleza eneo hili. Ninaomba Wizara ishughulikie ombi hili la wananchi kumilikishwa kihalali shamba hili ambalo wamekuwa wakilitumia tangu mwaka 1983.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwanza kwa maandalizi ya hotuba hii nzuri, inayoleta matumaini na pili nawapongeza kwa mipango mikubwa

na mizuri mliyopanga na inayoendelea. Mipango ni mingi, ni mizuri lakini Bajeti iliyotolewa haitoshi. Kwa kuwa ardhi ndiyo mhimili mkubwa wa maendeleo, basi Serikali itoe fedha za kutosha ili hii mipango mizuri iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ina thamani kubwa, lakini Watanzania wengi vijijini hawajui thamani ya ardhi, la sivyo wasingekuwa wanaitoa kwa bei karibu na bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi tuwe waangalifu na ugawaji wa ardhi hasa kwa wawekezaji wa nje. Sasa hivi kila mtu anatamani ardhi ya Afrika, kwa mwaka 2010 tu wawekezaji wameonyesha nia na kuomba zaidi ya hekta milioni 30 kutoka Afrika pekee ambayo ni 64% ya ardhi yote iliyoombwa na wawekezaji pote duniani. Kwa nini hatujiulizi *why now?*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2003 bei za mafuta zilianza kupanda na watu wakaanza kufikiria kupanda *Bio fuels* na tukumbuke mdororo wa uchumi wa mwaka 2008 na upungufu wa chakula unaoendelea kuongezeka kila kukicha hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Chakula Duniani walitoa tahadhari kuwa ukubwa wa tatizo utaendelea kuongezeka. Hivyo ukizingatia na athari za mabadiliko ya tabia nchi, Mataifa ya nje wanatafuta pa kukimbilia, wanawahi wachukue ardhi yetu bure na sisi tunawapa bure. Mfano Mkataba wa *Agrisol Energy Tanzania Ltd.* na Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kwa masharti ya kulipa kodi ya ardhi shilingi 200/= kila ekari, kuilipa Halmashauri shilingi 500/= kila ekari na wamepewa ardhi kwa miaka 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mkataba uliletwa kwenye semina ya *Land Grab*, ukionyeshwa na Mtaalam wa Mikataba aliyetoka Canada. Semina iliyofanyika Midrand, Afrika Kusini. Mkataba huu ukionyeshwa kama mkataba mbaya sana ambao hauwezi kuwanufaisha wananchi wetu wa Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ardhi tumewapa hawa kwa miaka 99 wakati watu wenyewe wanaihitaji. Huu sio uwekezaji, watu/Mataifa wamekuwa na wasiwasi na hali ya mafuta, chakula na kadhalika na hivyo wakakimbilia kwetu, kuchukua ardhi. Naiomba Wizara ipate taarifa ya makusudio yote ya kugawa ardhi kwa wawekezaji, mikataba yote hii, ichunguzwe na wataalam kabla ya kuwekewa sahihi, viongozi wa Kijiji/Halmashari waondoe usiri, mikataba iwe wazi, wenye ardhi waelezwe kwa nini na ni kitu gani kiko kwenye mikataba na mikataba ya ardhi yote mibovu kama wa *Agrisol*/Mpanda iwe *revised.*

Pia uwekezaji utakaofanyika uwape watu wa pale ajira, miundombinu, huduma za jamii na vijiji na Halmashauri vinufaike kulingana na ukubwa/ubora wa ardhi iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari Wizara yake kupitia mikataba ya ardhi/wawekezaji ili kunusuru ardhi ya Watanzania isiporwe?

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na kuipongeza Wizara kwa juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja nina maeneo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upimaji wa ardhi ya vijiji na upimaji wa viwanja, kazi ya upimaji wa ardhi ili kuainisha matumizi bora ya ardhi kwa kutenga maeneo ya ufugaji, kilimo na misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana hii ni nzuri sana ambayo inapaswa kuungwa mkono na Wizara zote kwani sekta ya ardhi ni sekta mtambuka hivyo naishauri Wizara iongeze kasi ili kuhakikisha kwamba wilaya nyingi zinafikiwa ikiwa ni pamoja na vijiji vya Wilaya mpya ya Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa viwanja umekuwa na kasi ndogo sana isiyoendana na kasi ya ujenzi wa wananchi hivyo kujikuta kuendelea kuwa na ujenzi holela na makazi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza pale ambapo eneo lililowazi kupimwa viwanja inapotokea eti limekosewa kupimwa wakati wananchi wameshaanza kuuziwa viwanja vilivyopimwa katika Wilaya mpya ya Kalambo, Makao Makuu yaliyopo Mji Mdogo wa Matai na hiyo kuwazuia wananchi kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo machache ambayo tayati yamepimwa na kutolewa hati za kimila za ardhi na kuwa bahati mbaya sana hati hizi zimekuwa hazitambuliki na taasisi za kibenki zilizo Sumbawanga wakati hati hizi zimekuwa zikitambulika na kupokelewa na taasisi hizi zilizo Mkoa wa Mbeya. Naomba kauli ya Serikali juu ya uhalali wa hati hizi za kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba nilipongeze Shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi nzuri ambazo zinafanywa chini ya Menejimenti mpya, ile dhana potofu kwamba mambo mazuri yanaweza kufanywa na wageni imeonekana si kweli na sisi wazawa pia tunaweza na hasa tukiamua kwa moyo wa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila taswira hasi iliyokuwa imejengeka kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa kuwa ni miongoni mwa mashirika yaliyokuwa katika hali mbaya, nyumba zake chafu, matengenezo hayafanyiki, ujenzi wa nyumba mpya haufanyiki, yote haya yamekuwa tofauti kabisa chini ya uongozi wa menejimenti mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu wote kuhakikisha kwamba tunawatia moyo ili wafanye kazi kwa ufanisi na nchi nzima ya Tanzania na hasa kwa mikoa mipya na wilaya zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukatambua uhusiano uliopo kati ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara nyingine ili kupunguza migogoro ya ardhi.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na Bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kuunda Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wa Serikali mwaka 1992. Kwa kweli, nitoe rai kwa Serikali kuboresha utendaji wa mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha tunapoelezwa kwamba kwa miaka 19 ni watumishi 1,480 tu ndiyo wamefaidika na mikopo hii, ni idadi ndogo sana. Idadi ya waliokopeshwa ni ndogo sana na vilevile, kiwango kilichokopeshwa ni wastani wa shilingi milioni tano, wakati kiwango cha chini kinachoombwa ni shilingi milioni 13. Chanzo cha fedha cha mfuko huu ni kipi? Na je, masharti ya mikopo yake yakoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri anipatie orodha ya waliokopeshwa kuanzia mwaka 1992 mpaka hivi sasa ili kuweza kutathmini watumishi wa aina gani/ngazi ipi ya utumishi (ya chini au ya kati au ya juu) ambayo imekopeshwa kwa wingi zaidi? Ni vema, Wizara ikafanya jitihada za makusudi ili kuongeza fedha za mfuko huu ili watumishi wengi zaidi waweze kufaidika na mikopo hii na pia mfuko ujitangaze kwa watumishi ili waweze kuufahamu na wao waweze kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kubadilisha mfumo wa mfuko kwa kuweka utaratibu mpya kwa kuufanya kuwa wa kuwapatia watumishi wa umma dhamana ili waweze kupata mikopo inayotosheleza mahitaji yao kutoka katika taasisi za fedha badala ya kutegemea mtaji wa Serikali pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Shirika la Nyumba la Taifa. Naupongeza uongozi wote wa *NHC*. *NHC* inayo mipango mkakati mizuri sana, lakini bado katika uendeshaji wa Shirika hili kuna mapungufu mengi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuelezea upungufu mmoja ambao nina ushahidi nao. Kumekuwa na tabia kwa *NHC* na uongozi mzima wa Shirika hili hata wa juu, unakuta mtu anaenda kuomba kukodishwa nyumba, halafu unaambiwa kwamba ili upatiwe nyumba ni lazima ulipie deni la mpangaji aliyepita ndiyo uingie wewe.

Mimi binafsi niliienda kuomba kupangishwa ofisi na nilielezwa nijikadirie kuanzia shilingi milioni tano na kuendelea na endapo wakitathmini, wakinikubalia nitalipa kiwango hiki. Lakini jamani hebu tuambizane ukweli. Mimi nikishalipa deni la mpangaji aliyepita, nitajiridhishaje kwamba mdaiwa aliyepita hatadaiwa tena? Na akidaiwa tena, pesa hiyo itaenda wapi? Huu ni mwanya mkubwa wa rushwa na hata Mkurugenzi Mkuu nilimweleza hili na yeye alisisitiza kwamba wana *operate commercially* huo ndiyo utaratibu, inatia mashaka sana kwa sera ambayo haijaandikwa na wala haiko rasmi.

Ningependa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake alizungumzie hili na kutoa ufafanuzi au tamko kwa *NHC;* kwani huu ni uonevu na unyanyasaji mkubwa kwa mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu makubwa yanayoikabili Wizara ya Ardhi napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kisarawe ina migogoro mingi ya ardhi ambapo watu wengi wamechukua maeneo ya watu kinyume na taratibu na sheria. Wizara imeshapelekewa malalamiko juu ya utendaji wa Afisa Ardhi ambaye amekuwa chanzo cha kuleta migogoro lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hii inakatisha tamaa wananchi kwa Serikali yao na inawapa kiburi watendaji wabovu ambao wanaipaka tope Serikali iliyo madarakani kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ichukue hatua za haraka za kumleta Afisa Ardhi mwenye uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uboreshaji wa mji wa Kisarawe mwaka 1982 kuna wakazi kadhaa ambapo makazi yao yaliathirika kutokana na kupitisha barabara. Lakini mpaka sasa wakazi kadhaa hawajalipwa fidia ya kuathirika kwao kwa kipindi chote. Je, Serikali kwa nini isilipe wazee hawa ambao wengine wamedai mpaka wamefariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakazi wa eneo la Kibong'wa katika Kijiji cha Kisarawe ambao wamefanyiwa tathmini maeneo yao toka mwaka 2007 lakini wengine wameshalipwa na wengine hawajalipwa. Kibaya zaidi maeneo yao yameshachukuliwa na kupimiwa watu wengine hivyo kuleta migogoro mikubwa kwa wananchi wa Kigong'wa. Baadhi wamelipwa lakini wengine mpaka sasa hawajalipwa, naiomba Serikali imalize kulipa fidia wakazi wa Sanze ambao mpaka sasa hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Kisarawe kuna tapeli mmoja aitwae Sanjula ambaye alivamia mashamba ya Wilaya ya Kisarawe na Kibaha Vijijini. Mkuu wa Mkoa wa Pwani alifanya juhudi mpaka alikamatwa mtu huyo ambaye alikuwa akishirikiana kwa karibu na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Ardhi. Naiomba Serikali kuwawajibisha baadhi ya watendaji wasio waaminifu ambao wanashirikiana na matapeli wa ardhi na hivyo kuipaka matope Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Wizara itamaliza tatizo la utoaji wa Hati za Kimila katika vijiji vyote vilivyopo Wilayani Kisarawe? Tunaomba lifanyike zoezi hili kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata hati ili wazitumie katika mambo mbalimbali ya kujenga uchumi wao ikiwemo upatikanaji wa mikopo katika taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kisarawe kuna Kiwanda cha Saruji ambacho kimejengwa na Mtanzania mwenzetu lakini cha kusikitisha mpaka sasa mwekezaji huyo hajapata hati ya eneo

hilo. Wizara imekuwa ikichelewesha sana utoaji wa hati hiyo. Hii ni kukatisha tamaa wawekezaji kutoka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara impatie hati miliki mwekezaji huyo ili shughuli za kiwanda ziweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Kiwanda litenganishwe na Reli ya *TAZARA*. Watendaji wa ardhi bado wanakwamisha utoaji wa kibali cha ujenzi ili shughuli zote ziende sambamba. Naiomba Wizara isimamie jambo hili ili lilete taifa katika uchumi wa nchi yetu na kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ni nzuri na Waziri anajitahidi na ana uwezo wa kumudu wadhifa wake vizuri na kwa ujasiri. Naungana na Waheshimiwa wenzangu kuhusu Maafisa wa Wizara hasa Dar es Salaam wanatuangusha, matapeli na si aina ya watumishi wanaoweza kumsaidia Mtanzania maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kupoka maeneo ya wananchi kwa utaratibu wa fidia ndogo kuliko hata bei ya *plot* moja ni kudhuluma wananchi wanaotumikiwa na Serikali ile ile walioiweka madarakani hii haikubaliki, kama mtu hana uwezo angalau apimiwe eneo lake na kama kubwa apewe viwanja viwili kimoja auze ili ajenge kimoja na siyo fidia ya visenti ambavyo kwa namna nyingine anapokonywa viwanja na anabaki hana pa kukaa, aende wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama ya Ardhi, kuanzia Mabaraza ya Kata haki hazipatikani kwa wasio na fedha. Wale ambao wanashiriki katika mchakato wa kuamua kwenye Mabaraza ya Kata hawana taaluma yoyote na wanatoa haki kwa misingi ya rushwa peke yake, una fedha huna haki, je, tutafika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Ardhi ya Wilaya hakuna na Mahakama ya Mkoa inaonekana nayo meno yake si ya msumeno ambao makali yake yanaonekana, ipewe meno Mahakama hii inajitahidi sana kuiona haki hasa haki za wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi ya vijiji, hili lingekuwa suluhisho la uharibifu wa mazingira unaoshambuliwa kila kunapokucha na kupunguza kabisa migogoro ya ardhi wananchi wa Tanzania wangepimiwa ardhi yao kila mtu angekuwa makini kutunza ardhi yake na kuiendeleza katika matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ranchi na mashamba ya wawekezaji, yapo mashamba ya wawekezaji ni makubwa mno kuliko hata shughuli wanazoziendeleza huku wananchi waliokuwa na ardhi hiyo wakibaki hawana ardhi na hatuchukui hatua zozote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nkasi Kusini, shamba la mwekezaji Mzindakaya limewabana wananchi huku mmiliki huyu hana uwezo wa kulitumia lote, lazima Serikali iangalie tatizo hili ardhi isiyotumika wapewe wananchi wa vijiji vya Nkundi, Kahundi, Fyengelezya, Kalundi na Sintali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji huyu alikuwa Mbunge na aliweza kushawishi Serikali kuchimba bwawa la maji la Kawa kwa fedha za Serikali zipatazo shilingi bilioni 1.91 kwa maelezo kuwa wananchi wangeweza kupata huduma hiyo ya maji lakini hawajawahi kupata badala yake maji yapo kwa ajili ya mifugo yake kwa gharama ya Serikali na inaelekea anasaidiwa na vingozi wa Serikali jambo hili linaangusha *intergrity* ya Serikali yetu ya CCM, litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la *NARCO* Kalambo, shamba hili lina eneo kubwa sana na limekuwa na maendeleo siyo mazuri sana na walipoanza kugawa *plot* na kubinafsisha kwa wafugaji walitokea wafugaji wa kutoka mbali na wengi ni maofisa wa Serikali wakabana maeneo badala ya wananchi wa maeneo yanayohusika. Jambo hili limeacha sura kuwa hizi sera za

kubinafsisha zinalenga kunufaisha maafisa wahusika kuliko wenyeji kwani ni kikundi kimoja tu cha wananchi wa kijiji cha Sintali ndiyo walioweza kupewa *plot* moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo ni mingi inatuharibia ardhi nashauri elimu kwa wafugaji itolewe zaidi ili wawekeze katika mambo yenye tija kama kusomesha, kujenga majengo ya kisasa mijini na kubadili aina ya ufugaji wa kuchunga ambao mtu anatumikia mifugo zaidi kuliko kujitunza mwenyewe.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na usemi wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere amesema; "Ili tuendelee tunahitaji mambo manne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora."

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kuna takriban zaidi ya watu milioni 40 lakini hadi leo hii kuna baadhi ya vijiji havina hali nzuri ya maisha na wala havina maendeleo yanayostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wana mifugo lakini hawana maeneo ya kulishia mifugo yao na ardhi tunayo ila Serikali za vijiji bado hazijawabainishia wafugaji maeneo ya kufugia na ndio maana matatizo ya wafugaji na wakulima hayaishi katika baadhi ya vijiji vyetu kwani wakulima wanaona ardhi yote ni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji hawana kitu, ushauri Serikali za vijiji waweke maeneo ya wakulima na maeneo ya wafugaji kwani Serikali inasema inaleta ufugaji wa kisasa. Lakini mwananchi wa kijijini sidhani kama ataweza kwa maisha ya sasa kwani ardhi tunayo ya kutosha, yagaiwe tu maeneo ya wafugaji mbali na wakulima mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi bora ni lazima Serikali za mitaa zipate uongozi bora kwa kutokuikosesha Serikali mapato. Ni lazima Serikali iangalie utaratibu wa watu wanaomiliki majumba ya kupanga kulipa kodi Serikalini kwani mara nyingi huwa wanaikosesha mapato Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hao wanaojenga nyumba za kupanga karibu na vyuo vikuu sheria iangalie upya utaratibu wa mkodishaji na mkodishwaji kwani mara nyingi mkodishwaji huwa inamkaba kwani sheria hii inakandamiza upande moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanja, huu uuzwaji wa viwanja ni lazima utaratibu unaotumika ni wa kibaguzi, unamnyima mnyonge asiyeweza kununua kiwanja kwa kweli sio haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba viwanja viuzwe bei ambayo mwananchi wa hali ya chini naye apate fursa ya kununua viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi ni suala mtambuka yaani linagusa karibu kila sekta, Serikali itoe kipaumbele kwa kuongeza Bajeti ili Wizara iweze kufanya kazi zake vizuri, kwa mfano, kupima na kupanga matumizi ya ardhi kwa mfano, mifugo, kilimo, viwanda, huduma za jamii na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusiana na rushwa hasa kwa watumishi waliopo Halmashauri za Wilaya, kwa mfano wananchi wanalazimika kutoa chochote ili wapate kiwanja kikubwa na kilicho katika eneo zuri. Pili, ni ile hali ya watumishi wa ardhi kuhodhi viwanja vingi wakati wa upimaji na baadaye kuviuza kwa wananchi kwa bei kubwa zaidi. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hilo? Tatu ni watumishi wa ardhi kuuza viwanja zaidi ya mara moja. Je, Serikali/Wizara inatoa tamko gani/lipi kuhusiana na watumishi kama hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa ushauri kuwa Serikali iruhusu wahitimu wa fani za ardhi waajiriwe moja kwa moja kama ilivyo kwa fani zingine kama ualimu wa fani za afya ili kupunguza matatizo ambayo yamekuwa ni sugu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga hoja mkono.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia afya na uzima kwa kuweza kuhudhuria Bungeni. Pia ninaipongeza Wizara husika kwa kujitahidi kuandaa hotuba mzuri. Naomba nichangie katika suala la ardhi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anapotokea mwekezaji asiuziwe ardhi kama sio Mtanzania. Watanzania wanaomiliki ardhi kihalali wafanye uwiano na wawekezaji wa kigeni. Kama ardhi ina thamani ya asilimia ishirini ya mradi wote basi mwekezaji avune 80% ya faida ya biashara inayohusika na mradi ukiisha ardhi ibaki kwa yule mmiliki ambaye ni Mtanzania. Akija mwekezaji mwingine afanye naye ubia kwa uwiano mwingine. Jambo hili ni kuwanyanyua kiuchumi na kupunguza umaskini na utaongeza *GDP* ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 14 ukurasa 31 wa hotuba inatamka nia njema ya uanzishaji wa vyama vya ushirika wa nyumba. Na Wabunge wanatakiwa waunge mkono jitihada hizi za Serikali. Jambo hili ni jema lakini maandalizi ya kwanza iwe ni vikao vya warsha, semina na makongamano juu ya dhana hii. Hii ni dhana mpya, wananchi ni lazima waelimishwe kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi iliyopo sasa ni ardhi. Baadhi ya migogoro hiyo ni watu kumiliki ardhi pasi na kupimwa wala kumilikishwa. Ninashauri hati miliki zitolewe bila ya masharti magumu na wale wanaomiliki kwa mirathi ya wazee wao ni vema wakamilikishwa kisheria, pindi mkono wa Serikali uliopo katika eneo linalohusika wanakubali mirathi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nyumba zinajengwa na Serikali *(NH)* zizingatie wafanyakazi wa kipato cha chini na sio vinginevyo, hii ndio njia ya kuwasaidia wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara itarekebisha mapungufu haya, nitaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali kubwa kwa wananchi, Tanzania ina ardhi kubwa sana na kama itatumiwa vizuri basi kutakuwa na mabadiliko makubwa sana kuhusu maisha ya raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi ni vema Wizara iandae mipango mizuri ya matumizi ya ardhi kwa manufaa ya wananchi, mipango hiyo ni lazima iwahusishe wadau wote kwa kuzingatia mipango ambayo Wizara itaipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya ujenzi mzuri kwa nyumba, wananchi wengi sana ni maskini, uwezo wao wa kujenga nyumba ni mdogo sana na kwa maana hiyo wananchi wanashindwa kujenga nyumba bora kwa kutumia vema ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kutoa msukumo kwa wananchi ili waweze kujenga nyumba bora na pia nyumba hizo ziweze kuwasaidia kuweka dhamana Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kufanya mazungumzo na ushirikiano na Wizara ya Biashara jinsi gani na kutafuta uwezekano wa kupunguza bei za zana za kujengea ili kuwawezesha raia wa Tanzania kujenga nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukodishwaji wa ardhi upo katika nchi mbalimbali kwa utaratibu fulani ili kuleta maslahi kwa wananchi. Napendekeza kuwepo na viwanja maalum na muda maalum ambavyo havitaathiri mwananchi ili raia aweze kama anataka kukodisha ardhi kuwe na viwango maalum na wakati maalum ili hatimaye ilete faida kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu utasaidia na kutajirisha wananchi na hivyo kubadili maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuuzwa kwa ardhi, kwanza ardhi ni mali, sio vema kuruhusiwa kuuzwa, ni vizuri kuwe na utaratibu wa ukodishaji wa ardhi kwa maslahi ya Watanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri.

Napenda kuchangia kwa kutoa ushauri katika MKURABITA. Dhana ya kurasimisha mali za wanyonge inagusa zaidi mashamba (ardhi) ya wakulima walio viijijini. Hata hivyo, kasi ya upimaji wa mashamba na utoaji haki milki za kimila ni ndogo sana kutokana na ufinyu wa Bajeti na uchache wa wataalam. Ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa mashamba, mashamba yenye miundombinu ya umwagiliaji yanafanyiwa upimaji *(Topographical Survey)* kabla ya kuendelezwa. Aidha, mashamba yenye umwagiliaji yanapewa kipaumbele na taasisi za fedha kwa kuwapa mikopo kwa sababu *risk* ya ukame inakuwa imepungua, kwa hiyo, taasisi za fedha zinakuwa na imani kwamba mkulima atazalisha mazao na kuweza kurejesha mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mambo matatu yafuatayo; kwanza tufanye ubia kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kuharakisha upimaji wa mashamba. Pili, mashamba ya umwagiliaji yaliyokwishapimwa yawekewe mipaka ya wakulima wadogo wadogo kwa kutumia (kwanza na) ramani zilizopo kupunguza gharama na muda na tatu, mashamba ya mpira na mkonge bado yana matatizo kwa sababu upimaji wa maeneo ili kukamilisha zoezi la ubinafsishaji na uainishaji wa maeneo yanayoombwa kumilikiwa na wakulima bado linasubiriwa.

Aidha, mashamba yanayotakiwa kufutiwa hati (Manispaa ya Mtwara na Lindi) *process* imekuwa ya muda mrefu sana! Nashauri Wizara ya Ardhi ifuatilie hatua za kuchukuliwa badala ya kuahirisha uamuzi kwa muda mrefu ili tujenge imani ya wananchi. Halmashauri ya Manispaa ishauriwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuunga hoja mkono na kuipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uvamizi wa ardhi katika maeneo yanayokaa Wahadzabe vijiji vya Michibwi, Ikolo, Ilamoto na vijiji vingine. Makabila mengine kama ya wafugaji Wasukuma, Wabarbaig na wakulima wanavamia wanamoishi Wahadzabe. Kwanza wanaleta uharibifu mkubwa sana wa mazingira kwa kukata miti, pamoja na maeneo hayo huwa yanatunzwa na Wahadzabe. Wavamizi hawa wanaleta ugumu wa maisha kwa Wahadzabe kwani maisha yao wanategemea asali, mizizi na nyama. Uharibifu huu unawapa ugumu wa maisha na kuishi kwa shida. Je, ni lini Serikali/Wizara itawapa au kuwamilikisha ardhi yao ili wasiingiliwe na watu wengine? Naomba Waziri anipe jibu katika majumuisho ya hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie sisi wananchi wa Iramba Mashariki tujue mpaka halisi wa Wilaya ya Hanang, Mbulu na Jimbo la Iramba Mashariki. Mipaka iliyowekwa na Wakoloni haiheshimiwi. Jiwe la mpaka linasogezwa kuingia Iramba Mashariki. Hivyo ardhi ya Iramba Mashariki inazidi kumegwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iwafikirie Wahadzabe kuwajengea nyumba ndogo ndogo za kuishi ili watulie, waache kuhama hama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa uwezo wao mkubwa wa namna ya uwasilishaji wao mzuri na wa aina yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa viongozi wa Wizara hii wanaushirikiano wa juu kabisa katika Wizara yao na kwa kweli inaanza kuleta sura ya Wizara sasa ukilinganisha na Wizara ilivyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni miongoni mwa Wizara nyeti kabisa katika Serikali hii, hili halitaki mjadala. Hivyo ni vema viongozi wa Wizara kutambua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi sana inayoibuka katika nchi yetu inasababishwa na watu ambao aidha ni wakulima au wafugaji ama wawekezaji. Migogoro hii ni migogoro ambayo inaweza kuepukika, kupungua au kumalizwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na gharama kubwa ya kupima ardhi ambayo ni kitu cha lazima kufanyika, Serikali ingeweza kujipanga ili kuelewa, kupima na kutambua eneo gani la ardhi linafaa la wafugaji na lipi kwa ajili ya kilimo, lipi kwa ajili ya ujenzi na makazi baada ya tafiti na ufafanuzi huo bila shaka Wizara pia itaelewa ni eneo gani litakuwa la uwekezaji na aidha, itakuwa lipi ni eneo la akiba kwa ajili ya Serikali. Lakini pia kuna haja ya kuelimisha umma kwamba ardhi ni mali ya Serikali iwapo Serikali itakapoona kuna mradi ambao utakuwa na manufaa zaidi kwa umma na kwa Taifa basi taratibu zifuatwe ili eneo au ardhi ile inaweza ikatumika kwa manufaa ya wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu baada ya suala hili la kupima na kutambua kama nilivyotangulia kusema. Nina uhakika kwamba kwa uelewa wa Mheshimiwa Waziri na kutambua uwezo wa Katibu Mkuu basi ufumbuzi wa migogoro ya ardhi itaisha na isipoisha kabisa basi itapungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kuniweka hai na uzima hadi leo. Nikushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi hii ya kuchangia. Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba nzuri na mpango mzuri ambao ukitekelezwa kama ilivyopangwa Tanzania na wananchi wake watanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai yangu kuwa ardhi ya Watanzania isitolewe kwa wageni kiholela na kama wanapewa basi kuwa na *limits* za ekari za kuwapa (kuwauzia) na wananchi wakishirikishwa katika maeneo husika *(Community Participation)* hasa wa vijijini *(Rural).* Maeneo yanapotolewa wasiachiwe wanavijiji peke yao kwani umaskini walionao, pia wanajikuta wanauza ardhi zao kwa ekari nyingi sana na kwa pesa kidogo. Kizazi kijacho kitatuuliza/kulalamikiwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Ardhi wagawe viwanja kwa kuzingatia sSheria, kiwanja kimoja mmiliki mmoja na sio kiwanja kimoja wanagawiwa watu zaidi ya mmoja (ni migogoro).

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi wananchi wanapewa viwanja bila kupimwa na hata kama vimepimwa Ardhi hawawasaidii wananchi wakati wa kufuatilia hati ya kumiliki tunaomba Wizara/Idara yenye dhamana kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai yangu kwa Wizara husika washirikiane na Wizara ya Katiba na Sheria ili wananchi waelimishwe, wahamasishwe juu ya Sheria ya Ardhi, Ardhi Vijijini – Sheria ya Mirathi, mjane ana haki ya kumiliki ardhi aliyokuwa anamiliki na mumewe kabla hajafariki dunia, wananchi wa jinsia zote, rika zote wafundishwe ili wanapotokewa na unyanyasaji au

kuwakatili, waweze kuchukua hatua zinazostahili wao wenyewe siyo waende kuzinduliwa na wafuasi wa vyama vya siasa au wasamaria wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai yangu kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwamba isimamie Halmashauri zetu ambazo zipo karibu na jamii hasa ya vijijni ili wawe karibu na wanavijiji katika mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya na vijiji, wasiishie tu katika kilimo tu bali na matumizi mengine ya ujenzi wa nyumba zao na barabara pia (miundombinu) uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai yangu kuwa Serikali inapoamua kupima mipaka kati ya Wilaya na Wilaya, Kijiji na Kijiji, Kitongoji na Kitongoji wataalam wa Wizara husika wasifanye hili peke yao bali wawashirikishe wazee wa maeneo hayo, kwani wamekuwapo tangu enzi na enzi wao wanayajua maeneo na mipaka vizuri na kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kuwa kila mwananchi anayepewa kiwanja kilichopimwa basi apewe na ramani ya kiwanja/kitalu kinachohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi huvamia maeneo ya wazi na kuanza kujenga hadi kukamilisha ujenzi ndipo huwekewa alama za 'X' je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na wakaguzi watakaokagua maeneo ya wazi ili kubaini uvamizi mapema wa maeneo ya wazi? Kwa nini hatua zinachukuliwa baada ya wavamizi kuvuta maji, umeme na kadhalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itangulize miundombinu ikiwemo barabara, mfumo wa maji taka kabla ya kugawa viwanja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inazofanya *so far.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza hatua ya kutolewa kwa hati miliki za kimila katika Wilaya ya Manyoni ambapo hati 6,428 zimetolewa. Hii ni hatua muhimu sana kuelekeza kwenye maendeleo ya kweli. Mimi ni mmojawapo niliyemilikishwa ardhi kwa mpango huu katika Kijiji cha Sanjaranda. Wananchi wamefurahishwa sana na mpango huu. Hatua inayosubiriwa ni ya kutumia hati hizi kuweza kukopa kwenye mabenki ili wananchi walime kilimo chenye tija na cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ichangie mabenki kutambua hati miliki za kimila ili wananchi wakope.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afisa Ardhi wa Wilaya ya Manyoni amekuwa akilalamikiwa sana na wananchi kwa ugawaji usioridhisha wa viwanja na uchelewefu wa kupatikana kwa viwanja. Wananchi wameenda mbali kudai kwamba kuna vitendo vya rushwa. Nashauri Wizara ilichunguze suala hili na pia mtumishi huyu amekaa Wilaya ya Manyoni kwa muda mrefu sana, ingelifaa kama angesogezwa kituo kingine cha kazi ili aweze kuchunguzwa vizuri zaidi kama na huko nako vitendo hivyo anavyolalamikiwa vitaendelea. Nashauri Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanashindwa kufanya kazi kwa sababu hayawezeshwi kifedha kufanya vikao kutatua matatizo ya ardhi yanayowakabili wananchi. Nashauri Serikali itenge fedha za kutosha katika mpango wa *D by D.*

Pia Halmashauri za Wilaya ziwe macho kuona kwamba Mabaraza ya Ardhi hayajanyakuliwa kuongozwa na watu ambao si wa maeneo hayo kwa asili. Tunashuhudia baadhi ya mabaraza yameingiliwa kwa hila za fedha wakachaguliwa wenyeviti ambao si wazawa wa maeneo hayo, matokeo yake wamezua migogoro zaidi na Serikali za vijiji kuhusu ugawaji na matatizo ya ardhi. Wizara ione hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kijiji cha Kitaraka, Tarafa ya Itigi hawataki ardhi yao iliyokuwa *holding ground* ya *Tanganyika Packers* itolewe kwa wawekezaji. Wanaomba ardhi hiyo imilikishwe Serikali ya kijiji cha Kitaraka na si vinginevyo. Naomba Wizara ilione hili, vinginevyo mgogoro mkubwa utazuka siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri Waziri na Naibu wake katika kazi zao ngumu sana. Nawaomba wawe wajasiri zaidi kama ambavyo wameonyesha *so far*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye kukidhi matakwa ya Watanzania, nawapongeza na watendaji wake kwa msaada wao kwake na kukamilisha hotuba hii kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ni nyingi sana zinazoikabili Wizara naomba Waziri awe mkakamavu sana kuzikabili. Matatizo ya migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji kuwe na sheria ndogo ndogo ambazo zitatumiwa kwenye maeneo husika na kuweza kutatua matatizo hayo hususan maeneo haya yote ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Usimamizi wa Ardhi, ningeiomba Serikali ikae pamoja na kujadili suala hili la Mamlaka ya Usimamizi wa Ardhi libakie wapi ili kuondosha misigano inayoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo ya udogo wa fidia suala hili Wizara iangalie kwa kina na ifikie hatua ya kufanya marekebisho kwenye fidia ili wananchi walipwe fidia stahili na inayofanana na hali ya sasa ili wananchi walio na kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia mawazo yangu kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ningependa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali kubwa kwa viumbe hususan wanadamu na hata wanyama, katika ardhi kunapatikana maji ambayo ni sehemu moja ya uhai wa wanadamu yaani bila ardhi hakuna maji, hakuna miti na kwa hiyo, hakuna uhai na wala hakuna ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali ya ardhi katika nchi yoyote inatoa Pato kubwa la Taifa endapo ardhi hiyo haitatumiwa vibaya. Ardhi kama rasilimali inatumiwa katika uwekezaji katika sekta ya kilimo, usafiri wa ardhini, utuaji wa ndege na viwanda kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba Wizara hii itaachana na mtindo wa kutoa ardhi hii kwa wageni kama inavyofanya sasa na kusababisha wazawa kukodi ardhi kwa wageni kwa ajili ya kuendeleza kilimo jambo ambalo linakwenda kinyume na upatikanaji wa ushuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ikiwa Mtanzania ambaye ni mzalia na mkulia wa nchi hii, ni raia anayetambuliwa na sheria lakini anaendesha maisha yake kwa kuendesha kilimo lakini ardhi hiyo anayolima anakodi kutoka kwa mwekezaji ni dhahiri kwamba uhuru huo utakuwa una kasoro na kamwe kujitawala kwetu huko ni kwa njia ya kuwadhalilisha ndugu, jamaa ambao ni tabaka la watawaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni uonevu wa kiasi gani kwamba Mtanzania anaishi Tanzania anafikia hatua ya kukodi ardhi kwa ajili ya kuendeleza kilimo na pengine kiasi cha fedha ambazo anatumia kukodi ardhi hakiwezi kumpatia yeye kipato cha angalau gharama alizokodia ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mtanzania huyu ni kweli kwamba amejitawala katika nchi yake au bado unaendelezwa kunyanyasika na uhuru wake umebanwa? Je, ukoloni tulioukataa si

bado unaendelezwa na wale ambao tuliwapa uongozi wa nchi hii ili watutoe katika dimbwi la ukoloni mamboleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama azma ya kujikomboa ni kuwanyanyasa walio chini kujitawala huku kunaweza kukaja kukatugharimu baadaye, kwa nini haki ya ardhi kwanza asipewe mzawa bila ya kukodishwa ili ajione kama kweli ana uhuru wa kuishi na kuendesha maisha yake katika ardhi ya nchi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Watanzania kama Watanzania hawatendewi haki katika nchi yao, watu wanavunjiwa hovyo, hovyo, wanahamishwa hovyo hovyo wananyang'anywa maeneo ambayo wapo kabla ya Uhuru kwa sababu hawana namna ya kuweza kujitetea, hata fidia hawapatiwi wanaishia vilio vya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawajibu wa kuhakikisha kwamba kwa kuanzia sasa hakuna wawekezaji kutoka nje watakaouziwa maeneo ya ardhi ya Watanzania. Wajibu wa kuuziwa ardhi iwe ni kwa Mtanzania tu na sio kiasi ambacho kitaweza kuzuia vizazi vijavyo kukosa maeneo ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhai wa mwanadamu unahitaji mahali pazuri pa kuishi pamoja na familia na pahala pazuri pa kuishi ni pamoja na kupata nyumba, ni aibu kwa Tanzania ambayo tayari tunadai kwamba tumejitawala kwa muda wa miaka 50 lakini mpaka leo kuna Watanzania ambao wanaishi ndani ya vibada vya nyasi visivyozidi futi 12 pamoja na familia zao. Hivyo ni viongozi wangapi ambao wanaweza kuishi katika vibanda vya nyasi vyenye futi 12 pamoja na familia zao kama ambavyo Watanzania wengine wanaishi? Si vema wala si wema na ni kinyume na haki za binadamu juu ya maisha wanayoishi wananchi wengi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nchi yoyote yanapatikana endapo wananchi wataishi bila ya matatizo na migogoro inayotokana na ardhi ambazo zimekuwa zikimilikiwa na baadhi ya wawekezaji lakini vilevile mipaka baina ya wamiliki hao wa ardhi pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba matajiri, wageni na viongozi wa nchi wasipewe maelfu ya mahekta ya ardhi kwa kufanya kuwa na milki zao au kwamba wao tu ndio wenye haki ya kumiliki maeneo makubwa ya ardhi kinyume na wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha bila ya kuunga mkono hoja mpaka pale ufafanuzi wa kina utakapotolewa kwa kina.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Shirika la *CDA* (Dodoma) kuanzishwa mwaka 1973 kwa ajili ya ujenzi wa Mji wa Dodoma, nyumba nyingi zimebomolewa na mashamba mengi kuchukuliwa na *CDA.* Wakati zoezi hili linafanyika, watu wamelipwa fidia kidogo sana kiasi kwamba watu wameshindwa kujenga tena nyumba nyingine na kuingia katika ufukara mkubwa. Malalamiko mengi ya wananchi/wakazi wa Mji wa Dodoma yanahusu malipo ya fidia ya nyumba zilizobomolewa na mashamba yao yaliyochukuliwa na *CDA* kwa fidia ndogo sana. Kwa sababu suala hilo la fidia linaleta mgogoro mkubwa sana hapa Dodoma, napendekeza kuwa Serikali iweke mpango wa makusudi kabisa wa kukusanya malalamiko yote yanayohusu fidia duni iliyotolewa kwa nyumba zilizobomolewa na mashamba yaliyochukuliwa na *CDA* hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa Wizara itoe agizo kwa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba (Dodoma Mjini) wawe wamekusanya malalamiko yote ya fidia za ardhi na nyumba kwa muda mfupi usiozidi miezi mitatu (Septemba – Novemba, 2011). Inawezekana mabaraza haya kwa uhakika, wangeweza kukusanya takwimu kutoka Kamati za Maendeleo za Kata *(WDC),* ambao wangeratibu kukusanya malalamiko ya wananchi waliopo kwenye kata zao. Baada ya hapo ni vema Serikali ikalipa fidia ili kuepuka malalamiko ambayo yamedumu kwa muda mrefu hadi sasa. Wananchi wamejipanga maandamano mengi hapa Dodoma, lakini yote yamedhitibiwa. Lakini udhibiti wa maandamano kwa kutumia vyombo vya dola (polisi) siyo ufumbuzi wa kweli wa matatizo ya fidia. Fidia ni sawa na deni. Dawa ya deni ni kulipa deni, na

wala siyo kutumia polisi kumdhibiti mdai. Yapo malalamiko mengi na makubwa sana ya madai ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Nzuguni ambapo wananchi waliondolewa kupisha jeshi, na bado hawajalipwa fidia zao, Kata ya Ngh'ongh'ona ambapo wananchi waliondolewa kupisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* na Kata ya Msalato, ambapo wananchi waliondolewa kupisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni hiyo hiyo kwenye Kata za Chang'ombe, Ipagala, Ntyuka, na Tambukareli ambayo imelalamikiwa na wenzetu wa Kambi ya Upinzani (Ukurasa 21 wa hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Bungeni).

Kwa nyongeza tu haipendezi kuona kuwa Bunge lipo Dodoma, Makao Makuu yapo Dodoma, Ofisi Kuu ya Chama Tawala CCM ipo Dodoma lakini Dodoma ukiwa ndiyo mji wenye migogoro mingi ya fidia ya ardhi na nyumba, *charity begins at home,* tusafishe kwanza Dodoma ambapo ndiyo Makao Makuu ya Chama Tawala na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi baada ya hapo twende na sehemu nyingine kama Dar es Salaam na miji mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CDA* wakabidhi ardhi Manispaa ya Dodoma, kimsingi kazi ya *CDA* ni kuchora mji, kusimamia ujenzi wa miundombinu (nyumba, barabara na kadhalika) ili ujenzi wa mji wa Dodoma uwe ni wa viwango. Sasa hivi *CDA* wamepewa kazi nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachora ramani wanasimamia ujenzi wa nyumba, barabara, ujenzi wa mabomba ya maji safi na maji taka, kupeleka umeme wenye makazi mapya, kuupamba mji *(city landscaping),* kugawa viwanja, kubomoa na kulipa fidia. Matokeo yake, kazi zote zinakuwa hafifu na migogoro ya ardhi kuzidi kupita kiasi. Ujenzi wa Mji Mkuu sasa unasuasua kwa muda wa miaka 37 (1973 – 2011) na Wizara nyingi bado zipo Dar es Salaam.

Napendekeza *CDA* wapunguziwe kazi, wabaki na kazi ya kuchora, kusimamia ujenzi na kupamba mji. Kazi ya maji wakabidhi *DUWASA,* kazi ya barabara wakabidhi *TANROADS,* kazi ya kugawa ardhi wakabidhi Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ambao kisheria ndiyo wenye ardhi. Mgawanyo wa kazi *(delegation of duties),* utarahisisha utendaji wa kazi, kero nyingi zitatatuliwa mapema na utawala bora kuimarika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni matumaini yangu kwamba Serikali itajali kutumia Mabaraza ya Ardhi (ukurasa 6 na 16) ili kumaliza matatizo yote ya ardhi Dodoma kwa kushirikiana na Kamati za Maendeleo ya Kata *(WDC),* na kukabidhi ardhi ya Dodoma Mjini kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ili kupunguza au kumaliza kabisa migogoro ya ardhi na fidia katika jimbo letu la Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninazipongeza hotuba zote zilizowawasilishwa na Waziri kwa niaba ya Serikali, Kamati ya Kudumu ya Ardhi pamoja na ile ya Kambi ya Upinzani. Naiomba Serikali izingatie yote yaliyowasilishwa na upande wa Upinzani kwa manufaa ya nchi yetu na ustawi wa jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi na makazi ni tete kiasi kwamba limewagawa Watanzania kimatabaka. Tumeshuhudia Serikali ikiwajali sana wawekezaji kuliko Watanzania ama wananchi wazawa. Serikali imekuwa ikigawa ardhi kwa wawekezaji bila kuwaandaa Watanzania kwa maana ya kuwahakikishia makazi mapya, gharama na usumbufu mwingine unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliyo madarakani inapaswa kufahamu uwezo wa raia wake, mara nyingi fidia zinazotolewa kwa waathirika hawa ni ndogo na hazitoshi kuandaa makazi mapya na hivyo kupelekea mgogoro kama vile maeneo ya Kigamboni na Chasimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iutatue mgogoro wa ardhi uliopo Mkoani Mara kati ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) na wananchi wa Bukanga na Buhare kutokana na Jeshi

kujimilikisha maeneo hayo jambo ambalo linazusha mtafaruku mkubwa sana. Serikali iingilie kati na ajulikane mmiliki halali. Sambamba na hilo ardhi ambayo imechukuliwa na wakubwa katika Halmashauri ya Mvomero (Shamba la *NARCO)* ardhi ambayo ilikuwa inapangwa kugawiwa wanakijiji wa Wami, bado ni mgogoro mkubwa. Tunaitaka Serikali iwarejeshee ardhi hii Wanawami kwani waliopewa yaani wakubwa hao sio wanakijiji wa Wami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na siungi mkono hoja hata kidogo kwani raia wanaonewa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali. Kwa thamani ya ardhi ikiwa ardhi imesajiliwa na ina hati ni dhamana tosha kabisa kwa mwananchi kutumia hati hiyo kupata mikopo kwenye mabenki. Hata hivyo benki zetu hapa nchini zimekuwa hazitoi mkopo kwa kiwanja ambacho hakijajengwa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi anataka akope ili ajenge, ananyimwa mkopo wa kujenga kwa maelezo kwamba hakuna kitu cha thamani pale, napenda kujua Wizara ya Ardhi inashirikianaje na Wizara ya Fedha kuongea na mabenki ili mikopo itolewe kwa dhamana ya hati za viwanja ili wananchi waweze kujenga nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatamka wazi kwamba Serikali inawajibika kuwafidia wananchi wanaotoa ardhi yao kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kata ya Kaliua Wilaya ya Urambo wapo wananchi waliobomolewa nyumba zao miaka ya 2003 wakati wa kupanua barabara ya Kaliua kwenda Usinge – Nguruka. Wananchi wale wamefuatilia Wizara kila mwaka tangu mwaka 2007 hadi leo hakuna majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aeleze wananchi wale wa Kaliua ni lini watalipwa fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa kupanua barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali iweke utaratibu wa kulinda ardhi ya nchi hii tuliyojaliwa kwa ajili ya Watanzania wa leo na vizazi vijavyo. Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ilikataza wawekezaji wageni wamilikishwe ardhi kwa muda mfupi kuendana na mradi anaotaka kuanzisha. Sheria ya Ardhi ya mwaka 2001 imeruhusu wageni kumilikishwa ardhi. Hapa kuna tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilete Sheria hapa Bungeni tuirekebishe tuondoe mwanya wa kumilikisha wageni wawekezaji ardhi. Tuweke kipengele cha mwekezaji kulazimika kuingia ubia na mzawa Mtanzania na ardhi ya mwekezaji iwe ndiyo sehemu (mchango) wa Mtanzania na mwekezaji atoe fedha za kuendeleza mradi lengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tutaweka mazingara ya Watanzania kushiriki kwenye miradi mbalimbali na pia tutaondoa migogoro ya ardhi inayomilikishwa kwa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuzwaji wa viwanja vya ufukweni, kitendo cha Serikali na baadhi ya Watanzania kuuza viwanja vya ufukweni kwa Wasomali ni hatari sana kwa amani ya nchi na usalama pia. Huku ni kuweka nchi hatarini kuvamiwa na watu kutoka nje kwani ni maeneo haya ni *entry point* (milango ya kuingilia).

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunaelewa jinsi ambayo Wasomali wamekuwa wanavamia meli baharini kila leo na kuharibu maisha ya watu na hata kuteka watu. Ikiwa tunawapa viwanja hivyo wakajenga chochote kama nyumba au hoteli na kadhalika hatuoni tunatoa mwanya kwa wao kuweka mazingira ya kuweka maficho na hivyo kuweza kufanya uharamia usiku na kuweka mali za wizi maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ieleze nini mikakati wake wa kuondoa tatizo hili ambalo ni *timed bomb?* Na kwa viwanja ambavyo tayari wamemilikishwa wageni nini kitafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itoe majibu ni kwa nini Serikali inajichanganya? Inakuwaje Serikali inasajili ardhi na vijiji na mipaka yake kisheria halafu Serikali hiyo hiyo inaendesha operesheni za kuwachomea wananchi nyumba zao walizojenga kwa zaidi ya miaka 30?

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Shela na vitongoji vyake vyote katika Kata ya Usinge Wilaya ya Urambo kimesajiliwa kisheria na kimewekewa alama za mipaka lakini kila leo wananchi wanabugudhiwa kwamba wako hifadhini. Kama wapo hifadhini kwa miaka 30 Serikali ilikuwa wapi? Na kama wapo hifadhini kwa nini kilipimwa na kusajiliwa kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ieleze kwa nini haya yanatokea na wananchi wanaonekana kama wakimbizi wakati wapo kisheria kwenye maeneo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Tabora linaloendelea wanaotoa maeneo yao wanatakiwa kulipwa fidia kuendana na eneo walilotoa. Kuna dhuluma kubwa inafanywa na watendaji wa Serikali ngazi ya Kata na Afisa Ardhi Wilaya kuingiza ufisadi. Wanaostahili kulipwa fidia hawa hawajawekwa kwenye orodha ya majina badala yake (kwa taarifa) yamewekwa majina bandia ili wasiohusika wachukue haki za waliotoa maeneo yao.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu katika Wizara hii muhimu kwa maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nizungumzie juu ya matumizi yasiyo sahihi ya fukwe zetu zilizopo katika Bahari ya Hindi hususan katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, fukwe zote za Dar es Salaam ambazo zinafaa kwa matumizi ya umma na kupumzikia zimejengwa, zimeuzwa na kusababisha wananchi wanaotaka kupumzika ufukweni kulipa kiingilio ili waweze kuingia katika fukwe hizo. Hivi ni sahihi kwa majengo ya kiuchumi kujengwa pembeni kabisa mwa bahari? Je, ni sahihi kwa watu wachache kumilikishwa maeneo ya ufukweni na kuwanyima wananchi wa Dar es Salaam kutumia maeneo hayo ambayo wamejaliwa na Mwenyezi Mungu? Leo hii mkazi wa Dar es Salaam hana tofauti na wa mikoani kwani bahari wanaisikia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia juu ya migogoro ya ardhi iliyopo katika maeneo mbalimbali yenye machimbo ya madini hapa nchini. Kipekee katika jambo hili nizungumzie juu ya migogoro ya ardhi iliyopo katika machimbo ya dhahabu yaliyopo katika kijiji cha Sambaru, Kata ya Mang'onyi Jimbo la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupatikana kwa dhahabu katika eneo hili imekuwa siyo neema bali ni maafa kwa wanakijiji wa vijiji hivi. Wanaoitwa wawekezaji wamefika katika vijiji hivi na kuzungushia uzio katika mashamba ya wanakijiji kwa madai kuwa ni maeneo ya machimbo na hivyo wananchi kukosa ardhi ya kulima mazao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwa ni jambo la kawaida kuwa Serikali yetu kuwanyanganya wananchi maeneo yao na kuwagawia wanaoitwa wawekezaji na tena bila kuwalipa fidia au kuwapa fidia ndogo sana wananchi na hivyo kushindwa kuendesha maisha yao na hasa mahitaji yao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgogoro huu wa vijiji vya Sambaru na Mang'onyi naitaka Serikali iwatendee haki wananchi ili kama ni sahihi kwa ardhi yao kutwaliwa basi walipwe fidia wanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie juu ya urasimu uliopo katika Wizara ya Ardhi. Ni vigumu sana kupata huduma kama vile vibali vya kujenga, hati za viwanja na kadhalika katika Wizara ya Ardhi. Jambo hili linasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi ambao mara nyingi hulazimika kulipa/kutoa rushwa ili waweze kupata huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mimi mwenyewe nilinunua kiwanja *Plot No. 2027 Block L* Mbezi Dar es Salaam lakini tangu mwezi Machi, mwaka huu nimekuwa nikifuatilia kubadilisha jina toka mmiliki wa mwanzo ili hati iwe kwa jina langu lakini hadi leo hii sijafanikiwa katika Wizara ya Ardhi. Hiki ni kiwanja ambacho hakina mgogoro wowote na kilikuwa na hati, kubadilisha jina tu imekuwa muda mrefu na wala sijui nitafanikiwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimu huu unasababisha wananchi waishi katika maeneo yasiyorasimishwa na washindwe kunufaika kiuchumi na ardhi wanazomiliki au nyumba wanazoishi kwa kutokuwa na hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri afuatilie kwa Katibu Mtendaji katika Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu litambue umuhimu wa ardhi, pale kwenye Azimio iliposema, maendeleo yanapatikana kwa kuwa na ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ardhi ndiyo utajiri na rasilimali ya asili kwa mwanadamu, hivyo haingii akilini kwa wanaopewa dhamana ya ardhi kutokuona umuhimu wa kuwarithisha wananchi ardhi yao. Madhumuni ya Serikali kuimiliki ardhi hii kuhakikisha kila Mtanzania anapata ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima ijipange kupima ardhi kwa ajili ya makazi, michezo, kilimo, mifugo na ardhi kwa wawekezaji. Ili kufanikisha hili nashauri kila kata igawe ardhi kama nilivyoeleza hapo juu. Madhara ya kuwahamisha watu kunawatia umaskini watu, kuchelewa kutolewa uamuzi watu kama vile Kigamboni, ni dhahiri kuwa wanawaelekeza watu katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba, Wizara kwa kushirikiana na *NHC* lazima wabuni teknolojia ya kujenga nyumba kwa teknolojia rahisi kama Malysia/Iris wanajenga nyumba kwa siku saba kutumia takataka na vyuma kidogo tu na leo Malysia wana nyumba za ziada. Kwa teknolojia ni miaka miwili Manzese itakuwa na taswira mpya, *NHC* tunawapongeza watafute teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bajeti ya Serikali, Bajeti ya Wizara kupata 60% kwa *recurrent* na 25% kwa *development* hatuwezi kufika pahala.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa Wizarani, ili kupambana na rushwa Wizarani, wahamishwe, zipatikane sura mpya, pengine itasaidia pia uchunguzi ufanywe kwa kutumia *forensic experts* kugundua tatizo la *double allocation* na uchakachuaji wa nyaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya Sheria ya Ardhi ni jambo muhimu lakini usimamizi wa sheria ni jambo muhimu sana. Wenye fedha hawasukumwi wala kuhamishwa lakini wanyonge ndio kila wakati wanatakiwa kufuata sheria. Wizara ijipange katika kutatua migogoro kwa kuunda *task force* kila Wilaya na *time frame* ya kutatua migogoro. Pia Wizara iwachukulie hatua wale waliobainika kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya viwanja, watu walioishi kwa muda mrefu katika eneo ambalo Serikali inataka kuendeleza, ni vema katika ujenzi kama alivyofanya Mzee Karume walipewa waliovunjiwa na bila ya malipo huku watu wanalipwa fidia ndogo na hapati hata kiwanja kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku ni kumuongezea umaskini raia wa kipato cha chini. Bei za viwanja ni kubwa, watu wa kawaida hawawezi hivyo pengo baina ya walio nacho na wasio nacho inaongezeka hii ni hatari kwa Taifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa hotuba nzuri iliyotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Halima Mdee, vilevile Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na mwisho nimpongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka kwa hotuba yake kubeba wazo zuri la kujenga *city centre parks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yangu nitaielekeza katika makundi makuu matatu kama vile Wizara yenyewe ilivyojieleza yaani nitazungumzia Kitengo cha Ardhi, Kitengo cha Nyumba na mwisho Kitengo cha Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia migogoro ya ardhi ambayo kwa sasa imekithiri sana na migogoro hii ni kati ya wananchi na mwekezaji, mwananchi na JWTZ, mwananchi na wasiokuwa wazalendo (wakora) mwananchi na wageni (wasiokuwa Watanzania) na wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia migogoro iliyopo kati ya wananchi na mwekezaji, tumekuwa tukishuhudia migogoro na manyanyaso yanayoambatana na kutolipwa fidia kabisa au kulipwa fidia kiduchu ambayo haiendani kabisa na ardhi husika pamoja na hali anazokuwa nazo mwananchi mwenye milki ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata majibu yenye kukidhi ni kwa nini wawekezaji wanapokuwa wampewa ardhi na Serikali, Serikali inashindwa nini kuhakikisha kwamba maeneo yaliyopangiwa kazi mpya na Serikali fidia zinalipwa mapema na kupima sehemu mbadala ili wahame na ndio kazi mpya ya ardhi ianze. Kwa kuzingatia hili na kukazia hoja hii, ni kuhusu eneo ya Nyabigena na Nyabitama lililopo katika eneo la Mgodi wa *North Mara* huko Nyamongo. Inasikitisha kuona Barrick wanaendesha shughuli za uchimbaji na kumwaga vifusi kwa umbali wa mita mbili toka nyumba za wakazi wa eneo la Nyabigena na Nyabirama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi majuzi siku ya tarehe 8.8.2011, tulipozuru eneo lile hakika tulisikitishwa na hali ile na nilimhoji meneja kwa nini wanaendelea na shughuli ilhali wananchi hawajahama, wakasema ndio wapo kwenye *process,* ina maana fedha ni bora kuliko maisha ya binadamu wale. Siku ile tupo pale Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, tulishuhudia wakimwanga vifusi na vumbi lote likaingia ndani ya zile nyumba za wakazi wale na mbaya zaidi wakazi wale wanalalmika kwa vumbi, kelele na hata watoto wao kufukiwa na vifusi, kwani kuna *incidence* watoto chini ya miaka mitano waliokolewa na kufukiwa na kifusi, wanaathirika na kelele na hata nyumba zao zinaingia nyufa. Watoto wanapata *brain damage* na madhara mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka katika majumuisho yake Waziri atuambie ni lini ile shule ya Nyabinege itahamishwa pale maana hamna elimu inayotolewa wala kupokelewa pale na majengo yale yamejaa nyufa sana, vilevile aniambie ni lini tena iwe ndani ya mwezi ujao sababu wakaz wote wale zaidi ya kaya 54 inabidi zihamishwe mapema sana, naomba majumuisho kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusiana na hii dhana ya JWTZ kuvamia ardhi ya wananchi kisha bila hati miliki, kisha Serikali inawakingia kifua kwa kusema kuwa imetwaa eneo hili kwa usalama wa nchi, hivi ni kweli ni haki usalama wa nchi mfano wa ardhi ya Ronsoti ambayo wanajeshi wale walikaribishwa kwa muda tena kuwa kupewa heka moja leo hii wanaamua kuvamia na kuwafukuza wananchi. Hivi kwa sheria inavyotamka kwamba Kambi ya Jeshi lazima iwe mbali na makazi ya wananchi na ndio maana Serikali mwaka 1978 waliwapa hawa JWTZ 28 KJ kumpa *Nyandoto farm* eneo ambalo ni kubwa na mbali na makazi ya watu na ndio ingekuwa eneo muhimu kiusalama kwani halitoi muingiliano na wananchi wengine. Mbaya zaidi Waziri alisema wananchi wameridhia, ukweli ni kwamba wananchi hawajawahi kuambiwa kuhusu fidia na kukubaliana na isitoshe kaya ambayo zilifanyiwa tathmini ni 14 tu wakati pale kuna kaya zaidi ya 158. Sasa hawa wengine walioachwa bila kuingizwa kwenye tathmini hii ini nini hatima yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile uvamizi mwingine uliofanywa na hawa JWTZ ni ule wa Musoma Mjini kwenye maeneo ya Bukanga na Buhare (Mgaranjabo) ambapo jeshi limevamia na

kujimilikisha maeneo ya kiasili ambayo kabila la Wakurya walikuwa wakitumia kwa shughuli za kimila, sasa kwa jeshi kuchukua ina maana Serikali haitambui mchao wa mila za makabila mbona huwa naiona Serikali ikiongea na wazee wa mila, iweje leo inashindwa kuthamini mchango wao? Na bila hata aibu inatwaa maeneo hayo na kuwa JWTZ. Naomba sana watu hawa wa kabila la Wakurya wapewe maeneo yao ya asili na JWTZ watafute maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni uvamizi wa wageni na kumilikishwa ardhi ya Watanzania. Mfano katika swali langu la msingi la tarehe 10.8.2011 Waziri alisema hawana taarifa ya wageni (Wakenya) kuvamia maeneo ya Watanzania ambapo niliainisha kuwa kuna wageni wamemilikishwa au jimilikisha ardhi ya kijiji cha Ikoma upande wa Ponga na vijiji vya Nyabirongo na Kiongera ambapo Wakenya hawa majina niliwapa Waziri (Mheshimiwa Ole-Medeye) naomba ayafanyie kazi majina hayo ili Watanzania hawa waliopokonywa ardhi warudishiwe ardhi yao ambayo kuna makaburi ya babu zao na sehemu ambazo Watanzania wa vijiji hivi hutumia kwa kulima na Serikali hii hii inasisitiza Kilimo Kwanza. Sasa hivi kwanza itafanyika wapi? Naomba majibu katika hili pia. Wakenya baadhi waliovamia eneo hili ni Ochola Obobo, Okothi Obobo, Peter Oto, Elias Oto, Opeyo Onunu na Obuolo Nyamtemwa, fuatilieni haya na mtagundua mengi kwa sababu umilikishaji huu wa ardhi kwa wageni unavunja Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 ambayo inapiga marufuku ardhi kupewa kwa wageni kwenye vifungu 19(2), 20(2) 20(3) na 20(4).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika kipengele hicho cha ardhi napenda kuonyesha masikitiko makubwa kabisa kwa Serikali kushindwa kulipa fidia pale inapoamua kutwaa ardhi kwa matumizi mengine. Mfano ni ule wa kuhamisha wananchi wa Mbarali ili waondoke na kupisha upanuzi wa Mbuga za Ruaha. Kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani ukurasa namba 18, ambapo ameainishwa kuwa wananchi kaya 16,000 wamehamishwa na Serikali ilitenga shilingi bilioni 6.5 ambayo kwa wastani ni shillingi milioni 4.5 kwa kila kaya. Hapa kuna maswali mengi ya kujiuliza je, ni wakazi wote walilipwa na je, malipo yalikuwa na *flat rate* ya kulipa na kumbe wote walikuwa na thamani sawa ya ardhi?

Jibu ni hapana kwani tumeshuhudia wahanga wa kupisha upanuzi wa Ruaha wakiteseka kama ilivyoainishwa kwenye Gazeti la Mwananchi toleo la tarehe 2 Agosti, 2011 siku ya Ijumaa, ukurasa wa 4 na 5 ambalo limebeba kichwa cha habari kisomekacho; "Leah Mwasimini: "Naishi chini ya mti na familia yangu" ukiona picha ya mama huyu na wanawe wawili wenye umri wa miaka miwili na mwingine miezi mitatu hivi, hakika utaona machozi kwani watu hawa wanaishi chini ya mti hawana nyumba wala hifadhi kwa malaika hawa wadogo na mama yao wasiokuwa na hatia. Nataka kujua kama Wizara kwa maana ya Waziri na watendaji wao wameshaliona gazeti hili na tukio la huyu mama na kama ndio ni hatua gani zimechukuliwa. Maana inatia uchungu sana na nataka kupata majumuisho kwa hili. Huyu mkazi wa mahali alilipwa halali yake na kama bado kwa nini na Serikali inachukua hatua gani? Mama huyu Leah yupo kijiji cha Luhanga, Wilaya ya Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kuhusu nyumba. Ni dhahiri kabisa kuwa ulimwengu wa sasa ambapo ustawi wa miji umekuwa ukiongezeka kwa kazi kubwa na hii inapelekea wimbi kubwa la watu kuhama toka vijijini kwenda mijini ni hii inapelekea uwepo wa uhitaji wa nyumba za kuishi hii inaongezewa pia na kiasi kikubwa cha wahitimu wa Vyuo Vikuu na vyuo vingine nchini ambavyo vinatoa idadi kubwa ya watu wanaoingia katika soko la ajira na kundi hili halina nyumba kwa maana ya kuhitaji nyumba za kupanga, na tuzingatie kuwa kuainisha vipato vya watu hawa na gharama za nyumba ambazo kodi zao zimekuwa zikipanda siku hadi siku. Mfano leo hii chumba maeneo ya Dar es Salaam cha kawaida kabisa kama Simba chumba kimoja na sebule au vyumba viwili vyenye choo cha kuchangia na wapangaji na au kipo nje lakini utashangaa bei ni shilingi 100,000 na zaidi. Tena ukiona tunyumba twenyewe utalia machozi na ada au pango lazima ilipwe kwa mwaka au miezi sita, na mijini kuna watu ambao wana vipato tofauti kuna dereva teksi, mama ntilie, wafanyabiashara wadogo wadogo na wengine wengi wa kada ya chini ambao kipato kwa mwezi si zaidi ya laki na nusu, na mahitaji si pango tu, kuna kula, kutibiwa, kusomesha watoto na kuweka akiba. Hivyo kama Kambi ya Upinzani ulivyoshauri ni dhahiri sasa tunahitaji kuwa na chombo cha kuthibiti bei za pango la nyumba *(Real Estate Regularoty Authority)* au wakala wa bei za pango la nyumba *(Real Estate Rented Agent).* Hii itasaidia sana kuwepo na *standard* za bei kulingana na vyumba yenyewe, eneo iliopo baadhi ya vitu vingine kama ukubwa wa vyumba, hivyo kuwepo na bei ya chini *(minimum rate*). Hivyo *range*

hii itasaidia kama *indicator*. Hili pia litasaidia Serikali kupata kodi kutoka kwenye pango kwani kwa sasa hamna ufuatiliaji wa karibu. Kwani wenye nyumba za upangishaji wa kati na chini hawalipi kodi kabisa na hii hupoteza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya mwisho ni kuhusu maendeleo ya makazi, katika hili napenda kuelezea juu ya mawazo mazuri kabisa ambayo aliyekuwa mgombea Urais kwa tiketi ya CHADEMA (Mheshimiwa Wilbroad Slaa) alielezea mikakati ya kuondoa kabisa nyumba za tembe. Ingawa watu wengi na hasa wale wa Chama Tawala walibeza hili wazo pasikuomba ushauri wa dhati toka kwetu. Leo hii mfuko wa *cement* inauzwa kwa bei ya kati ya shilingi 14,000/= hadi 20,000/= inategemea inauzwa Mkoa gani. Lakini kama kwenye hotuba ya Kambi ilivyojieleza, kwamba leo ukinunua *cement* toka Pakistan zaidi ya tani 600,000. Bei hadi bandarini ni shilingi elfu tano na mia tatu hivi. Sasa hapo ikiweka *freight* tuseme gharama ya juu kabisa ni shilingi 7,000/= na hapo ni kama Serikali wataondoa kodi kama kweli wana nia ya kuendeleza makazi ya wananchi wake. Vilevile kwenye michango yangu ya Bajeti kuu, nilitoa ushauri wa kupunguza vifaa vya ujenzi moja ila wa kutoa ruzuku. Lakini sasa ukiangalia pia kuwa viwanda vya kuzalisha *cement* mfano *Twiga Cement* inashapandisha bei kuwa juu licha ya kwamba wanatumia gesi katika kuzalisha na si umeme. Je, Serikali inaona hili na hatua gani inachukua? Vilevile bidhaa zingine kama nondo, bati vyote vipo juu na hii inapelekea kuona makazi bora kuwa ni ndoto ya Abunuiwasi. Naomba Serikali ilitazame hili kwa upekee kabisa ukizingatia fidia yenyewe inayotolewa ni shilingi 200,000/= hadi 4,500,000,000. Hii ni aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nitoe tena pongeza kwa wazo zuri la Waziri la kujenga *park.* Nimekuwa nikijiuliza hivi viongozi wetu hawaoni nchi za wenzetu wana *park* zenye kila aina ya viwanja vya michezo kwa watoto wetu? Maana kwa sasa kupumzika ni kwenda *beach*, vinginevyo watoto wetu tunawapeleka baa ambapo kuna vibembea eti hapo ndio *park,* aibu kabisa. Nashauri wazo hili lisijikite tu Dar es Salaam, bali liwe ni la nchi nzima hata kwenye Manispaa walau moja kila Wilaya au Jimbo. Hii itasaidia kuleta maadili mema kwenye jamii yetu kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasubiri sana hoja hii ili nichangie kwa mdomo, kwa sababu Wizara hii ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya watu. Kwa sababu nimekosa nafasi hiyo naomba nichangie katika maeneo yafuatayo kwa ufupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Sheria ya Ardhi na yaliyopo juu ya ardhi, chini (madini, mafuta na kadhalika), mito na misitu hii ndio maliasili ya nchi. Kwa umuhimu huu umiliki wa ardhi ingetakiwa iwekwe kwenye Katiba, hii haijafanywa. Napendekeza kama ilivyo katika Katiba za Ghana, Kenya, Afrika Kusini, Nigeria na Uganda ardhi ya nchi hii umiliki wake uwekwe kwenye Katiba inayotarajiwa kuandikwa upya ikiwa ni masharti kwamba ardhi ya kijiji isimamiwe na wanakijiji na endapo Serikali ikitaka kufanya lolote iwe ni lazima wananchi hao waridhie na mikataba mikubwa idhibitiwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuzaji wa ardhi iwe ni *lease* sio moja kwa moja. Wageni wasipewe *lease* ya ardhi kwa zaidi ya miaka 50 duniani kote wageni hawamilikishi ardhi wala *lease* wanayopewa haizidi miaka 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi yamekuwa kero hasa za Wilaya na Mkoa. Nashauri Sheria ya Ardhi irekebishwe ili Wenyeviti wa Mabaraza wadhibitiwe barabara. Kuhusu Mabaraza ya Kata nashauri Mabaraza haya yaboreshwe, nampongeza Waziri amesema katika hotuba yake kwamba viwango vya mamlaka kukosa thamani *(Perceniary Jurisctcation)* itaongezwa hapo sawa. Nashauri ili kuondoa migogoro sugu ya ardhi, Mabaraza ya Ardhi ya Kata wapatiwe Makatibu wakome na wajumbe wapangiwe posho itakayolipwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maafisa Ardhi, hawa waondolewe katika TAMISEMI warudishwe Wizara ya Ardhi kwa ajili ya uwajibikaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji ardhi naungana na wenzangu katika hili ikiwa kila mtu apewe hati miliki yenye mipaka migogoro yote ya miaka na urithi zitaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Baraza la Ardhi katika Wilaya ya Mbulu, Wilaya hii ipo pembezoni, Baraza lililopo ni la Mkoa – Babati ambalo ni umbali wa kilomita 106. Kutokana na miundombinu iliyopo inachukua siku nne, mbili kwenda na mbili kurudi. Naomba Wilaya ipatiwe Baraza la Ardhi na Nyumba. Halmashauri iko tayari kutoa ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji na ubinafsishaji kwenye ardhi. Miaka ya hivi karibuni nchi yetu imekuwa ikihamasisha wawekezaji kutoka nje ya nchi, kuja kuwekeza kwenye shughuli za kilimo, migodi na viwanda shughuli ambazo zimekuwa zikichukua sehemu kubwa ya ardhi na kuwaacha Watanzania kubaki na tatizo la uhaba wa ardhi. Mfano kupitia miradi ya *EPZ* ambapo mwekezaji anamilikishwa sehemu kubwa ya ardhi na kuanza kutozwa kodi baada ya miaka kumi ya uwekezaji kupita jambo ambalo wananchi wanahamishwa kupisha mwekezaji, kulipwa fidia ndogo inayowaacha Watanzania kubaki maskini katika nchi yao na kubaki vibarua kwenye miradi ya wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ina dhamira ya dhati ya kutengeneza ajira na kuboresha maisha ya Watanzania kwa nini uwekezaji wa kilimo usishirikishe wanavijiji kwa kupewa elimu ya kutosha ili waweze kuzalisha na wawekezaji kununua kwa bei iliyo nzuri badala yake wananchi wanahamishwa kupisha uwekezaji. Jambo ambalo kwanza wananchi hawafaidiki na miradi hiyo pia inawaongezea umaskini kwani wanalazimika kuhamishwa maeneo mapya kwa kupewa fidia ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa uendelezaji wa miji. Katika mpango unaowataka wenye ardhi walipie maboresho ya ardhi ili waweze kuepukana na kero ya ardhi yao kutwaliwa, wao kupewa fidia na viwanja kugawiwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mpango huu hauwashirikishi wananchi wenye kipato cha chini ambao ardhi ni mali yao ili waweze kuwa na hisa kwenye miradi hiyo mipya katika ardhi yao badala yake Serikali inataka kuwahamisha na kuwapeleka maeneo mapya ambayo hayana huduma za kijamii za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mipango yote ya miji haipo rafiki kwa wananchi walio maskini na kuwapendelea wenye nacho tu. Mipango yote imewageuza wananchi wenye kipato cha chini kama makatapila ya kusafisha maeneo halafu baadaye wanahamishwa kupisha wawekezaji wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *double allocation* kwenye ardhi. Kumekuwa na migogoro ya viwanja hasa maeneo ya mijini ambapo wamiliki zaidi ya mmoja wanapewa hati kutoka Wizara ya Ardhi. Lakini mgogoro inapotokea wamiliki hawa Wizara inajitoa na kuacha wananchi kudhulumiwa ardhi na kusababisha mrundikano wa kesi za ardhi mahakamni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inawezaji kutoa hati ya umiliki kwa zaidi ya mtu mmoja na maafisa hawa wa Wizara wanaoshiriki kitendo hicho wanajulikana na hawachukuliwi hatua yoyote, je, Wizara haioni inapoteza imani kwa Watanzania na kuonekana ni matapeli?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifanye maboresho kwenye mfumo mzima wa utendaji Wizarani, kutazama kwa makini mikataba ya uwekezaji kwenye ardhi ili wananchi waweze kufaidika na maeneo katika ardhi na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Lakini nipate maelezo juu ya mambo yafuatayo:-

Kasi ndogo ya upimwaji viwanja katika maeneo mbalimbali nchini likiwemo Jimbo la Lushoto, Wizara lazima iwe na mpango mkakati wenye kutekelezeka. Ahadi zimekuwa nyingi za uboreshaji wa upimaji viwanja.

Ugawaji mbaya wa viwanja Jimboni Lushoto, nimeandika barua TAMISEMI na makala nimetuma kwako kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia fupi ya migogoro ya ardhi Lushoto mwaka 1999/2000 Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ilisitisha ugawaji wa viwanja eneo la Hospitali ya Wilaya kwa ahadi kwamba walionyanganywa viwanya watafidiwa viwanja vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhaba wa ardhi Mjini Lushoto ilibidi Mbunge wa Lushoto wakati huo ambaye ni mimi kuomba Wizara ya Maliasili na Utalii iruhusu kufutwa kwa hati ya hifadhi katika eneo la shamba la miti ili kuruhusu upimaji viwanja hatimaye kulitatua tatizo la wananchi walionyang'anywa wa viwanja. Kwa bahati mbaya viwanja hivyo havikupimwa mpaka mwaka 2009/2010. Baada ya viwanja hivyo kupimwa, utendaji wa wilaya umevigawa viwanja hivyo na kuwanyima haki wananchi walionyang'anywa viwanja vyao mwaka 1998/1999. Kwa bahati mbaya viongozi wamejigaia viwanja hivyo kwa ubinafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa mji wa Lushoto wamenituma niiombe Serikali kusitisha mgao huo vinginevyo wataandamana kudai haki zao. Busara hazinitumi kuchelewa kuchukua hatua mpaka wananchi wadai haki kwa maandamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaondoa heshima na mapenzi ya wananchi kwa Serikali yao. Naomba Serikali ichukulie jambo hili hatua za haraka ili tuwape wananchi moyo na waipende Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Benki ya Ardhi *(Land Bank).* Suala la Benki ya Ardhi ni muhimu sana. Ninajua ni jambo zito, kwa kuwa Sheria ya Ardhi inahitaji suala hili twende kwa uangalifu. Mikoa ishirikishwe na isaidiwe katika kupima maeneo ya Benki ya Ardhi. Pia Sheria ya Ardhi Na. 5 ya 1999 iangaliwe upya na ifanyiwe mabadiliko. Ni muhimu vijiji vijue ardhi yao na mahitaji yao wakishajua maeneo yao ardhi ya ziada katika mipango yao iorodheshwe kama ardhi ya akiba *(land bank)* na isimamiwe na Mkoa kwa ushirikiano na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili itakapohitajika ipatikane kwa urahisi kwa matumizi ya Taifa na mikoa yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Ardhi, upo umuhimu kuiangalia Sheria Na. 4 na 5 ya Ardhi ya 1999 ili iendane na wakati tulionao.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ksuala la umiliki wa ardhi, ardhi ni mali, ni haki na vyema Serikali ikahakikishe kuwa ardhi yote ya nchi hii iwe imemilikishwa kwa Watanzania. Ardhi ipimwe, imilikishwe na kupangiwa matumizi. Hii itaharakisha maendeleo ya nchi hii na watu wake. Ardhi tafsiri yake ni vitu vyote vilivyo juu/chini yake, hapa nataka kusema umiliki uwe kwa pamoja mawe, mchanga, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wa kuandikwa kwa Katiba mpya umiliki wa ardhi uwekwe Kikatiba na wageni wasipewe kumilikishwa badala yake wapewe *lease* na *lease* hii iwe ya miaka 20 *renewable* kama ina tija kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya *lease* hii iridhiwe na wanakijiji (wananchi) wa eneo husika. Hii itaondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ardhi yote iliyo chini ya udhamini wa Rais (trust) ya Rais basi ipate kuridhiwa na Bunge kabla ya maamuzi yoyote kuwa-*implemented.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba mibovu inayofanywa bila na Serikali bila wananchi kushirikishwa mfano ni mikataba iliyofanywa katika mauziano ya ardhi ya Kijiji cha Chemchem, Karatu kwa wawekezaji bila ya wananchi wenye dhamana ya ardhi kufahamu (ulaghai mtupu).

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya wananchi/wanavijiji wanaopakana na Hifadhi za Taifa kuhusu Ardhi (mipaka) makazi, Serikali iweke mipaka wazi (makazi) kati ya wananchi/makazi – wakulima/wafugaji na hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabaraza ya ardhi ya vijiji, kata na wilaya, mabaraza haya yaimarishwe na kuboreshwa, iwe katika Bajeti ya Wizara itengewe fungu la fedha ili kuweza kutatua migogoro mingi ya ardhi. Waajiriwe wahitimu wa Chuo cha Ardhi kuwa makatibu wa mabaraza hayo wenye ufahamu wa Sheria za Ardhi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali hiyo kila Mtanzania apewe hati miliki *(Title Deed)* ya ardhi anayoimiliki ili aweze kupata mikopo katika vyombo vya fedha kwa maeneo yake binafsi na ya Taifa kwa ujumla. Huu ndio mkombozi wa Mtanzania mnyonge.

Pia Serikali ihakikishe kila Mji/Jiji/Manispaa kuwa na *master plan* hii itasaidia kuwa na miji ya kisasa na kuondokana na kero nyingi zinazotokea sasa katika miji yetu kama ujenzi usio na utaratibu. Watendaji wa idara hii kutokuwa maadili katika kazi yao mfano kiwanja kimoja kuuzwa mara mbili, tatu na kadhalika na kadhalika na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa pamoja wana uwezo wa kupunguza kama si kuondoa kabisa migogoro ya ardhi iliyokithiri nchini.

**MHE. ANNAMARYSTELLA MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia ardhi, naona kwamba ardhi ndio mtaji wa Mtanzania yeyote ndani na nje ya nchi, lakini ardhi ndio imekuwa chanzo cha migogoro na uvunjifu wa amani baina ya wananchi wenyewe, wananchi na Serikali, wananchi na wawekezaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi hubeba kilimo, hubeba mifugo, madini na shughuli zote za uzalishaji mali huwa juu ya ardhi, lakini kinachoniuma zaidi ni hii migogoro ambayo pia naona Serikali inafumbia macho. Nianze kuichanganua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro baina ya wananchi na Serikali hutokea pale Serikali inapoamua kuweka matumizi tofauti ya ardhi ya wazawa kinyume na kazi zinazoendeshwa na wazawa na bila fidia au maridhiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kuepuka migogoro hii kwa kuhakikisha kuwa na maelewano kati ya wananchi na Serikali, pia katika ugawaji wa mashamba na viwanja baadhi ya Maafisa wa Ardhi wamekuwa chanzo cha migogoro kwa kujipatia fedha kwa kuwauzia wananchi viwanja vivuli na mashamba pia. Hali hii imekuwa hatari kwa wananchi wasio na pesa kwa sababu hawana pa kushtaki na kukimbilia matokeo yake wanadhulumiwa na hakuna mtetezi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuhakikisha migogoro kama hii inamalizwa, hasa migogoro ya viwanja vya nyumba, mashamba, ardhi za kufugia au malisho ya wanyama. Pia Wizara ihakikishe Maafisa wa Ardhi wanafuata sheria na kanuni za ugawaji wa ardhi kwa wananchi bila uonevu tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii naomba iwaonee huruma wananchi wasio na uwezo wala hawajui haki zao watazipataje, inasitikisha. Wananchi unakuta anamiliki eneo lake la mashamba miaka mingi lakini kutokana na uongozi usio imara, uliojaa uonevu,

kupitia watendaji wa kata anakuja mgeni kuomba eneo la mwananchi maskini ili mradi tu ametoa pesa (rushwa) kwa mtendaji na Maafisa wa Ardhi ndipo anapokonywa yule maskini na kupewa mwenye pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ionyeshe ukomavu kwa kuwachukulia hatua watendaji wote wenye tabia hiyo ya kupewa rushwa na kuwasumbua maskini wasio na mtetezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naiomba Serikali kupitia Wizara hii iwaongezee mishahara mizuri mahakimu wawe na kipato cha kuridhisha ili wasiwe na tamaa ya kupewa rushwa kwa ajili ya kuhukumu wananchi waliopokonywa mashamba yao na kurudi kufungwa wao wenyewe kwa kisingiziwa kuwa wao wenye mashamba ndio wakorofi, inasikitisha sana. Ni laana kubwa Mungu atatulaani viongozi kwa ulafi na wala sio sifa kuwadhulumu ardhi wananchi maskini. Serikali irekebishe sera na sheria zake za ardhi mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Nkasi Kaskazini hakuna haki yoyote inayotumika katika ardhi ya Nkasi maana kila kiongozi anayekuja kikazi katika Wilaya yetu anachukua ardhi isiyo pungua ekari tano kwa kuwarubuni wanavijiji wetu, pia kuna baadhi ya wafanyabiashara haswa wafugaji wameingia mikataba na Serikali za vijiji na kupewa ardhi ya ukubwa wa ekari zaidi ya 500 mpaka ekari 1,000. Naomba Wizara yako ifike Wilaya ya Nkasi, wananchi wamebaki hawana pa kulima, mimi binafsi niliwahi kuzungumza na Waziri Mheshimiwa Mama Anna Tibaijuka kuhusu suala hilo pia katika mchango wangu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu nilichangia kwa uchungu sana kwa hiyo, mikataba wanayodanganywa wanavijiji wetu kuna mashamba makubwa sana yaliyoporwa kwa ujanja ujanja na hata hawayatumii na wanayakodisha kwa wengine, je, hiyo ni Sheria ya Ardhi ya nchi hii ya mtu kupora ardhi na kuikodisha?

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti iliyosomwa ni nzuri, lakini inahitaji usimamizi thabiti kwani watendaji wa ardhi waliopo katika Halmashauri na miji ambao ndiyo kikwazo kikubwa katika kusimamia kutokana na kutanguliza maslahi yao binafsi kama wamekuwa wakigawa viwanja na kuviuza *(double allocation)* jambo ambalo linawasumbua sana wananchi na kusababisha migogoro mikubwa hata ya kufikia kuumizana wananchi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kitengo hiki wanatanguliza maslahi ya fedha kwa wananchi pale wanapohitaji huduma yao, bila kuwa na uwezo wa fedha wanazungushwa hadi kufikia kukata tamaa na kupoteza haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Shirika la Nyumba *(NHC)* naipongeza kwa hatua walizoanza kuchukua kuwafuatilia wapangaji wake kwa kumfahamu kama kila iliomo ndani ya nyumba hizo ndiye aliye kwenye mkataba. Kitendo hiki kitasaidia kuwafahamu maharamia wanaoibia Serikali mapato yake kwa kupangisha kwa gharama kubwa na yeye anapangishwa kwa bei ya chini ya Serikali. Ujenzi wa nyumba ambazo zinajengwa sasa na Shirika ziangalie pande zote kwa maana ya walionacho na wale wa kipato cha chini ili nao waweze kunufaika na mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa Halmashauri (Maafisa Ardhi na Mipango Miji) wasikae muda mrefu katika eneo moja kutokana na kuzoea na kusahau wajibu wao wa kazi na kuendelea na kufanya uharamu kwa kushirikiana na wenye uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi husababishwa na Maafisa Ardhi/Mipango Miji kwa kuungana na wenye uwezo wa fedha kupora maeneo ya wazi kama shule, viwanja vya michezo, kama Shule ya Sekondari Weruweru, Wilaya ya Karatu imenyang'anywa eneo na kugawiwa viwanja, naomba Wizara irejeshe eneo hilo kwa Bodi ya Shule ambayo imelalamikiwa kwa muda mrefu hadi Wizarani hakuna majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Arusha Mjini katika Kata ya Themi lililokuwa shamba la *Themi Estate* wananchi wa eneo hilo wamenyanyasika muda mrefu bila mafanikio kulalamikia

unyanyasaji unaofanywa na wenye uwezo wa fedha kupewa eneo lenye Kiwanja Na. 2 na 3 ambao hakustahili. Naomba Wizara kuingilia kati malalamiko hayo ambayo yalishatolewa maelekezo ya kufuta hati na aliyekuwa Waziri wa Ardhi wakati huo Mheshimiwa Edward Lowassa ili warudishiwe wananchi wa eneo hilo bila mafanikio.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kuanzia na ucheleweshaji utoaji wa Hati Miliki za jadi. Suala hili ndio muafaka sahihi wa kukomboa wananchi wetu kupata hati za kuwawezesha kupata mikopo katika mabenki ili kuendeleza kilimo vilevile ni njia mojawapo ya kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji maana kila mmoja atalazimika kutunza eneo lake la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, utoaji ardhi kwa wawekezaji bila kungalia utoshelezi wa ardhi kwa wananchi wazawa na wakulima wadogo. Serikali imeweka kipaumbele kuwapatia wawekezaji wakubwa ardhi bila kuangalia kwamba wapo wananchi ambao hawana mahali pa kulima. Hivyo kipaumbele kwanza kiwekwe kwa wakulima wetu na vizazi vyao bila hivyo wananchi wetu watendelea kuwa maskini na kuwa watumwa wa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wawekezaji waliomiliki maeneo makubwa ya ardhi bila kuendeleza wanyang'anywe. Serikali imetoa maeneo makubwa ya ardhi kwa wawekezaji na wawekezaji hao hawaiendelezi ardhi hiyo, matokeo yake wao wanaikodisha kwa kodi kubwa kinyume na mikataba yao. Naomba Serikali ifuatilie na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali iandae mpango rasmi wa utatuzi wa migogoro ya wakulima na wafugaji. Nchi hii, Serikali itambue kwamba isipochukua hatua za makusudi juu ya tatizo hili, ni hivi karibuni vitazuka vita ya wakulima na wafugaji. Waswali walisema ukiona pahali panafuka moshi ujue ipo siku moto utawaka. Naomba Serikali ichukue tahadhari mapema juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Serikali ipime makazi ya vijiji na miji ambayo inaendelea kujengwa kiholela bila mpangilio unaotakiwa. Ifahamike kwamba vijiji ndio imekuwa Miji Midogo na Miji Midogo ndio imekuwa Miji mikubwa hivyo basi ni vema Serikali ikaanza mipango kuanzia sasa ili isije ikafika wakati kuanza kubomoa makazi ya watu na kuwatia hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, ukosefu wa fedha na nyenzo za kufanyia kazi katika Halmashauri zetu ili kuleta ufanisi wa kazi. Serikali inatakiwa kutoa nyezo za kufanyia kazi kwa Mabwana Ardhi wa Wilaya ili kurahisisha ufanisi wa kazi ikiwa ni pamoja na upimaji wa ardhi na kutoa elimu ya manufaa ya matumizi ya ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, ahadi ya Wizara kujenga jengo ambalo litatumika kama Masijala ya Ardhi ya Wilaya ya Sumbawanga. Wizara ilitoa ahadi ya kujenga Masijala ya Ardhi toka mwaka 2006 lakini hadi leo hii ahadi hiyo haijatekelezwa, tunaomba Wizara itekeleze ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Serikali iwarejeshee wananchi wa Kijiji cha Sikaunbu ardhi yao ambayo Serikali imemilikisha kwa mwekezaji EFHATA kinyume cha Sheria na kufanya wananchi wakose kuwa na ardhi ya makazi na ya kulima japo Kijiji kilisajiliwa na kupimwa mipaka yake kisheria.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia katika uboreshaji na utendaji wa Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu itajikita katika mambo matatu ambayo kwanza ni, umuhimu wa ardhi kwa Watanzania. Pili, wawekezaji na ardhi ya Watanzania na mwisho ni Shirika la Nyumba la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi mahali popote duniani si la utani kwani unapozungumzia nchi fulani maana yake ardhi yenye mipaka iliyo ardhini. Unapotambulisha Taifa

pia unazungumzia jamii katika ardhi yenye mipaka ardhini. Kwa hiyo, ardhi ni kitu cha thamani sana katika uhai na maendeleo ya nchi fulani. Hakuna maendeleo yoyote kwa jamii inayohangaika bila utulivu katika ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalohuzunisha ni lile la ardhi kutokuwepo katika Sheria Mama za Nchi. Matokeo yake ni kila mjanja kuibuka na hoja yake isiyokuwa na mashiko ya kuona kuwa ardhi ni nyenzo ya kutumiza malengo ya ubinafsi. Ardhi badala ya kutamkwa waziwazi katika Katiba kuwa mgeni yeyote hataweza kumilikishwa kwa karne (miaka 99 si sawa tu na miaka 100?) Wapi na wapi nchi ya Watanzania kunyimwa haki yao ya kuwa na *asset* yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, la kuchekesha ni pale ilipokuwa inatayarishwa Sera ya Ardhi ya 1994/1995, wale wajanja kwa manufaa yao wakatenganisha madini na ardhi! Hivi ni kweli unaweza kupata madini bila ardhi au nyumba ikajengwa juu ya ardhi, sasa tatizo la mikataba mibovu ni lile la kutenganisha ardhi na madini. Huu utenganishi wa ardhi na madini si sahihi. Sheria hii ya Madini na Ardhi viunganishwe na Sheria ya Fidia itakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wawekezaji na ardhi ya Watanzania. Katika utekelezaji wa uwekezaji wa aina yoyote katika ardhi ya Watanzania haujawa wa haki hata kidogo. Wananchi wengi wa Tanzania wanaishi katika falsafa za ujamaa za kuaminiwa na hasa kuamini kuwa Serikali iko kwa ajili ya manufaa yao na ulinzi wao lakini kwa hakika, kiutendaji si hivyo ni kinyume chake. Ardhi ya wanyonge wanakuwa wakinyang'anywa na Serikali ile wanayoitumainia kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kuwa watu wamedanyangwa kabisa kwa vile Serikali yao hii ya CCM imekuwa ikitumia vyombo vya dola, vya mabavu kuwanyang'anya ardhi na kuwapa matajiri wachache wa ndani wakishirikiana na wageni kuwarubuni wanyonge wa Tanzania. Ni suala la msingi sasa Katiba itamke kuwa rasilimali adimu hii pekee waliyojaliwa Watanzania, itamkwe kwenye Katiba kuwa hakuna mgeni yeyote atakayemiliki ardhi bila ya kushirikiana na Mtanzania mzalendo kuwe na *partnership.* Ushirika huu utampa maamuzi ya juu yule Mtanzania mwenye kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwe kama panzi ambaye anaporuka kukimbia adui akifika mahali huficha kichwa chake kwenye shimo na kiwiliwili nje/juu; hiyyo akija adui humdokoa kwa urahisi. Migogoro ya ardhi inayoendelea katika nchi yetu, wafugaji, wakulima, makazi, barabara na kadhalika yote ni ardhi yenye rutuba ya kuchochea upotezaji wetu wa Uhuru. Waziwazi tunaona jinsi Ukoloni Mamboleo ulivyo kazini ukitumia umaskini wa Watanzania kuuza haki zao kwa vipande vya chupa kwa dhahabu *(unequal exchange).* Tukumbuke kuwa migogoro ya Afrika Kusini, Zimbabwe na mahali kwingine kwenye migogoro ya utawala chanzo ni ardhi ambayo ilitolewa kwa wageni kama hivi tufanyavyo sisi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni hili la *National Housing* ambapo kuna masuala mawili yaliyofichika humo. Kwanza, makazi ya Upanga, nyumba zilizokuwa za Msajili wa Nyumba zisije zikaishia kuleta matabaka ya makazi ya Wahindi na Waarabu pekee na Waafrika wote kusukumiwa pembezoni. Pili, ni suala la nyumba za Serikali za Oysterbay wala suala hili halijaisha, suluhisho lake ni kuzirejesha Serikalini hasa *site*/viwanja vyake. Ujanjaujanja haufai ni bomu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nawasilisha.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pia nawapongeza kwa hotuba nzuri ya bajeti waliyoileta hapa Bungeni. Pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Baraza la Ardhi la Kata na Mahakama ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Wazee wa Baraza wanalipwa fedha kidogo sana kiasi ambacho hakikidhi haja. Pamoja na malipo haya kuwa madogo lakini hayapatikani kwa wakati. Mfano Wazee wa Baraza katika

Wilaya ya Karagwe hawajalipwa posho zao kwa muda mrefu sana. Malalamiko yao ni makubwa sana. Aidha, Wazee wa Baraza hawana uwezo wa kuamua migogoro hiyo kwa haki. Mara nyingi wanapendelea kwa makusudi au kwa kutojua. Nashauri Sheria hii ibadilishwe, migogoro ya ardhi itatuliwe na Mahakama za kawaida. Mamlaka ya kusikiliza migogoro ya ardhi ihamie Wizara ya Sheria kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, naomba Mabaraza haya yaende Wilayani kama Sheria inavyotaka badala ya kukaa Makao Makuu ya Mkoa mfano kwa Wilaya ya Karagwe hadi sasa Mahakama ya Ardhi na Nyumba bado inafanyia kazi zake Mkoani Kagera (Bukoba Mjini). Wananchi wa Wilaya hii husafiri mwendo mrefu zaidi ya kilomita mia moja kutafuta haki yao. Haya ni mateso makubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Karagwe. Mateso haya yataisha lini? Je, bajeti hii imetenga fedha kwa ajili ya kuwanusuru wananchi wa Wilaya ya Karagwe? Nitashukuru sana kama Serikali itakuja na majibu mazuri ya maswali haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ya Karagwe kukaa Bukoba lakini bado Baraza hili lina tatizo la usafiri yaani magari. Naomba Serikali iwapatie magari kwa ajili ya kusafiri kwenda Wilayani Ngara, Biharamulo, Chato, Karagwe, Muleba, Misenyi na Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ardhi ya Ranchi ya Kitengule *(NARCO)* Wilayani Karagwe. Ardhi iliyokuwa Ranchi ya Kitengule ilibinafsishwa na kugawiwa kwa wananchi wafugaji pamoja na Kampuni ya *Super Doll*. Wananchi wamemegewa vipande *(blocks)* vyenye ukubwa upatao hekta 2,000 na zaidi kwa kila mfugaji. Baadhi ya watu waliopewa hawana mifugo wanakodisha, wengine ni wageni haramu kutoka nchi jirani za Rwanda na Uganda. Wananchi wanaopakana na Ranchi hii hawakupewa *open area* kwa ajili ya mifugo yao. Hali hii imesababisha mgogoro mkali sana kati ya wafugaji na wananchi wa vijiji vya Kihanga, Katanda, Kibwera, Mlamba na Mushabaiguru. Kwa kuwa maeneo yaliyogawiwa kwa wafugaji ni makubwa sana na kuna wananchi wengine wanahitaji maeneo ya kufugia, ugawaji wa eneo hili urudiwe ili baadhi ya wafugaji wapate maeneo ya malisho. Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza eneo kubwa alilopewa *Super Doll* karibia hekta 40,000 na kugawia wananchi wa Karagwe ambao wanahangaika bila msaada wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwanyang’anye haraka sana wageni toka Rwanda ambao wamemilikishwa maeneo hayo. Pia Serikali iwanyang’anye wale wote ambao wanapewa ardhi lakini hawana mifugo kazi yao ni kuikodisha kwa wananchi toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nyumba mijini. Kama tulivyoona katika ziara ya Rais huko Shelisheli jinsi nchi hiyo ilivyojenga nyumba na kuwakopesha wananchi wa kipato cha chini kwa kipindi cha miaka 15 na kisha nyumba hizo kuwa zao basi Serikali yetu iige mfano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ardhi. Nchi yetu inayo ardhi kubwa na ya kutosha lakini migogoro ya wafugaji na wakulima imeshamiri. Je, ni kwa nini Serikali isipime ardhi ya kutosha kwa ajili ya wafugaji na wakulima ili wote wakafanye shughuli za uzalishaji mali kwa amani na utulivu. Naomba Serikali ichukue hatua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuongelea huduma za kupata Hati Miliki ya Kudumu ya Nyumba, Shamba au Kiwanja. Nasikitika sana kusema kuwa nimechangia mara nyingi sana juu ya kupeleka au kusogeza huduma ya kupata Hati Miliki ya Kudumu ya Nyumba, Shamba au Kiwanja Mikoani ili wananchi waweze kupata huduma hii kwa gharama nafuu. Hadi sasa huduma hii bado inatolewa Kikanda mfano wananchi wa Singida mpaka waje Dodoma. Napenda kujua azma ya Serikali ya kupeleka huduma hii karibu na wananchi yaani Mikoani itafanyika lini. Nasuburi kusikia wakati Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wanajibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wahitimu wa Chuo cha Ardhi kupata ajira mapema. Napenda kuwapongeza Watanzania wakiwemo wanawake na vijana kwa bidii zao za kujiendeleza kitaaluma. Wengi wanapata taaluma mbalimbali ikiwemo Maafisa Ardhi, Mahakimu na kadhalika lakini wanapomaliza wengi wao wanakosa ajira. Napenda kujua mpango wa Serikali wa kuwapatia ajira wahitimu wa Chuo cha Ardhi ukoje. Nasubiri jibu ambalo litawatia moyo wahitimu wa Chuo cha Ardhi ambao wako mitaani bila ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, operasheni ya kuondoa Matembe Singida. Napenda kupongeza juhudi za Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mkakati wake wa kuwaelimisha na kuwasaidia wananchi wa Jimbo lake kuondoka kwenye nyumba za Matembe na kujenga nyumba za kisasa yaani za bati au vigae. Ni ukweli usiofichika kuwa uwezekano wa wananchi kuondokana na nyumba za tembe upo kwani wanazo mali za kutosha mfano mifugo na hupata mazao ya biashara ya kutosha bali hawana mwamko na elimu. Napenda kujua kwa nini mikakati huu usiwe wa Serikali ili nchi nzima wananchi waelimishwe juu ya kufaidi mali zao na wengine wenye sifa za kukopeshwa wakopeshwe ili wajenge nyumba za kisasa. Nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kodi za Nyumba za Serikali *(NHC)* kupanda kila wakati. Naipongeza Serikali kwa mpango wake mzuri wa kujenga nyumba za makazi kwa lengo la kuwasaidia Watanzania kupanga hususan wafanyakazi wanaofanya kazi mijini. Matatizo ni kama ifuatavyo:-

(1) Nyumba hizi ni chache, hazitoshelezi mahitaji. Naomba ujenzi huu uendelee hadi Mikoani, Wilayani na Makoa Makuu ya Kata. Nasubiri majibu ya Waziri au Naibu Waziri.

(2) Serikali ipange kiwango cha kodi kulingana na vipato vya jamii iliyokubwa mfano Walimu, Wauguzi na wafanyabiashara wadogowadogo tuache kulenga watumishi ngazi ya juu na wafanyabiashara wakubwa. Nategemea majibu Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, viwanja visivyojengwa na nyumba mbovu katikati ya miji yetu hasa Makao Makuu ya Mkoa. Napenda kuungana na Serikali kuwa viwanja kukaa bila kuendelezwa kwenye Miji mikubwa au nyumba zilizochakaa sio vizuri kuendelea kuonekana Mijini kwani zinaleta picha mbaya katika miji. Naiomba Serikali kufanya mazungumzo na wenye viwanja au nyumba mbovu ili kuwatafutia viwanja vingine nje ya Miji ili Serikali ichukue nyumba au viwanja hivyo ili iweze kuviendeleza. Hii itasaidia sana kuleta picha nzuri za miji yetu Mikuu ya Mikoa. Waziri au Naibu Waziri watoe maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Shirika la Nyumba la Taifa kujenga nyumba za ghorofa za Ofisi na Maghorofa ya makazi. Napenda kuiomba Serikali kujenga nyumba hizo Singida kwa kuwa Mkoa na Wilaya zake una tatizo kubwa la kupungukiwa na majengo ya kupangisha ofisi mbalimbali na majengo ya ghorofa za makazi. Hii itasaidia kuongeza mzunguko wa fedha Mkoani Singida na Wilaya zake na mandhari pia kuwa na mvuto.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa shughuli maalum kuvamiwa na baadhi ya watu. Bado kuna matatizo ya baadhi ya watu kuvamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kazi maalum mfano michezo kwa watoto na kadhalika. Kwa hali ya kusikitisha, wako Maafisa Ardhi ambao kwa kupewa rushwa na huharibu mfumo mzima wa ugawaji wa viwanja. Napenda kujua Serikali ina mkakati gani wa kukomesha tabia hii ili isitokee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, wapangaji wa *NHC* kuachiana nyumba bila utaratibu. Bado kuna utaratibu mbaya kwa wachache pamoja na juhudi ya Mheshimiwa Tibaijuka Waziri mwanamama kukomesha hali hii. Ninamwomba Mheshimiwa Tibaijuka, Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri kuendelea kufichua tabia hii chafu ili wapangaji wajulikane kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, ukarabati wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC).* Napenda kuijulisha Serikali kuwa inasahau sana kukarabati nyumba hizi hatimaye zinaharibu shoo ya Miji yetu, hivyo naomba mikataba yake na wapangaji iwe wazi, nani anatakiwa kukarabati

nyumba hizi za *NHC*, ni mpangaji au Serikali? Vilevile usafi wa nyumba hizi ni tatizo mfano nyumba za *NHC* karibu na Mtaa wa Zima Moto Dar es Salaam, mazingira yake ni machafu sana, napenda kujua ni nani anatakiwa kusafisha mazingira yanayozunguka nyumba hizi na zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, mikopo ya kujenga nyumba kwa wafanyakazi. Kuna tatizo la utoaji wa mikopo ya kujenga nyumba hasa kwa wafanyakazi wa kawaida mfano Walimu, Wauguzi na kadhalika. Kwa kuwa watumishi wana dhamana ya mishahara yao, naomba Serikali kutoa kipaumbele ili kuwasaidia wafanyakazi, walio wengi wanapostaafu wanakosa pakukaa, kusubiri kujenga kwa pensheni ni utaratibu wa umaskini kwani fedha zote huishia kwenye ujenzi na kukosa fedha za kujikimu. Naomba Serikali inipe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Prof. Tibaijuka, Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii yenye mikakati mizuri ya kuendeleza Wizara pamoja na kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja, nawatakia utekelezaji wenye tija, nasubiri ufafanuzi wa hoja zangu zote.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya wananchi kwa sababu inagusa maisha ya wananchi. Ili mwanadamu yeyote aishi lazima awe na makazi aidha kwa kupanga au kwa kujenga lakini inasikitisha kuona makazi holela utadhani Serikali haipo, ninamaanisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi. Ni ushauri tu kwa Wizara kwamba iwe na maono makubwa ya kuanzisha maeneo mapya ya makazi, yapimwe na kuwagawia wananchi. Kwa Miji iliyokua haraka sana, ni vema Wizara iwe na namna ya kupeleka huduma za upimaji ardhi kwa haraka sana la sivyo baadaye wananchi hawa wanyonge, wasiokuwa na uwezo wanabomolewa nyumba zao na kuambiwa walijenga mahali ambapo ilitakiwa kupita barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Busanda, Wilayani Geita, Mji wa Katoro/Buseresere, ni miongoni mwa Miji inayokua kwa kasi sana kutokana na uchumi wa madini ya dhahabu. Sasa basi iko haja kuangalia namna ya kuiboresha Miji hii mapema. Nashukuru Wizara kwa utayarishaji wa ramani nikirejea katika hotuba, ukurasa wa 17 ambao tayari umekamilika katika Miji hii. Kinachobaki sasa ni hatua ya kupanga Mji na kupima viwanja na kuwagawia wananchi viwanja vilivyopimwa. Hivyo basi, naomba Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ifanye utaratibu huo haraka kwa sababu Katoro/Buseresere ni Miji inayokuwa kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu Wizara hii ni ukiritimba uliopo ndani ya Wizara hii. Utaratibu mzima wa kupima viwanja mpaka upate Hati Miliki inachukua muda mrefu sana na ni lazima ufanye ufuatiliaji wa hali ya juu sana kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. Kama kweli Wizara inayo nia ya dhati ya kufuatilia utendaji mzima ndani ya Wizara, namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie kwa karibu sana utendaji ndani ya Wizara. Endapo kutakuwa na ukiritimba, nina uhakika wananchi hasa walio wengi wanyonge watainuka kiuchumi kwa kupata Hati Miliki za maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA M. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri ambayo kama itatekelezeka, wananchi wataondokana na usumbufu katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na ardhi ya kutosha na ziko sehemu kubwa za mapori ambayo hayajatumika. Kwa nini Serikali isiyatambue maeneo hayo kwa kuyapima na kama akitokea mwekezaji akapelekwa maeneo hayo badala ya kuwasumbua wananchi kwa kuwanyang'anya maeneo yao na kuwabomolea makazi yao na fidia inayolipwa haitoshelezi na pia haitolewi kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Hati Miliki ni kikwazo kikubwa kwa Mtanzania. Je, vipi tutamwezesha Mtanzania kwenda kutumia fursa zilizopo za benki kuweza kukopa?

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa Mji wa Kigamboni umepangwa ujenzi wake kuanza lini na wananchi wanaendelea kujenga. Hivi sasa wapo wananchi wengi ambao wanahangaika kwa miaka mingi kudai fidia zao. Je, fidia za Mji wa Kigamboni kweli zitaweza kufidiwa pindi mradi huo ukitekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango bora ya matumizi ya ardhi kwa kushirikisha makundi maalum kama vijana, walemavu na kadhalika. Asilimia zaidi 50 ya nguvu kazi ni vijana na sehemu kubwa ya kujiajiri vijana wakiandaliwa vizuri ni ardhi kwa kilimo au kuingia ubia na wawekezaji. Je, Wizara ina mpango gani kwa makundi hayo wakati huu ambapo ajira kwa vijana ni tatizo kubwa? Katika Halmashauri zetu wana mikakati gani ya kutenga maeneo mahsusi kwa kuwaendeleza vijana kwa kuwawekea miundombinu ili waweze kujiajiri kupitia sekta ya kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi na mipaka. Katika Jimbo la Mvomero, kuna tatizo la migogoro ya ardhi katika vijiji mbalimbali naomba niyaainishe kama ifuatavyo:-

(i) Eneo la Newland – Kata ya Mtibwa. Eneo la Newland mpaka miaka ya 1992 lilikuwa mali ya wananchi wa vijiji vya Kidudwe, Lango, Madizimu na vijiji vingine ndani ya Tarafa ya Turiani walilima kwenye eneo hili. Cha kushangaza, wananchi walitangaziwa kuwa eneo hili ni la Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa. Hivi sasa wananchi zaidi ya elfu moja hawalimi tena na kiwanda wanadai eneo hili ni lao. Kimsingi kiwanda kimechukua eneo hili kinyemela na naomba Wizara itoe tamko inakuwaje kiwanda kichukue eneo hili. Naomba Serikali itangaze kuwa eneo hili limilikishwe kwa wananchi. Naomba majibu la sivyo siungi mkono hoja. Taarifa za ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wananchi hawazielewi na katika hili wanaonekana Mtimbwa Sugar wanapika nyaraka za kumiliki eneo hili, jambo hili halikubaliki, naomba haki itendeke, wananchi wapewe eneo hili.

(ii) Shamba la Sumaye Kijiji cha Mvomero. Kwa muda mrefu suala la wananchi kutaka Serikali iwape eneo hili limekuwa wimbo pasipo Serikali kutoa majibu ya eneo hili. Shamba hili lilikuwa la Ushirika lakini uuzwaji wake ulifanywa kinyemela na kuuziwa Mheshimiwa Sumaye. Kitendo cha kuuziwa mtu mmoja badala ya wananchi hakikuwa cha wazi na hili limeleta manung'uniko sana kwa wananchi wa Mvomero. Rais alipokuja Mvomero mwaka jana aliwaahidi kuwa suala la shamba la Sumaye litapatiwa majibu. Sasa Serikali itoe majibu nini hatma ya wananchi wa Mvomero kuhusu eneo hili. Ushauri ni Serikali kufuta umiliki wa Mheshimimiwa Sumaye na kurudisha fedha ili kuwapa wananchi kulima na kujenga makazi ikizingatiwa Mji wa Mvomero unakua siku hadi siku. Mheshimiwa Waziri namwomba atoe majibu. Mimi binafsi sikubalinani na utaratibu mzima wa uuzaji wa eneo hili kwa Mheshimiwa Sumaye.

(iii) Eneo la makazi na wafugaji wa asili – Wami Sokoine. Nimeshasema sana hapa Bungeni kuhusu Serikali ya Wilaya kusitisha ujenzi wa makazi kwa wananchi wa Wami Sokoine. Nilisema sana wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, kwa nini wananchi (kijiji cha Sokoine) viwanja vimepimwa ndani ya kijiji kwa kuwapa wananchi toka Mjini Morogoro na Dar es Salaam na kuwaondoa wanakijiji wa Sokoine? Iweje Serikali imewakataza Wanasokoine kujenga ni miaka takribani nane sasa?

Naomba pia Serikali iwape haki hekta 5000 wafugaji wa asili. Block 299/3A waliopewa *Katenda Group* na 299/3B aliyopewa Elisa Molel haya maeneo ndiyo ilikuwa sehemu ya hekta 5000 zilizokuwa za wafugaji wa asili. Hao *Katenda Group* inasemekana ndiyo Fredrick Sumaye. Naomba sana wafugaji wa asili wapewe hekta 5000 kama ilivyoamuliwa na Waraka wa Baraza la Mawaziri mwaka 2002.

(iv) Mgogoro wa mashamba na mipaka kijiji cha Manza na Kitongoji cha Kinyenze – Kata ya Mlali. Wananchi wa kijiji cha Manza wanakabiliwa na uhaba wa ardhi ya kulima na hii inasababisha ukosefu wa chakula. Wananchi wa kijiji cha Manza wamezuiwa kulima kwa mdai ndugu Simbabwene kudai eneo hili ni lake. Hivi sasa kesi ipo Mahakamani.

Naomba Waziri afike maeneo yote niliyoyataja Newland, Mvomero, Wami Sokoine, Manza na Kinyenze kijiji cha Kipera. Pamoja na kuwa suala la shamba hili la Manza lipo Mahakamani, mmiliki anaendelea kujipanua kimipaka na wakati mwingine hata maeneo mengine kudai ni yake. Naomba sasa Serikali ichukue hatua, haiwezekani hata maeneo ya huduma kama shule anadai ni yake.

Kuhusu kero ya shamba Kitongoji cha Kinyenze, katika kijiji cha Kipera ni kwamba mmiliki wa awali wa shamba hili Bwana Badru ameshamuuzia Mzungu na kero kubwa ni kwamba mipaka sasa imemegwa hata maeneo ya wananchi wa Kinyenze yamechukuliwa kwani mmiliki ameongeza maeneo ya mipaka. Hii ni kero naomba sana Serikali iingilie kati wananchi wa Kinyenze wapate haki yao.

(v) Mipaka ya Hifadhi ya Wami Mbiki na vijiji na vitongoji. Maeneo ya vijiji vya Mlumbiro, vitongoji vya Mbagati, Makwalu na Njenila vinapakana na hifadhi ya Wami Mbiki na mara kwa mara wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wanasumbuliwa na Askari wa Hifadhi hii. Naomba Serikali iingilie kati wananchi wa vijiji hivyo na vitongoji vya Njenila na Makwalu waishi kwa amani wasisumbuliwe. Haiwekezani wananchi kila mwaka wasumbuliwe kwa kisingizio cha kuingia eneo la Hifadhi.

Serikali sasa iingilie kati mipaka ya Hifadhi ili kuwatendea haki, wananchi wangu waishi kwa amani na kufanya shughuli za maendeleo. Naomba Wizara ya Ardhi na Maliasi zishirikiane kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja hii endapo Waziri atatoa ufafanuzi wa kutosha wa kushughulikia matatizo niliyoyaorodhesha.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu wa kuzungumza, naomba nichangie pia kwa maandishi. Suala la fidia kwa wananchi wenye migogoro ya ardhi limekuwa halipewi umuhimu unaostahili. Hii inatokana na Serikali kutokuwa na mipango mikakati endelevu kwa matumizi sahihi ya ardhi ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kuna eneo la Rukarangata ambalo kuna viwanja vilipimwa kwa nia ya kuboresha makazi ya watu. La kushangaza wamiliki halali wa eneo hili bado Serikali haitaki kuwalipa kwa fidia ambazo ni za sasa. Pamoja na suala hili kupelekwa Mahakamani bado halijapata uamuzi mpaka sasa. Naomba Serikali ilipe fidia stahili kwa watu kama hawa kwani wamejitoa kusaidia jamii lakini Serikali haijali stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna suala la nyumba za viongozi zilizouzwa mwaka 2004/2005. Suala hili limepelekea viongozi wengi kuhamia uraiani na wakati huo hawana nyumba kulingana na hadhi zao. Viongozi kama *OCD*, baadhi ya wafanyakazi wa ngazi za juu wa Halmashauri zetu, ni wazi uamuzi huu umeipaka matope Serikali kwani mpaka sasa hawajajengewa nyumba kulingana na hadi zao na hii imepelekea hata ufanisi wa kazi umepungua kwa kujenga mazoea na baadhi ya viongozi hawa. Naishauri Serikali kurudisha nyumba hizo kwa wahusika na aidha wale waliouziwa nyumba hizo wapewe viwanja vipya na walipwe fidia stahili kwa gharama walizotumia kukarabati nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupandisha gharama za upimaji wa viwanja, zimepandishwa mno katika Halmashauri ya Jimbo la Biharamulo Magharibi. Leo hii kuna pendekezo la kupima kiwanja kwa gharama ya Shilingi 200,000/= na bado mtu huyu anapoanza kujenga anatozwa Shilingi 30,000/= bado kila lori la mchanga au tripu ya mawe inatozwa Shilingi 1,000/= hivi hizi gharama mwananchi huyu hapaswi kuonewa huruma? Gharama hizi ni kubwa mno. Mwananchi huyu apate kiwanja cha gharama kubwa bado vifaa vya ujenzi navyo gharama kubwa! Je, ni lini tutatimiza azma ya wananchi wetu kuwa na nyumba bora, kuwa na makazi bora kuwa na ardhi yenye matumizi sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upimaji ardhi ni nyenzo moja muhimu na kubwa ya kuondoa umaskini kwa wananchi wetu. Kuna wananchi wengi wapo kwenye maeneo ambayo yamegundulika kuwa na madini, Serikali imetangaza kuwepo Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji vipya lakini kutangaza kwa mipaka hiyo hakujaenda sambamba na utoaji wa Hati Miliki. Huyu mwananchi tunamwandalia mazingira gani ya kumwondolea umaskini? Tunapopima tutoe Hati Miliki ili mwanachi huyu aweze kupata hati ya kukopeshwa hata wawekezaji wanapopewa maeneo haya basi thamani ya mwananchi huyu ijulikane vinginevyo ndiyo mikataba inayofungwa na matokeo yake wananchi wanafukuzwa ovyo na kuwa wakimbizi ndani ya nchi yao. Wapo wananchi wengi wanayo mashamba makubwa mfano mashamba ya miti, lakini kwa kuwa mfumo ndio huo basi wananchi wanakuwa hawafaidiki na ardhi yao na wala hawafaidiki na mazao waliyoyapanda kwenye ardhi ile. Serikali ilishughulikie suala hili kwa haraka sana na jitihada za makusudi zifanyike kunusuru rasilimali hii muhimu, ardhi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tunapita katika wakati mgumu sana juu ya usimamizi na matumizi bora ya ardhi ambayo imekuwa haiongezeki na matumizi ya binadamu na mahitaji yake yanaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tunajidanganya sana kama tutaendelea kujifanya ni vipofu na hatuoni hatari na migogoro ya ardhi inayozidi kuongezeka. Nashangazwa sana na viongozi wetu ambao migogoro ya ardhi ya watu wetu (wananchi) haiwanyimi usingizi na kuendelea na mnada wa kuuza na kugawa ardhi yetu kwa kisingizio cha uwekezaji wakati wazawa wakitangatanga kutafuta ardhi na hata kama wanapata na wanayo lakini wazawa hawa hawamilikishwi ama kisheria au kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa ni lazima tutafakari kwa pamoja na kuwa na mjadala mpana wa Kitaifa juu ya ardhi kuhusu umiliki, ugawaji na matumizi yake na kamwe tusikubali watu au kundi dogo kuhodhi na kumiliki ardhi na kuwa na mamlaka yasiyohojiwa ya ugawaji wa ardhi hata kama itakuwa lazima kuangalia upya au kubadili Sheria zetu tulizonazo ambazo zinatoa mamlaka kwa watu wachache kugawa au kuuza ardhi yetu wapendavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliachia, tulishindwa kuhoji na tulipohoji tulipuuzwa juu ya kufungua milango kwa ukoloni mamboleo kwa kisingizio cha uwekezaji na kuwekeza katika sekta ya madini na kama nchi tumefaidika kwa kiasi gani na uwepo huu wa migodi kadhaa katika nchi yetu. Mimi sioni kama ipo faida, ni ndogo mno kuliko chumo walilopata wawekezaji hao katika sekta ya madini. Leo Serikali hii imefungua dirisha la mnada wa ardhi eti sasa wanayo Benki ya Ardhi *(Land Bank)* hivi ni lazima tuigawe hii rasilimali ardhi? Kwa maoni yangu, tunakosea sana na ni wajibu wetu kuwakumbusha watawala tumewapa mamlaka ya kulinda na kuhifadhi rasilimali zetu na kamwe wasitufanye wajinga na kuuza au kugawa ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mtazamo na fikra za viongozi wetu ni uwekezaji na hakuna njia nyingine ya mafanikio ila ni kuruhusu uwekezaji katika kila kitu, tunapaswa kuwakumbusha watawala wetu kwamba ni Taifa gani duniani ambalo limelisha watu wake kwa kutegemea wageni/wahisani/wafadhili na wawekezaji. Mataifa yote yaliyoendelea leo duniani na kuwa Mataifa ya viwanda, msingi wake ulianzia kilimo, sisi kwa miaka 50 leo si haba tunajivunia nini kama watawala wetu leo baada ya miaka 50 wanatafuta kila kona ya dunia watu waje watulishe kwa kutulimia chakula. Ni aibu gani hii, China, India, Mataifa ambayo yana watu wanaozidi bilioni moja wanajitosheleza wenyewe kwa chakula na wala hawakualika Wamarekani au Waingereza kwenda kuwalimia chakula. Tatizo letu kama Taifa ni mipango tu. Watanzania wachache Mbeya, Rukwa, Iringa na Ruvuma wanazalisha chakula cha kutosha kwa Taifa na ziada kwa jembe la

mkono na kingine kinaoza kule Rukwa tunashindwa kusafirisha tu, tunafikiria lazima ardhi tumpe Mzungu, Mmarekani aje alime mahindi Rukwa, ni aibu kwa Taifa hili na mnakamilisha hivi sasa kuwapa ardhi Katumba na Mishamo katika Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema mipango. Leo hebu fikiria tu unapopita katika barabara kuu ya kwenda Dar es Saalaan yapo matrekta yameanikwa juani, tuliambiwa sijui wameleta trekta 1000, sina hakika lakini yapo mengi pale yamewekwa kama maonyesho. Msimu wa kilimo umekaribia sana trekta hizo tangu zifike zaidi ya miezi tisa wanashindwa kukokotoa tu gharama halisi ili trekta hizo ziuzwe au kukopeshwa kwa bei inayolipika na ya soko, kwa staili hii ni lazima viongozi wetu watawaita Wazungu na kuwapa ardhi. Trekta hizo ni lazima kwa watu makini zingekuwa tayari zimesambazwa Mikoani kwa jembe tu la mkono mahindi yanaoza hizo trekta zilizopo pale zingetumika tungezalisha kiasi gani,

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi haja ya kumpa Agrisol ardhi yetu inatokea wapi? Naomba kupata maelezo ya kina hatua iliyofikiwa ya kugawa ardhi huko Mpanda tena kwa miaka 99. Leo mpo tayari kuwapimia ardhi Wazungu (Wawekezaji) kwa gharama ya kodi zetu na mzawa akitaka kupimiwa ardhi japo eka moja ni lazima alipe gharama zote za upimaji, wageni ni bure kupimiwa ardhi, wazawa walipe kwa lugha ya sasa kuchangia mahitaji pia kupata maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi kutopata ufumbuzi ni tatizo na kero kwa wananchi wengi. Mgogoro wa Shamba la Benki Mpanda kule Kakese, kata ya Kakese leo ni zaidi ya au takriban miaka 10 uamuzi hautolewi kulikoni? Tarehe 3.7.2008, kikao cha 17 cha Maswali kwa Waziri Mkuu, aliahidi kuangalia njia bora ya kumaliza tatizo hilo. Isitoshe nimechangia mara kadhaa katika Wizara hii na Waziri mwenye dhamana kuahidi kushughulikia na kulimaliza tatizo hili hadi leo tatizo liko vilevile kama miaka 10 iliyopita eti mnasema Serikali ni sikivu, Serikali inayojali matatizo ya watu kweli miaka 10 mnashindwa kumaliza mgogoro huu? Nataka leo nipate kauli ya mwisho juu ya kumaliza tatizo hili la eneo ambalo limekuwa likifahamika kama Shamba la Benki huko Kakese Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na uendelezaji wa Mji wa Mpanda, ni jambo jema na nalipongeza sana. Eneo la Kasimba Serikali imechukua ardhi hiyo kwa fidia ndogo na inauza viwanja hivyo bei kubwa maradufu ambayo Mtanzania maskini wa kipato cha kawaida hawezi kumudu gharama zake wakati wamelipa fidia ndogo sana huku Serikali ikijua kwamba Mtanzania huyu maskini inamwondoa mahali pake na kazi yake maana ameendesha maisha yake na familia yake kwa kilimo katika ardhi leo unaichukua na kumpa fidia isiyostahili ambapo hawezi kujenga msingi mpya wa maisha yake au hata kuweza kupata ardhi nyingine ili aendelee na kazi zake za kilimo. Niiombe Serikali kuangalia upya fidia walizotoa kwa ardhi ambayo sasa inaendelezwa kama makazi kwani ilikuwa ndogo sana na haikidhi kwa thamani ya ardhi Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, watumishi ambao wamekaa kwa muda mrefu katika vituo mbalimbali nchini kuna utaratibu gani kama Serikali, wafanyakazi kuwa katika kituo kimoja cha kazi kwa miaka 20 au zaidi mnatarajia nini kama si mtumishi huyo kufanya kazi kama vile ni kampuni yake? Hawajibiki, hakuna ufanisi wala kumjali mteja. Ipo haja sasa Serikali ikaangalia upya utaratibu wa watumishi hususan katika Idara za kero nchini kama Ardhi ikiwa ni mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la utoaji wa viwanja, Serikali kwa nia njema imekuwa ikitoa viwanja kwa ajili ya wananchi wake, hata hivyo viwanja hivyo vinakuwa ni ghali sana na wale wananchi wa kipato cha chini wanashindwa kuvipata. Hivyo, naishauri Serikali kuweka utaratibu maalum wa kuwakopesha viwanja wananchi hao kwa mikataba ambayo itakuwa nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, ni muda mrefu tumekuwa tukisikia migogoro ya ardhi ambayo inasababishwa na Maafisa wa Ardhi, tabia ambayo inalitia aibu Taifa. Hivyo naishauri Wizara kuwaondoa mara moja wale wote ambao wamehusika na kashfa hizo na pia iweke utaratibu maalum wa atakayefanya makosa ajijue hana nafasi ya kusamehewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za Serikali. Serikali yetu imejenga nyumba nyingi sana na kuwapangisha watu mbalimbali hapa nchini, jambo ambalo ni jema na napongeza. Hata hivyo, kuna baadhi ya wapangaji wamekuwa na tabia ya kutolipa kodi na wengine wanaziuza kwa watu wengine bila mkodishaji kujua. Hivyo, naishauri Wizara kuanzisha *Task Force* ya kupitia kila nyumba iliyokodishwa kujua malipo pamoja na kuelewa mkazi anayeishi katika nyumba hizo ndiye mkazi halali. Sambamba na hili Wizara iweke adhabu kali kwa wakodishwaji na hata kama kuna Maafisa wanaohusika nao pia wachukuliwe hatua.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ardhi kwa maandishi. Awali ya yote, naunga mkono hoja na kuwapongeza sana kwa hotuba nzuri na utendaji wake pamoja na Naibu Waziri wa kutukuka na ninaamini Wizara hii itafanya maendeleo makubwa katika miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuongelea migogoro ya ardhi vijiji vya Malangali Mpanga na Luduga. Mnamo miaka 1990, Serikali ilianisha Hifadhi ya Taifa ya *Mpanga Game Reserve*. Ramani zilitengenezwa na watu walilipwa fidia na kuhamishiwa maeneo mengine. Baada ya miaka 15, *TANAPA* walipima eneo la ziada na kubadili ramani za awali na wameweka mawe ya mpaka tofauti na ile ya awali. Sasa wanataka kutathminisha mali za wahusika ili wamahishwe tena. Jambo hili halikubaliki kwa sababu zifuatazo:-

(1) Hakuna kwa kuwapeleka wananchi hawa ambao kwa miaka hiyo 15 wameshajenga nyumba za kudumu, shule, Makanisa na kadhalika.

(2) Wananchi hawako tayari kuhamishwa tena hata kama watafidiwa.

(3) Kutokana na ongezeko kubwa la watu, ni bora kujali binadamu kuliko kutaka ardhi kwa ajili ya wanyama ambao kwanza hawako. *TANAPA* wana mpango wa kuleta wanyamapori toka maeneo mengine.

(4) Nashauri *TANAPA* wasahau mpango huu wa kutaka ardhi ya ziada. Sheria ya Kutwaa ardhi ya mtu lazima akubali na siyo lazima. Pia lazima kipaumbele wapewa wananchi kwanza ili watu wasiwe watumwa ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, upimaji wa vijiji. Hivi kuna ardhi ndani ya vijiji isiyo na mwenyewe? Hivi wakati wa kupima vijiji, maeneo ya watu ambayo toka awali yamemilikiwa na watu iwe kwa kurithi, kwa kuuziana wao kwa wao au mtu ana Hati Miliki, je, ukipima kijiji na ukatoa Hati Miliki kwa kijiji maeneo hayo yaliyo ndani ya ramani hiyo yanakuwaje? Nani mwenye mamlaka na ardhi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, umiliki wa Mashamba ya TAUWAT – Njombe. Serikali imewamilikisha TAUWAT eneo kubwa sana. Inawezekana kwa wakati huo hakukuwa na tatizo lakini sasa hivi Mji wa Njombe umetanuka na sasa hivi hakuna pa kuendeleza mji huu kwa kuwa umezingirwa na mashamba ya TAUWAT. Sasa hivi TAUWAT imeuza eneo hili kwa kampuni nyingine. Kwanza kabisa, Kodi ya Ardhi iliyolipwa ni kidogo sana kuliko thamani ya ardhi ya sasa. Naomba Serikali ipitie upya umiliki wa mashamba haya na nasisitiza eneo lipunguzwe ili Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na Vijiji vyake liweze kutulimia. Pia mikataba ya uwekezaji kwenye ardhi iwe ni kulima au kupanda miti na iwe marufuku kwa mwekezaji kutumia ardhi aliyopewa kwa kukodisha badala ya kutumia yeye au kupanda miti yeye na endapo mwekezaji anakodisha ardhi ambayo naye amekodishwa na Serikali anyang'anywe mara moja.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuzungumzia Amadori, Kata ya Pembamnazi. Kuna mwekezaji kwenye eneo kubwa katika Kata hii. Mwekezaji huyu amefanya maendeleo kidogo sana huku wananchi hawana maeneo ya kulima au kujenga. Napenda kujua masharti ya mkataba huu. Kwa nini Serikali isitwae eneo hili na kuligawa kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mradi wa viwanja 20,000 Kibada. Baadhi ya viwanja kwenye baadhi ya vitalu viliuzwa bila ya barabara kutengenezwa. Kwa kuwa gharama ya uuzaji wa

viwanja ilijumlisha gharama za miundombinu, kwa nini miundombinu hii haijawekwa? Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha zoezi hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, *Dungu Farm*, Somangila. Kuna wananchi 105 ambao walitathminiwa mali zao wakati wa zoezi la kupima viwanja eneo la Mwongozo. Wananchi hawa walilipwa ardhi na mimea lakini waliokuwa na nyumba na mabanda hawakulipwa fidia yoyote. Naomba watu hawa walipwe fidia stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Vijibweni. Kuna taarifa kuwa Serikali inataka kutwaa eneo la takriban ekari 200 kwa ajili ya upanuzi wa bandari. Taratibu za zoezi hili hazikufuata Sheria ya Ardhi na Mipango Miji. Naomba zoezi hili lisitishwe na taratibu za Mipango Miji ziweze kufuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, viwanja vya mradi Kisota. Kuna taarifa kuwa wapimaji walipima viwanja zaidi ya vile vilivyotolewa. Maeneo haya yamekuwa pori hali inayopelekea uhalifu kuongezeka. Naomba mambo mawili yafanyike, kwanza, ufanyike *Land Audit* katika eneo hili na pili, Wizara itoe tamko kwa wamiliki kusafisha maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Mji Mpya wa Kigamboni. Wananchi wa Kigamboni walizuiwa kuendeleza na kujenga katika eneo la mradi kwa tamko la Serikali la Oktoba, 2008. Hadi sasa hatma ya mradi huu haijulikani huku wananchi wakitaabika sana. Wananchi wa Kigamboni wanataka majibu ya Serikali kwa maswali yafuatayo:-

(a) Mradi huu unaanza lini?

(b) Mradi unaanzia wapi?

(c) Haki na stahili zao ni zipi?

(d) Hatma yao ikoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kigamboni wanasema kuwa baada ya tarehe 30 Juni, 2012 hawatakuwa tayari kutoa ushirikiano kwa Serikali katika suala hili iwapo Serikali haitakuja na mpango thabiti unaojibu hoja na maswali yaliyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, kutokana na mpango kuwa na gharama kubwa, kwa kuwa utafutaji wa fedha kutoka vyanzo vya nje na toka kwa wawekezaji utachukua muda, ni vema Serikali ikaachana na mpango huu wenye kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Kigamboni.

**MHE. DKT. TEREZYA P.L. HUVISA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kujituma na kuhakikisha kuwa maendeleo ya ardhi yanafikiwa katika nchi yetu. Shukrani za pekee zimwendee Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka (Mb) kwa jitihada zake za kutumia uzoefu alioupata *UN Habitat* ili kuboresha masuala ya ardhi nchini Tanzania. Tunajivunia uzoefu alioupata na ni hazina kubwa tulioipata Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana masuala ya kisheria yanayohusu ardhi yazingatiwe. Bila kufuata Sheria ya Ardhi, migogoro nchini haitaisha. Kwa kuwa ardhi ni rasilimali pekee kwa Watanzania wote kwa ajili ya chakula na kukuza uchumi wa nchi, namwomba Waziri kuhakikisha kuwa Sheria za Ardhi hazipuuzwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la utunzaji wa mazingira ni lazima lipewe kipaumbele hasa kwenye fukwe za bahari na vyanzo vya maji. Viwanja visigawiwe kwenye vyanzo vya maji na fukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili nichangie walau machache juu ya Wizara hii. Kwanza, nianze na masuala ya ardhi. Mabaraza ya Ardhi kuanzia ngazi ya Vijiji na Kata inaonekana wahusika hawakupatiwa elimu ya kutosha kwa kazi yao na mipaka ya majukumu yao. Vijiji vingi kwa upande wa makazi, hakuna utaratibu mzuri wa ujengaji wa nyumba. Watu hujenga kiholela na kupelekea kutokuwa na sura nzuri, ikitokea haja ya gari kutaka kufika nyumba fulani, barabara za kupita kufikika mahali husika hukosekana. Sio hilo tu, watu huzuia viwanja kwa kudai ni sehemu za mababu zao. Badala yake huuza kwa bei watakayo na pengine kuzua migogoro isiyo ya msingi. Kwa hali hii, nashauri Serikali izidi kutoa elimu kwa Mabaraza haya kwani chombo hiki mara nyingi baadhi yao huwa ni wapenda rushwa hasa watakiwapo kusuluhisha habari au migogoro ya mashamba, mmoja wa wagonganao kama hana pesa hata kama ana haki hupelekea kukosa haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuzungumzia juu ya nyumba za Serikali ambazo ziliuzwa kwa watumishi waliokuwa wanaishi miaka ya nyuma ya 2005. Ukweli tendo hili Serikali ilikuwa imeteleza. Ingawa ilifanya hivyo wakati ikijulikana kabisa kwamba kutakuwa na watumishi wengine watakaopelekwa pale na kwamba wangehitaji mahali pa kuishi wakati hakuna nyumba zingine za mbadala, walitegemea watu hawa wataishi wapi? Licha ya hayo, bei iliyouziwa nyumba hizo ilikuwa ni ndogo kiasi cha kuonyesha wazi kwamba ulikuwa ni mpango maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nyumba za Serikali za hapa Dodoma ambazo Wabunge wanakaa, ni jambo la kushangaza kuona baadhi ya Wabunge waliopita ambao hawakubahatika kurudi tena Bungeni bado wanazimiliki nyumba zile kwa kuwapangisha Wabunge waliopo. Je, ni kwa nini Shirika la Nyumba hawaoni ya kuwa tendo hili linafanywa kinyume na taratibu za umiliki wa nyumba?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakumbuka ilitamkwa hapa Bungeni ya kwamba hadi kufikia mwakani kutakuwa na kijiji cha Wabunge. Je, utaratibu au ujenzi huo umeanza? Maana baadhi yetu bado tunaishi katika nyumba na mitaa ambayo haina usalama tunaostahili Wabunge kuishi. Hivyo naomba suala hili litiliwe maanani.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepima viwanja ya mradi, viwanja 20,000 na wananchi waliopata bahati ya kupata viwanja hivyo toka mwaka 2006 hadi leo Serikali imeshindwa kupeleka miundombinu hasa ya barabara na hivyo kuwazuia watu kuweza kufikia viwanja vyao kwa urahisi, huku ikizingatiwa Wizara imeviwekea Sheria viwanja hivyo ambavyo miaka mitatu kama hujajenga unanyang’anywa. Kwa mfano sehemu ya Mbuyuni toka mwaka 2006 watu wamemilikishwa ardhi lakini hadi leo ni pori tupu. Je, hapa wamesaidiwa au wamezidi kukandamizwa wananchi na Serikali yao? Kwa hivyo, naishauri Serikali kupeleka miundombinu ya barabara ili wananchi waweze kufikia maeneo yao na kuweza kujenga na kuhamia na kujipatia makazi bora. Kwa kuwa watu hawa wameshalipwa gharama zote na Serikali si vizuri wananchi hawa wakazidi kuteseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua ni vipi ardhi katika nchi yetu wanapewa wageni na sisi Watanzania tunabaki kuwa vibaraka, je, kesho na kesho kutwa tutakwenda wapi? Hakuna hata nchi moja duniani ambayo ardhi yake wanapewa wageni hata wakiwa na uwezo gani wa fedha bali ardhi inabaki kuwa rasilimali ya wananchi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihamishe ardhi mikononi mwa wageni na kurudisha kwa wananchi na mgeni awe anakodi tu ardhi hiyo na sio kumiliki kama ilivyo sasa tunaona fahari ardhi yetu kuwapatia wageni kwa kisingizio cha uwekezaji. Naishauri Serikali izuie wananchi wasiuze ardhi kwa wageni bali waingie ubia na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanja vya wazi kwa ajili ya michezo na mapumziko vyote sasa hivi vimevamiwa na kujengwa au kuwekwa uzio hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Kweli Serikali haioni umuhimu wa kuwa na viwanja vya wazi? Naishauri Serikali kuvirejesha viwanja vyote vya wazi vilivyo katika mpango wa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa Hati Miliki, Wizara ya Ardhi kunakuwa na rushwa kubwa katika utoaji wa huduma zake. Pia rushwa katika kutoa *form* ya kupata kiwanja au kutoa hati ya kiwanja au kupata nyumba za *NHC*. Katika kupata nyumba za *NHC,* kuna

wafanyakazi wanatumia madalali juu ya upatikanaji wa huduma hizi. Nyumba ni ya Shirika lakini kuipata lazima upitie kwa dalali kwanza. Je, Wizara ina utaratibu gani wa kupata Nyumba za *NHC* na kwa nini madalali wanakuwa wanajua siri zote za *NHC*? Taarifa hizi wanapata wapi kama si kutoka kwa wafanyakazi wa Wizara, naomba ufafanuzi kuhusu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapimaji wa ardhi. Kumekuwa na gharama kubwa za upimaji wa ardhi, watu wetu ni maskini pale wanapohitaji kupimiwa ardhi gharama wanazopewa ni za kukatisha tamaa na ndio maana watu wengi wanashindwa kulipa kwa ajili ya kupimiwa ardhi zao kwa sababu ya gharama za upimaji kuwa kubwa. Naiomba Serikali iweke kiwango cha wazi cha uthamini wa ardhi ili wananchi waweze kuthaminiwa ardhi zao na kupimiwa na kupata Hati Miliki ili kuepukana na migogoro ya ardhi. Mtu anakaa miaka 30 na eneo ni lake lakini mwisho wa siku anajikuta anahamishwa kwa sababu hana Hati Miliki. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kupima ardhi za wanyonge kwa gharama ndogo kabisa? Naomba nipatiwe ufafanuzi kwenye hizi hoja zangu kwenye majumuisho.

**MHE. JEREMIAH S. SUMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Tibaijuka, Anna Kajumulo, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na hongera kwa hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, andiko hili linahusu hasa mashamba makubwa yaliyoko eneo la Hamashauri ya Wilaya ya Meru, Arusha ambayo hapo awali yalikuwa "*Coffee Estate*" ambayo sasa yamekuwa *seriously abused* kwa kubadilisha matumizi yake. Kwa kuwa hati za ardhi zinapotolewa na Serikali zinakuwa na masharti hasa ya matumizi, ni hatua gani Serikali inachukua pale matumizi hayo yanapobadilishwa na mwenye hati? Je, hatua hizo ni pamoja na Serikali kufuta hati husika? Ikiwa Halmashauri ya Meru itamletea/kumpatia Mheshimiwa Waziri vielelezo vya wazi kuwa mashamba hayo hayatumiki kulingana na hati inavyosema ikiwa ni pamoja na:-

(1) Total *neglect* ya shamba hadi linakuwa pori.

(2) Kupima viwanja na kuuza kwa bei ambayo mwananchi wa kawaida hawezi kununua.

(3) Kupima viwanja na kujenga nyumba za kuishi – etc.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kumshauri Mheshimiwa Rais afute hati husika na kuagiza mashamba hayo wapewe wananchi wayaendeleze kwa lengo la kuongeza mapato yao na pia kuchangia uchumi wa nchi?

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipongeze utendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao umekuwa ukiboreka siku hadi siku na kujiondoa na sifa mbaya ya rushwa iliyokuwa ikiiandama Wizara hii kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba kupewa ufafanuzi ni lini Wizara itaweka mkakati na kuutekeleza wa kupima makazi katika Miji Midogo na Vijiji kwani kukua kwake sasa kunapelekea ujenzi holela au *squatters.* Kuacha hali ya sasa iendelee hatimaye tutakuwa na Miji michafu, isiyopendeza kwa sababu haikupangwa. Haifai nchi yetu iwe na Miji na Vijiji vya ovyoovyo ambavyo hata jinsi ya kufikisha miundombinu ya maji, umeme na majitaka inakuwa vigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Ardhi anifafanulie kuhusu mkanganyiko wa kiwanja kilichogawanywa mara mbili katika eneo lililokuwa *"site"* ya ujenzi wa barabara ya Nyanguge – Musoma katika kijiji cha Yitwimila A, Wilaya ya Magu. Katika namna ya kutatanisha, Watendaji wa Wizara ya Ardhi waliligawanya eneo hilo bila ridhaa ya wananchi na kumgawia Mhindi – *Ask Investment* na hivyo kukwamisha matumizi ya majengo yaliyopo kuanzia Sekondari ya Kidato cha Tano na sita. Jimbo la Magu halina hata Shule moja ya *"A Level"* na tulitegemea kuyatumia majengo hayo kuanzisha shule moja. Naomba Waziri anifafanulie, ni lini kero ya uwanja na majengo hayo itatatuliwa ili wananchi waweze kuendelea na mpango wao kwani hali ya

mahusiano kati ya mwekezaji huyo bandia na wananchi wa kijiji cha Yitwimila A ni tete na inaweza kupelekea uvunjifu wa amani. Naomba majibu thabiti ya kuwatia imani wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia majibu, mbona ramani iliyowasilishwa Wizarani kwa ajili ya kupitishwa ya Mji Mdogo wa Lamadi inachukua muda mrefu? Mji wa Lamadi ambao uko kwenye eneo la kitalii karibu na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Ziwa Victoria unakua kwa haraka sana. Tunaomba ramani hiyo ipitishwe ili wananchi waweze kuanza kuendeleza maeneo yao kwa kufuata Mpango Mji na kuruhusu kupata mapato kutokana na uwekezaji unaosubiriwa wa viwanda, mahoteli, stendi ya mabasi na kadhalika. Naomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi katika majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linalolikumba Jimbo langu ni utata wa mpaka uliopo kati ya Vijiji vya Lamadi, Mwakiloba na Kijilishi kwa upande mmoja na Pori la Akiba la Kijereshi na Hifadhi ya Taifa Serengeti. Eneo hili limekuwa na mgogoro mkubwa kwa muda mrefu. Hakuna alama za dhahiri. Tunaomba maeneo ya Vijiji yapimwe ili kuondoa msuguano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kuonyesha wasiwasi wangu kuhusu ongezeko la migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima. Je, Serikali ina mipango gani thabiti ya kuhakikisha kwamba migogoro hiyo kati ya wafugaji na wakulima inakwisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa katika Wizara hususani kwa Mabwana Ardhi imekithiri kutokana na ukweli kwamba kila viwanja vinapopimwa, sehemu kubwa ya viwanja hivyo humilikiwa na Mabwana Ardhi kwa kutumia majina mbalimbali. Je, Wizara ina mikakati gani kukomesha tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wangependa maeneo yao yapimwe ili pamoja na mambo mengine ardhi iliyopimwa iwe dhamana kwa kupata mikopo kwa ajili ya maendeleo. Kwa bahati mbaya, gharama za upimaji ni kubwa sana kiasi kwamba wananchi wengi wanashindwa kumudu gharama hizo. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuwawezesha wananchi wapimiwe ardhi yao?

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudi za Wizara kwa kusimamia vizuri majukumu yote yaliyo chini ya Wizara. Nawapongeza sana uongozi wa Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wengine wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara, naomba suala la migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ishughulikiwe. Katika baadhi ya maeneo, Maafisa wa Ardhi wamekuwa chanzo cha migogoro hiyo na kuichochea kwa kutofuata haki katika kutatua migogoro. Naomba Wizara ifuatilie kwa karibu sana mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji kwenye eneo la Kitongoji cha Wali - Kijiji cha Izava, Wilaya ya Chamwino na baadhi ya wafugaji wanaosemekana ni wakazi wa kijiji cha Chitego, Wilaya ya Kongwa. Mgogoro huu ni mkubwa na umeshagharimu maisha ya watu. Jambo hili ni zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo pia tatizo la migogoro ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya, nalo lisipoandaliwa mikakati ya kukabiliana nalo, amani na utulivu vinatoweka. Yapo maeneo mengi yenye migogoro ya aina hii. Kwenye Jimbo langu la Chilonwa, migogoro hii ipo kwenye mipaka ya Chamwino na Kondoa, Chamwino na Kongwa. Ni vema wataalamu wa ardhi wakajipanga kukabiliana nayo.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sambamba na shukrani hizo, naomba pia kuunga mkono hoja hii.

Aidha, nampongeza Waziri wa Wizara hii, Profesa Anna Tibaijuka kwa moyo wake wa kuwatumikia Watanzania. Sambamba na pongezi hizo, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu katika Wizara hii ni ukuaji wa haraka wa Miji yetu lakini ukuaji wake unakuwa holela, hakuna mpangilio wowote wa Miji yetu. Hali hii inatisha. Bila shaka hii ni changamoto kubwa sana kwa Wizara. Serikali inasubiri kwanza watu wajenge nyumba ndipo upimaji wa viwanja unaanza. Gharama pia ya kupima viwanja ni kubwa na hivyo mwananchi wa kawaida kushindwa kumudu gharama hizo. Naiomba Serikali ipunguze gharama za kupimia viwanja na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wananchi wachache sana wanaojua kwamba ardhi ni mali na ndio maana wananchi wanajiuzia ardhi kwa bei ndogo. Suala la ardhi kuwa ni mali linahitaji elimu ya hali ya juu kwa wananchi la sivyo wageni hasa Wakenya na kadhalika wanaojua kwamba ardhi ni mali watanunua yote na kuwafanya wananchi kuwa wageni kwa nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuangalia upya gharama za upimaji viwanja na mashamba, sambamba na hilo uanzishwaji wa Miji mipya uende sambamba na kutolewa kwa *master plan* ili wananchi wasijenge holela. Kuna haja pia ya kuangalia uimarishaji wa Sheria *(enforce)* ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nimpongeze Waziri na timu yake kwa jinsi walivyoonyesha juhudi zao za kuboresha utendaji wote wa Wizara hii. Hata hivyo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Tibaijuka (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole-Medeye, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni yangu kuhusiana na utendaji mbovu unaofanywa na Halmashauri zetu. Halmashauri zetu nyingi hapa nchini zimekuwa chanzo cha ugawaji mbovu wa ardhi. Wananchi wengi wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana kwa viwanja kuwa na *double allocation.* Hali hii imesababisha kuwa na kesi nyingi sana za ardhi mpaka kusababisha wananchi wengine kubomolewa nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona wafanyakazi wa Ardhi katika Halmashauri mpaka wafanyakazi wa Wizara hii Makao Makuu wanakula njama na wenye pesa na kuwanyang'anya umiliki wa ardhi wananchi wasio na uwezo sababu ya tamaa zao. Naomba hili liangaliwe sana na Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni urasimu uliopo katika Wizara hii katika ugawaji wa ardhi. Kwa kuwa kumiliki ardhi ni haki ya kila Mtanzania, naomba Idara hii uwepo uangalizi maalum. Wananchi wanawalalamikia sana Maafisa Ardhi kuanzia ngazi ya Halmashauri mpaka Wizarani, Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona mara nyingi Maafisa Ardhi hawa wanapoharibu sehemu moja hatua wanazochukuliwa ni kuhamishwa tu kutoka sehemu aliyoharibu na kupelekwa sehemu nyingine. Matokeo yake yule mfanyakazi mbovu anakwenda kuharibu tena kule anakohamishwa na mbaya zaidi unaweza hata ushahidi ukawepo kabisa kwa sababu zisizoeleweka Mtendaji huyo mbovu analindwa. Naomba kama kunakuwa na uthibitisho wa tuhuma basi wafanyakazi hao wabovu wasimamishwe mara moja au wafunguliwe kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuzwaji wa ardhi katika Halmashauri. Kumekuwepo na malalamiko makubwa sana kwa wananchi wetu kuhusu bei wanazopanga kwa ajili ya ununuzi wa viwanja. Kutokana na malalamiko hayo, Wizara ingeweka chombo cha kusimamia upangaji wa bei katika maeneo hayo kwa sababu wananchi wengi hali zao za kipato ni ndogo na mbaya

sana, wananchi wengine walikuwa wamiliki wa maeneo hayo kabla hayajapimwa. Naomba Wizara hili iliangalie kwa umuhimu wake ili wananchi wasipoteze imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR**: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake kwa ushirikiano mzuri katika utendaji wa kazi, napenda kuunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja kuhusu tatizo la ugawaji wa viwanja. Kuna tatizo kubwa la kiutendaji katika Halmashauri zetu katika zoezi la ugawaji wa viwanja hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

(1) Viwanja kugawiwa (kutolewa) kwa zaidi ya mtu mmoja.

(2) Bei ya viwanja ni kubwa sana hailingani na eneo vilivyopo.

(3) Ucheleweshaji wa kupatikana viwanja kwa wahusika.

(4) Kuna harufu ya rushwa kwa baadhi ya Watendaji wanaohusika na zoezi hili wakati wanagawa viwanja (viwanja vingi wanapeana wao kwa wao kwa maana ya urafiki au ujamaa.

(5) Mwombaji mmoja anaweza kupewa zaidi ya viwanja viwili mpaka vitatu na wengine kukosa.

(6) Viwanja kupatiwa wageni ambao sio Watanzania katika maeneo makubwa sana (hakuna uzalendo).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mengineyo, napenda kuishauri Serikali iweze kurekebisha matatizo hayo na mengine mengi yanayowapata wananchi, matatizo juu ya upatikanaji wa viwanja. Pia naishauri zaidi Serikali kuwatengea wananchi maskini maeneo ili waweze na wao kuuziwa viwanja kwa bei ya afadhali (bei ya chini) ili na wao wawe na nyumba za kuishi na familia zao na sio kuwapatia viwanja watu walio na fedha nyingi tu. Kufanya hivyo ni kuwafanya walio nacho wawe nacho zaidi na wasio nacho wasipate zaidi. Lazima Serikali iwe na huruma na wananchi maskini wa nchi hii maana na wao wanatozwa kodi kama wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya Watanzania waliopata fursa ya kumiliki ardhi ni wale wenye uwezo kifedha, wenye ajira rasmi na wengi wao ni vigogo na wafanyabiashara wakubwa. Asilimia 60% ya Watanzania ni vijana ambao wanatengeneza asilimia 14.4% ya Watanzania wasiokuwa na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashuhudia wawekezaji wamekuwa wakimilikishwa ardhi kwa madai kwamba wanawekeza kwenye kilimo, kwa lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo. Pia kumekuwa na migogoro ya wananchi wenye uwezo wa chini au maskini kushindwa kumilikishwa ardhi na wengine kunyang'anywa na kulipwa fidia ndogo. Je, Wizara ina mkakati gani wa kumlinda Mtanzania maskini aweze kumiliki na kunufaika na ardhi ambayo ndiyo mkombozi pekee wa maisha yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia kwamba Wizara imeanzisha kitengo kwa ajili ya utaratibu wa kugawa ardhi kwa ajili ya kuwapa wananchi ili kuendeleza mpango wa Kilimo Kwanza. Je, katika utaratibu huo, Wizara imeweka utaratibu upi utakaomwezesha kijana wa Kitanzania naye aweze kupata fursa hiyo ya kumiliki ardhi ili aweze kuendesha kilimo kitakachoweza kumuinua kiuchumi na kumuondolea umaskini kwa kuweza kujiajiri mwenyewe?

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri yenye kutoa sura ya matumaini makubwa katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie hotuba ya Wizara katika utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Wizara katika kipindi kilichopita (2010/2011) iliandaa na kutoa Hati Miliki za Kimila katika Halmashauri mbalimbali lakini Wilaya ya Ulanga haikuwemo. Napenda kujua sababu zilizosababisha kwa Wilaya kutofanya hivyo licha ya maombi mbalimbali toka katika vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Ardhi watuangalie kwa ukaribu na kuipa kipaumbele Wilaya ya Ulanga kwa kutuwezesha kuanza na kukamilisha zoezi la kusajili na kutoa Haki Miliki za Kimila. Zoezi hili ni mojawapo ya Ahadi/Ilani za Chama cha Mapinduzi (CCM) ndani ya Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayofanywa na Wizara ni nzuri. Changamoto kubwa ni kuwa na wataalam wa kutosha ili kila Halmashauri ya Wilaya iwe na wataalam wanaohitajika kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa urasimu na malalamiko ya rushwa yamepungua lakini bado upo ucheleweshaji mkubwa wa kupata hati hasa Wilayani. Pengine tatizo ni uwajibikaji wa wafanyakazi kwenye Halmashauri au Wizarani. Ni wakati gani wafanyakazi hawa wanaitwa na kupewa miiko ya kazi kadri ya weledi wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mbinga, nina haya ya kuchangia:-

(i) Ingekuwa vyema kuendeleza mradi wa Masijala za Ardhi ili ifike ngazi ya kila kijiji ikiwa ni pamoja na kuwapa vitendea kazi kama *computers.*

(ii) Kuna kiwango kikubwa cha migogoro ya mipaka kati ya vijiji.

(iii) Mamlaka ya Mji Mdogo Mbinga unahitaji kupimwa upya ili kuandaa majukumu ya kuwa mji kamili. Nitafurahi kupata ushirikiano na maongozi ya Wizara katika jambo hili. Ni tamaa yangu kuwa tunajenga Mji mzuri wa kisasa. Nitafurahi kupata msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshwaji wa makazi. Ni vyema kuwa na chombo kinachoweza kutoa *grant*/mikopo ya bei nafuu sana ili kutoa fedha ya kuboresha makazi.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nyumba kwa mikakati yake mizuri, angalau kwa kiasi fulani Wizara hii imeweza kufuatilia mambo mbalimbali yanayohusu ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile nyumba ambazo zimewekewa alama ya ‘X’ kwa maana kwamba zinatakiwa zibomolewe ili kupisha ujenzi wa barabara, kwa kweli ni kero kubwa. Wananchi wamewekewa ‘X’ katika majumba yao, hawajui wanalipwa lini, malipo hakuna na ujenzi wa barabara haupo, ila watu wamebaki na ‘X’ katika nyumba zao na hivyo kushindwa *either* kufanya muendelezo wowote wa ujenzi au kusitisha mradi na biashara zao zilizokuwepo katika maeneo hayo. Naiomba Wizara ikishirikiana na Wizara ya Ujenzi iliangalie suala hilo, mara maamuzi yanapofanyika ya upanuzi wa barabara, nyumba zilizowekewa ‘X’ ni vema zilipwe mara moja na ujenzi unaokusudiwa ufanyike ili wakazi wa maeneo husika waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kufoji hati katika Wizara bado lipo na *definitely* linafanywa na *staff* walioko ndani ya Wizara hii. Naiomba Wizara iendelee kusimamia suala hili ili mchezo huu wa kudhulumiana viwanja ukome kabisa. *Either* naendelea kuiomba Wizara kuendelea kusimamia urasimu wa kutoa hati za viwanja. Tarehe za kurudi Wizarani zinakuwa

nyingi mno, njoo kesho, njoo kesho kutwa na ukifika kesho kutwa, faili halipo, vipimo havionekani, kwa kweli hali hii hainifurahishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kiwanja kimoja kumilikiwa na watu wawili linatokeaje kama kweli *staff* wa Wizara hii hawahusiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri ya kuiweka Wizara hii vizuri, tunaomba akaze buti bado mambo yasiyofaa ambayo nimeyataja hapo juu na mengine yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka (MB) na Naibu wake, Mheshimiwa Goodluck Ole- Medeye (MB), kwa hotuba nzuri ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012 ya Wizara yao. Naunga mkono hoja yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara tu baada ya kuteuliwa kwao, niliwafikishia ombi viongozi hawa wawili wa Wizara la Wilaya ya Kyela kuanzishiwa Baraza la Ardhi la Wilaya. Ombi langu walilipokea na kuahidi kulifanyia kazi baada ya kuzingatia kuwa kwa miaka mingi sasa wananchi kutoka Wilaya ya Kyela hulazimika kusafiri hadi Wilaya jirani ya Rungwe kwa ajili ya rufaa zao kutoka Mabaraza ya Ardhi ya Kata. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wanieleze hatua ya hili suala kwa maslahi ya Wanakyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono kwa asilimia 100/100.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi kubwa ya vijiji vya Hingawali, Simana, Navanga na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo yalikuwa ni mashamba ya Katani Lindi lakini sasa ni mapori matupu, hayahudumiwi tena. Wananchi wa maeneo hayo wameomba ardhi hiyo ifutwe umiliki wa mtu aliyekuwa analima katani ili wapewe wananchi, kwani sasa ardhi hiyo ni mapori matupu, je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi hatuna nyumba bora, tunaomba wafadhili waje kama *NSSF* na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi za nyumba za kuishi ni adhabu kwa wananchi. Tunaomba suala la kodi za nyumba ambazo wananchi wanaishi tu zisitozwe kodi za Serikali, suala hilo liangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa 100/100.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo zimepiga hatua kubwa juu ya kuhifadhi na kulinda ardhi kwa maslahi ya wananchi wake lakini yapo matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza katika sehemu mbalimbali za Tanzania, hii sio ishara nzuri kwa Taifa lolote lenye kujali maslahi ya watu wake na ustawi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi hivi sasa hapa nchini inaonekana inakaribia hatua ya kupelekea uvunjifu wa amani katika Taifa letu. Hali hii inahitaji jitihada za makusudi katika kukabiliana na changamoto mbalimbali. Awali migogoro hii ilikuwa ikitokea kwa jamii moja na nyingine za Watanzania lakini sasa uingiaji wa wakimbizi katika maeneo mengine ya Tanzania imekuwa ni changamoto ya pekee kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wakimbizi ambao wameanza kumiliki ardhi na huwasababishia wazawa hasara kubwa na misuguano ambayo haimaliziki. Tunaelewa kwamba mara nyingi kama migogoro ya ardhi haikudhibitiwa husababisha mauaji ya watu katika sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa wageni katika ardhi ya Watanzania. Ni kweli kwamba Taifa linaendelea kwa kupitia nyanja mbalimbali ambazo ni pamoja na uwekezaji, lakini basi hatua za makusudi lazima zichukuliwe ili kuhakikisha wawekezaji wanafuata Sheria za nchi na watu wenye maeneo wanafaidika na ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kupitia wananchi kwa wawekezaji, hii ni pamoja na kuchukuliwa ardhi kwa nguvu na malipo yasiyoridhisha kutokana na thamani ya ardhi hiyo, kucheleweshwa kwa malipo kwa wananchi husika na pia kupewa mikataba hewa ambayo utekelezaji wa shughuli za mikataba hiyo unakuwa sio endelevu na kupelekea wananchi kuishia Mahakamani bila ya mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Serikali ijitahidi katika kusimamia na kuangalia taratibu zote za ardhi na kuhakikisha kila kero inapatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mungu kuniwezesha uhai na uzima nami nichangie Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu kaijalia Tanzania kuwa na ardhi kubwa ya kutosha, ardhi ambayo ikisimamiwa vizuri basi ni hazina tosha kwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ya Tanzania imekusanya mali mbalimbali mfano gesi asilia, mafuta na madini. Kwa maana hii, ardhi ndio nchi, ardhi ndio Tanzania kama hapana ardhi hapana nchi, hapana Tanzania kwa sababu hakuna nchi yoyote duniani ipatikanayo katika hewa. Kwa misingi hii, naishauri Serikali kuhusu utunzaji bora wa ardhi, matumizi bora ya ardhi na hifadhi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yoyote ambayo nimesema hapo juu ni lazima tupange mikakati maalum na hatua madhubuti za utekelezaji. Ni muhimu kuwa na wataalam wa kusimamia na kutoa ushauri wa matumizi na hifadhi bora ya ardhi yetu. Ikiwezekana wataalamu wapatikane katika kila Kata kwa ajili ya usimamizi na kutoa elimu yenye tija, elimu endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni kisiwa cha amani na utulivu duniani, Mungu atuzidishie Amina. Matatizo mengi ya uvunjifu wa amani katika nchi nyingi duniani husababishwa na siasa au migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pasi na darubini utagundua ndani ya Taifa letu Tanzania tayari migogoro ni mingi sana na hasa kwa matajiri na maskini, wazawa na wageni, wakubwa Serikalini na wadogo. Hii ni mbegu mbaya sana na haifai kupandwa. Ushauri wangu wa bure kwa Serikali ni kuunda Tume adilifu ishughulikie matatizo yote ya ardhi Tanzania nzima pasipo upendeleo wala chuki na haki itendeke kwa wote. Malenga husema, 'kinga ni bora kuliko tiba', 'Mbuyu umeanza kama Mchicha', hivyo kuondoa matatizo mapema ni bora kuliko kusubiri kuwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Dar es Salaam, ni Jiji kubwa Tanzania ambalo linaongoza mkusanyiko wa watu wengi kuliko Mikoa yote. Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na matatizo makubwa sana ya maeneo ya mapumziko, maeneo ya burudani na michezo kutokana na ujenzi holela ambao unasababishwa na usimamizi mbaya. Watoto wadogo wamekosa sehemu za viwanja vya michezo na wamekuwa wakicheza mipira barabarani. Kitendo hiki husababisha ajali. Mimi naiomba Serikali iangalie kwa makini sana miundombinu ya Mikoa yote ya Tanzania kwa ajili ya mipango bora ya Miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba limegubikwa na wimbi kubwa la wizi na rushwa. Kwa mfano, kuna taarifa kuwa wafanyakazi wa Shirika la

Nyumba wanashirikiana na wapangaji wenye asili ya Kihindi kuliibia Shirika mabilioni ya Shilingi. Vilevile mwaka 2010, Katibu Mkuu wa Wizara alikemea kuhusu hali ya ubadhirifu iliyopo kwa kutoa mfano wa pesa za pango kuingia katika akaunti binafsi ya Watendaji wa Shirika. Inasikitisha sana, hatua madhubuti za kung'oa mtandao huu wa wabadhirifu hazijachukuliwa na Wizara. Hivyo, naitaka Wizara itoe ufafanuzi wa suala hili katika majumuisho ya kuwaondosha wale wote wanaohujumu Shirika pamoja na kubadilisha uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Nyumba za Wabunge. Wabunge wengi hawajapata nyumba za kuishi wanapokuwa Dodoma. Wengi wanakaa katika hoteli zilizokuwa na hali duni na zenye kuhatarisha mali na maisha yao. Wizara imeshindwa kuwapa nyumba Wabunge hawa wanaoishi katika hali hatarishi? Kuna Wabunge wa zamani ambao hawajarejesha nyumba ili wapatiwe wale wanaohitaji. Baadhi ya Wabunge hao wa zamani ambao sasa si Wabunge tena wana nyumba mbilimbili na wengine wanafanyia uganga wa kienyeji. Namwomba Waziri atoe tamko rasmi kuhusiana na suala hili, Wabunge waliokosa Ubunge wanyang'anywe nyumba na wapewe Wabunge wapya.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la mikopo ya nyumba. Sheria hii ijapokuwa imeshapitishwa na baadhi ya benki kutoa mikopo, lakini bado riba ni kubwa sana. Inakuwa vigumu kwa wananchi na hasa wa kati kuweza kupata mikopo. Ni vizuri Serikali ikaharakisha uanzishaji wa *Tanzania Refinancing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Land Bank* nalo ni la muda mrefu sana lakini inaonekana bado kuna kusuasua katika kuanzisha. Nashauri taratibu za kuanzisha *Land Bank* ziharakishwe ili ianze kwani hii itasaidia sana katika kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upimaji Miji, hivi sasa nyumba nyingi za ghorofa zinajengwa Jijini Dar es Salaam. Si jambo baya lakini ni vizuri kuwe na ufuatiliaji wa Sheria za ujenzi katika Miji yetu, si ajabu siku hizi kuona nyumba mstari mmoja, zingine zina ghorofa tatu zingine tano, zingine 10 na kadhalika pamoja na zile za kawaida. Kimandhari haipendezi na inatoa hisia ya kufanya mambo bila kufuata Sheria yoyote. Pamoja na ujenzi wa ghorofa, tatizo la miundombinu ya majitaka na kadhalika ni kubwa. Kwa maana hiyo, nyumba hujengwa bila ya utaratibu wa kuwa na mifereji ya kupitisha maji ya mvua. Nyumba kadhaa zinajengwa bila ya kuwa na sehemu za kuegesha magari kwa hivyo kwa sehemu kubwa magari huegeshwa barabarani na kuleta adha kubwa kwa waenda kwa miguu mfano ni ujenzi unaoendelea barabara ya Mindu – Upanga, pande zote za barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kawaida ya kupanga mipango ya miji yetu kwa zaidi ya ujenzi wa nyumba, ni muhimu suala la kuangalia kuweka maeneo ya burudani mfano bustani, *parks* na kadhalika. Nilikuwa Berlin (Ujerumani) na ni jambo la kufurahisha kwani maeneo mengi kati ya eneo wanapoishi watu kuna *parks* ili watu waweze kujipumzisha na watoto wawe na maeneo ya kucheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni sekta mtambuka, lakini ni sekta muhimu kwa maendeleo na kwa uwekezaji. Hivi sasa kuna migogoro mingi inayohusu ardhi. Mara nyingine sekta hii haionekani kwa umuhimu huo. Ni muhimu mwakani Wizara hii ipewe bajeti kubwa zaidi. Pia inapokuja katika suala la *"Retention"* wapewe kubaki na hiyo asilimia 100. Itasaidia nao kuongeza fedha kuwapa Halmashauri yaani gawio ili waweze kufanya kazi kubwa zaidi katika ukusanyaji wa kodi na hivyo kuongeza mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kasi ya upimaji wa Vijiji na utoaji wa Hati za Kimila iongezwe. Hii itasaidia sana kupunguza migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi. Serikali ina haja ya kufanya mikakati ya makusudi kutatua migogoro hii ya ardhi ambayo inagharimu maisha mengi ya Watanzania haswa Vijijini ambako kuna mila za kuwakandamiza wanawake pindi wenza wao wanapotangulia mbele za haki. Ni wajibu wa Serikali kuangalia matatizo ya ardhi katika mgawanyo ambao umeibuka kwa wakubwa kupewa ardhi kubwa sana na wanyonge kunyanyaswa hata kuhamishwa katika makazi yao mfano halisi ni Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kuhusu ugawaji wa ardhi iliyokuwa ya *NARCO Ranches*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi kupewa wageni. Kama Sheria ya Ardhi inavyobainisha, ni marufuku kwa wageni kumiliki ardhi isipokuwa chini ya Sheria ya Uwekezaji. Je, Serikali ina habari katika maeneo ya Arusha na Kilimanjaro kuna wananchi wengi wa nchi jirani wamekamata ardhi yetu? Tukumbuke Jumuiya ya Afrika Mashariki inakuja, je, Sheria inasemaje kwa wanachama wa Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi. Pamekuwepo na vifaa duni vya kuweza kutekeleza upimaji wa ardhi pote nchini. Kuna baadhi ya Maafisa hawana darubini, magari, pikipiki kama tujuavyo miundombinu ya nchi yetu ni migumu sana na sehemu moja mpaka nyingine ni mbali sana. Je, Serikali katika bajeti hii imetenga fedha zozote zipelekwe katika kila Mkoa ili waweze kupata vifaa vya kupima ardhi ikiwa ni pamoja na vitendea kazi vingine kama *computer,* magari na kadhalika ili waweze kutimiza kazi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya malipo ya fidia. Pamekuwepo na matatizo makubwa na malalamiko mengi kwa wananchi kutokulipwa au kupunjwa fidia zao pindi Serikali inapowataka wahame katika maeneo yao ili kupisha matumizi hayo kwa ajili ya shughuli za Serikali. Mfano halisi wananchi wa Kigamboni wanaishi kwa matumaini, wameambiwa waondoke watalipwa kwa sababu patajengwa Mji Mpya wa Kigamboni ambao utajengwa kisasa. Wananchi wale wamelipwa kiasi kidogo sana. Badala ya Mji kujengwa sasa viwanja vile vinauzwa kwa bei ya juu sana. Naomba maelezo kuhusu hili. Je, Mji ule bado unajengwa na mchakato umefikia wapi?

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawapongeza sana Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya nchini kote katika kusimamia haki na Sheria ya Ardhi na Makazi. Nawapongeza wote kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kusimamia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja kadhaa ambazo ni kero kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Shinyanga ambapo wananchi wamesisitiza nisiunge mkono hoja endapo kero zao hizi kubwa hazitachukuliwa hatua na Serikali. Ni matumaini yangu hoja hizi watazichukua kwa uzito mkubwa kwa kuwa tumezizungumzia kwa muda mrefu sasa baina yetu:-

(1) Serikali inawasaidiaje wananchi wa Shinyanga Mjini ambao wapo Mahakamani na wengine wameshahukumiwa na Mahakama ya Ardhi kuhama kwenye maeneo yao ya asili wanayoyamiliki kwa Hati za Kimila kwa mujibu wa Sheria? Je, Serikali ipo tayari kutengua maamuzi gandamizi ya Baraza la Ardhi?

(2) Sheria ya Ardhi (Hati za Kimila) zimevunjwa kwa kiasi kikubwa na Watendaji wa Idara ya Ardhi katika Manispaa ya Shinyanga na kusababisha uvunjifu wa amani. Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi waliodhulumiwa haki yao ya msingi kwa maeneo yao kuuzwa ama kupewa watu wengine haki ya kumiliki ardhi?

(3) Je, Wizara inachukua hatua gani kwa Watumishi wa Umma waliojihusisha na vitendo vya uvunjifu wa Sheria kwa kuwa katika maeneo ya Ndembezi, Kitangili na Kizumbi, Ndala na Masekelo ambapo kiwanja kimoja kimeuzwa mara mbili mpaka mara tatu? Je, Serikali ipo

tayari kufuta *offer* zote zilizotolewa kwa kukiuka Sheria ya Ardhi katika maeneo ya Ndembezi, Kitangili, Ndala, Masekelo na maeneo mengine ya Manispaa ya Shinyanga?

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba yake nzuri yenye kutia matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie migogoro katika Wilaya ya Misungwi hasa katika Kijiji cha Usagara ambapo Watendaji wa Ardhi wa Wilaya wamekuwa wakipima ardhi bila kuwahusisha wenye mashamba. Hii imesababisha wananchi kugomea upimaji wa kijiji hiki ambacho kiko karibu sana na Mwanza na hatari ni kwamba Mji utafika eneo hili likiwa halijapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maeneo ya Mwasonge na Nyanhomango ambayo yametengwa kwa ajili ya *EPZ* yapimwe na wananchi wapewe fidia ili kuondoa usumbufu uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri yeye binafsi na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kuiongoza Wizara ya Ardhi.

Baada ya pongezi hizi, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu ujenzi holela Mijini. Ni tatizo la hatari kwa usalama wa wakazi wa Mijini. Nimesoma mikakati ya Wizara ya kukabiliana na changamoto hii lakini sikuona nini Wizara itafanya kwa maelfu ya nyumba zilizojengwa Mijini kiholela. Maeneo haya magari hayawezi kupita na wala hakuna uwezekano wa kuorodhesha mitaa na kuweka alama *(identify)* ya kila nyumba wala kuweka huduma za jamii. Je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, matatizo ya ujenzi wa nyumba holela unachangiwa sana na *speed* ndogo ya upimaji ardhi kwa ajili ya viwanja vipya ili wakazi wa Mijini wanapoomba ardhi ya kujenga wapate maeneo yaliyopimwa tayari katika kila Mji. Maeneo hayo zaidi ya ulazima wa kuyapima vilevile ni lazima utayarishaji wa miundombinu ya barabara, maji, umeme viwe tayari. Je, Wizara inasema nini juu ya hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni *Land Bank* na changamoto zake. Ni kweli tunahitaji chombo kitakachosimamia hazina ya ardhi ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa shughuli za uwekezaji *(Land Bank).* Navyoamini taratibu za *Land Management* kisheria na *Land ownership* zinasuasua mno wakati *demand for land* unakua kwa *speed* kali. Kwanza, tunahitaji kuharakisha kuweka mipaka ya Vijiji ili kila Kijiji kijue kinaishia wapi ili kuepuka migogoro ya ardhi. Pili kutambua mapema maeneo ya uwekezaji na kuyapima yote nchi nzima kwa shughuli zote za uchumi kama kilimo, viwanda na ufugaji.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya upimaji wa Miji yetu na upangaji wake hauendi sambamba na wimbi la mahitaji ya viwanja. Naishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuzisaidia Halmashauri kupanga Miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kumteua Mheshimiwa Anna Tibaijuka ambaye alikuwa Mkurugenzi wa *UN- Habitat* kuwa Waziri wa Ardhi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atumie uzoefu wake wa Kimataifa na kutafuta misaada ya fedha ili tuwe na Mfuko Maalum utakaotumika katika kuweka Miji yetu vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anayo kazi kubwa katika kurekebisha mwenendo wa Watendaji wengi wa Ardhi. Naomba Serikali ihakikishe inawachukulia hatua Watumishi wa Ardhi ambao si waaminifu na wanaochelewesha upatikanaji wa hati na vibali vya ujenzi. Wananchi wanasumbuliwa sana na Serikali ikitaka kujua kero wanazosababisha Maafisa wa Wizara, wapite Mikoani na Wilayani na kupata maoni ya wananchi.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi inaendelea kufanya vizuri katika Idara zake tofauti na hususani upimaji wa viwanja Mijini na uandaaji wa *Letters of Offer* na Hati Miliki za viwanja. Naipongeza Serikali kwa hilo na naomba iendelee kwa kasi kubwa zaidi ili kuondoa kero wananchi wanazopata katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kujenga Masijala za Ardhi katika Vijiji ili kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja vilivyoko Vijijini. Inawezekana kabisa Halmashauri ya Wilaya wakaelekeza Vijiji viibue ujenzi huu kama *priority* katika bajeti watakazopeleka Wilayani. Viwanja vikipimwa ni rahisi wananchi wakatumia Hati Miliki kuomba mikopo kutoka Benki na hatimaye kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naishauri Serikali ipeleke Maafisa Ardhi Wateule Wilayani ili waweze kusaidia kuandaa Hati Miliki katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, naipongeza Serikali kwa azma yake ya kujenga nyumba nyingi kupitia Shirika la Nyumba. Naishauri Serikali nyumba hizi zijengwe kwa gharama za *categories* tofauti katika eneo moja. Mfano Mijini ziwepo za bei nafuu kwa ajili ya mfanyakazi wa mshahara wa kati na za gharama zaidi kwa wale wenye uwezo kifedha. Serikali ikiendelea kujenga kwa mtindo inavyojenga, Miji yote itachukuliwa na wenye fedha nyingi. Inawezekana Mjini Dar es Salaam eneo la *Upanga Seaview* yote yakawa ni makazi ya Watanzania wenye asili ya Asia. Watanzania wazawa watashindwa kukodi au kununua nyumba hizo. Nashauri Serikali ipitie upya mkakati huo. Mheshimiwa Waziri Tibaijuka alikuwa Mkurugenzi wa *UN-Habitat*, nina imani kubwa hili analiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kwa vile nyumba hizo wapangaji wanalipa pango, ni haki nyumba hizo mkodishaji *(NHC)* wa-*renovate* kila baada ya kipindi fulani. Nyumba nyingi zinaonekana chakavu kwa sababu tu ya kutokufanyiwa *maintenance*. Kama jukumu la ku-*renovate* ni la mpangaji, basi ni budi mpangaji aelezwe tangu siku ya mwanzo ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Halmashauri nyingi za Wilaya hakuna kifaa cha *Total Station*, kinachosaidia upimaji ardhi kwa sababu hiyo Halmashauri za Wilaya haziwezi kupima viwanja vya Watanzania hata wale walio tayari kulipia huduma hiyo. Naishauri Serikali iwazielekeze Halmashauri za Wilaya zote nchini ziweke katika bajeti zao fedha za kutosha kununua kifaa hicho muhimu ili kuwapunguzia wananchi kero ya upimaji wa viwanja vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, naipongeza Serikali kupitia Mkurugenzi Mkuu wa *NHC,* kwa kuanzisha upya namna ya kushirikiana nyumba zinazojengwa kwa ubia wa Shirika na wafanyabiashara na hasa wenye asili ya Asia. Zamani nyumba ya ghorofa 10, ghorofa ya 1-5 ziligawiwa Watanzania Waasia na ghorofa ya juu wanapewa Watanzania wazawa. Mkurugenzi huyu amekuja na *style* ya *one by one* (flati ya kwanza Mhindi, flati ya pili Mwafrika, flati ya tatu Mhindi, flati ya nne Mwafrika). Mkakati wake huu ni mzuri na unaondoa dhana ya ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Serikali ilihamisha wananchi eneo la Luguruni Dar es Salaam na kuuza viwanja kwa bei ya ghali (Milioni 20 kwa kiwanja kimoja) kwa maelekezo kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha *Satellite Town*. Ziko tetesi pia za *Satellite Town* Bunju. Sasa hivi ni zaidi ya miaka miwili hakuna kinachoendelea. Naomba Serikali iwaambie Watanzania ni nini kinaendelea katika eneo la Luguruni na kama kweli kuna mpango wa *Satellite Town* Bunju.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, baada ya ujio wa Soko la Afrika Mashariki, ile dhana/sheria ya mgeni asipewe au kumilikishwa ardhi inatoweka. Mkoani Kilimanjaro na Arusha (Monduli) wageni wengi wanachukua ardhi kwa dhana ya kuwa wameoa Watanzania. Nina hofu inawezekana ndoa nyingine ni za *convenience*. Naishauri Serikali ipeleke agizo kwa Maafisa Ardhi

Wilayani na iwafikie Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wa Kata kukataza ardhi isiuzwe kabisa kwa wageni. Ni vema pia watakapokuwa wananunua, ndoa za aina hiyo zichunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo sahihi mpaka wetu Tanzania na Malawi kupitia Ziwa Nyasa uko katika eneo gani? Pamoja na majadiliano mnayofanya baina ya Serikali mbili na Watanzania walio katika eneo hilo linalopakana na Ziwa Nyasa wana changamoto gani za kibiashara na jirani zao wa Malawi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu kuna manung'uniko wa kuondolewa kwa baadhi ya mawe *"beacons"* katika mpaka wa Tanzania (Tarime) na Kenya (Migori) katika vijiji vya Pangakoo, Ronche na Ikoma na hadi leo hazijarudishwa na waliohusika hawajapatikana na ni kwa nini Serikali ina kigugumizi cha kurudisha *beacons* hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mawe *(beacon)* katika mpaka wa Tanzania (Tunduma) na Zambia pia baadhi zimeondolewa. Ni mara kadhaa Serikali imekuwa iko katika mchakato wa kushirikisha Wizara za Ulinzi, Mambo ya Nje ya nchi husika kuzirudisha *beacons* hizo. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili Tukufu ni lini *beacons* hizo zitarudishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji imekuwa ikiendelea na kupelekea kutofahamiana kwa makundi hayo mawili na wakati mwingine kuhatarisha amani katika maeneo hayo. Hii inatokana na maeneo hayo kutupimwa na mipaka yake kujulikana kati ya wafugaji na wakulima. Hivyo, naishauri Serikali kuandaa mazingira ya kuyapima maeneo ili wananchi watambue mipaka ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la bomoabomoa linalotekelezwa hapa Manispaa ya Dodoma linadhoofisha maendeleo ya wananchi kiuchumi. Miaka michache iliyopita bomoabomoa iliyofanywa Kijiji cha Mjimpya, Chang'ombe kilichokuwa na nyumba zaidi ya mia moja na hamsini (150), iliibuwa kilio kwani wananchi waliokuwepo zamani hawakupewa fidia zao na wanatetereka na maisha na hata maeneo ambayo Serikali ilidhamiria kutoa walengwa walilazimika kutoa fedha za upimaji lakini nyumba zao walizobomolewa hawakulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ludewa, Kata ya Mundindi na Nkoming'ombe, kuna madini ya chuma na wananchi mara wanaambiwa wajiandae kuhama, mara wanaambiwa wasihame! Kumekuwa na kauli tofautitofauti kutoka kwa viongozi. Je, wananchi wa Iwela, Mundindi na Nkoming'ombe waendelee kuishi na kuweka uwekezaji kwenye ardhi yenye madini chini au wahame?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yametengewa kiasi gani cha fedha?

(a) Je, Mabaraza haya huwa yanapata elimu ya kuendesha Mabaraza?

(b) Kwa kuwa Mabaraza haya huwa hayatengewi fedha, hamuoni kama ni chanzo cha rushwa?

(c) Malipo wanayolipwa wananchi ya faini na fidia katika Mabaraza haya huwa yanakwenda *account* ipi?

(d) Je, yanakatiwa risiti zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lote la Wilaya ya Ludewa lina madini chini ya ardhi kama Mchuchuma, Makaa ya Mawe, Chuma na *Gold* na inasemekana leseni za utafiti *PL* zimetolewa

kwa Wilaya zote, je, hii ni halali? Wilaya haina Afisa Madini wa Wilaya, suala la ardhi linaenda sambamba na malighafi zilizopo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ni namna Serikali inavyofanikisha uzalishaji wa viwanja kupitia Halmashauri, Wizara ya Ardhi katika maeneo ya Mijini. Dhana ya utwaaji wa ardhi kwa ajili ya maendeleo ya Miji haijaeleweka na wananchi wao wanadhani Serikali inawanyang'anya na wakati mwingine fidia imekuwa changamoto kulipwa. Wananchi hawajajua kuwa ardhi ikiwa *planned* na kupimwa thamani inapanda. Sheria Na.47 ya 1967 na 6 na 7 za Mipango Miji zimekuwa ngumu kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza maboresho katika Sheria za Ardhi sasa wanawake wanaweza kurithi, kumiliki na ku-*transfer* ardhi sawasawa na wanaume. Hivyo wanawake wa Ludewa/Makete/Njombe wana haki sawa na wanaume tofauti na zamani. Sasa wanawake tutajenga/kununua na kurithi ardhi sawasawa na wanaume hivyo tutaingia ubia na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi holela upunguzwe, maelekezo yatolewe, ushirikishwaji wa Serikali za Mitaa ni muhimu katika masuala ya viwanja Mijini na Vijijini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Mabaraza ya Ardhi. Kuna tatizo kubwa la ardhi leo katika nchi yetu. Kuna migogoro mingi ya mipaka na umiliki wa ardhi yenyewe. Ili kukabiliana na migogoro hiyo, ilikuwa ni kuanzishwa kwa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi mbalimbali, Wilaya, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, inasikitisha kuona kwamba tangu Mabaraza hayo yaanzishwe zaidi ya miaka 15 (kumi na tano), bado Mabaraza hayo hayajaundwa katika maeneo mengi sana. Huu ni udhaifu wa Wizara. Nashauri Wizara sasa ilisimamie suala hilo kwa karibu ili Mabaraza ya Ardhi yaweze kuanzishwa. Kwa kufanya hivyo, tutapunguza sana migogoro ya ardhi na hivyo kuwafanya wananchi wetu waishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni elimu ndogo kwa Wajumbe wa Mabaraza pale ambapo yameanzishwa. Nashauri Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ihakikishe kwamba Wajumbe wa Mabaraza hayo wanapatiwa semina/mafunzo ili kuboresha utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kubinafsisha ardhi kubwa kwa wageni/watu wachache. Ardhi ndio kila kitu, tunaishi juu yake, tunalima juu yake, shughuli zote za binadamu hufanywa juu yake. Ongezeko la idadi ya watu katika nchi yetu ni kubwa sana. Wakati wa uhuru idadi ya Watanzania ilikuwa karibu milioni tisa leo tunakisiwa kuwa milioni zaidi ya 40. Aidha, inakisiwa kuwa ifikapo mwaka 2050, Watanzania watafikia milioni zaidi ya 60!

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu ni kwamba Serikali inauza/kubinafsisha ardhi kwa kasi kubwa sana. Najiuliza hivi watu hao wanaoongezeka kwa kasi kubwa tutakuja kuwaweka wapi? Hivi hatuoni kwamba tunatengeneza 'Zimbabwe' nyingine? Kwa leo kazi ambayo haina masharti magumu ambayo Watanzania wengi wanaweza kuifanya ni kilimo, kilimo hufanywa juu ya ardhi, hivi Serikali ikiuza/kubinafsisha kwa miaka karibu 99 ardhi tena yenye rutuba karibu yote, Watanzania hawa wa kesho na keshokutwa watakuja waishi wapi? Walime wapi? Hili ni bomu tusipolishika kwa masharti yake litatupasukia mikononi mwetu!

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Mji mpya wa Kigamboni. Nachelea kusema kwamba Mji Mpya wa Kigamboni *(Kigamboni New City),* unaweza kugeuzwa kuwa hadithi ya kwenye makaratasi. Nasema hivyo kwa sababu leo tunaambiwa kwamba Wizara hii inaendelea kuzungumza na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia stahiki kwa wananchi, (Ukurasa wa 26, kitabu cha hotuba ya Wizara). Hii ina maana kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012, hakuna kazi yoyote ya maana itakayofanyika. Nashauri pia fidia kwa wananchi wote watakaoathirika katika zoezi hilo walipwe kwa mujibu wa Sheria. Aidha, wakati wa

kufanya zoezi la tathmini, uadilifu usisitizwe sana, maana wapo watumishi ambao wanategemea wanufaike hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ujenzi Kituo cha Masijala ya Ardhi kwa ajili ya Hati Miliki za Kimila Wilayani Mbozi. Wilaya ya Mbozi ni miongoni mwa Wilaya za mwanzo kufaidika na zoezi la upimaji na uandikishwaji wa Hati Miliki za Kimila. Kutokana na ukweli huu, iliamriwa kijengwe Kituo cha Masijala ya Ardhi katika Kijiji/Kata cha/ya Halungu na kuwekwa kompyuta. Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Masijala hiyo mwaka 2009 na aliahidiwa kwamba Kituo hicho kingeanza kufanya kazi mara moja. Hadi leo karibu miaka miwili tangu Rais alipoahidiwa, hakuna kazi inayoendelea. Hakuna cha kompyuta wala cha wataalamu. Nataka kujua ni lini hasa Masijala hiyo ya Ardhi itaanza kufanya kazi pamoja na kuweka kompyuta na wataalamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ujenzi wa nyumba 15000 na *NHC*. Tumeelezwa kwamba Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* linatarajia kujenga nyumba 15000 (elfu kumi na tano) katika kipindi cha miaka mitano (2010 – 2015). Ni jambo jema na kupongezwa sana. Hata hivyo, nataka kujua nyumba hizo zitajengwa katika Mikoa ipi na Wilaya zipi? Ushauri wangu, ujenzi wa nyumba hizo uzingatie Mikoa yote lakini pia idadi ya wakazi wa Mikoa/Wilaya izingatiwe. Nakusudia kusema Mikoa yenye watu wengi na Wilaya zenye watu wengi zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono na nawasilisha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wachangiaji wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na asasi zote zilizo chini ya Wizara. Kazi zinazofanywa na Wizara zinatoa matumaini, naomba Wizara na asasi zilizo chini ya Wizara kutekeleza yote yaliyoainishwa katika kitabu cha hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti, inasimamia ardhi na makazi ambayo yanamgusa mwananchi moja kwa moja, mwananchi anahitaji ardhi kwa wageni mbalimbali na mwananchi huyo anahitaji makazi ya kuishi katika maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi naipongeza Wizara kuanzisha Idara ya Nyumba ambayo itaweka stahiki ya uendelezaji wa nyumba hapa nchini, naiomba Serikali iweke mfumo mzuri wa kiutawala katika mamlaka za Serikali za Mitaa na Miji ili zile changamoto zinazojitokeza ziweze kukabiliwa. Wananchi wanataka mikopo, wanataka ardhi, wanataka nyumba na vifaa vya ujenzi na kadhalika ili kutekeleza hayo pia yafanyike vizuri na kuomba Mheshimiwa Waziri uwasiliane na Waziri wa TAMISEMI au Waziri Mkuu kila Wilaya kuanzishwe Idara au Kitengo cha Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Sheria ya 2008 ya *Mortgage Financing, Act Na.* 17 iliyoanza kutumika Mei, 2009 kupitia mabenki wananchi wamenufaika kiasi gani na sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua nyumba iliyoko Upanga *Etienes Hotel* imefikia wapi kwani ilikuwa na mgogoro wa siku nyingi tangu nikiwa *board member* wa *NHC*, naisema hili kwani NHC imesema imetatua migogoro mingi sana. Je, *Etienes* ni mojawapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ardhi, Jiji la Mwanza kuna matatizo ya rushwa na suala hili nilishamdokeza Naibu Waziri wa Ardhi, wananchi wakazi wa Jiji la Mwanza wanadaiwa rushwa, naiomba Serikali iliangalie linachafua *image* ya Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie *NHC*, kwanza naomba nimpongeze *CEO* wa *NHC* wa sasa kwa ubunifu alionao wa kui-*transform NHC*, kwa sasa inaheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi, nasema Shirika linatakiwa lijiendeshe kwa uwezo wake na lifanye shsughuli zake kwa misingi ya kibiashara kama Sheria Na. 2 ya 1999 na Sheria ya *NHC* na ya 1999. Kwa kuzingatia hayo nimewasikia baadhi ya wapangaji kudai wauziwe nyumba walizopanga kwa sababu eti mwaka jana Waziri alisema *NHC* itauza nyumba zake, labda niwakumbushe, katika hotuba yake 2010/2011 Waziri alitumia neno Azma ya *NHC* ni kuuza baadhi

ya nyumba zake ambazo gharama ya kuziendesha ni kubwa kuliko mapato na zoezi hili linahitaji maandalizi makubwa yakiwemo ya kuwatambua wapangaji, kujua uwezo wa wapangaji kama wana uwezo wa kumilikishwa na kadhalika. Naungana na *NHC* kwa utaratibu huo, vinginevyo *NHC* ikienda kichwa kichwa nyumba nzuri, hizo hasa za Upanga zitanunuliwa na matajiri wakubwa na sifa walete hao. Lakini nitashangaa sana endapo nyumba hasa za Upanga ambazo lazima gharama za uendeshaji zikiuzwa nitapinga kwa nguvu zangu zote na hili tulishalikataa tangu nikiwa Mjumbe wa Bodi. Nasisitiza zoezi la kuuza nyumba za *NHC* lifanywe kwa uangalifu mkubwa sana vinginevyo kashfa ya ufisadi itakuwa imelikumba shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalishukuru shirika kwa kutathmini na kujua inamiliki majengo mangapi ya makazi na ya biashara. Naomba mjiridhishe tena kwa kurudia kuhesabu nyumba hizo hasa zile za ubia na *NHC* zina mushikeli, narudia kusema upo ufisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHC* wamesema wanamiliki majengo 2,310, si vibaya Bunge linajulishwa thamani ya majengo hayo ni shilingi ngapi? Lakini pia *NHC* mwaka jana ilikusanya Sh.36 bilioni (2009/2010).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010/2011 ilikusanya Sh.41.9 bilioni na 2011/2012 imepanga kukusanya Shilingi 48.1 bilioni, tunalipongeza shirika lakini ningependa kujua makusanyo hayo ni yapi ya pango na yapi ya malimbikizo. Hii itatusaidia kujua kama *NHC* imetilia mkazo katika kukusanya malimbikizo ambayo ni makubwa sana, kwani tunaweza kuamini kuwa Shirika linakusanya pesa nyingi kumbe ni zile za pango wakasahau kuwa malimbikizo, ningependa kujua ni shilingi ngapi ni malimbikizo ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati nchi yetu ikatenga maeneo kwa matumizi mbalimbali, Tanzania haina tatizo la ardhi, iseme eneo fulani ni kwa ajili ya makazi, viwanda, kilimo, ufugaji na eneo lingine vitengwe kama akiba, ardhi ni mali, tuitumie vizuri, tuihifadhi ili baadaye ivinufaishe vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Mwanza hakuna Afisa Mteule anayetakiwa kusaini *Deed Plans* ambayo ni nyaraka muhimu sana kwa ajili ya kutengeneza hati miliki za viwanja vilivyopimwa yaani *Certificate of Title*. Afisa aliyekuwepo ni mgonjwa, amepooza kwa zaidi ya miezi minne sasa kwa sababu *Deed Plans* zinawekwa saini na mteule mmoja tu ambaye kwa sasa anaumwa, Wizara kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Uchoraji na Ramani inasema nini kuhusu kumteua mtu mwingine ili aweze kufanya kazi za kusaini *Deed Plans* hasa ikizingatiwa Mkoa wa Mwanza ni Mkoa unaokuwa kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu uliyoyaanisha katika hotuba yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kushukuru japo kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii. Naomba nijikite hasa katika Mkoa wa Shinyanga hususan Manispaa ya Shinyanga yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Shinyanga kuna tatizo kubwa la migogoro ya ardhi iliyopo katika Kata za Ngokolo na Kitangili. Kuna wananchi ambao wamerithi maeneo tokea vijiji vya ujamaa lakini sasa wanatolewa na kuambiwa maeneo hayo si yao. Wananchi hawa wamekuwa wakifuatilia haki yao bila mafanikio. Watendaji wa Idara ya Ardhi walifikia hata kuwalaghai kuwa watoe kati ya Sh.40,000/= hadi 80,000/= ili wapimiwe viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake mpaka sasa hawajapimwa viwanja na badala yake wanakuja watu wengine na *offer* wakidai viwanja hivyo vya kwao huku wakionyesha hati zao. Tatizo hili ni kubwa kwani Wizara isipotoa ufafanuzi damu itamwagika na kwa nini tufike hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hao wenye *offer* na wanaodai viwanja hivyo ni vyao, wamekuwa wakipeleka mchanga, mawe na kokoto chini ya ulinzi wa polisi, maana ni hatari wanaweza kupigwa na wenye maeneo yao. Hii ni sababu tosha kuwa mgogoro huu ukiendelea unaweza kusababisha umwagaji damu. Naomba sana Waziri afuatilie hili suala ili kujua tatizo ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona mwananchi wa hali ya chini anapokonywa haki yake pamoja na kutoa pesa kwa ajili ya kupimiwa viwanja vyao lakini hakuna kiwanja kilichopimwa na pesa yao imeliwa na Manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina Sheria za Ardhi mojawapo ni kuwapa maeneo wazawa waliokutwa kwenye maeneo baada ya kupimwa. Hili halikufanyika katika Manispaa, wananchi hao wamekuwa kama wakimbizi katika nchi yao sasa waende wapi? Maana hapo ndio kwao na ndipo walipozaliwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia nikawa mzima wa afya na nikawepo hapa katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa katika mchango wangu wa maandishi naomba nilieleze Bunge langu Tukufu, kwamba lazima Serikali ielewe na izingatie kwamba ardhi ndio rasilimali yetu inayochukua nafasi ya kwanza kubeba umuhimu wa kwanza kwa Watanzania wote. Katika nyanja zote za maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni ushahidi tosha kwamba Mwenyezi Mungu aliumba watu na ardhi ili tupate neema kubwa sisi watu kupitia ardhi hiyo. Tunalima, tunajenga, tunacheza, tunapata maji, tunafuga, tunafanya mambo yote kuhusu maisha yetu kupitia ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umilikaji. Naomba nishauri Serikali na vyombo vyote vinavyosimamia utaratibu wa kugawa wa ardhi vitumie vigezo vifuatavyo katika udhibiti wa ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wawekezaji wa kigeni wasiuziwe ardhi yetu kuweko na mikataba kimatumizi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, muda wa kuwekeza usiwe wa miaka mingi kupita kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wazawa wa nchi hii wasitaifishiwe maeneo yao ya ardhi, bali Serikali ilipe fidia kwa wazawa ili wafaidi matunda ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba (*NHC*) Dodoma. Naomba niishauri Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) liongeze juhudi ya ujenzi wa nyumba za makazi, ili iongeze tija hapa Dodoma kwani Wabunge wengi, tuna tatizo kubwa la nyumba katika muda wote wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kesi za ardhi. Inaonekana maswali mengi katika Bunge lako yanahusu matatizo ya ardhi, kwa hiyo, kuna haja ya kuweka utaratibu mzuri, yaani, Wizara imilikishe ardhi kwa kila aliye na ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hati miliki itawasaidia wamiliki kujipatia mikopo ya benki zetu, jambo ambalo mikopo hiyo itawasukuma wananchi kuendeleza maisha yao kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali kupitia hati miliki ya ardhi inasaidia kuondoa matatizo kuhusu ugavi wa mirathi kuhusu mipaka ya mashamba ya Watanzania (ndani ya jamii zetu).

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii ya kuchangia kwa maandishi, niombe yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa makazi ya mji wowote kuzaliwa na msingi wa viota vya miji, vijiji vinavyotoa huduma za mitindo mipana ya miji mikubwa. Kwa hiyo, sasa naomba Wizara na vile vile namwomba Waziri aje Maswa kutambua utayari wa wananchi kupokea taaluma ya mipango endelevu ya kuzaa miji ya mipango bora. Maswa tunahitaji ushauri wa kutatua kasoro za kutokuwepo mipango miji ya muda mrefu ambayo kuzaa kubomolewa nyumba, kutokuwa na maeneo ya miundombinu ya kukidhi kukua kwa mji na idadi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ipo tayari kuja na wataalam ambao sasa Maswa itakuwa na vijiji vya mfano wa kukua kuwa majiji makubwa polepole ndani ya miaka 50 ijayo. Naomba kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maswa tuna maji ya kutosha. Je, Shirika la Nyumba lipo tayari kuingia ubia na Halmashauri ya Maswa, waje wajenge nyumba za kupangishwa watumishi na kuzindua mantiki ya makazi bora na mantiki ya nyumba bora. Naomba kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti maeneo ya miji kuwe na matabaka ya Uzunguni, Uhindini na Uswahilini? Adha ya matabaka huondoa utulivu wa kijamii wa muda mrefu. Vita ya ukombozi bara la Afrika, uhalifu wa kuvamiwa maeneo ya tabaka la ufahari na wavamizi ni *agenda* ya hoja ya kuondoa tabaka la Umwinyi na Utwana. Je, kodi zinajenga au zinadhibiti maibuko ya matabaka. Naomba kauli ya Serikali yenye maono pevu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimwa Waziri Profesa Anna Tibaijuka na Naibu wake Mheshimiwa Ole Medeye kwa kazi yao nzuri na yenye kuleta matumaini makubwa kwa Watanzania kulingana na shida kubwa ya ardhi inayokabili nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mambo yafuatayo:-

Kwanza, wawekezaji wanaopewa maeneo katika nchi yetu wapewe maeneo yasiyoleta migogoro. Kwa maana hiyo, wasipewe maeneo ya wafugaji au ardhi nzuri na kwa kilimo, ikibidi maeneo mapya yatafutwe.

Pili, matumizi ya ardhi ya Tanzania yaendane na karne ya leo. Ardhi yetu ikidhi matarajio ya kuondoa umaskini wa nchi yetu, Ardhi yetu iendane na sera ya kukuza uchumi wetu, iendane na ushindani ulioko kwenye soko la Kimataifa *Global Market.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakoelekea kwenye soko la pamoja, tunategemea ardhi yetu itufikishe huko kwa sababu Watanzania (80%) wengi ni wakulima. Hakuna kilimo kwanza bila ardhi, *production* Serikali ipange vizuri sana matumizi ya ardhi hasa maeneo yanayofaa kwa kilimo.

Tatu, ifike mahali kilio cha migogoro ya ardhi Wilaya ya Mbulu, Kiteto, Babati, Simanjiro na Hanang kiishe. Migogoro hii ni mingi mno. Debe likilia sana mwisho hupasuka. Tunaomba Serikali ielekeze macho Mkoa wa Manyara kuondoa matatizo ya ardhi.

Nne, wafugaji waelimishwe kumiliki ardhi, la sivyo, baada ya Serikali kuandikisha na kumilikisha ardhi, hawatakuwa na maeneo ya kumiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Mchango wangu ni kama ifuatavyo, ambayo wananchi wanahitaji ni :-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu migogoro. Mkazo mkubwa lazima uwekwe kwenye kutatua migogoro inayojitokeza ya Mipaka ya ardhi, vijiji na vijiji; Hati zinazotolewa mbilimbili ndani ya eneo moja na Taasisi na vijiji, mfano *MUHAS* na Mlonganzila na Kwembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu *NHC*. Wananchi wanataka nyumba za watu wa kima cha chini. Kuendelea kujenga nyumba za bei kubwa ni kuendelea kuiangusha Serikali kwani wananchi wanatafsiri kwamba Serikali ni ya matajiri. *We have to mix the type of the houses.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhusu Mabaraza Wilayani. Tunatoa wito kwa Serikali kuwezesha Wizara kuanzisha Mabaraza kila Wilaya kwani kwa kutoanzisha kumesababisha migogoro kuwa mikubwa na hivyo kuchafua utendaji wa Serikali au Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni kuhusu upimaji ramani. Serikali iongeze upimaji wa ramani ufanywe kwa maeneo makubwa. Ni vizuri kuwa na mchanganuo wa matumizi ya ardhi. Je, Serikali mnashindwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wito rasmi kwa Mheshimiwa Waziri, nakuomba ufanye yafuatayo yatakayokupa sifa:-

(a) Adhibu Maofisa wanaotoa hati mbili au feki. Adhabu ziwe hadharani.

(b) Anzisha siku ya kutatua migogoro kwa kukutanisha Wizara au Idara zinazohusika. Siku hiyo uiite Tatua Migogoro *Day*.

(c) Pima ardhi za maeneo mbalimbali.

(d) Jenga nyumba za bei rahisi (*NHC*).

(e) Toa hati za majengo/nyumba kwa siku chache. Tatizo nini Waziri?

(f) Simamia Afisa Ardhi wa Mikoa na Wilaya kwa ukaribu. Toa tamko na tishio hata kwenye radio. Mmelala!

(g) Jenga utamaduni wa kuamka baada ya vikao vya wananchi. Hili ni tatizo

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakutakia mafanikio mema kwenye Wizara hii ambayo inabidi kuvunja mazoea ya utendaji uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ila changamoto lazima zifanyiwe kazi.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongezeni sana kwa hotuba na kazi nzuri. Nina hoja mbili tu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi walipewa ardhi na kibali cha Kijiji toka mwaka 1972 na wengine toka mwaka 1974, miaka ya hivi karibuni vijiji hivyo vinaambiwa vivunjwe na kwa kuwa vipo kwenye maeneo ya hifadhi, hivi huu si uonevu kweli? Watu wanajenga nyumba zao hapo, wamezaa watoto na wao wakajenga, wamelima, wamejenga shule, zahanati, wanakuja kupokea taarifa zinazowatia mashaka wanaishi kwa wasiwasi ndani ya nchi yao! Haki ya kumiliki ardhi iko wapi hapa Mheshimiwa Waziri? Kwa nini tunawanyanyasa Watanzania wenzetu hawa? Kwenye Jimbo langu maeneo yanayoguswa ni Kata za Nkiniziwa, Puge, Magengati, Milambo, Itobo, Muhugi na Mizibaziba. Naomba maelezo ya kina, la sivyo nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, linahusiana na Afisa Ardhi wa Wilaya ya Misungwi (ambaye ni Afisa Mipango Miji) alikaguwa eneo lililonunuliwa, kwa wanakijiji wa Nyang'homango, Misungwi na akaahidi kulipima kwamba hakuna shida akadai milioni sita. Kampuni ya *MSK*

*Refinery Limited* ikakubali, akachelewa kwa zaidi ya miezi sita, kampuni ikampa *surveyor* mwingine akapime kwa gharama nafuu. Bwana huyu alipotakiwa kusajili alikataa na mpaka leo amekwamisha uwekezaji. Naomba Mheshimiwa Waziri ulifuatilie hili ili *MSK Refinery Limited* apewe haki yake. Naomba *ku-declare interest* kwamba nina *share* 17% kwenye Kampuni hii. Tumekwamishwa bila sababu kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna wananchi wa Nzega, wafanyakazi wa Halmashauri wanaishi kwenye nyumba za *NHC* pale Nzega, walishawasilisha maombi yao kuwa wauziwe kama wengine walivyouziwa lakini hawajajibiwa. Wamewahi kuwasiliana na Mama Tibaijuka lakini bado hakuna hatua zilizochukuliwa mpaka leo hii. Wao wanasikitika wanazungushwa kwa kuwa ni *cadre* za chini, kwa kuwa mabosi wao wamekwishauziwa nyumba kwenye eneo hilo. Kama utawakumbuka ni Bwana Mayombo, Abdu Masimbila na wenzao. Naomba ufafanue kwamba ni kwa nini wafanyakazi hawa wanabaguliwa kwa kuwa wana vyeo vya chini kazini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na bajeti kuwa nzuri lakini bado kuna masuala ambayo napenda kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengi nchini yanatokana na kero za ardhi. Pia kuna maeneo mengi nchini Serikali inazitoa kwa wawekezaji hali ambayo baada ya miaka 30 – 50 ijayo inaweza kusababisha vurugu nchini kwa sababu kila mwaka watu wanaongezeka na kila mwaka watu wanaimarika kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya miaka kadhaa mbele ya safari pale ambapo wananchi watakapokuwa na uwezo wa kumiliki na kuendeleza ardhi watakuta hakuna maeneo lakini pia baada ya miaka kadhaa Watanzania watakuwa wameongezeka. Je, ongezeko la Watanzania watalimia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe maeneo kwa wawekezaji kwa kuona miaka ijayo na ongezeko la Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Uyui na Jimbo langu la Tabora Kaskazini kuna Kata mbili ambazo zinapakana na eneo la JWTZ na mipaka ipo hata *Bicon* zipo, lakini cha kusikitisha ni kwamba JWTZ wamepora sehemu kubwa ya vijiji vilivyopo Kata ya Ilolanguru na Kata ya Ibiri. Suala hili tulilijadili kwenye *RCC* mwezi wa Aprili mwaka huu. Je, Wizara inatoa kauli gani? Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu pia linapakana na Wilaya ya Urambo, kuna Kijiji kinaitwa Katunda, Kata ya Mabama ambapo kuna hifadhi hapa mipaka haieleweki jambo ambalo linasababisha kila leo wananchi wanabugudhiwa kwa madai kwamba wanaingia katika eneo la hifadhi na kuombwa rushwa, naomba msaada Serikali itutatulie mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Jimbo langu kuna Kata mbili ambazo ni Kata ya Ikongolo na Bukumbi. Katika Kata hizo kuna vijiji sita jumla ambazo zimesajiliwa kisheria, sasa wananchi hao wameelezwa kuwa maeneo hayo ni ya hifadhi na misaada ya maendeleo imesitishwa je, hii ni haki? Naomba usuluhisho wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kigezo gani kinachotumika katika kuweka mipaka ya Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka nchi yetu ipate uhuru, mipaka ya Mkoa wa Dar es Salaam imekuwa ikisogea na kumega eneo la Mkoa wa Pwani. Je, tatizo ni nini linalopelekea Serikali kusogeza hiyo mipaka? Naomba nipatiwe majibu ya vigezo na hata ikibidi ifahamike rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuna migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji. Makundi haya yanazo zana hata kupigana na kuuana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mitafaruku hii wafugaji wanaonekana kama ndio wachokozi kwa maana ya kwamba mifugo yao inavamia mashamba. Mifugo, kama ilivyo kwa mashamba, ni muhimu kwa uchumi na ajira ya wananchi. Swali ni kwamba tuondokane na mifugo ili watu waishi kwa amani? Jibu ni hapana, kinachotakiwa ni kwamba kila kijiji kitenge maeneo kwa ajili ya ufugaji. Ni muhimu sekta hizi mbili ya mifugo na mashamba, waishi kwa maelewano. Tukitaka hilo liwe ni lazima Serikali iainishe maeneo gani ya kilimo na yapi ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hitaji la kumiliki nyumba bora ni la msingi tunapozungumzia maisha bora kwa kila Mtanzania. Idara ya Mipango Miji inafanya kazi nzuri ili kuondokana na *squatters*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika viwanja vilivyopimwa nyumba zitajengwa, lakini nyumba hizo si bora hadi hapo zitakapopatiwa huduma za umeme, maji safi na uendeshaji wa majitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ninaouona ni kwamba mtu akipata kiwanja, anajenga, anavuta umeme na maji. Wakati mwingine umbali wa kuvuta huduma hizi ni mkubwa kwa maana hiyo gharama ni kubwa. Watakaojenga baadaye katika viwanja vya jirani wanaunganishiwa huduma na vishoka na madhara yanayoambatana na kazi ya vishoka tunayajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pendekezo, baada ya kazi ya upimaji viwanja kukamilika, miundombinu ya umeme na maji isambazwe na Serikali kabla ya viwanja kugawiwa. Gharama za kupeleka huduma hizi zichangiwe na wote watakaopewa viwanja zijumuishwe katika *letter of offer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru sana Waziri mwenye dhamana kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nimshukuru pia Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa kiasi fulani utoaji wa hati miliki kidogo unaridhisha, lakini naomba jitihada zaidi zichukuliwe ili watu wote waweze kupata hati bila usumbufu, kwani hati ni haki ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea pia Mfuko wa *Housing Loan* ambao unapatikana pale Wizara ya Ardhi. Mfuko huu ni mzuri sana na unasaidia sana wafanyakazi wa Serikalini. Lakini sasa masikitiko yangu Mfuko huu unawafikia wafanyakazi wa mjini tu kitu ambacho siyo haki kwani wafanyakazi hawapo mijini tu wapo vijijini pia. Nashauri Mfuko huu uwafikie pia wafanyakazi wote wa Tanzania nzima na siyo mjini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia isiwe kwa wafanyakazi wa Serikali kuu iende mpaka Halmashauri ili watu wote wanufaike na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naunga mkono hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi kwa kuendelea kunipa uhai unaoniwezesha kuendelea kutimiza majukumu ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya tangu wateuliwe iliyopelekea mafanikio yanayoonyeshwa kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza zaidi katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu uuzwaji holela wa ardhi katika maeneo ya Mkoa wa Pwani. Katika Mkoa wa Pwani kuna tatizo kubwa la wawekezaji feki kununua ardhi na kuhodhi maeneo hayo bila ya kuendeleza kwa miaka mingi. Ununuzi huo wa ardhi haufuati utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji hao wanashirikiana na viongozi wa vijiji wasio waaminifu wanaofoji mihtasari ya mikutano ya wananchi wa vijiji hivyo kuridhia uuzwaji wa ardhi. Mara nyingi ardhi hiyo inauzwa kwa bei chee au rahisi isiyoendana kabisa na thamani ya bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iingilie kati uuzwaji huo holela wa ardhi katika Mkoa wa Pwani na kubatilisha baadhi ya hati kwa wawekezaji waliohodhi ardhi hasa katika Wilaya za Kibaha, Kisarawe kwa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Vijiji vilivyokaguliwa kubaini maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jedwali Na. 9, limeonesha orodha ya vijiji vilivyokaguliwa kwa ajili ya kutekeleza kilimo kwanza. Katika Mkoa wa Pwani maeneo hayo yamebainishwa katika Wilaya za Kisarawe na Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka sana na ukaguzi huu kama ulishirikisha wananchi wa maeneo ya vijiji vilivyotajwa kwani tumeshuhudia maeneo mengi ya Mkoa wa Pwani hasa katika Wilaya hizo yanachukuliwa na wawekezaji lakini hakuna uendelezaji wowote uliofanyika mpaka sasa. Hivyo, naiomba Wizara ishirikishe wananchi wa maeneo husika wakati wa kubaini maeneo yenye ardhi ya akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Mfuko wa Kupima Viwanja. Awali ya yote nashukuru Mfuko huu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Bagamoyo kwa Mfuko huu kuikopesha Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo milioni 400 kwa ajili ya kupima viwanja pamoja na Halmashauri au Mji wa Kibaha milioni 220. Viwanja vimepimwa katika maeneo hayo na vigawiwe kwa wananchi na vingi ya viwanja vilivyopimwa katika Wilaya ya Bagamoyo na Kibaha vimekwishalipiwa. Lakini nashangaa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Ukurasa wa 22 kwamba pesa hizo zilikuwa hazijarejeshwa Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa mbalimbali tunazosomewa kwenye Halmashauri zetu hasa ya Bagamoyo inaonesha asilimia 60% ya mkopo huo imerejesha Wizarani. Kwa nini asilimia kubwa ya uwanja vilivyotolewa imelipiwa lakini mkopo haujarejeshwa? Wizara ifuatilie isije kuwa pesa hizo za viwanja zimeishia kwenye Mifuko ya wajanja wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango huu wa kupima viwanja kuwa mzuri, lakini Wizara iangalie upya taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi. Kwa viwango vinavyolipwa haviendani kabisa na bei ya soko na viwanja hivyo vinauzwa kwa bei ya soko. Je, mapato hayo yanapelekwa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za viwanja hivyo vinavyopimwa haizingatii kabisa hali ya kipato cha chini cha Watanzania walio wengi ambao ndio wamiliki wa ardhi hizo wanaishia kupata fidia ya kiwanja kimoja na wanashindwa kabisa kumudu kununua viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni uonevu hasa kwa wananchi walio wengi hasa wa vijijini ambao rasilimali yao ya pekee waliorithishwa na mababu zao wanaoishia kuwa manamba na matajiri ndio wananyimwa ardhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa. Nichukue fursa hii kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa chini ya uongozi wa Mkurugenzi mpya kwa kazi nzuri na mipango iliyonayo juu ya kuboresha na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya mwaka 2010/2011 na 2011/2012 ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara zipatazo 400 kwa mwaka 2010/2011 na nyumba za makazi 2,721 na majengo saba ya biashara kwa mwaka 2011/2012. Hata hivyo, mipango yote hiyo haijagusa kabisa Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani kwa sasa tunashuhudia wimbi la wahamiaji toka Mkoa wa Dar es Salaam, hasa baada ya Mkoa wa Dar es Salaam kuwa hauna uwezo wa kutoa makazi ya kutosha. Hivi kwa nini shirika hili halioni kuna haja ya kujenga nyumba za makazi na biashara, Mkoa wa Pwani hasa katika Makao Makuu ya Wilayani Kibaha ambako watumishi wengi wanaendelea kuishi Dar es Salaam licha ya kuhamishwa Mkoa wa Pwani hasa Kibaha kutokana na uhaba wa nyumba za kuishi uliopo Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kumshauri Waziri, achukue hatua za haraka kukomesha rushwa katika Wizara ambayo imeshamiri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya dhuluma wanavyovifanya maafisa ardhi vya kumiliki viwanja vingi vilivyopimwa na kuacha wananchi wengi wakikosa fursa hiyo. Maafisa hao wa ardhi baadaye huuza viwanja hivyo kwa bei ya juu sana, huko ni kuwanyonya Watanzania na Mwenyezi Mungu ipo siku atawalipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yao ya wataalam kwa hotuba inayoonyesha kuwa wanachapa kazi kwa makini. Nampongeza pia Waziri Kivuli wa Wizara hii aliyewasilisha mawazo ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Naiomba Serikali iyapokee mawazo ya Kambi Rasmi ya Upinzaji na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusika na maeneo yafuatayo:-

(1) Ardhi kwa jumla.

(2) Migogoro ya ardhi Bukombe.

(3) Nyumba na maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia ardhi kwa jumla. Sekta ya ardhi imegubikwa na ufisadi kwa muda mrefu na ufisadi huu una sura mbalimbali, baadhi ya sura hizi ni pamoja na:-

(a) Maafisa Ardhi, kwa kutumia nafasi zao, kujimilikisha viwanja vingi sana katika maeneo mbalimbali.

(b) Maafisa Ardhi kufanya biashara ya ardhi kwa wenye haja na viwanja au ardhi.

(c) Uuzwaji wa maeneo ya wazi (*open spaces*) hasa katika Jiji la Dar es Salaam.

(d) Tatizo la viongozi wakuu wa kisiasa au Kiserikali kujilimbikizia ardhi. Tatizo hili limeenea nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwamba haya yote yamefanyika na yanaendelea kufanyika kutokana na uzembe katika mfumo wa usimamizi wa sheria na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo hayo, kuna tatizo la kuwamilikisha ardhi wawekezaji kwa kipindi kirefu (miaka 99) bila hadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nitoe mapendekezo au ushauri:-

(a) Nakubaliana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba ardhi iwe chini ya Mamlaka moja, itakayowezesha kupima ardhi yote nchini na kuwamilikisha kwanza wananchi kwa hati. Ardhi inayobaki ipangiwe matumizi mengine kuwekezaji na kadhalika).

(b) Wizara iwe na mpango mkakati wa kupima ardhi yote nchini kwa kipindi kifupi (mathalani inaweza kujipa miaka mitano kwa kuanzia).

(c) Maafisa Ardhi wote wenye tuhuma za ufisadi wafukuzwe kazi baada ya kuthibitishwa, kwa ushahidi mbalimbali, kuwa wamekiuka maadili ya kazi yao.

(d) Sheria za Ardhi zidurusiwe ili ziwalinde wamiliki wazawa hasa vijijini na kuweka kikomo cha umiliki kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichangie kuhusu migogoro ya ardhi, Bukombe. Migogoro ya ardhi, Bukombe ina sura mbili:-

(a) Ile inayosababishwa na Halmashauri.

(b) Ile inayotokana na ongezeko la mifugo na upungufu wa malisho na hivyo kuwafanya wafugaji kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro inayosababishwa na Halmashauri inahusiana na vitendo vya Halmashauri kuchukua maeneo ya wananchi katika eneo la uhamiaji, Katente, Butinzya na Businda. Eneo la uhamiaji ardhi ilichukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Halmashauri (kujenga nyumba na kadhalika), maeneo ya Katente, Butinzya na Busenda yalichukuliwa kwa ajili ya kupata maeneo ya kujenga shule. Migogoro hii imetokana na Halmashauri ama kuwapunja malipo wananchi au kucheleweshewa malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri aje Bukombe kushughulikia matatizo haya ya muda mirefu. Mgogoro mwingine wa ardhi ni ule ulio baina ya wafugaji na wakulima. Sababu ya msingi ni kwamba kuna upungufu wa maeneo ya malisho unaosababisha wafugaji kuchungia kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pendekezo au ushauri. Mpango wa upimaji wa maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo utekelezwe haraka ili wafugaji wapate maeneo yao Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu nichangie kuhusu nyumba na maendeleo ya makazi. Shirika la Nyumba la Taifa limelenga kuboresha makazi mijini tu. Lakini kwa mpango wa muda mrefu wa makazi bora nchini kote, tunahitaji mipango miwili ya nyumba na maendeleo ya makazi mpango wa Mjini na ule wa Vijijini. Ili mipango hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi, ingefaa itekelezwe na mashirika mawili tofauti kwa kuwa nyumba za mijini zitakuwa tofauti na zile za vijijini. Kadhalika, Wizara inapaswa kuishauri Serikali ili vifaa vya ujenzi (simenti, mabati, nondo, nyavu za mbu na kadhalika) viondolewe kodi ya ongezeko la thamani ili watu wa kawaida waweze kumudu na kujenga nyumba au kununua nyumba zilizojenjwa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kuhusu maendeleo ya nyumba. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri kuwa kuwekeza katika sekta ya nyumba inasaidia kuongeza nafasi za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kuwa nyumba na majengo mengi yaliyouzwa kwa wawekezaji hayakidhi mahitaji ya Watanzania wengi kwani wanapojenga maghorofa hupangishwa kwa bei ya juu inayoanzia Dola 1500 kwa mwezi na kuendelea.

Mtanzania wa kawaida hawezi kumudu kodi hizi za juu ambapo wageni walioko nchini ndio wanaonufaika na majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali isitishe kutoa vibali kwa wawekezaji wanaowekeza kwenye majengo ambayo Watanzania wakiwemo Wabunge hawawezi kupanga kwa sababu ya kodi kubwa zinazotozwa. Inasikitisha kuona nyumba nyingi za wawekezaji zinakaliwa na watu wa nje ambao ndiyo wanaoweza kulipa hizo kodi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa tuwaambie wawekezaji wawekeze kwenye nyumba za bei ya kawaida na siyo zile za dola 1500 kwa chumba (*studio*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itawaamuru wawekezaji watujengee nyumba za bei ndogo au ya kawaida, hakika Watanzania hawatajisikia kubaguliwa na kusukumiwa maeneo ambayo wala hayana *infrastructure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Pili, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi wanayoifanya kwa ustawi wa nchi yetu. Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Ardhi ndiyo inategemewa na kila mtu. Hivyo, Wizara ipewe rasilimali za kutosha ili kuweza kupima ardhi za vijijini na kutoa hati za kimila ili kuondoa migogoro inayojitokeza katika vijiji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba bora. Napongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa katika kujenga nyumba na kuuzia wananchi na kuwawezesha wananchi kumiliki nyumba. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na shirika hili na Halmashauri yatengwe maeneo na ujenzi wa nyumba uhusishe Wilaya za Kilolo, Makete, Njombe na Mufindi. Ujenzi wa nyumba hizi utawezesha wafanyakazi kupata makazi bora na pia wananchi wanaweza kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha utaratibu wa upimaji wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam kwa bahati mbaya maeneo haya hayana miundombinu ikiwemo maji na umeme maeneo haya ni pamoja na Bunju, Tuangoma na kadhalika. Wizara ihakikishe wakati wanapima viwanja uwepo ushirikiano na Wizara zingine ili kuweka miundombinu ili kuwezesha wananchi kupata huduma muhimu. Kukosekana kwa huduma muhimu kunafanya wananchi kusita kuendeleza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Upimaji na Ramani iandae ramani kwa ajili ya wananchi vijijini wanaohitaji kujenga nyumba za kuishi. Wananchi wanahangaika hakuna ramani, matokeo yake wananchi wanajenga holela badala ya kujenga kwa vigezo vilivyokubalika katika Wilaya husika. Wanavijiji kuhamasishwa kuunda ushirika wa ujenzi wa nyumba na hivyo wapewe mikopo ya ujenzi. Pia Vijana wahamasishwe na wapewe mafunzo ya ujenzi ili waweze kuunda vikundi vya ujenzi vijijini. Idara ya Ardhi kwenye Wilaya ziwezeshwe kuweza kupima vijijini, pia kutoa elimu ya umiliki wa ardhi.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitambue uwezo mkubwa wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi katika ujenzi wa Taifa lake kwa miaka mingi. Namwamini. Napenda kujua ni lini mkandarasi wa ujenzi ambaye anajenga jengo la Baraza la Ardhi, Kigoma atakamilisha ujenzi na kukabidhi jengo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Hakimu wa Baraza la Ardhi Kigoma amepewa vyumba viwili tu, kwenye jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Wakati anahudumia wananchi wa Mkoa mzima wa Kigoma kwa maana ya Wilaya zake zote. Kitu kinachosababisha wananchi wanaotoka Kasulu Vijijini, Kibondo na maeneo mengine kama haya ya mbali kupata usumbufu mkubwa kwa kukosa mahali pazuri pa kukaa na kusubiria kesi zao zitajwe. Mbaya zaidi kwa wananchi wanaotoka vijijini ambao uwezo wao wa maisha ni duni kabisa hakika wanalazimika kuwahi Mahakamani kabla ya tarehe ya kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi hawa hawana uwezo wa kufikia hotelini unakuta wamejazana hapo hapo Mahakamani na wanalala ovyo ovyo. Aidha, hapo hapo Mahakamani nje na chini, ukizingatia wateja wengi wa kesi hizi ni akinamama ambao wengine wana watoto, naomba suala hili liangaliwe upya ili kulinda haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itusaidie wananchi wa Wilaya ya Kasulu na Kibondo, katika mchakato wa kuongeza Mabaraza katika Wilaya. Wahakikishe wanatoa kipaumbele cha kuhakikisha wanaanzisha Baraza la Ardhi Wilaya ya Kasulu ili kupunguza msongamano wa kesi katika Baraza la Ardhi Kigoma na ikiwa ni pamoja na kuwapunguzia umbali wananchi wa Wilaya ya Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hakimu wa Baraza la Ardhi Kigoma kwa zaidi ya mwaka, alipewa gari na Wizara ili kumrahisishia utendaji wa kazi, lakini jambo la kushangaza, tangu amepewa gari na Wizara mpaka leo hawajampatia dereva wa kuendesha gari hilo. Jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa Mheshimiwa Hakimu wa Baraza la Ardhi, Kigoma. Lakini pia hii ni hatari kwa Mheshimiwa Hakimu mwenyewe na uangalizi wa uhakika wa chombo chenyewe kwa akili ya kawaida tu. Sioni sababu ya kutoa gari na usitoe dereva, binafsi hainiingii akilini. Naomba Wizara ifanye haraka iwezekanavyo kupeleka dereva Kigoma ili wananchi waweze kupata huduma kama za kutembelea mashamba na kadhalika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaandika barua kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi nikiomba apange ziara ya kuja Kasulu na hasa atembelee Jimbo la Kasulu Vijijini ikiwa ni pamoja na kuniletea wataalam wa kuja kupitia na kupima upya mipaka ya vijiji hasa vile ambavyo vimepakana na hifadhi ya Taifa, hasa kwa kuzingatia ongezeko la watu ni kubwa sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize katika jambo hili kwamba, mpaka leo hii kuna usumbufu mkubwa sana kwa wakulima wanaolima karibu na hifadhi wakisumbuliwa na watu wa maliasili kwamba wamevamia hifadhi. Wakati huo huo kwenye Jimbo langu la Kasulu Vijijini kuna vijiji ambavyo vimesajiliwa kisheria na viko ndani kwenye hifadhi mfano, Kijiji cha Kagerankanda, Mvinza, Kigembe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, naishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio cha wakulima wote ambao walikuwa wamepewa amri ya siku 21 wawe wametoa mazao yao yote shambani kwa madai ya kwamba ni wavamizi wa hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba niwataje Waheshimiwa Mawaziri waliojitabisha kuhakikisha wanalinda na kuisimamia Ilani ya chama chao kikamilifu kama ifuatavyo: Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Mkuchika, Mheshimiwa Maige kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mlitenda haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na Mungu awabariki sana sana.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba yake nzuri ambayo aliitoa jana. Nampongeza pia kwa jitihada zake za hali ya juu za kuhakikisha sheria inasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri Ole Medeye kwa jitihada zake za hali ya juu ambazo zimezaa ufanisi wa hali ya juu katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya za Siha ni wilaya mpya. Tunakumbushia ombi la awali la Wilaya yetu ili *NHC* watuingize katika utaratibu wa kujenga nyumba katika Makao Makuu ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Tumewaandaa wananchi wetu vizuri ili waweze kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* kwa rehema na neema zake nyingi alizonijaalia na bado ananihurumia, ni budi kusema *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nyumba wala maendeleo ya makazi bila ya kuwepo ardhi. Ardhi ni rasilimali nyeti na muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote. Ardhi ndio rasilimali ya pili kwa umuhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ikiwemo nchi yetu Tanzania baada ya rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa kwa Serikali kuithamini kwa maendeleo ya watu wetu na kwa mustakabali mwema wa nchi yetu. Ardhi ni mali! Serikali iwe na utaratibu wa kuipima ardhi yote na ifanyiwe tathmini ya matumizi yake lakini pia wamilikishwe ardhi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ardhi kupimwa na kumilikishwa wananchi, kuwepo na sheria zinazoelekeza matumizi ya ardhi hiyo ili itumiwe vizuri!

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria pia iwe wazi kwa wawekezaji kuwa ni lazima katika uwekezaji waingie ubia na wazawa. Ardhi ni ya wazawa na rasilimali zinazokuja ziwe za Mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana kuinua uchumi wa nchi, lakini pia hali za maisha ya watu wetu, kuwe na mgao wa uwiano katika uwekezaji wowote baina ya wazawa na wageni ili kuilinda ardhi isimilikiwe na wageni kwa manufaa ya nchi yetu na vizazi vyetu, ili Tanzania iendelee kubaki kuwa ya Watanzania. Mzawa mwenye ardhi awe na hisa japo 10% au 15%, lakini isiwe ardhi kunyang'anywa mzawa na kupewa Mwekezaji na kumwacha Mtanzania wa kawaida akiendelea kuwa maskini. Ardhi ifanywe iwe ndio mtaji wa Watanzania maskini na sio nguvu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Makazi. Serikali kupitia Wizara hii ipime viwanja vingi zaidi ili kutoa fursa zaidi za makazi bora. Viwanja baada ya kupimwa vitolewe kwa Watanzania maskini kwa bei nafuu! Hali ilivyo sasa ni tofauti! kwa mfano, viwanja vilivyopimwa hivi karibuni maeneo ya Gezaulole ni ghali sana kiasi ambacho Mtanzania wa kawaida hawezi kumudu. Kiwanja cha *high density* lenye ukubwa wa mita za mraba 2000 ($2000M^2$) kinagharimu million 12! (12,000,000/=).

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni gharama kubwa sana kwa Mtanzania wa kawaida kuimudu. Sera ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania haitowezekana. Maisha bora bila makazi (nyumba) bora yatakuwaje? Ikiwa kiwanja cha *high density* Gezaulale gharama yake ni 12,000,000/=!! Ni mazingira gani ya maisha bora? Au ni maisha bora kwa Mtanzania yupi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba (*NHC)*. Shirika lijenge nyumba za kisasa na za bei nafuu kwa ajili ya Watanzania maskini ili kuhuisha kwa ajili ya Watanzania maskini ili kuhuisha dhana au kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa pamoja na kuwa linafanya biashara lakini ni Shirika la Taifa, lisifanye ushindani na wafanyabiashara binafsi kupandisha bei za nyumba kiholela! Nyumba za watu binafsi sababu moja ya kuwa ghali ni kuwa wananunua maeneo maalum Mijini hasa Dar es Salaam kwa bei ghali sana na kisha ndio wanajenga nyumba. *National Housing* hawanunui ardhi, ni gharama tu za ujenzi. Mara nyingine bei ya kununua eneo (ardhi au nyumba ya zamani) inakuwa kubwa kuliko gharama ya kujenga jengo la ghorofa kumi? Mfano, nyumba ya miti iliyopo Kariakoo au Upanga inauzwa mpaka 1,500,000,000/=! Vipi *National Housing* watake kushindana bei na wafanyabiashara binafsi? Je, *National Housing* kwa nini wanaendelea kupandisha kodi kiholela nyumba zilizojengwa miaka 40 iliyopita? Nyumba hizo zilikusudiwa zikaliwe na wananchi wa kawaida? Mfano, Maghorofa ya Ilala, Temeke na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii isafishwe ili kupunguza ukiritimba wa kupatikana hatimiliki. Pia ugawaji wa viwanja mara mbili udhibitiwe. Ugawaji wa maeneo ya wazi ukomeshwe na hatua zichukuliwe kwa waliogawa sehemu za kuchezea watoto. Adhabu ziwe ni pamoja na kuwafunga jela watendaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa masikitiko yangu jinsi Mkoa wa Morogoro unavyoonewa na Serikali hii kwa kuwapa maeneo na wenyeji kunyanyaswa. Iko mifano mingi ya wananchi kukodishwa mashamba na hao wanaojiita wawekezaji badala ya kuyaendeleza mashamba hayo. Nashauri Wizara ikague na ifanye tathmini upya ili kubaini matatizo hayo na kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inieleze na iwaambie wananchi wa Kilombero wanaoishi na hapo awali walikuwa wanaishi pembezoni mwa hifadhi ya Udzungwa ambapo kwa sasa inamilikiwa na Malkia wa Uingereza kwa habari nilizonazo toka kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao kabla ya umiliki wa mwekezaji huyo, wananchi wa Kata za Kidatu, Sanje, Mkula, Mang'ula na Kisawasawa, walikuwa wanaokota kuni, matunda ya porini pia walipanda miti aina tofauti ikiwemo na mitiki, ndizi na kadhalika. Lakini hivi sasa wananchi hao wamekatazwa kufanya shughuli zote kutokana na hifadhi hiyo kusogeza mipaka ambapo hata wananchi hao hawakushirikishwa. Nashauri Serikali iende kufanya tathmini upya na ikawasikilize wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa ardhi Wilaya Kilombero unachangiwa kwa kiasi kikubwa na Mkuu was Wilaya aliyopo katika Wilaya ya Kilombero. Hivyo nashauri Serikali ifuatilie haraka na kupata ufumbuzi wa mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilombero wananchi wake ni wakarimu sana. Mfano, hai ni jinsi hayati Mwalimu Nyerere tangu miaka ya sabini aliwapeleka wazee (watu) kutoka Dar es Saslaam na kupewa hifadhi katika Kijiji cha Sonjo na wakati huo baba yangu Mzee Aloyce A. Limbweni ndiye aliyekuwa Jumbe wa Kata ya Sanje na Mkula na hakuna mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia miaka ya 80 Marehemu Mwalimu Nyerere aliruhusu wananchi toka Mikoa ya Kaskazini (Wachaga) wahamie Mkoa wa Morogoro na hadi leo hakuna migogoro ya ardhi na wageni hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi ya ardhi Wilaya ya Kilombero imekithiri kuanzia miaka ya 2000 (elfu mbili) na Serikali imeshindwa kutatua migogoro. Nashauri Serikali iharakishe kupima vijiji na kuainisha mipaka ya vijiji vyote kwani kuna vijiji hadi leo havijui mipaka yao mfano, Kijiji cha Katurukila Kata ya Sanje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifuatilie kwa haraka uporaji au ulaghai wa hekari 300 za Kata ya Mvuha, Kijiji cha Dala uliofanywa na Mbunge wa Kisesa kwa kuwarubuni wananchi wachache kwa kuwapa mpira, Sh. 500,000/= na Sh.1,000/=, kila aliyekuwepo kwenye kikao akishirikiana na Diwani na viongozi wa Serikali ya Kijiji cha Dala.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba umilikishwaji huo usitishwe mara moja. Ahsante.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja hii kwanza kwa kutazama sura ya dunia na mahitaji ya ardhi na hasa katika nchi zilizoendelea kutokana na mabadiliko ya tabia nchi sasa wanatafuta mahali pa kuvamia ardhi kwa mgongo wa uwekezaji *(Land Grading).* Uwekezaji huu unalenga katika nchi zenye *management* mbaya ya ardhi kama Tanzania, kutokana na hali hii watu hawa aidha wenyewe au kwa kuingia ubia na wenyeji huandika mikataba mibovu. Kwa kushirikiana na watendaji wetu ambayo huwaangamiza wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba mibovu kwa mfano, mkataba wa Mkoa wa Rukwa wa AGRISOIL. Huu ni mkataba mbovu kati ya Mikataba mibovu duniani iliyowahi kutokea. Matokeo ya mikataba hii haileti sura nzuri miaka ya mbele. Serikali ilitazame hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee upimaji wa viwanja Manispaa ya Bukoba, yapo malalamiko kuhusu upimaji wa viwanja katika Kata Vijiji (*Greenbelt*). Maeneo haya ni vijiji kwa hiyo wenyeji wanamiliki sehemu zao kimila. Kupima na kuwanyang'anya maeneo yote ni kuwaua kiuchumi, maana wanatumia ardhi hiyo kujipatia mahitaji, wananchi wa Kata ya Buhembe, Kagondo, Nyanga na kadhalika wanalia kwa kuwa Manispaa ya Bukoba inapima viwanja na kuwauzia maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vilio vingi vya kuporwa ardhi na wawekezaji. Malalamiko katika Kata ya Izimba, Kijiji Izimbya. Wananchi wanalia na kunyang'anywa ardhi. Waziri Mkuu alipofanya ziara Mkoa wa Kagera alimwagiza *DC* ashughulikie adha hiyo lakini hadi leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee fidia katika Kata ya Muleba, Halmashauri ya Muleba ilipima viwanja Makalwe Omundagala. Viwanja vimeuzwa na wananchi hadi sasa hawajalipwa fidia zaidi ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera umekumbwa na uvamizi wa wafugaji kutoka nchi jirani hasa kutoka Rwanda, Burundi na kufyeka migomba ya wanavijiji na kujiwekea makazi. Vilio vya wananchi ni vikubwa na hawasaidiwi. Mfano, kilio cha wananchi wa Vitongoji vya Karugwebe na Mtakuja na Itera katika Kata ya Rwabwere, wananchi hawa ardhi yao imepokonywa na wafugaji toka Rwanda na wananyanyasika. Wamepeleka malalamiko kwa *DC,* Karagwe lakini hawajapatiwa suluhisho. Wizara isaidie hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa na ubinafsi katika baadhi ya watendaji husababisha haki katika usimamizi wa ardhi kutokuwepo. Serikali ijitahidi kuweka utawala thabiti wa ardhi na hasa kwa kuondoa sheria zisizofaa na kuruhusu wananchi kumiliki ardhi, (*native ownership*) ili wananchi wawe na kauli ya kutosha.

**MHE. DKT. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa hotuba nzuri na niseme toka awali kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ningependa kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika hotuba ya bajeti sikuona vizuri mipango ya Wizara kuendeleza ile program ya kupima makazi yaliyojengwa kiholela na kutoa leseni za makazi kwa nyumba hizo katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Segerea, baada ya leseni za makazi kutolewa katika maeneo kadhaa ya Kata za Buguruni na Vingunguti, wananchi walitegemea program hii iendelee kwenye maeneo ya Kata za Kiwalani, Kipawa, Tabata, Kimanga na Segerea. Lakini haionekani kama mpango huu utaendelea. Utoaji wa leseni za makazi ni moja ya njia ya kuondoa umaskini wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ili Jiji la Dar es Salaam liwe endelevu, suala la kupima na kuendeleza *Sattelite cities* ni muhimu sana. Pamoja na Mji mpya wa Kigamboni na Lugwauni zinazopangwa, kuna haja ya kuongeza mipango zaidi ya *Sattelite cities.* Nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Ujenzi kupima *development corridor* kutoka Wilaya ya Bagamoyo kupitia Kibaha na kupita Wilaya ya Kisarawe, Msongola/Mkuranga, Kongowe, hadi Kigamboni. *Corridor* hii iwe na *Highway (six lane) Industrial corridor* na *satellite cities* kadhaa. Mpango huu utaondoa msongamano wa nyumba, watu na magari, pamoja na kuondoa viwanda katikati ya Jiji, na kuendeleza Jiji la Dar es Salaam kwa mpangilio mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamekuwa wakipoteza maisha yao kutokana na migogoro ya ardhi isiyokwisha, wakiishi kama wakimbizi, wakiishi katika mazingira magumu kwa kuzuiwa kutokuendeleza chochote kwa maeneo yaliyopimwa. Huishi kwa umaskini na kushindwa kuwasomesha watoto wao na kukidhi maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sababu zifuatazo ndo zinazosababisha yote:-

(a) Wananchi kutokushirikishwa katika mchakato ya utwaaji wa ardhi;

(b) Maeneo mengi kumilikiwa lakini bila kumjua anayemiliki na hivyo kuzuia uendelezaji;

(c) Fidia ambazo hazilingani na thamani ya ardhi;

(d) Serikali kutojali maslahi ya umma na badala yake hujali maslahi ya wageni zaidi;

(e) Kasi ndogo ya utekelezaji wa sheria ya ardhi; na

(f) Ukandamizaji unaofanywa na wawekezaji. Mfano, ni katika mashamba ya Bonde la Kiru, Wilayani Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ugawaji wa ardhi. Kwa kuwa wapo wataalam wanaofahamu kanuni za ardhi pamoja na taratibu zake, ni bora shughuli za ugawaji wakaachiwa wataalam ili waweze kutekeleza majukumu yao. Bila shinikizo la mtu, wanasiasa, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na watendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hayo kutokana na ugawaji mbovu unaofanyika katika Wilaya ya Hanang.

(a) Maeneo ya Serikali au nyumba za watumishi na majengo mbalimbali ya Serikali katika Mji wa Katesh ulitengwa mwaka 1985. Cha kushangaza miaka ya hivi karibuni kuanzia 2005 umetokea ugawaji holela katikati ya majengo ya watumishi wa Serikali kugawiwa kwa baadhi ya watu na kujenga nyumba zao binafsi bila ya vikao vya ugawaji wa ardhi na idhini ya vikao vya Halmashauri.

(b) Uuuzwaji wa nyumba ya *DMO,* Mganga Mkuu wa Wilaya.

(c) Ugawaji wa maeneo yaliyotengwa kama hifadhi ya Mlima kwa ajili ya mazingira bora.

(d) Ugawaji mbovu wa mashamba ya *NAFCO* yaliyorudishwa kwa wananchi, shamba la Warret, Gawal, bila kutumia wataalam wa ardhi bali waliokuwa wanagawa ni Idara ya Kilimo na mpaka leo bado kuna mgogoro mkubwa kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ugawaji ulikuwa unafanyika kisiasa kama kugawa ili wapate kwa kipindi cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabovu ya fedha za umma bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni kuhusu Fidia. Ulipwaji usioridhisha na kutolipwa fidia kwa wananchi wanaodai maeneo yao yaliyopimwa katika Mji wa Katesh, Mji mdogo Basotu, Mji Mdogo Endesak, Masakta, Nangwa. Hili liaangaliwe kwa karibu sana, ni vema Waziri au Naibu Waziri kufika na kuonana na wananchi wahusika kutatua tatizo. Wananchi walitoa fedha za viwanja mpaka leo hawajagawiwa maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ndogo. Kutokana na matatizo makubwa ya Wizara hii ni vema Wizara inastahili kuongezewa fedha ili kupunguza migogoro yote na kwa kuwa Wizara ya Ardhi inaingiliana na Wizara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji na ubinafsishwaji wa ardhi. Michakato ya ubinafsishwaji wa ardhi imekuwa haiko huru katika kutoa udadisi wa wananchi kuhoji. Ardhi nyingi

ya wananchi wa Tanzania imekuwa ikibinafsishwa kinyemela na hata wawekezaji wanaopewa ardhi hawana uwezo wa kuiendeleza na kutoa uzalishaji uliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, katika maeneo yaliyokuwa mashamba ya Hanang *Wheat Complex,* Mwekezaji Rai *Group* anayemiliki mashamba ya *Setchet* Marjanda, na Gidagamoud amelima ekari 9,000 tu kati ya ekari 35,000. Hivyo, ni bora ardhi hiyo wangepewa wananchi na wakulima wadogo wadogo ili waiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Nyumba na Makazi. Katika nchi zilizoendelea suala la ujenzi wa nyumba ni la Serikali ili kuweza kutimiza dhana ya makazi bora, ni lazima Serikali iangalie urahisi wa upatikanaji wa zana za ujenzi. Serikali ijitahidi kujenga nyumba za bei nafuu zaidi. Mfano, katika nyumba mpya zinazojengwa za *Medeli Project* bado nyumba hizo zinauzwa bei ghali kumpa fursa mwananchi wa kawaida kumudu gharama kwani zinauzwa kuanzia milioni 99 hadi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa. Hili shirika linahitaji kutengenezwa upya yaani lifanyiwe *reformation* katika *body* na *management* kwani limekuwa likihudumia idadi ndogo mno ya Watanzania yaani asilimia 0.5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baadhi ya wapangaji wamekuwa wakitumia shirika hilo kujinufaisha kwa kupangisha watu wengine. Mikataba ya mapango iangaliwe pamoja na kufanya ukaguzi upya ili kuondoa mianya ya mpangishaji anayefahamika kumkodishia mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubia kati ya Shirika la Nyumba na Mashirika mengine ya Hifadhi za Jamii kama *NSSF*, *Local Authority Pension Fund (LAPF)*. Kwa kuwa Shirika la Nyumba utendaji wake ni wa kusuasua, ni bora kukawa na ushirikiano na mashirika hayo ili kuweza kujenga nyumba nyingi zaidi na ili Watanzania wengi zaidi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuzwaji wa Nyumba za Serikali. Serikali itoe ufafanuzi juu ya nyumba za Serikali zilizouzwa huku zikiwaacha watumishi wengi wa Serikali wakiwa hawana makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, ni nyumba za Idara ya Mifugo za Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Jambo hili limekuwa likiigharimu Serikali fedha za mapango kwa watumishi ambao tayari nyumba zao zilikuwepo hivyo kuwa mzigo kwa walipa kodi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni lile ambalo Maofisa wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kujigawia maeneo ambayo awali yalitengwa kwa ajili ya nyumba za Halmashauri na matumizi mengine ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uuzwaji wa maeneo ya wazi. Maeneo mengi ya Serikali ambayo yamekuwa yakitengwa kwa madhumuni ya matumizi ya viwanja vya watoto yamekuwa yakiuzwa kinyemela hivyo, kufanya msongamano na mpangilio mbovu wa makazi. Serikali itoe ufafanuzi wa maeneo yote ya wazi ambayo hivi sasa yanamilikiwa na watu matajiri bila maelezo yoyote ya kueleweka.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namwomba Mheshimiwa Waziri apokee pongezi zangu za dhati kabisa kwake na Naibu wake kwa jinsi walivyoanza vizuri kazi. Nasema mmeanza vizuri, kazi hasa kwa kuamua kufuatilia watu waliohodhi ardhi na waliovamia maeneo ya wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika walipata pongezi kwa wananchi wengi sana kwa mwanzo huu mzuri. Tumeona walivyoanza na hakika nawapongeza kwa dhati kabisa na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasaidie ili waweze kukamilisha kazi hii ngumu inayohitaji kufanya maamuzi magumu ambayo yatapelekea lawama nyingi sana kwa wale waliovamia maeneo ambayo yataamuliwa yavunjwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ni ngumu sana Mheshimiwa Waziri amepewe Wizara ambayo kuna matatizo mengi. Tena makubwa. Pengine ameshapewa vitisho na hata kama hajapewa vitisho anaweza akatishwa sasa. Wengine wanaweza wakataka kumnunua inabidi awe ngangari kweli kweli, afanye maamuzi mapema ya utekelezaji maeneo yote aliyoyagundua yamevamiwa watu waone utekelezaji kama alivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amekuwa nje amefanya kazi nzuri na ametuletea heshima Watanzania na hasa sisi wanawake kwa yeye mwanamke mwenzetu kufanya vizuri ametujenga na sisi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo ameaminika na ndiyo maana aliporudi nchini amegombea Ubunge akashinda na Mheshimwa Rais akamwona anafaa kupewa Wizara na hata Waheshimiwa Wabunge wengi wanamkubali. Afanye kweli ili watu wazidi kukubali zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako katika kazi.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kwa kusema, ardhi ni mali, ardhi ni mtaji, hivyo basi kama tunayo nia basi njia ipo. Kwanza, naomba kumwambia Waziri, hawa watu wanaitwa Mipango Miji na wale wanaoitwa Afisa Ardhi ndani ya Halmashauri zetu ni tatizo kubwa. Katika Jiji la Mwanza kuna maeneo mengi ambayo sasa yamepimwa ambayo yalikuwa mashamba ya watu. Kuna shamba ambalo lilikuwa zaidi ya heka mbili, shamba hili lilipimwa, mwenye shamba amepewa kiwanja kimoja tu, viwanja vilivyobaki vyote vinachukuliwa na hicho kiwanja kimoja pia anauziwa anaweza lipwa Sh.180,000/= kwa viwanja vilivyopimwa lakini alichopewa atauziwa Sh.300,000/=, huku ndiko kumkomboa Mtanzania mnyonge?

Mheshimiwa Naibu Spika, na ni kwa nini kiwanja alichopewa asipewe bure kulingana na utunzaji wa ardhi kwa miaka mingi na ardhi watakayochukua wamlipe malipo yanayokidhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza kuna mtumishi amekuwa kikwazo kikubwa na kilio kikubwa kwa wakazi wa Mwanza, anaitwa Otieno. Tunaomba Wizara mumchukue na mtajua cha kumfanya, mimi na wananchi wa Jiji la Mwanza hatumhitaji, ni bingwa wa kubadilisha viwanja vya watu na ni dhuluma mkubwa huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Waziri aniambie ni lini wananchi wa Kata ya Ilemela, eneo la Bukombe jirani na Ma-*sister* wa *RC* walioambiwa wapishe ujenzi wa vituo vya kijamii kama Polisi, Shule na kadhalika. Leo ni miaka zaidi ya saba watalipwa na fidia ya ucheleweshaji wa fidia hiyo? Kwani walizuiliwa kufanya chochote, hata kama nyumba itaanguka upande, walale hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa kama hawatokuwa tayari kwa malipo, hakuna haja ya kufanya tathmini kwa wananchi na kuwazuia kuripea nyumba zao na kulima mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sasa kujenga nyumba pia za kupangisha na kuuza na haki itendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii nyeti na pia kwa kutoa hotuba yako iliyosheheni mikakati mingi inayoonesha uwezo wako mkubwa kwa maslahi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Naibu Waziri, Ole-Medeye ambaye namfahamu uchapakazi wake, uadilifu wake na upendo wake ambao unampelekea kuwa mcha Mungu na Mzalendo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mtendaji Mkuu, Wakurugenzi, Kamishna na watendaji wote katika Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kuhusu ardhi haiuzwi inakodishwa kwa kipindi maalum na kutathminiwa kabla ya kukodishwa tena. Nasema hivyo kwani imezoeleka mtu anachukua ekari kibao halafu anaamua aiendeleze ardhi au la! Bila kujali kuna mipango gani katika eneo husika. Wanasema ni eneo langu, amenunua hata kama hakufuata taratibu. Maeneo mengi huko vijijini wanaochukua maeneo wanadhani ni yao milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili si sahihi, kumbuka vizazi vinaongezeka, watoto wa leo ndiyo wazee wa kesho, wanahitaji ardhi na kadhalika. Hili naomba liwekwe wazi kwa viongozi na watendaji ndani ya Halmashauri na ikiwezekana kuendesha semina kwenye Baraza la Madiwani ili wao pia waelewe. Suala lisiwe bajeti kwani tunaweza kuunganisha na siku ya kikao cha Baraza tukafanya semina.

Pili, Kilindi hakuna ardhi ya kutoa. Nasema hivyo kwa maana ukienda Arusha na Moshi, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, utakuta matangazo yanasema "Karibuni Kilindi Ardhi inauzwa, eka Sh.10,000/=". Kweli walifurika watu kutoka maeneo mengi na kuchukua maeneo makubwa, lakini taratibu hazikufuatwa. Hali hiyo imepelekea migogoro mikubwa ya ardhi na mauaji baadhi ya maeneo. Hivyo, Baraza tumeamua kusitisha utoaji wa ardhi na kuruhusu kufanyika tathmini ya ardhi iliyotolewa bila kufuata utaratibu ili tuweze ku-*revoke* kwa ajili ya matumizi mengine. Zoezi hili linahitaji fedha, naomba watusaidie kwa hilo. Maombi yamekwishapelekwa mezani kwao.

Tatu, uwezeshaji Maafisa Ardhi. Maafisa hawa ambao ni muhimu sana hawana usafiri wala nyenzo za kufanyia kazi wala bajeti inayoeleweka. Imebidi tujitahidi kumnunulia pikipiki ili kumwezesha kufika maeneo mbalimbali katika vikao husika. Nimezungumzia Mfuko wa kupima viwanja, naomba uzingatie kuwa, kuna viwanja 500 vilivyopimwa katika Makao Makuu ya Wilaya ya Songe na hivi sasa tumeshindwa kulipa fidia. Matokeo yake wenye mashamba hawaruhusu kutoa maeneo kwa walioomba, matokeo hatusongi mbele. Hatujapewa mkopo na tunahitaji kupima viwanja vingine 500. Wilaya hii ina umri wa zaidi ya miaka nane sasa. Tunaomba mtuangalie kwa jicho la huruma.

Nne, kwenye taarifa yenu mmeonyesha hadi kufikia Juni, 2011 vyeti vilivyopatikana Kilindi ni 42 na Hati za Kimila 42, si kweli, *data* hii ni ya uongo, nimethibitisha kwa Afisa Ardhi wangu leo hii vyeti ni sita tu, hatimiliki tatu na tunashughulikia vingine vitano. Naomba sahihisho hilo lifanyike.

Tano, nawapongeza sana *NHC* hasa Nehemia Mchechu na wote husika, ni wasikivu, mara zote nikiwaona kwa shauri lolote linatekelezwa mara moja. Ombi tu, waangalie pia maeneo kama Kilindi ambapo ni Wilaya mpya zisizo kabisa na nyumba za kuishi watumishi, hivyo, kusababisha watumishi kukimbia kujenga makazi angalau *cheap housing,* maeneo yapo, naamini kwa ushauri wako wafike, mimi na madiwani tutatoa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wake bila kuwasahau watendaji wakuu wa Wizara husika kwa lengo la jitihada wanazozifanya za kufanikisha shughuli za kijamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii, binafsi napenda kumwuliza Waziri Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgogoro wa ardhi, Wilayani Tarime. Ifahamike wazi kuwa moja ya sababu kubwa inayosababisha uhasama baina ya koo na koo, Tarafa na Tarafa, Kata na Kata, Kijiji na Kijiji hata kaya na kaya ni mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali yafuatayo:-

(1) Je, Waziri analifahamu hilo?

(2) Je, Waziri anachukua hatua zipi madhubuti za kulitatua tatizo hilo?

(3) Je, ni lini Waziri atatembelea Wilaya ya Tarime ili kujionea migogoro ya ardhi isiyokwisha inayoikabili Wilaya ya Tarime?

(4) Je, ni lini Waziri atatamka hadharani kuwa mgogoro huo utakwisha kwa kupima ardhi yote ya Wilaya ya Tarime ili kila mtu apate haki yake?

(5) Je, ni lini Wizara itatoa hati za kimila Wilayani Tarime?

(6) Waziri anasema nini juu ya watendaji wabovu wa Idara ya Ardhi Wilayani Tarime? Kwa nini Serikali inaendelea kuwalea hao watendaji wabovu?

(7) Serikali inasema nini juu ya vigogo waliojitwalia ardhi Wilayani Tarime kutoka kwa watu maskini na kupewa hatimiliki na Wizara husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuisemea Wizara kuhusu hatimiliki zinazotolewa. Hati miliki zinazotolewa na Wizara mara nyingi zimekuwa na matatizo kwa sababu zifuatazo; rushwa, Watendaji wabovu na udanganyifu wa watendaji wakuu wa Wizara. Katika hili nina maswali yafuatayo:-

(1) Je, ni kwa nini baadhi ya viwanja hupewa au hutolewa hatimiliki zaidi ya moja hadi hata sita?

(2) Je, kwa nini kuna rushwa kubwa kubwa katika upatikanaji wa hatimilki?

(3) Je, Waziri anatoa kauli gani juu ya hatimilki ambazo hadi sasa hazijatolewa katika eneo la Mbezi Juu –Jogoo kwa visingizio vya kwamba Wizara haijabadilisha matumizi ya ardhi?

(4) Wizara imejipangaje kukabiliana na tatizo la rushwa katika Wizara husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuzisemea Nyumba za Serikali na za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*). Katika Wilaya yangu ya Tarime kuna tatizo kubwa sana la nyumba za Serikali. Pia kuna uhaba mkubwa sana wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*). Vile vile katika hili nina maswali yafuatayo:-

(1) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za Serikali katika Wilaya ya Tarime?

(2) Je, ni lini Shirika la Nyumba la Taifa litaanzisha ujenzi wa nyumba za bei nafuu Wilayani Tarime?

(3) Je, Waziri anatoa kauli gani juu ya ulanguzi wanaofanyiwa Watanzania hasa wa Kariakoo kwa kupangishwa nyumba za *NHC* kwa bei ya ulanguzi?

(4) Kwa nini nyumba za *NHC* sehemu za Kariakoo (Dar es Salaam) na sehemu nyingine za mijini zimegeuzwa kuwa vitega uchumi vya Wahindi na baadhi ya Waafrika wasio na uzalendo na nchi?

(5) Je, ni lini Serikali itawatimua wapangaji wote wa *NHC* wanaokwenda kinyume na taratibu za upangaji wa nyumba hizo?

(6) Serikali inatoa kauli gani juu ya nyumba za Serikali zilizouzwa kwa vigogo, kwa bei ya kutupwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuyasemea makazi ya wananchi, Wilayani Tarime. Maendeleo ya makazi Wilayani Tarime yanaathiriwa na vikwazo mbalimbali hususan, vita vya koo na koo, migogoro ya ardhi isiyokwisha na hata wizi wa mifugo. Hivyo, ili makazi hayo yawe bora yanahitaji upimaji. Nina maswali yafuatayo kuhusu jambo hili:-

(1) Je, Serikali inatoa kauli gani ya uhakika juu ya upimaji wa Mji wa Tarime?

(2) Je, Serikali itapima lini Miji midogo ya Sirari, Nyamongo, Nyamwaga, Komaswa na Masanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa yote naunga hoja mkono lakini natoa msisitizo kuhusu suala la mgogoro wa ardhi Wilayani Tarime utatatuliwaje?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Babati Vijijini. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Anna K. Tibaijuka na Naibu Waziri Goodluck Ole-Medeye kwa jitihada zao kwa pamoja kuendeleza na kuboresha Wizara hii nyeti na masuala ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe ushauri kwa kuboresha Wizara hii. Kwanza Wizara ishirikiane kwa karibu na Wizara za Maliasili na Utalii; Mazingira; Kilimo, Chakula na Ushirika; Maji; Mifugo na TAMISEMI. Kwa pamoja pekee ndiyo matatizo na kero ya ardhi itatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kushauri Mabaraza ya Ardhi. Ifahamike uhakiki wa namna ya kuboresha Mabaraza kuanzia Vijiji, Kata na Wilaya wapate mafunzo, vifaa na vitendea kazi, pia wapate mafunzo ya *customer charter* na waambiwe washirikiane na Idara ya Ardhi kwa utaalam, utapunguza migogoro, pia namna ya ku-*computerize* Mabaraza haya.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba suala la ardhi ya kilimo kuchukuliwa na maeneo ya makazi kwa ajili ya ujenzi, tutafika mahali tutakosa eneo zuri la kilimo. Naomba mahali ambapo kuna eneo ambalo halifai kwa kilimo ndipo miji na makazi yajengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni suala la fidia. Tunashauri fidia halali na ambayo ni *market value* alipwe mwathirika na anahitaji eneo na Serikali ikusanye kodi, ushuru na mwananchi apate haki yake. Kama ni bei kubwa na wanyonge hawataweza kupata eneo, basi maeneo ya biashara yapigwe mnada na yafidie maeneo ya makazi ya kuishi. Pia bei ya *reform* ya fidia ifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, tunaomba Wizara na Serikali itatue mgogoro katika eneo langu la Babati Vijijini, Bonde lote la Kiru ili wananchi na wawekezaji waweze kukaa kwa amani na washirikiane kuleta maendeleo. Maeneo ya mashamba ya Serikali, Chama cha Ushirika na mashamba ambayo hayaendelezwi wapewe Watanzania wa maeneo hayo ili kutatua migogoro. Tunaomba migogoro ya ardhi ya Kata ya Mawire, Endakiso, Galapa, Kash, Arri, Magasa, Magogo na Kiru yafanyiwe kazi ya kudumu. Tunashauri viongozi wanaotumia ardhi kama njia ya kujipatia umarufu wa kisiasa na kuleta uchochezi wachukuliwe hatua ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, elimu juu ya sheria ya ardhi itolewe kwa raia kwani wengi hawajui Sheria hizi na 4 na 5. Ni kusababisha migogoro mikubwa sana ya ardhi pia vitabu vya sheria vifike vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, tunaomba *NHC* iangalie namna ya kuwekeza Babati Mjini na Vijijini, iwe ya mfano Manyara. Pia tunaomba *NHC* iangalie kodi zake na namna ya kuongeza kila mwaka au miwili, wadaiwa sugu watolewe ili mapato ya NHC yaboreke na waweze kuendeleza katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, tunaomba Wizara isaidie kwa nguvu zote, kununua vifaa vya kisasa vya kupima ardhi kwa ajili ya Wilaya na Wizara. Itasaidia kupima ardhi ya wananchi na

hasa wa Babati ili kuondoa umaskini, pia upimaji wa ardhi ya makazi ufanyiwe kazi kwa haraka zaidi. Kama vifaa vingekuwepo na wataalam wengi zaidi gharama pia ingepungua na upimaji ukiwa hadi vijijini basi maendeleo yatakuwa kwa usawa nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Idara inayohusika na utoaji wa hati pia iboreshwe, hati iwe na muda maalum kutoka. Pia suala la rushwa na uwazi katika eneo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba elimu juu ya mwananchi kuwa katika eneo lenye mipaka ya Vijiji, viwili, Kata mbili au Wilaya mbili haimwondolei haki ya umiliki, bado atakuwa Tanzania na ana haki ya kuwakokota wanasiasa, ndiyo wanakwamisha suluhu za migogoro ya mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara na Serikali ifanye utafiti wa namna ya kumaliza mgogoro wa Babati Vijijini, Bonde la Keru kwa haki na usawa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee mchango wangu kwa kutoa maelezo yafuatayo. Mwaka 1974/1975, Serikali iliamua kuwahamisha wananchi kwa kuwaweka pamoja ilijulikana kama Vijiji vya Ujamaa. Hivyo, wananchi waliokuwa wanaishi Ushora/Ndago Iramba walihamia Songambele. Lakini Serikali iligawa viwanja vya kujenga tu, lakini hawakuwapa mashamba. Hivyo, waliendelea kurudi kwenye mahame yao kwa ajili ya kilimo, lakini Jeshi la Magereza walikuja na kuwatoa kwenye mashamba yao na Jeshi la Magereza wakaanzisha Gereza la Kilimo na kuwaacha wananchi wakilalamika kwa kuanzisha mashamba mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Magereza yale ni zaidi ya miaka sita hawalimi tena. Je, Serikali au Wizara hii sasa itakuwa tayari kurudisha ardhi ile kwa wenye mashamba ili waendelee na shughuli za kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgogoro wa upimaji ardhi Muhonze, Bugogwa. Kwanza, naomba kupatiwa ufafanuzi juu ya suala la kuhamishwa wananchi wa maeneo ya Muhonze, Kata ya Bugogwa ambao hivi sasa wako njia panda kutokana na kukanganywa na watendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza ambao kimsingi wanapotosha dhumuni la Mradi huo ujulikanao kwa eneo la (*UN habitat*) ambao kimsingi ulilenga kuboresha makazi ya maeneo hayo kwa maeneo ya kupima viwanja vyao wananchi hao na maeneo hayo ambayo kimsingi shughuli zao ni uvuvi na wamekaa maeneo hayo kwa miaka mingi wakitaka kupimiwa maeneo hayo, jambo ambalo kwa muda mrefu hawakufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Waziri wa Ardhi, naomba kupitia Bunge hili Tukufu utoe ufafanuzi na tamko kwa niaba ya wananchi hao wa Muhonze juu ya dhumuni la mradi huo wa uendelezaji makazi hayo ili wao ndio wawe wa kwanza kunufaika na upimaji huo tofauti na upotoshwaji unaotoka kwa watendaji wa Jiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa migogoro ya ardhi katika Jimbo la Ilemela ni kwa takriban asilimia 90% inatokana na watendaji na wasimamizi ambao wamekuwa na wakijihusisha na vitendo vya rushwa ambavyo vimesababisha upindishwaji wa haki za wananchi walio maskini na kupelekea wengi wao kupokonywa kwa ardhi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri awe tayari kuunda Kamati Maalum ambayo itachunguza migogoro yote au kuhakikisha haki inapatikana na Waziri aje Jimboni Ilemela ili kujionea mwenyewe hali ilivyo.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu urasimu wa watendaji katika ofisi za ardhi, takribani katika kila Ofisi ya Ardhi kama ni Wilaya au Mkoa ukienda utapata usumbufu usio na lazima. Kwa

mfano, unaweza kujibiwa tu, faili halionekani, namba ya kiwanja chako imekosewa, stakabadhi muhimu haipo! Kimsingi majibu hayo yote hayana maana na hayalengi huduma bora kwa mteja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa najiuliza mara nyingi, kama mimi Mbunge nakwenda kwenye Ofisi ya Manispaa ya Ardhi, nafuatilia suala la kiwanja, unajibiwa faili la hicho kiwanja chenye namba hiyo halionekani, je, wananchi wa kawaida wangapi wanaingia katika Ofisi za Ardhi hawapati majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sahihi na ushirikiano? Hawa watendaji kwa nini wanakuwa Miungu watu? Kwa nini wanakuwa wakorofi? Jibu ni rahisi wanafanya kazi kwa uzoefu wa kutegemea rushwa na kitu kidogo, wanasahau kabisa rushwa ni adui wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuhamisha watendaji walioharibu Dar es Salaam kuwahamisha Mtwara, Lipo tatizo la kiutendaji kwa Maafisa Mipango Miji, kwa nini watendaji wanalalamikiwa katika Manispaa ya Dar es Salaam ambao ni wabovu wakiharibu wanahamishiwa katika mikoa mingine ikiwemo Mtwara? Napendekeza watendaji wanaoharibu katika eneo moja wasihamishiwe katika maeneo mengine wanaoharibu wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini watu wa ardhi wanachelewa kutoa *title* za viwanja na kwa nini upimaji wa mashamba ili mtu aweze kupata *title deed,* gharama yake ni kubwa na hata hivyo zinachelewa kupatikana? Tatizo liko wapi? Hizi gharama kubwa Wizara haioni kuwa kwa wananchi wa kawaida ambao ndio wengi wana mashamba watawezaji kugharamia?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Dodoma, sote ni mashahidi kwa namna ambavyo wakazi wa Dodoma wanavyoilalamikia Mamlaka ya Ustawishaji. Suala la watumishi wa *CDA* kujimilikisha viwanja vingi mara nyingi utawakuta wanauza viwanja ambapo vingeuzwa moja kwa moja na Mamlaka vingeuzwa kwa bei nafuu badala yake wao wanaviuza mara tano au mara kumi ya bei halali! Kwa nini wafanyakazi wa *CDA* wanaruhusiwa kununua viwanja vingi? Napendekeza uwekwe utaratibu wa kuwataka wafanyakazi wasinunue viwanja zaidi.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kabla sijaendelea kuchangia hoja hii,, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusu ardhi kwa sababu wananchi wengi wanalalamika kuhusu ardhi au maeneo kuchukuliwa na Serikali bila hata wao kufidiwa au kuelezwa jambo ambalo si zuri hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kusikitisha zaidi hasa kwa baadhi ya maeneo yanayohamishwa wananchi ambao walikuwepo kwa muda mrefu sana. Leo mwananchi unamwondoa bila hata kumfidia chochote kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuwe na mpango wa kulipwa fidia wananchi kabla ya kuondoshwa sehemu zao. Vema zaidi wakiondolewa katika sehemu hizo, watafutiwe sehemu ya ardhi nyingine ili wasihangaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nyumba za Serikali huachwa ovyo sana bila kuboreshwa na nyumba nyingine hubomoka hali ya kuwa kama zingewahiwa mapema zisingeharibika, hali hii ni kuitia hasara Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, ni vizuri nyumba zote zipitiwe na kukaguliwa na zile zinazotaka kuboreshwa ziboreshwe ili ziweze kutumika kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii kwa mara ya pili. Ahsante.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na uongozi mzima wa Wizara. Lakini pamoja na yote haya budi nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya wazi yamevamiwa, hatua gani zimechukuliwa? Makazi holela ni mengi sana mfano kule Mbeya maeneo ya Jijini kama Iyunga, Nzovwe, Isanga, Mwakibete na kadhalika ni *squatter* sana, kipi kifanyike ili Serikali iweze kuokoa janga hili? Mfano mwingine hai, ni eneo la Itende Jeshini pale ambapo inabidi wananchi wakatize jeshini sababu tu ya makazi holela hata barabara haijulikani ya kupita ni ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgogoro kati ya wanaomiliki ardhi na maliasili kama vile kule Iringa. Kama Serikali, hatma yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni uhai, ardhi ni uchumi wa wanyonge, sasa hivi tuna *federation*, hii ya Afrika Mashariki. Mwanzoni tulikuwa na *common currency, free common labour.* Tukumbuke Tanzania ni tajiri wa ardhi. Hawa wenzetu watakuja na kupata ardhi yetu, wanaililia kwa sababu kwao hakuna ardhi. Je, Serikali imejipanga kwa manufaa ya Watanzania kwanza? Je, utaratibu gani umewekwa kwamba na Watanzania wakienda kwenye hizo nchi zao watapata ardhi? Hapa budi kuwa na *win win situation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hati ni tatizo, ukiritimba Wizarani katika upatikanaji wa Hati umekithiri. Mfano, unaomba hati kupitia Wilayani unazungushwa, unaambiwa tayari imepelekwa Wizarani na Wizarani nako wanarusha danadana kama mpira, kuna urasimu sana usio na tija katika hili. *Solution* itafutwe kuondoa kero hii na inachukua muda mrefu sana. Wizarani pia umakini haupo, mafaili hayapo kwa mpangilio, yanapotea ovyo na picha za waombaji hazizingatiwi, waweza kuzikuta kwenye makorido zimedondoshwa tu *and no one bothers*. Hayo mafaili yanafanyiwaje kazi? *What is going on there?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ifumuliwe ili kuwezesha mfumo mzima wa utendaji kazi kuwa wa spidi na viwango maana kwa sasa hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa viwanja ni tatizo sana, ukoje? Misingi gani ifanyike ili kujua nani anastahili kupewa na kihalali?

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi kati ya miji na vijiji kupitia Tume ya Ardhi imefikia wapi. Hii Tume ya Ardhi inatakiwa iongezwe meno ili kuepukana na adha zisizokuwa na tija na waweke utaratibu mzuri wa *reporting channel* huko vijijini na kwenye miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli nachukua fursa kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kwa kuwa na sura mpya katika utendaji mzuri wa matendo. Katika kujenga miji/nyumba/*flats* katika maeneo mbalimbali kwa viwango mbalimbali na hii itaepusha makazi holela pia, ingawa wakumbuke kujenga nyumba za gharama ndogo (*planned*) ambazo Watanzania walio wengi ndio wanaoweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Shirika la Nyumba linaendelea kuumia kuchangia VAT katika vifaa vya ujenzi vyote wanavyonunua na wakati huo huo inachajiwa *VAT* mwishoni, Shirika linaumia, litapataje faida na kujiendesha? Hili lazima liangaliwe upya kupitia Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Shirika likitaka kukopa hadi lipate kibali cha Hazina? Huu ni urasimu wa ukiritimba usio na taji. Shirika hili lipewe *full mandate* ya kujiendesha bila kuingiliwa ingiliwa ili liweze kukamilisha ndoto yake inayohitaji kufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tathmini inayotolewa ni hafifu sana? Wananchi wanafanyiwa tathmini na kuachwa muda mrefu na tathmini pia huchukua muda mrefu na hawa wanaachwa *idle* kwa kipindi kirefu sana, ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini mtu mmoja anaweza kuhodhi viwanja vingi na kuanza kuviuza kwa bei mbaya kwa wengine? Ni akina nani hawa na Serikali itachukua hatua gani kukomesha hili? Huu si utaratibu hata kidogo na *unethical*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji nipate maelezo ya kina katika kuwasilisha majibu.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa vile kuna migogoro mingi ya ardhi Wilayani Serengeti hasa kutokana na uhamiaji holela toka Wilaya jirani, Mkoa jirani na nje ya nchi. Wizara itoe msaada katika Wilaya na Mkoa kukabiliana na hali hii kwa sababu Wilaya haina uwezo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, MKURABITA inatekelezwa kwa pole pole mno katika Wilaya ya Serengeti. Tangu mpango huo uanze katika vijiji vitano mwaka 2009 hadi leo hii hakuna mtu aliyepewa hati na hata upimaji bado haujakamilika. Wizara ina mpango gani kuharakisha utekelezaji wa mpango huo mzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa vile tatizo la mpaka wa Wilaya ya Serengeti, Bunda na Musoma Vijijini ni la muda mrefu sasa (tangu 1978) na Mkoa umeshindwa kiutaratibu kumaliza mgogoro huo ambao imefikia hatua wananchi wa Wilaya hizi tatu kuchukua silaha kwa ajili ya mapigano ya mpaka. Ni vema Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutatua mgogoro huu? Hasa ni vizuri mipaka ya asili iliyopo Mabonde na Mito ya Tipina na Mto Mekamariro ifuatwe na kuheshimiwa, ndivyo wananchi walivyozoea tangu enzi ya utawala wa Watemi na inasaidia kuweka utulivu na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipatiwe majibu ya kina ili niunge mkono hoja.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimechangia kwa kuongea lakini sikumaliza, naomba sasa niendelee kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgogoro uliopo kati ya Tanga *Cement* na wanakijiji wa Pande B. Wanakijiji hawa kabla hawajatatuliwa malalamiko yao tarehe 13/06/2011. Saruji walipata ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya kuchimba na akashirikiana na baadhi ya viongozi wa Kijiji wale waliopata marupurupu na mgambo juu, walilinda kama vile watu wako vitani, je, wanaogopa kitu gani? Lengo ni kuchimba tani 5,000 za majaribio ya malighafi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakijiji waliodhulumiwa walitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya lakini hawakushughulikiwa ndipo uvumilivu ulipowashinda, walikwenda *site* na mgambo walipowaona mapambano yakaanza na watu kujeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndipo wale waliodhulumu walipopata nguvu, wakatumia nguvu za dola kuwakamata hata wale walioshiriki ili kupoteza ushahidi. Wanaume wengi walikimbilia maporini na kijiji kilibakia wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakijiji hawa walimwandikia Mheshimiwa Waziri barua tarehe 21/12/2010 juu ya malalamiko yao hayo, sijui amechukua hatua gani mpaka sasa. Namwomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi suala hili haraka kadri inavyowezekana kwani wanakijiji hawa wamevumilia sana. Uongozi wa Wilaya na Mkoa hawawezi kulitatua tatizo hili kwani rushwa imetembea kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mapendekezo yangu kwa Mheshimiwa Waziri, naomba aliyafanyie kazi. Zoezi la uthamini lifanywe upya ili kuondoa mazingira ya rushwa na upotevu wa fedha nyingi za wanakijiji na Serikali kwa ujumla. Serikali iwachukulie hatua za kisheria siyo kinidhamu viongozi wa Serikali ya Kijiji, Kata na Halmashauri kwa ujumla katika uhusika wao katika uwekezaji Pande B. Uchunguzi ufanyike ili kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani wote walioingiza watu hewa katika kupata fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine katika Wizara ya Ardhi ni tathmini, sheria za ardhi zina mapungufu makubwa katika hili, kwani watu wanaotathminiwa ardhi leo huwa wanakuja kulipwa baada ya muda mrefu, sehemu nyingine mpaka miaka mitano hali hii inapelekea wananchi wengi kulipwa pungufu au kupunjwa kwani thamani halisi ya ardhi wakati wanalipwa

huwa haiendani na thamani waliyofanyiwa tathmini muda uliopita ukizingatia kuwa ardhi thamani yake haishuki, hupanda kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano halisi ni kwa wakazi wa Kipawa waliofanyiwa tathmini ili walipwe kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege pesa walizolipwa hazikuendana na thamani ya ardhi kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuhamisha wananchi sio mzuri, wananchi wengi wamekuwa wakilalamika kuwa utaratibu wa kuwahamisha kupisha shughuli za mradi fulani ni mbovu na ni wa kibabe na uvunjwaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikutumia nguvu, kuwafungulia mashtaka. Mfano, Mwekezaji wa Mgodi wa North Mara pamoja na mradi kuwakuta wananchi wanamiliki maeneo yale, bado utaratibu haukufuatwa na matokeo yake mabovu ya Serikali yamepelekea kutoelewana mpaka leo kati ya Mgodi wa *North* Mara na wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utata wa Sheria na Sera ya Madini iliyokuwepo kuhusiana na fidia, Mwekezaji hakutaka kufanya utaratibu mzuri hasa kuendeleza majadiliano na wananchi kutafuta njia mbadala ya kuhamisha wananchi na kuwapeleka katika maeneo mengine na kupisha shughuli za uchimbaji ambazo ni hatari kiafya kwa wakazi wanaozunguka mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wananchi vijijini, sio mzuri. Wananchi wengi hawashirikishwi katika maamuzi ya ardhi vijijini. Hali hii hupelekea watu wachache kuuza ardhi na maeneo muhimu ya vijiji kinyume cha sheria. Mfano, mgogoro wa ardhi wa *NAFCO*, Arusha kati ya wawekezaji na wananchi, wananchi wanalalamika kwamba hawakushirikishwa katika kumleta mwekezaji katika eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu ulileta maafa kwa mali zote za Mwekezaji kuchomwa moto ikiwemo nyumba, magari na vifaa muhimu vya kilimo na wananchi pia kupoteza maisha kwenye mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi katika matatizo haya Serikali huwa inajitokeza mwishoni kutafuta ufumbuzi na hii imekuwa desturi kwa mamlaka kwani wakati malalamiko yanaanza ngazi za Wilaya na Mkoa zilipewa taarifa lakini kwa kupuuza kwao ikapelekea madhara na hasara kubwa kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimwa Waziri atakapofanya majumuisho atoe kauli ya Serikali kwenye suala la mgogoro wa ardhi wa Kijiji cha Pande B, ni muhimu sana.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa ya kuchangia kwa maandishi ili kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Wizara hii na sekta zote zilizoko chini yake ni muhimu na zinaweza kuwa mhimili na ustawi wa Taifa letu iwapo juhudi za makusudi zitafanyika. Hii ni pamoja na kutenga rasilimali zinazolingana na mahitaji ikiwa ni rasilimali yenye weledi na uadilifu, fedha na *organization* inayolenga mahusiano ya sekta zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la matumizi ya ardhi. Jitihada zifanyike awali ya yote kuwawezesha kwa kuanzia na elimu viongozi wa vijiji ambao sheria inawapa mamlaka ya kusimamia sehemu kubwa ya nchi yetu. Viongozi wa Vijiji wamepewa jukumu linalowazidi uwezo. Watu hawa wamevuruga mno mfumo wa ardhi kuanzia ule wa jadi na hata wa kikoloni. Maeneo ya vijijini akinamama wamefukuzwa katika sehemu walikozoea kulima mazao ya msimu kama njugumawe, karanga na viazi, maeneo mengi yamelimwa miti bila kujali ni ardhi tabaka gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matumizi ya ardhi linapaswa liendane na kuweka au kutenga ardhi kwa matumizi na mahitaji ya baadaye. Hii ni elimu ambayo Viongozi wa Vijiji na Halmashauri, wanapaswa kuwa nayo. Katika hilo ni pamoja na haja ya kuondoa mkanganyiko

wa kiutawala na mawasiliano kati ya Wizara na TAMISEMI, weledi uliopo Wizarani unapaswa kutumika mpaka ngazi ya vijiji. Jambo linalopashwa kufanyika ni kuelimisha wahusika waliozoea madaraka, majukumu na mamlaka ya mtiririko (*hiarachy structure*) na kuwaelekeza katika mfumo wa sasa ambao unaelekea kuwa *matrix structure*. Chini ya mfumo huu wataalam wakati chini ya Halmashauri, TAMISEMI wanapaswa kutambua kuwa wanawajibika pia kwa Wizara kwa weledi wao. Suluhisho hili linawezekana iwapo na Serikali itaelewa hivyo. Kinyume chake utendaji wa Wizara nyingi ambazo sehemu ya majukumu yake yanasimamiwa na Halmashauri za Wilaya utakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tatizo la migogoro ya ardhi Mkoani Kagera. Migogoro hii inaelekea kubaya na imekwishaleta madhara kwa wananchi. Ushauri wangu ni kuwa tatizo hili si kubwa au gumu kulitatua kama walio wengi wanavyotaka kutuaminisha. Tume na Kamati nyingi za Serikali zilizopewa jukumu hili kazi yao inaweza kuhitimishwa kwa kufuata yafuatayo:-

(a) Wizara ya Ardhi kuchukua jukumu la kuongeza usuluhishi na kumaliza tatizo hili.

(b) Pamoja na kuzingatia miongozo, sheria na taratibu zinazotawala uendeshaji wa sekta ya ardhi, Wizara ya Ardhi ikutane na uongozi wa Wabunge wa Kagera kupata maoni ya wananchi.

(c) Mipaka yenye migogoro kati ya *NARCO* na wananchi itatuliwe kwa kuzingatia mahitaji ya wakulima (wananchi) ambao hawana sehemu nyingine za kwenda.

(d) Sehemu ambazo *NARCO* itachukua kama ranchi zizingatie na kutii njia za asili na zisizuie vyanzo vya maji.

(e) Ugawaji wa ardhi iliyoko chini ya *NARCO* iwatenge waendelezaji makini watakaotumia maeneo hayo (*blocks)* kwa misingi iliyokusudiwa.

(f) Tatizo limekuwa kubwa kutokana na wafugaji toka nchi jirani ama kuleta mifugo na kuchunga nchini au kumiliki hizo *blocks*. Wageni hawa waondolewe na Serikali ihakikishe hakuna uingizaji wa mifugo toka nchi jirani.

(g) Wizara isimamie mipaka ya hifadhi lakini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine, utaratibu endelevu uanishwe ili kuzuia wafugaji wawe wageni au Watanzania hawaingii kwenye hifadhi kwa shughuli yoyote.

**MHE. MAHOUD HASSAN MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu wake walivyojipanga katika kutekeleza majukumu yao katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kuchangia katika eneo la utawala hasa tabia za baadhi ya Maafisa Ardhi waliokuwepo katika nchi yetu, kuwa ndio chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado, Serikali haijachukua hatua za dhati kudhibiti hawa maofisa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imekuwa sio makini katika taratibu za kulipa fidia, kuna ujanja ujanja mwingi unafanyika wakishirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa mfano, maeneo ya Mwabo, Ibapunde, kuna ukiukwaji mkubwa wa taratibu zilizotumika kulipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatakiwa itoe tamko kuhusu matumizi ya leseni za makazi zinazotolewa, kuna baadhi ya benki hazitaki kuzitambua kama dhamana halisi na kuzuia haki zao za msingi za kuwasaidia watu wakope.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali imekuwa haina haraka ya kuhakikisha kuwa maeneo mengi yanapimwa, ili iwasaidie wananchi, wajenge nyumba kwa kufuata utaratibu, matokeo yake nyumba ambazo zinajengwa nje ya utaratibu zinakuwa nyingi na zimepoteza hadhi na mandhari nzuri ya miji na kusababisha wananchi wengi kuingia katika migogoro isiyo na ulazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kuzungumzia *Land Rent* inayotozwa na Serikali. Serikali Kuu imekuwa na utaratibu ambao unaziumiza sana Halmashauri zetu, hasa kwa walipaji wakubwa, kwani fedha zote huwa inakwenda kwenye Serikali kuu, Halmashauri husika hazifaidiki na lolote pamoja na vijiji husika. Mfano, kodi zinazolipwa na *Mufindi. Paper Mill (MPM)*. Maeneo yanayomilikiwa na Sao *Hill*. Serikali itoe tamko kwamba sasa ni wakati muafaka kuhakikisha sehemu ya kodi hizi zinabaki katika maeneo husika ili kuboresha maisha ya wananchi husika waliopo kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa unyonge kabisa, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kikao chetu kinaendelea, sasa nitamwita Naibu Waziri aanze kutoa majibu ya hoja.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi juu ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwa dhati kwamba, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kushiriki katika kikao hiki muhimu kinachojadili hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kushika wadhifa wa Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Nitumie pia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na napenda kuwahakikishia kuwa tutafanya kazi pamoja hadi kaulimbiu yetu ya “Nuru Mpya na Matumaini Mapya kwa Ustawi na Maendeleo ya Taifa letu” imeyakinika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mama yangu Naisiligaki Ngilisho Laiser ambaye wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu aligeuka kuwa mhamasishaji maarufu sana akihimiza na kusihi vizazi vyote kuchagua kiongozi atakayewaondolea kero zinazowakabili katika jamii. Vile vile namshukuru sana mke wangu mpendwa Antonia Kalist Lekule, watoto wangu Renalda, Naisiligaki, Maureen na Nariku Joan Josephine na Gregory Long’amuno pamoja na familia yote ya Ole Medeye. Pia Viongozi wa CCM Wilaya ya Arumeru hadi Taifa kwa kuniunga mkono kwa dhati hadi kupatikana kwa ushindi wa mafiga matatu katika Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilibahatika sana niliporipoti Wizarani kuanza kazi, niliwakuta ndugu ambao walinipokea na kunipa ushirikiano wa kila namna na kunielekeza mambo ya msingi ili niweze kutekeleza wajibu wangu. Katika hili namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mbunge wa Muleba Kusini kwa uongozi wake mwema kwani nakiri kuwa, hunishirikisha kila jambo analopanga kutekeleza katika Wizara na hivyo kunifanya kuwa *partner* katika usimamizi wa Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa kwa ushirikiano mkubwa anaonipa hata kabla ya kuweka kiapo cha kazi yangu na kuanza kazi hadi sasa. Nampongeza sana kwa kusimamia vema misingi ya utawala bora katika Wizara bila kujali vitisho anavyopata kwa kusimamia kweli daima. Napenda kumhakikishia ushirikiano wangu

wakati wote katika jitihada za kujenga timu ya ushindi dhidi ya kero kwenye Sekta ya Ardhi Namshukuru pia Naibu Katibu Mkuu Bi. Maria Bilia, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kuwa Walimu wangu hadi kuniwezesha kuiva na kuwa mmoja wa Watendaji wa sekta hii muhimu katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namshukuru sana msaidizi wangu Ndugu Godfrey Machabe, Katibu Mahsusi Bi. Khadija Karambo, dereva wangu Bwana Renatus Temba na wasaidizi wangu wote wa Jimbo wakiongozwa na Bwana Julius Makara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitumie fursa hii kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana wewe na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu kwa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Anne S. Makinda Spika wa Bunge letu kwa jinsi ambavyo amekuwa akituongoza. Naomba Mwenyezi Mungu apende kuwabariki ninyi nyote na kuwazidishia upendo kwa jamii yote na hususan sisi mnaotuongoza ili kwa pamoja tufikie dira ya Bunge letu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia ili kuboresha utendaji wa sekta yetu. Nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kufanya kazi nasi wakitupa ushauri na kutukosoa bila woga kwa nia njema ya kutaka kuboresha utendaji wa Wizara na Taasisi zake ili kufikia malengo ya sekta yaliyoainishwa kwenye Dira ya Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2011/2012 - 2015/2016 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Wizara yetu wametuonesha vibanzi vilivyo ndani ya macho yetu na hivyo tumepokea maoni yao kuwa changamoto na tutayafanyia kazi ili kurekebisha kasoro zote zilizoelezwa. Tunashukuru kwamba wametuunga mkono kwani tokea tuanze kazi sehemu kubwa ya muda wetu umetumika kutafuta chanzo cha kero zilizopo ikiwemo adui mkubwa wa maendeleo ya Taifa letu ambaye ni rushwa. Jambo muhimu ninalowaomba ni kutambua kuwa ugonjwa uliokomaa haung'oki kwa siku moja bali unahitaji muda wa kutosha kujua asili yake, msingi wake ulipojengwa na kisha kutafutia dawa sahihi. Jitihada tunazofanya zinahitaji mchango wa jamii nzima ya Watanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ndipo tutafanikiwa. Tunaomba sana mtupe muda ili tujipange ipasavyo kuondoa ugonjwa mlioueleza katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kuwa Waheshimiwa Wabunge wametambua kero zinazotukabili na kupendekeza namna ya kuzitatua. Napenda kuwahakikishia kuwa mapendekezo yote waliyoyatoa, tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo. Sasa kwa kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wametoa, kwanza, napenda kusema kwamba, haitakuwa rahisi kwetu sisi kujibu hoja zote tulizopokea kwa maandishi na kwa kusema katika kikao hiki, lakini napenda niwahakikishie kwamba tutatayarisha majibu yote kwa maandishi na kuwapelekea Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa mfano, kuna migogoro ya mipaka ya Vijiji, Wilaya na Mikoa. Tumepokea hoja zilizotolewa juu ya mgogoro uliopo kati ya Wilaya ya Kongwa na Kondoa, Wilaya ya Kondoa na Kiteto na naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba katika migogoro yote ya mipaka ya Wilaya, Vijiji na Mikoa tutashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba kasoro hizo za mipaka zinawekwa sawa ili wananchi waweze kushiriki katika shughuli za maendeleo pasipo kugongana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, tuna masuala ya mipango miji. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la mipango miji, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema amezungumzia suala la Mji Mdogo wa Himo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda amezungumzia

mgogoro wa ardhi unaotokana na kasoro za Mipango Miji katika Mji wa Morogoro na Mji wa Arusha. Pia kuna mgogoro katika Mji wa Mwanza ambao umezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza, tumepokea pia maelezo juu ya mgogoro katika Mji wa Tanga na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba kwanza, kuhusu viwanja vya wazi vimevamiwa. Kama alivyokuwa ameeleza Mheshimiwa Waziri kwamba tulianza na tulipoanza ni kweli kwamba tulikuta kuna migogoro ambayo ilikuwa inahitaji kushughulikiwa kwa haraka sana na ndiyo ile ambayo tulichukua. Kuna kiwanja kilichopakana na *Aghakhan,* kuna kiwanja kilichopakana na hoteli ya *Palm Beach,* kuna kiwanja kingine *Mbezi Beach* kwenye ufukwe wa Bahari ambapo kuna Bwana mmoja alijitwalia akajijengea na maeneo yale yote tuliyabomoa, tulivunja maendelezo yaliyokuwa yamefanyika na kuyaweka wazi. Tuna kiwanja kimoja Mivumoni ambacho kulikuwa na mtu amejitwalia na kuanza maendelezo, nacho hicho tumekirejesha kinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunachofanya na ni jambo ambalo tumewaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba tushirikiane kwani sisi peke yetu hatutaweza. Tunaomba tushirikiane na wananchi na Waheshimiwa Madiwani wa miji yote na hili ndilo ombi letu sisi, mtupe orodha ya viwanja vya wazi vilivyovamiwa katika miji yote na sisi kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 ambayo inakataza kubadilisha matumizi ya maeneo ya wazi kufanya shughuli nyingine yoyote ile tutachukua hatua ya kurekebisha kwa kuondoa maendelezo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala ya Shirika la Nyumba, tunashukuru sana kwa Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamechangia hoja juu ya Shirika la Nyumba kwa pongezi walizotupa sisi pamoja na uongozi wa Shirika. Tunasema ahsante sana, yote yamewezekana kwa sababu ya ushirikiano mliotupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema mfano, mliouona wa kasi ya maendeleo yanayotokea hivi sasa katika Shirika la Nyumba ndivyo tunavyotaka kubadilisha Wizara. Ukitaka kubadilisha chombo unabadilisha utamaduni wake kwanza, lazima *attitude* ya watu ibadilike ndani ya shirika hilo, vivyo hivyo, katika Wizara tunabadilisha *attitude*. Kwanza watumishi watambue kwamba, wateja si watumwa wao bali wao ndiyo watumishi wao. Watumishi wapo Wizarani kwa sababu ya wateja, kwani wateja ndiyo waliowaajiri na kwa hiyo ni lazima wawapigie magoti, wawapokee wanapoingia ofisini.

Waheshimiwa Wabunge ambao wamebatika kututembelea Wizarani, mfano ambao huwa natumia kuwapokea ninyi ndivyo ambavyo nataka watumishi wote nao wafanye kwa wateja wao wanapowatembelea na tumeanza kuwaelimisha juu ya hilo. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa ushirikiano ambao tumeupata ili kuweza kuboresha Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hoja za Wabunge wa Dar es Salaam kwamba mwaka 2009 kuna ahadi kwamba wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba watauziwa nyumba. Serikali ikiweka ahadi maana yake ni kwamba inasimama. Ninachoomba ni kwamba suala hili linachukua muda kwa sababu linahitaji kupanga taratibu za utekelezaji wa maamuzi yote yale. Tunachoomba ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam baada ya mkutano huu wa Bunge tutakutana pamoja nanyi na Viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam ili kwa pamoja tuamue kwamba tunatekeleza vipi sera ya kuuza nyumba za shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi holela. Tumepokea michango ya maandishi ikilalamikia ujenzi holela Mbeya na karibu miji yote imelalamikiwa kwamba kuna ujenzi holela ambapo ni suala ambalo tunakiri kwamba, ni kweli lipo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba tutashirikiana na MKURATIBA ili kuweza kurasimisha pale ambapo pamejengwa holela yaani hapajapimwa ili tuweze kupima maeneo yote yale na kuweza kuboresha makazi yale kwa sababu kwanza ni kwa manufaa ya wananchi wanaoishi katika eneo hilo kwa sababu unapokuwa umetengeneza eneo kwa kupima na hivyo kuweka njia za kupitisha magari na watu inaongeza huduma kwa wananchi hawa. Serikali inaweza kutoa huduma za dharura kama zimamoto na nyinginezo za uokoaji inapokuwa mji umepangwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hili tutashughulikia kwa kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais MKURABITA ili kuhakikisha kwamba miji yetu inakuwa bora na salama zaidi. Lakini tutambue kwamba hii yote ina gharama yake ambayo sisi wenyewe peke yetu hatutaweza kumudu. Kwa hiyo, tunaomba ushirikiano wenu ili Halmashauri ambazo ninyi ni Madiwani watenge fedha ili tuweze kwa pamoja kushirikana katika kutekeleza miradi ya uboreshaji wa miji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la vifaa vya ujenzi kwamba Waheshimiwa Wabunge wameomba ipunguziwe kodi ili kuweza kushusha gharama za ujenzi. Suala hili tumelipokea na tutaliwasilisha kwa Wizara inayohusika yaani Wizara ya Fedha ili Serikali kwa pamoja tuweze kuona ni jinsi gani suala hili litashughulikiwa bila kuathiri utekelezaji wa shughuli nyingine za maendeleo zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niseme kwamba suala la ukosefu wa vifaa vya upimaji na watalaam lililozungumziwa na Wabunge wengi tumetambua. Ni kweli tumesema na namshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani alitukumbusha kwamba tuna upungufu mkubwa wa watalaam katika sekta yetu jambo ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumzia katika hotuba yake kwamba, hadi sasa hivi idadi ya watumishi tulionao wanafikia 26% ya mahitaji ya nchi nzima. Kwa hiyo, tuna upungufu mkubwa. Tunachofanya hivi sasa tunajaribu kuiomba Serikali kwamba wahitimu wa Vyuo vya Ardhi wawe wakiajiriwa moja kwa moja toka vyuoni ili kupunguza pengo hili lililopo kwa sababu ni kubwa sana na migogoro mingi tuliyonayo katika sekta ya ardhi inasababishwa na watumishi ambao hawana utaalam au unakuta kwamba yuko mtaalam mmoja ambaye ana fani fulani anafanya shughuli za fani nyingine ambayo hana utaalam nayo. Hiyo ndiyo moja ya vyanzo vya migogoro ya ardhi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba yapo maombi ambayo tuliyapokea siku za nyuma na hata wakati huu wa Mkutano wa Nne kwamba, tutembelee kwenye Majimbo yenu ili kuona hali halisi na kutatua kero zilizopo. Napenda niwahakikishie kwamba maeneo yote ambayo niliahidi kwamba tutakuja, basi tutakuja ili tushirikiane nanyi pamoja katika kutatua kero zilizopo, migogoro ya miji kwa mfano Jimbo la Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akitukumbusha karibu kila wakati. Jimbo la Musoma Mjini tumekuwa tukikumbushwa mara kwa mara, Tarime tunakumbuka, pia kwa Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema ametuomba sana twende tukamsaidie pale kwake Vunjo, tutakwenda. Kule Mbeya pia katika Mji wa Mbeya na Iringa, Jimbo la Mufindi Kusini. Tutakuja maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametuomba twende ili tushirikiane kwa pamoja ili tuweze kutatua kero hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye kwa mchango wako, nakushuruku sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuwepo hapa leo kwa ajili ya hoja hii muhimu sana kwa Taifa letu. Lakini nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii angalau niweze kusema mawili, matatu si kwa maana ya kutaka kujibu hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao kwa namna moja au nyingine wamenihusisha na baadhi ya maeneo, lakini kutaka tu kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata nafasi ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wengi na naweza nikasema michango yao ni mizuri sana, imegusa maeneo karibu yote ambayo ndio kero hasa kwa Watanzania. Lakini suala la ardhi lazima tukubali ni suala kubwa na linatugusa wengi na msingi wake ni kwa sababu wananchi wengi wako katika maeneo ya vijiji, zaidi ya asilimia 80 tuko vijijini na hata kwa maana ya ardhi ilivyogawanywa utaona kwamba ardhi ambayo ni mali ya vijiji ni karibu asilimia 70 ya ardhi yote tuliyonayo. Maeneo ya hifadhi

yanachukua kama asilimia 28, asilimia mbili zinazobaki ndio maeneo yale ambayo tunaweza tukasema kama ya Serikali. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa suala la ardhi lazima kama Wabunge tulizungumze na kwa kweli tuliwekee msimamo hasa katika maeneo yale ambayo ni ya msingi kwa sababu ndio msingi wa maisha ya Watanzania walio wengi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingi wala sio hofu, hapana, michango mingi iliyotolewa ni kuitaka Serikali itambue tu kwamba, ninyi mnavyoona mnatamani na sisi tuone hivyo hivyo. Ndio maana nimesema michango ni mizuri na mimi napenda niamini kabisa kwamba tumemsaidia kwa Waziri kwa kiasi kikubwa nadhani sehemu kubwa atakuwa na maelezo mazuri, lakini hata pale atashindwa kwa sababu ya muda naamini atatoa maelezo mazuri sana mmoja mmoja kulingana na hoja iliyokuwa imetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo la kisera ambalo nimeona hasa ndilo limenifanya nikaona nisimame nalo ni la uwekezaji katika eneo hili linaitwa ardhi. Nimepata nafasi ya kwenda kutembelea pale Kiwanda cha Sukari Moshi (*TPC*). Nikaondoka nikaenda Kagera, nimeona jitihada zinazowekwa pale katika kuwekeza kwenye eneo lile katika suala la sukari. Mimi binafsi nilifarijika sana, nimeona kwamba uwekezaji huu mkubwa katika maeneo ya ardhi unaweza ukawa ni ukombozi mkubwa sana kwa Watanzania. Viwanda vile vinatoa sukari angalau mchango kiasi fulani kwa ajili ya mahitaji yetu hapa nchini, vinginevyo tungelazimika kuagiza sukari yote kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimekwenda pale nimefaidika sana kuona kwamba hata ajira pale ipo, wako Watanzania wameajiriwa pale kutokana na uwekezaji ule ulivyo na nilipokuwa pale Kagera nilifarijika sana. Nimewakuta pale vijana ambao ndio wanasimamia kilimo kile cha miwa, ni vijana kutoka *SUA*. Wako Wahandisi pale, wako watu wa *Surveys,* utakuta vijana pale karibu 50, wote ni *product* ya *SUA and they are doing a very good job.* Kwa hiyo, nikaona hili jambo ni jema, kubwa ni kujipanga vizuri tuhakikishe uwekezaji huo unakuwa wa manufaa kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni kweli inatofautiana kati ya eneo na eneo. Nimekwenda Lushoto kule, nimekwenda maeneo ya Njombe yale, sehemu nyingine unakuta kwa kweli ardhi ni *issue* kubwa ni suala kubwa, ardhi haitoshi, nimetembea Mkoa wa Kilimanjaro, ardhi haitoshi na ndiyo maana miaka ya nyuma Serikali iliamua kusema nyie Wachaga kwani lazima mng'ang'anie huko Kilimanjaro njooni Mpanda na waliosikia walihama, wakaja Mpanda na wakapata maeneo mazuri tu, wameishi kule mpaka leo wengine bado tunao. Kwa sababu hoja wakati ule Baba wa Taifa ilikuwa ni kwamba maeneo mengine, mpende msipende ni madogo mno hamwezi yakatosheleza mahitaji yenu. Lakini kuna maeneo bado yako wazi, ruhusa mwende huko. Tukaenda mara ya mwisho nilifurahi sana tulikuta Mchaga mmoja alikwenda akafia Moshi akasema kwamba nataka nizikwe Mpanda Mwese, nikawaambia eeh mabadiliko makubwa hayo. Kwa hiyo, nchi hii ni moja, kwa hiyo Watanzania ni lazima wajisikie huru kuishi mahali popote ili mradi hawavunji sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa nia njema kabisa kwamba hamwezi mkawa na hekta milioni 44 za ardhi nzuri ya kilimo ninyi Watanzania mnalima *hardly 20 percent.* Kama asilimia 20 tu, kati ya hizo tuna hekta karibu milioni 30 ambazo ni za umwagiliaji maji. Watanzania tunalima asilimia moja ni hekta 300,000, sasa ndio maana nafika mahali nasema sawa tulizungumze hili, lakini tusije tukafanya makosa ya kuogopa kuwakaribisha watu katika maeneo ambayo bado yana fursa ya kuweza kuwekezwa. Acheni watu waje wawekeze, kubwa kama Serikali tujipange vizuri tuweze kunufaika na mipango hiyo kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda pale Morogoro juzi yuko mkulima mmoja pale amewekeza Mngeta. Nilipokwenda kumtembelea miaka miwili iliyopita nilikuta amezalisha tani 2,500 za mpunga. Juzi nimekutana naye anasema mwaka huu nimezalisha tani 13,000 za mpunga. Ameweka Kiwanda pale cha kukoboa kinafanya upembuzi, kinafanya *packaging* na anaweza akauza mpunga ule na sehemu nyingine tukautumia hapa nchini. Lakini nikamwuliza je, wale Watanzania niliowakuta pembeni pale umewasaidiaje? Akasema nimejitahidi sana kwa sababu tangu tulivyozungumza naye akasema ndio jukumu Lake. Kwa hiyo, wakulima pale zaidi ya 3,000 na wenyewe sasa wameingizwa katika ule mpango wa kusaidiana na huyu bwana ili na

wao wapate soko la uhakika kwa sababu wanatumia mbegu bora, wamesaidiwa vile vile *inputs* mbalimbali, wamesaidiwa hata katika kusafisha yale mashamba, itategemea mnataka mwekezaji awasaidie katika nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaombe Watanzania kwamba eneo hili ni suala la kujipanga tu vizuri. Lakini la msingi zaidi kwa Watanzania na ambalo kwa kweli kama Watanzania tunatakiwa tuipongeze sana Serikali kwa kutokuyumba katika hili. Ardhi ya Tanzania ni mali ya Serikali ni mali ya umma. Uwe nani, uwe nani utapewa ile ardhi kwa masharti kwamba unaiendeleza na si vinginevyo. Ndio maana mfumo wetu ni ule ambao unaitwa ni wa *lease,* ni wa kukukodisha kwa miaka 33, 66 au 99 na kadhalika. Katika kila hatua lazima tukupime, je, unaendelea kutimiza wajibu wako au hapana, hukutimiza mali ile ardhi yote inarudi mikononi mwa Serikali. Ndio maana Rais ataendelea kuwa ndio *custodian* wa ardhi yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nendeni tu nchi jirani hapo mkaone, wenye mfumo wa umiliki wa ardhi kwa asilimia mia moja. Wako watu pale wanamiliki ardhi kubwa tu. Nendeni Namibia, Afrika ya Kusini, Zimbabwe kulikozua mzozo ni kwa sababu mtu mmoja kwa mfumo wa kitu wanaita *freehold* ukishapata ardhi ni yako na unaweza ukafanya lolote na hiyo ardhi. Sisi hapa Chama Tawala, Serikali yake wamesema piga, geuza ardhi itabaki ni mali ya Serikali. Hiyo peke yake inapaswa kama Watanzania kutupa *comfort* kubwa kwamba mwisho wa yote hakuna mmiliki wa milele na milele na msije mkasahau huko nyuma tulikuwa hata na ukodishaji wa miaka 999 na Serikali hii ikasema haiwezekani miaka 999 unatafuta nini? Ndio kisa cha kutoka miaka 999 mpaka miaka 99. Wenzetu huko ni holela, ukishapata ndio basi, sisi hapa tumesema hapana. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo jema na lazima tuendelee kulienzi na tuhakikishe hakuna mtu atakayekuja akatutoa katika msimamo huo. Lazima tuendelee kulinda na tuheshimu sana hii tunu ambayo tumesaidiwa na waliotutangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi kwa vyovyote vile ni lazima uwe ni mtaji kwa Mtanzania. Sasa unafanyaje ili uwe ni mtaji, hiyo ndiyo kazi ambayo mnaona Serikali kwa sasa tunaifanya na lengo kubwa bado atakuwa ni mkulima mdogo. Naona tunapoteza nguvu nyingi tunatembea kweli kweli kujaribu kujibu hii hoja unafanyaje ili huyu Mtanzania mdogo ardhi iweze kweli kumnufaisha. Ukifika hapo ni suala la tija, ardhi ndogo lakini yenye tija. Ndio maana jamani nendeni kote Ulaya, kilimo sasa kimebaki kinaendeshwa na asilimia kumi, kumi na tano au tano, ndio wanaolisha asilimia nyingine yote inayobaki. Mimi nasema *Inshallah* naamini tutafika hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja tuliyonayo sasa ni ya umaskini tu na naamini ni ya mpito hamwezi mkawa na watu asilimia 80 wanahangaika kulisha asilimia 15 ni aibu. Lakini yote ni kwa sababu tija ndogo, uwekezaji mdogo, kwa hiyo lazima tulione hili kwa mtazamo chanya kwa sababu nafikiri ni jambo jema na lazima wote twende nalo. Vinginevyo nilitaka tu nimwombe Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wengine wote tusikae tunanung'unika juu ya watendaji wabovu kwenye Halmashauri. Hapana yatakuwa ni makosa yetu sisi wenyewe. Hakuna Waziri anayekatazwa kwenda kwenye Halmashauri yoyote ile awe wa Ardhi kwenda Mpanda, Nkasi, Kilimanjaro, nenda kazungumze na wataalam wote pale pamoja na Wakurugenzi wengine, foka kadri utakavyoweza na ukipewa maelezo ya kutosha kwamba huyu hafai wewe mtimue, wewe si ndio Waziri. Usinung'unike, wewe fanya hilo mengine yatafuata baadaye. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Wizara ya Ardhi wote tunaijua ina matatizo chungu nzima na wakati mwingine Madiwani pale hawana uwezo, uelewa pengine mdogo wewe Waziri umekwenda mwenye sekta nenda kalizungumze, chukua hatua bila ya kuchelewa kwa sababu ni mtu wako bado. Afisa Ardhi yule sijui niseme nini sio *property* ya TAMISEMI, yule ni mtumishi wa Serikali. Kwa hiyo, matumaini yangu ni kwamba Mawaziri wenzangu huku hili mtalibeba kwa namna ambavyo Wabunge wangetamani sana mfanye. Nendeni mkatimize wajibu wenu kule foka, chukua hatua ili mradi unamfokea mtu ambaye unajua yuko chini yako mambo utaona yatakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nitumie hizi dakika kidogo kuhusu eneo hili kwa sababu ni la msingi sana kwangu. Lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Mama Anna Tibaijuka ni mama mwenye uwezo mkubwa kabisa. Namfahamu, nimeshirikiana naye hasa

alipokuwa Nairobi, najua uwezo wake na hata wakubwa waliokuwa naye wanamfahamu kiuwezo. Ndio maana nimefarijika sana na maelezo yake kwenye hotuba amekuwa muwazi, ameonesha changamoto zote ambazo amezibaini kwenye Wizara, lakini ameweka vile vile mikakati ya namna ya kushughulikia. Tumpe nafasi, tumpe muda, ana uwezo mzuri sana na najua ataweza tu. Amepata bajeti ndio ndogo kuliko hata ya mwaka jana, tatizo ambalo karibu Wizara zote hapa zimepambana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema hivi, jana tukiwa kwenye *Cabinet* tumemuidhinishia huyu mama kwamba wewe mama ile fedha yote ambayo utakuwa unakusanya kutokana na shughuli zako za ardhi baki nayo yote, chukua yote ikusaidie wewe katika uendeshaji wa Wizara hiyo. Kwa hiyo, tunatambua changamoto alizonazo na naamini tutamsaidia vizuri sana na najua ataweza. Kwa hiyo nataka nimwombe sana ndugu yangu Nyerere pale maana alisema wewe mama achia ngazi, hapana. Mpe nafasi kidogo miaka mitatu, minne utaona tu mambo yatanyooka vizuri sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako masuala mengine mazito mazito mengine nimeyasikia atayazungumza mama, lakini naomba mimi kama Waziri Mkuu, niyasemee kidogo hasa hili la Kigamboni na maeneo mengine hasa Dar es Salaam ina pilikapilika nyingi sana. Nataka nichukue tu dhamana kumsaidia Waziri. Kwa ukubwa wa matatizo ya ardhi yalivyo sisi tutakachofanya ni kumsihi tu pengine baadaye tukipata nafasi Wabunge wale wote wa Dar es Salaam si vibaya tukakaa pamoja. Hebu tulizungumze hili jambo tuone matatizo yalivyokaa, tuone tunaweza tukafanya nini kupunguza matatizo yanayozunguka masuala ya ardhi katika Mji wa Dar es Salaam. Dar es Salaam ni eneo dogo ndio maana mnaona tunagombana kweli kweli, tusipojipanga vizuri haitatuletea amani hata kidogo. Kwa hiyo, niko radhi na nitamwomba na Waziri naye alipe uzito nadhani tukikaa pamoja na Wabunge hawa tunaweza kabisa tukalimaliza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, basi niseme kidogo sana juu ya suala hili la Mpanda na uwekezaji wake. Mimi natoka Mpanda, naomba ku-*declare interest*, lakini sitoki Mpanda tu, mimi ni mkereketwa mkubwa sana wa maendeleo ya Mpanda na Rukwa kwa ujumla. Eneo ambalo linazungumzwa hili la Katumba liko Jimboni kwangu, wale ni wapiga kura wangu wanaozunguka eneo lote lile la Katumba, kwa hiyo, nikimsikia mtu analisema kwanza namsikiliza tu, hivyo ananisaidia nini pale hasa, maana mwenye Jimbo ni mimi hapa. Kwa hiyo, nikiona mchango anaoutoa ni wa kuniondoa katika mawazo niliyonayo na mimi nasema aah bwana kama kufa acha tukafe huko huko. *(Makofi)*

Jamani Mkoa wa Rukwa na Kigoma, mikoa hii ya pembezoni tuko nyuma kweli kweli. Si kwa barabara hata kiuchumi pamoja na kwamba sisi ndio tunazalisha na kulisha karibu Tanzania yote hapa, lakini ndio watu ambao tuko nyuma kweli kweli. Nashukuru tu wengine mmeelewa kidogo hata tulipozungumza vilamilami pale mkatuelewa, mkoa mkubwa kama ule unatoa tija ya chakula eti unakwenda pale unakuta mkoa mzima tuna lami kilomita 10 sijui 12 tena za kwenye vidaraja tumeunganishiwa unganishiwa hivi, mtu hakuelewi, hakuelewi kabisa. Kigoma ile ndio juzi tu nyota imeanza kuwaka, vinginevyo *western corridor* yote ile ilikuwa haina kitu, lakini ndio chimbuko na msingi wa uzalishaji. Tulichofanya sisi Kigoma na Rukwa ilikuwa ni kukaa pamoja tukaulizana uamuzi wa Serikali wa kuwataka Warundi warudi kwao umeshafanyika. Lazima warudi hata ingekuwaje lazima warudi kwao, kwa sababu amani imesharudi pale, demokrasia sasa tunaona inang'arang'ara, mnakaa kaa hapa mnangoja nini? Tukasema mrudi kwenu imetosha.

Kwa hiyo, mtihani uliofuata ni tunatumiaje maeneo sasa waliyokuwa wanaishi? Ndiyo swali tulilokuwa tunaulizana. Halafu tumekaa pamoja, tumezungumza kweli kweli na mwisho ndiyo tukaanza kupata haka kamwanga kidogo kwamba kuna watu wanataka kuwekeza katika kilimo Lugufu pale Kigoma, pamoja na ukubwa wa Lugufu, karibu hekta 25,000. Lakini Mkoa umesema hapana, tutawapeni hekta 10,000. Fanyeni *study* yenu pale, tutakapofika mwisho tutaelewana kama mnahitaji zote au hapana. Sasa hatua waliyofikia na wao siyo mkataba ambao mama pale alikuwa anazungumza. Ni makubaliano ya awali. *Memorandum of Understanding (MoU),* tena Kigoma wamesaini juzi tu. Afadhali hata sisi Mpanda tuliwahi. Mpanda tulichofanya ni *MoU* tu, nikamsikiliza dada pale anasema iko *document*. Iko wapi hiyo ambayo Mbunge siijui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mkataba wowote ambao tumeingia kati ya *Agri Sol Energy* na mtu mwingine yeyote. Hakuna. Mimi vikao vingi wakati mwingine ndiyo nilikuwa naamua kuwa *chairman,* lakini lengo langu ni moja tu, kwamba tuone kama na sisi kwenye ukanda huu tunaweza tukapata wawekezaji katika eneo hili la ardhi. Ndiyo hicho tu tulichokuwa tunakitafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kutazama ile *MoU* pale Mpanda tumesema waziwazi, fanya hatua zote za kutafiti juu ya ardhi, ubora wake, tukishafika mwisho tutakaa tukubaliane na wewe tukupe eneo kiasi gani. Naona Mheshimiwa Halima Mdee anatikisa kichwa, labda kama ana *MoU* tofauti na mimi, *I would be happy* kuipata hiyo. Kwa sababu *MoU* niliyonayo mimi ndivyo inavyoniambia hivyo tangu mwanzo. Tumesema kwamba katika zoezi hili kama tutafanikiwa kufika mwisho, hatuna ujanja, lazima twende kwa Waziri wa Ardhi kumshirikisha kwamba sasa tumefika mahali pazuri na tumeona ziko dalili za makubaliano, tunakuja kwako. *TIC* hatuwezi kumkwepa. Masharti yote yanayotakiwa kufuatwa yatafuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ardhi ambayo tumekaa mnatu-*accuse* tumeuza, tumefanya nini, iko wapi? Siyo hilo tu, tumeeleza wazi kwenye *memorandum* hata ingekuwaje hatutaruhusu mtu kuanza kuwekeza pale kama bado wale Wahutu watakuwa hawajaondoka. Mpaka mtu wa mwisho atakapokuwa ameondoka, ndipo tutaingia katika utaratibu wa kuanza kutumia ardhi ile. Sasa hili linatoka wapi? Sisi watu wa Rukwa na Kigoma tumetenda dhambi gani? Ninyi mna mashamba ya miwa huko, mmewekeza, mna mashamba sijui ya nini mmewekeza, mimi kutumia ardhi ile kwa nia njema, sasa inageuka inakuwa nongwa? Watu wamewekeza miti aina ya miwati huko, mnalima miti sijui wapi, mimi nikipanda miwati tu pale kupitia kampuni nongwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tuwe wakweli tu katika mambo ya msingi kama haya. Naomba sana tusije tukafika mahali mkaamua kufukuza watu bila sababu, mtu ukaanza kuwatukana watu wenyewe hata bado hawajakwenda popote. Mwisho wa safari, bado. Tupeni nafasi watu wa Kigoma na Rukwa tutende wajibu wetu, mje mtushtaki kama mtaona tumekosea na mimi nataka niamini hatukosei ng'o na utaona mafanikio yatakuwepo makubwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Niliona na mimi nichangie kidogo mawazo yangu kwa lile la kisera, lakini kubwa ni hili la kwangu maana lipo Jimboni kwangu. Nikasema nikitoka hapa bila kusema neno dada yangu Halima pale atasema, unaona, Mheshimiwa Waziri Mkuu nimem-*fix* na ni kweli. Mimi nasema siyo kweli. Sasa labda mwende mkalianze tena upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kusema mawili matatu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Nakushukuru sana kwa ufafanuzi huo. Kwa hatua hii sasa naomba nimkaribishe Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka. Karibu sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote na mimi naomba nichukue nafasi hii tena kwa mara nyingine kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa vile alivyonijalia kwamba baada ya kurejea nyumbani wananchi wa Muleba popote pale mlipo mkanisimamia na kusema kweli katika kushukuru ninapofikia hatua hii, sina budi nitoe shukrani kwa wale waliolipa gharama za kazi hizi tunazozifanya, kazi za utumishi wa umma iwe ndani ya nchi au nje ya nchi.

Kwanza kabisa, naomba nimkumbuke mama yangu mzazi Mauleria Kajumulo pale alipo, alikuwa anaumwa. Vile vile nimkumbuke Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mama Salma Kikwete walipokuja kumwona juzi juzi pale hospitali, mama akaniambia unajua mwanangu, ninaumwa sana, lakini nadhani kwa kuwa na huyu baba unayemfanyia kazi amekuja, nadhani nitapona. Kwa hiyo, mama nakupa salamu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru viongozi wote wa Chama Cha Mapinduzi walionipa nafasi nikaweza kugombea Ubunge Muleba Kusini nikashinda na sina budi kutambua kabisa uongozi wa Muleba na kwa makusudi kabisa, ni lazima nimtaje Katibu wa CCM wa Muleba Bwana Wilbrod Msafiri, alinisaidia sana. Naomba niwashukuru pia kwa ukaribu kabisa watu walionisaidia katika kampeni. Wote mnafahamu kwamba nilikuwa mgeni kabisa na sikuwepo nchini takribani miaka 13. Kwa hiyo, niliporejea, walinisaidia nikaona yote yanakwenda vizuri. Sasa tunapokuja kwenye kazi ambazo nimepangiwa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye kiongozi wetu, mnaona kwamba anaendelea kunibeba na nashukuru kwa msaada na mchango ambao ameutoa sasa hivi. *(Makofi)*

Naomba niwashikuru Watendaji Wakuu, kwanza kabisa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, ni mtu ambaye tunafanya kazi kwa kiundungu, pale tumejenga kitu ambacho kinaitwa *team work* tunafanya pamoja. Kwa kweli ananipa nguvu zote ninazostahili, namshukuru sana. Katibu Mkuu - Bwana Patrick Rutabazibwa na timu yake ya Watendaji, kwa kweli wanafanya kazi ambayo mimi naweza kuipa *international rating.* Wanafanya kazi ambayo inatakiwa itambuliwe. Pale Wizarani mambo ni magumu, Mheshimiwa Waziri Mkuu kayafafanua sasa hivi kwamba tunajipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba yote kwanza kabisa nikiri kwamba mmenifariji sana, kwa sababu ningeshangaa kama mambo hapa yangeonekana kirahisirahisi, kwa sababu ni magumu sana. Ahsanteni sana kwa michango yenu kwa ujumla wenu. Kwa wale mlionipongez,a nawashukuru sana mimi na mwenzangu kwa kutambua kazi tunazozifanya. Lakini pia nataka kusema kwamba michango yote tumeipokea na sasa naomba niwatambue waliochangia kwa kusema hapa ambao ni Waheshimiwa Wabunge 23. Sina budi kabla sijaanza kujumuisha, nianze kwa majina kwa kuwashukuru sana.

Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Mary P. Chatanda, Mheshimiwa Abas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Mheshimiwa Antony G. Mbassa, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mheshimiwa Susan L. A. Kiwanga, Mheshimiwa Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye, Mheshimiwa Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki na Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa bila kumsahau Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hao ndiyo waliochangia kwa kuzungumza na sasa sina budi niwatambue Waheshimiwa Wabunge takribani 153 waliochangia kwa maandishi.

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Faith M. Mitambo, Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Lucy P. Owenya, Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mheshimiwa William A. Mgimwa, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mheshimiwa Rukia K. Ahmed, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi na Mheshimiwa Hawa A. Ghasia. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa Vick P. Kamata, Mheshimiwa Augustino L. Mrema, Mheshimiwa Sara M. Ally, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Mustapha B.

Akunaay, Mheshimiwa Mchungaji Israel Y. Natse, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Dkt. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu, Mheshimiwa Saleh A. Pamba, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Ally K. Mohamed, Mheshimiwa Mary P. Chatanda, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Naomi A. M. Kaihula, Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa David M. Mallole, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Daina M. Chilolo, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukwimba, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Antony G. Mbassa na Mheshimiwa Said Amour Arfi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Agness E. Hokororo, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage, Mheshimiwa Christina G. Ishengoma, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Dkt. Terezya P. L. Huvisa, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Selemani S. Jafo na Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa David E. Silinde, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Maryam S. Msabaha, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Zaynabu M. Vullu, Mheshimiwa Shukuru J. Kawambwa, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Zainab R. Kawawa, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Amina A. Clement Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Benedict N. Ole–Nangoro, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Vita R. M. Kawawa, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa John P. Lwanji na Mheshimiwa Margaret S. Sitta. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa John S. Magalle, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla, Mheshimiwa Shaffin A. Sumar, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mheshimiwa Josephine T. Chagulla, Mheshimiwa Subira K. Mgalu, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Susan A. Kiwanga, Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile, Mheshimiwa Rose K. Sukum, Mheshimiwa Chiku A. Abwao, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa kwa dhati, ninapanza hotuba yangu hii ya kujibu hoja zilizotajwa, kwanza kabisa kwa mara nyingine tena narudi kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, nikimtanguliza Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa ambaye aliiwakilisha Kamati na kutoa maoni ya Kamati ambayo sasa ningependa kidogo niyatolee majibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mambo mazuri ambayo wametushauri, nasema mazuri kwa sababu wachangiaji wengi katika suala zima la Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama ilivyosemwa, ni kwamba kwa kweli kwetu sisi tumepokea kila lililosemwa hapa kwamba kama ni jambo ambalo tulikuwa hatuna habari nalo, ni jambo la kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu mambo ambayo iliyabainisha na kutuelekeza, Serikali ilibidi itambue Sekta ya Ardhi kama sekta mtambuka ambayo kama haitapewa fedha za kutosha kila mwaka kama ilivyo sasa, Sekta ya Ardhi itakwamisha mipango ya sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni faraja kubwa sana kwangu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amelitangazia Bunge lako Tukufu kwamba kweli sasa hivi angalau bajeti yetu tayari tunasema kwamba tuna unakisi wa bajeti yetu. Kwa hiyo, tayari katika kitabu hiki, katika *budget speech*, hili suala na sisi tunalitambua, lakini na Serikali yenyewe inalitambua na tunasisitiza pamoja na kwamba siyo haba kama ikifanyiwa kazi, tunatambua kwamba bajeti hazitoshi. Lakini pia tuko ndani ya Serikali, tunatambua kwamba *budget cake* ni ndogo. Lakini pia tunatambua kwamba kinachohitajika na hapo ndiyo Sekta ya Ardhi, nyumba na makazi imejipanga.

Sisi tutahakikisha tunaleta *value for money*. Kile kidogo tulichokipata tutahakikisha kwamba kinatumika inavyohitajika. Maana siyo vizuri katika nchi zinazondelea wakati mwingine kutanguliza bajeti na fedha kuwa kubwa haimaanishi ufanisi ingawaje inasaidia. Lakini, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshawatangazia kwamba sasa Serikali imeamua kwamba tutakachopata, maduhuli tutakayopata yataelekezwa tena katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nashukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Kamati ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lembeli pia amelisimamia hili, na natoa shukurani zangu. Hata hivyo, kwamba sekta yetu ya ardhi ni mtambuka, nadhani ni jambo ambalo wengi mmelisemea, wengi tunalitambua na Baba wa Taifa mwenyewe, Muasisi wa Taifa, hili alisema kusudi nchi iendelee, kweli inahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Sasa mimi nafikiria kwamba sisi watu ambao tumepewa dhamana hii, hili tunalitambua, ni jukumu kweli tumelibeba kwamba tuna sekta ambayo Muasisi wa Taifa alitambua kwamba mambo ya ardhi yasipowekwa vizuri, basi hata na mustakabali unaweza kuwa ni wasiwasi. Kwa hiyo, naahidi kwamba Wizara imejipanga sasa. Katika kitabu hiki ambacho ni bajeti, lakini pia ni *strategic paper*, utaona kwamba inaanza na changamoto, lakini pia inasema umejipanga vipi kutatua changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kusema kwamba katika hili nilihakikishie Bunge lako Tukufu, niihakikishie pia na Kamati kwamba kwa kweli sisi tunatambua umuhimu wetu kwa sekta nyingine na tunaomba hapo hapo kwamba hili jambo pia litambuliwe. Kwa hiyo, suala la *retention* tumelimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inashauri Wizara kuongeza gawio kwa asilimia 10 na kufikia asilimia 30 katika Halmashauri. Sasa tu labda niseme kwamba, kwa kuwa sasa tumewezeshwa na *retention* ya asilimia 100, kwa hiyo, naomba nitoe rai sasa hivi kwa Wabunge wote tulio hapa, pia tuko katika Halmashauri mbalimbali. Kwa hiyo, sasa kitu cha msingi ni kwamba katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo kama mnavyojua haina ruzuku yoyote kutoka Serikali Kuu. Sasa basi tutakapokusanya, asilimia 30 ya sasa hivi, asilimia 20 ndiyo imepangwa kubaki pale. Lakini na mimi nasema hatuwezi kuwa wachoyo pale Wizarani, kwa kuwa na sisi tumeshapewa *preservation* ya asilimia 100. Basi naomba kusema kwamba nakubali hili na sisi tutaacha asilimia 30 pale kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, hili linakubalika kabisa.

Kwa hiyo, nitoe tu rai kwamba tukusanye basi. Lakini tutakapokusanya, hapo hapo nitoe kauli kwamba, nimesema kwamba Wizara yangu inafanya kazi kwa misingi ya *principle* ya *value for money*, yaani kile kidogo ulichonacho kiwe na tija. Kwa sababu unaweza kuwa na pesa nyingi lakini usikamilishe chochote. Sasa basi, kama Halmashauri na zenyewe zinapewa hiyo asilimia 30, tusije tena tukaanza kufukuzana huko tutakapoanza sasa kuona, haya kulikoni, asilimia 30 zimefanya kazi gani? Lazima bajeti ya Wizara yetu, kwa ujumla Serikali, lakini mimi nasisitiza kwamba inapokuja kwenye Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, fedha zitumike kama ilivyokusudiwa kwa sababu mtu atakayejaribu kupindisha hii, kwa kweli ajue kwamba atakuwa ameutafuta ugomvi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ianzishe kitengo cha elimu kwa umma na Wizara ikapitie kitengo hiki. Nakubaliana kabisa na maoni mazuri ya Kamati ya Ardhi. Wizara ina Kitengo cha Habari tayari ambacho tumekiweka juzi juzi katika jitihada nzima za kukiboresha. Tulikuwanacho,

tunakiboresha. Wizara itaendelea kuimarisha Kitengo hiki kwa kuajiri wataalam kama itakavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ishirikiane na Chuo cha Utumishi wa Umma – Magogoni, kuandaa utaratibu wa kuwaelimisha Maafisa Ardhi wa Wilaya namna bora ya utunzaji wa masjala. Hili nalo tunalipokea kwa moyo mkunjufu.

Kuhusu suala la elimu kwa umma, bajeti hii kimsingi fedha tulizonazo, nyingi zitajikita katika kuboresha tija, utendaji, maana yake ni *capacity building*. Lazima tuboreshe uwezo wa Watendaji wetu. Lakini labda na hapo hapo niseme, uwepo pia wa wafanyakazi wengine ambao tunafanya nao kazi kwa sababu tuko katika sekta mtambuka, katika kufanya kazi kwa ufanisi, kufanya kazi kwa weledi, kufanya kazi kwa maadili, tuseme sifa hizi, haziji hivi hivi, zinalelewa. Rais Mstaafu wa Kenya aliwahi kusema kwamba neno *corruption* siyo neno la Kibantu. Kwa hiyo, wakati mwingine tunapoambiwa *corruption*, lazima tuelewe kwamba tatizo hili pia linawakumba watu wengine mbali na sisi. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba suala hili la kujipanga kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa weledi ni kitu muhimu sana na fedha zitakazowekezwa pale zitakuwa kweli zimetuletea *value for money*, zimeleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, suala hili la Mji Mpya wa Kigamboni, Kamati imelizungumzia, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kalizungumzia katika Jimbo lake, amelizungumzia hapa, amezungumzia ofisini kwangu, amelizungumzia katika Mkutano wa hadhara tuliofanya kule Kigamboni. Nataka kusema kwamba katika bajeti hii, wananchi wa Kigamboni tuko pamoja. Mheshimiwa Ndugulile ametoa *deadline*, amesema itakapofika nadhani ilikuwa ni Juni, mwaka kesho. Lakini kidogo ametupa muda. Kimsingi, ametupa takribani miezi kama 11 kwamba tujiweke sawa kuyamaliza ya Kigamboni. Mimi naamini kabisa kwamba kwa kushirikiana na wadau wote Kigamboni, hili tunalifanikisha. Hatuwezi kurudi nyuma juu ya Kigamboni. Watu wa Kigamboni msife moyo. Mimi nilikuja, matatizo nayaelewa fika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ucheleweshwaji, labda nielezee kidogo. Tathmini ya Kigamboni pia imechelewa kidogo kwa sababu pia tumekubaliana katika Mkutano wetu wa hadhara kwamba tunarekebisha viwango vya tathmini. Sasa viwango vya tathmini ambavyo tulikuwa navyo kidogo vilikuwa chini. Kwa hiyo, inabidi sasa tuboreshe viwango, zoezi hilo linaendelea, karibu linakamilika, kusudi sasa tathmini zitakapotoka, watu waweze kupata bei ambayo ni nzuri zaidi. Misingi ya tathmini ambayo tumejiwekea, inayoandamana na misingi ya Ilani ya CCM ambayo inapigana na umaskini, maana sisi hapa tunapigana na umaskini, hatupigani na maskini, tunapigana na umaskini. *There is a difference, we are fighting poverty, we are not fighting the poor*.

Kwa hiyo, katika hali hiyo, tunahakikisha kwamba tunaleta tathmini endelevu. Tunaleta tathmini endelevu na hii kidogo inaleta ucheleweshwaji. Lakini tutakapokuja sasa Kigamboni, amini usiamini, tutakuja na nguvu kwa sababu Kigamboni nilipokuja pale mliniambia kabisa, mradi wenyewe utatekelezwa miaka 30, lakini wananchi wa Kigamboni walinipa mapendekezo wenyewe kabisa. Mheshimiwa Ndugulile tulikuwa wote, wakasema wenyewe wanataka wajue mustakabali wao. Eneo lote lile takribani hekta 6,500 ambazo ndizo zinatwaliwa kwa ajili ya mji mpya waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine tutazungumza nao, watakaopenda pia kuchukua hisa katika hiyo Kigamboni *Development Authority* ambayo tunaiunda na wenyewe itakuwa ni ruhusa kufanya hivyo. Lakini mimi naomba subira na pia naomba imani kwa sababu kusema kweli siamini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amenitangulia, yeye kaweka nguvu zake, na mimi nasema katika Bunge hili Tukufu kwamba pale hakuna mchezo. Ila sasa, subira yavuta heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kupanga mji mzuri kusudi na sisi tujione, Kigamboni ile ni lulu ya Taifa, tukiipanga vizuri, tutaweza kuwa na ajira pale. Tukijipanga vizuri, maana yake ule mji utakuwa na hoteli za kisasa, utaweza kuleta ajira kwa vijana wetu. Kuna Visiwa ambavyo viko karibu na Kigamboni. Kwa hiyo, ni lulu. Sasa lulu hii ya Taifa jamani mnajua, hata ukitaka dhahabu, kidogo lazima maumivu yanakuwepo. Lakini nataka kuwahakikishieni

wananchi wa Kigamboni, wale watakaokuwa wananisikiliza, lakini pia Bunge lako Tukufu hili mnaweza kuwapa habari kwamba la Kigamboni, kimsingi iko katika mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala kwamba Serikali izingatie umuhimu wa *sites and services.* Hapa pia Kamati inaelekeza katika jambo ambalo limezungumziwa pia na wachangiaji wengi. *Sites and services* maana yake ni miundombinu. Tayari mmeshasikia kwamba Shirika letu la Nyumba linapojenga nyumba siyo kwamba linapenda kuwauzia ghali, lakini inabidi lilipie gharama za kuleta umeme wa *TANESCO*, miundombinu, mifereji ya majitaka, na sasa hivi barabara. Vyote hivyo vinaingia katika gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la *sites and services* nimelizungumzia katika bajeti yangu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, mkalitafakari. Haka kakitabu ka bajeti kana vitu vingine ambavyo ni vipya na vitatusaidia kuondokana na matatizo ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia kwamba tunaanza mfumo wa *betterment fee*. Chini ya Sheria ya Ardhi ya Mipango Miji Na.8 ya mwaka 2007, *section* ya 70, unapopanga mji pia pale sheria ile inakuwezesha kuleta *betterment fee*. Nikachagua kwamba mpango wa mwanzo, *pilot programme* iko Makongo Juu. Makongo Juu, kwa nini? Mtu mwingine anaweza kusema ni-*declare conflict of interest*, mimi hapa ni mkazi wa Makongo Juu, lakini kwa hili ninajua kwamba nitaishia tu kuwa mwathirika kwa sababu ndiyo maana niliona hapa siyo *conlict of interest.*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza pia ukajikuta katika hali ambapo *initially* patakuwepo na machungu ya uzazi. Lakini kama mwanamama, naweza kusema kwamba bila miezi tisa ya mimba, huwezi kupata mtoto. Kwa hiyo, huyu mtoto lazima azaliwe na mtoto tunayetaka kumzaa, mimba tunayoibeba ni makazi bora, makazi endelevu. Hayawezi kuja hivi hivi, hayawezi kuja kwa *decree*, Mwenyezi Mungu peke yake ndiye alisema pawepo na Mwanga, pakawa na Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi wanadamu, ukitaka kitu kizuri, ukitaka uzuri, sharti kudhurika. *(Makofi/Kcheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hali hiyo, naomba Bunge lako Tukufu likubali, katika hili tudhurike kwa sababu nchi yetu ni nzuri. Nchi ya Mlima Kilimanjaro, Nchi ya Serengeti, Nchi ya *Lake Tanganyika*, *Lake Tanganyika* ndiyo Ziwa la pili *deepest* duniani, ina sifa lukuki. Lakini mtu anateremka mjini, anaangalia Jiji la Dar es Salaam linafanana kama uyoga. Kwa hiyo, inabidi tujipange upya jamani. Nawasihi mniunge mkono, tujipange upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la ukodishaji wa mashamba vizuri. Kwa hiyo, mimi sina haja ya kusema mengi. Ardhi ni mali, ndiyo tuliyonayo. Mwasisi wa Taifa alituambia; kizazi changu mimi tumelelewa na Mwalimu Nyerere, kwa sababu yule mtu alikuwa mzungumzaji, tunamsikia kwenye redio. Kwa hiyo kama uko kwenye rika langu mimi, utakuwa unamfahamu Mwalimu Nyerere kama vile ulikuwa unaishi naye kwenye nyumba kwa sababu ni mzungumzaji, unamsikia kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kati ya mambo ambayo aliyasema, na mimi nayakumbuka, alitoa changamoto za ardhi. Mwalimu Nyerere alisomea uchumi *Scotland*, alikuwa ni mchumi, alikuwa anaelewa anasema nini, hakusahau *capital*, maana sisi wachumi tunasema tuna *factors* nne za uzalishaji. Una ardhi, una watu, yaani ndiyo nguvukazi *(labour)*, una *capital,* ndiyo pesa na una *management*, ndiyo *organization*. Lakini yeye kwa makusudi aliacha pesa na akasema kwamba pesa siyo msingi wa maendeleo. Kwa sababu kama huna maadili, hata ukipewa bajeti kubwa, si inaweza ikaishia mfukoni! Kwa hiyo, katika hali hii, Wizara hii inajipanga kuboresha weledi, lakini pia ni Wizara ya kitalaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya mashamba yaliyobinafsishwa, matatizo ya migogoro ambayo tunaizungumza hapa, kila mgogoro uliokuwa unatajwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina wakati wa kutosha kwa muda ambao umenipa, nina kitabu hapa cha michango ya Wabunge na wengine najua mmeninunia mpaka nitoe tamko la Kijiji ‘A’ na Kijiji ‘B’, nitaweza kweli! Naomba mniangalie, sasa hivi ninazungumza kiujumla kwa sababu

tunasema michango mliyoitoa nimeichukua misingi yake kusudi niifanyie kazi. Ni lazima nifanye kazi *strategically*. Nikianza kuchambua hapa, hapa, pale, unaweza ukajikuta, wanasema una-*drawn in details*, yaani unazama katika vile vidogo vidogo unavyohangaika navyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, mambo ya msingi yaliyosemwa hapa, bajeti ya Wizara haikidhi mahitaji, hilo nimeshalimaliza. Mambo mengine yameshajibiwa na mwenzangu Naibu Waziri, sitayarudia. Kwa mfano, migogoro ya mipaka ya Vijiji, Wilaya na Mikoa, mimi nataka kusema kwamba pia mashamba, pia hifadhi, naomba nijibu kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nikiri kwamba kuna mkanganyiko wa sheria na wakati mwingine wa mamlaka. Lakini Wizara ya Ardhi, sisi hatuna shamba, hatuna mbuzi, hatuchungi na hatuna kiwanda. Wizara ya Ardhi ni Wizara ya kuweka *environment* (mazingira) kwa watu wengine kufanya kazi. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba kama hii migogoro inatokana na watu kuingia katika vitu wakati mwingine ambavyo siyo vyao, kwa mfano, sasa kama kuna tatizo kati ya hifadhi labda na wanakijiji, hapo mnatuita Wizara ya Ardhi. Waziri mwenzangu anajua kabisa siyo juu ya watu wa hifadhi kujiamulia mpaka. Siyo juu ya hifadhi. Ndivyo mambo yanvyokwenda, na mashamba hivyo hivyo. Profesa Maghembe, Waziri mwenzangu tena yule tulikuwa shule moja, yeye sasa ndiye mkulima, ana mashamba nimeyasikia, lakini sio juu ya wakulima kujiamulia mipaka ya mashmba yao.

Kama kuna matatizo, Wizara ya Ardhi ndiyo kazi yetu, na amini usiamini, mamlaka tumezikasimu tu. Maana wanasema kukasimu madaraka *(to delegate)*, lakini unapokasimu madaraka siyo kwamba unanyoosha mikono na kunawa wajibu. Ndiyo maana manung'uniko mimi nayapokea kwa moyo, kwa sababu *delegation of authority is not abdication of responsibility*. Kwa hiyo, Wizara ya Ardhi haiwezi kujikosha ikasimama kando ikasema hatukuwepo. Lakini, pamoja na hayo, sasa wale ambao mmekasimiwa madaraka ya Wizara ya Ardhi, naomba sasa mtu akikukasimu kitu, kama mambo yakienda vibaya, tunaweza pia tukakasirika, tukachukia. Sasa msitufikishe hapo jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mashamba yaliyobinafsishwa, naomba nitoe rai kwa wenye mashamba, Waheshimiwa Wabunge na Bunge Tukufu, michango niliyoisikia, mara baada ya Bunge hili, baada ya *budget session*, tutakwenda kufanya *independent audit* ya nani ametelekeza mashamba. Kwa hiyo, waliotelekeza mashamba, *the honeymoon is over*. *(Makofi)*

Mashamba yote ambayo hayalimwi, mengine nasikia yako katika Jimbo langu, lazima nikiri, Muleba Kusini kule Burigi, Butoro Wilaya ya Muleba kweli yamekodishwa kwa jirani zetu. Vitu vingine kusema kweli nakiri, naungana na Waheshimiwa Wabunge ni lazima tuvikomeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa nilikuwa nazungumzia suala la Tarime na Ronsoti nikasema kwamba tutarudi. Mwanasheria Mkuu ameshatuwezesha sana katika kutusaidia, kilio changu amekisikia kwa sababu ile Wizara kimsingi mambo mengi ni ya kisheria, lakini Kitengo chetu cha Sheria kilikuwa hakikidhi mahitaji. Kwa hiyo, sasa hivi tumeletewa wanasheria waandamizi ambao watatusaidia sana. Kwa hiyo, inapokuja kwenye mambo ya mashamba, kuna sehemu nyingine ambako nimeshasema kwamba kwa mfano Sheria ya mwaka 2004 ile *Land Amendment Act* kidogo imetuletea matatizo, suala hili tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishajipanga, tutarudi hapa katika Bunge hili Tukufu tukiomba marekebisho. Marekebisho tutakayoyaleta ni yale ya Mwalimu Nyerere. Hatuwezi kukubali. Nimesema sisi kizazi chetu tumemsikia, ametulea, Mungu amrehemu na mimi kama mtu wa Kagera nasema kwamba alitusaidia sisi watu wa Kagera, akafuta Nyarubanja. Hatuwezi tena kukaa kwenye nchi ambapo Nyarubanja imerudi tena. Nyarubanja ndiyo ile kukodisha ardhi. Wewe umeomba ardhi, Waziri Mkuu amefafanua vizuri kwamba ardhi yote iko chini ya Rais, ndiyo maana mnapewa *right of occupancy* kwa miaka ni *lease hold.* Sasa wewe upewe ardhi halafu na wewe unawapa watu wengine, kazi yako ni kukusanya hela za pango. Uliwahi kuona wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo lilikuwa ni kosa ambalo sasa tunarudi kurekebisha na ninaamini kwamba kwa sasa hivi nimeshawezeshwa, nina wanasheria waandamizi, haitatuchukua

muda mwingi tutarudi hapa, kwa sababu hilo lipo mikononi mwenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote nimeyasikia. Nimesema kwamba siwezi kuchukua shamba moja moja. Mheshimiwa Halima Mdee, Waziri Kivuli nikutambue kabisa kwa mchango wako ambao ninao hapa, naufanyia kazi. Lakini ninapokuja kwenye Jiji la Dar es Salaam tutakuwa wote. Mimi ni mdau wako, kama mimi ni mwanamakongo, wewe si ni Mbunge wetu wa Makongo! Sasa tutakapokuja kwenye ile kuathirika, tutakapoanza kukata barabara, tutakapoanza kuweka *betterment fee*, tuwe bega kwa bega hiyo ndiyo *by partisanship*. Kwa sababu kazi hii ya kupanga Miji haihitaji itikadi wala siasa. Ukiweka itikadi hufiki popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii inataka ushirikiano wa dhati kwa sababu inataka nidhamu, la sivyo unaweza ukawagawa wananchi na kuleta vurugu. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba masuala yote ya ardhi nitayashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda mwisho, kwa kuwa muda wangu ndiyo unanitupa mkono, niseme tu kwamba Mahakama zetu zipo, Mabaraza ya Ardhi yapo, yana matatizo, lakini pia yana nyenzo. Hii imezungumziwa katika bajeti *speech*. Labda tu niseme kwamba niliyojifunza huko nchi za nje ikiwemo Ulaya, wakati mwingine Mahakama inaweza ikashindwa kuwa suluhu ya mwisho katika migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi inakwenda *by mediation*, watu mnakaa mnajadiliana, mnatafuta muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kutoa rai kwa wananchi wa Chasimba, naomba *appointment* tukutane, na Waziri Mkuu ameshaniagiza tukutane tuongee. Mheshimiwa Halima naomba tuwe wote katika kikao hicho, maana pia ni lazima tukiri kwamba tunahitaji saruji, au siyo? Sasa huwezi kusema hatuhitaji saruji, lakini wananchi wa Chasimba wapo pale, hivyo hivyo Mlonganzira, Mheshimiwa Madabida amezungumzia Mlonganzira kwa uchungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Mlonganzira Mheshimiwa Kawambwa ndiye mwenye ardhi kwa maana ya kwamba Wizara ya Elimu Chuo Kikuu kinatakiwa kijengwe. Lakini pale ni ukweli usiopingika kwamba kuna wananchi wanakaa pale. Kwa hiyo, mtanikuta, nitajielekeza katika *mediation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kugongewa kengele, niwaambie kitu kimoja, nitakuwepo hapo mimi mwenyewe, nimejifunga kibwebwe, na wale mlionikaribisha wala msiwe na wasiwasi tutakuwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mchango wangu. Kwa sababu ya muda nimeshindwa kabisa kujibu hoja moja moja kwa sababu niliona kwamba niwe kwenye *strategic frontier* niangalie mambo ili kusudi mtu hapo aone tutakavyojipanga na mengine yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka. Makofi hayo yanaashiria kukubali kwa Waheshimiwa Wabunge kazi nzuri ambayo umeifanya katika kupitia hoja zao. Tunakushukuru sana, japo nimepata baadhi ya vikaratasi toka kwa Wabunge wengine toka Pemba nadhani, wanasema Nyarubanja ndiyo nini? Nikawaambia tutaelezana baadaye kidogo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujakwenda hatua inayofuata, naomba niwatambulishe wageni waliopo Bungeni ambao wapo jukwaa la Spika au majukwaa yaliyo karibu yake ambao ni wageni wa Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, ambao ni Dkt. Jeff Bach *Director European Parliamentarians with Africa*, karibu sana. Wageni 16 wa Spika kutoka Kanisa la

Agape Tanzania ambao nitawatambulisha mmoja mmoja. Kwanza ni Mtume Dkt. Vernon Fernandes kutoka Dar es Salaam. Wapo hao Maaskofu na wenzao?

**WABUNGE FULANI:** Wapo.

**NAIBU SPIKA:** Mpo eeh, naomba basi msimame kwa wakati mmoja. Karibuni sana wote wageni wa Spika, na wale ambao mtashiriki pamoja nao kule *VETA* saa 1.00 jioni, kuna maombi maalum.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wale ambao mmesaini karatasi iliyokuwa ikizunguka kutoka kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia kwamba siku husika ile shughuli ni leo na siyo kesho. Katibu

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 - *Administration and General*…………..................Shs. 5,365,766,600/=

**MWENYEKITI:** Vipi jamani, mnavunja Kanuni, mnawahisha shughuli! Eeh! *(Kicheko)*

*(Hapa Wabunge Walisimama na kutajwa Majina)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwe na maswali mafupi ili tuweze kupata majibu mafupi, Mheshimiwa Agripina.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niliochangia kwa maandishi ni pamoja na suala zima la kulalamikia Baraza la Mahakama lililo moja kwa Mkoa mzima wa Kigoma, na nimepitia taarifa nzuri ya Waziri ambayo inaoonekana kabisa kuna maandalizi ya mchakato wa kuanzisha Mabaraza mengine katika Wilaya. Nilikuwa naomba Waziri anithibitishie kama na sisi Wilaya ya Kasulu anaweza akatuletea Baraza hilo la Mahakama ili kupunguza msongamano unaojitokeza katika Baraza la Mahakama ya Ardhi Kigoma kwa wananchi wanaotoka Kibondo na Kasulu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu tutafanikiwa kuweka Mabaraza takribani sita, lakini kwa mujibu wa Ilani ya CCM angalau Mabaraza kumi kama tukifanikiwa. Kwa hiyo, kwa kazi hii ambayo tunakwenda kujikita na *tension scheme* tuliyopewa, nafikiria kwamba Kasulu, Mungu bariki kama bajeti itaruhusu ndiyo, *inshaalah*.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Ludewa, hususan akina mama ambao wanaishi Tarafa ya Liganga ambapo chini yake kuna madini ya chuma katika eneo kubwa la Tarafa ikiwa ni pamoja na Kata ya Mundindi, Mkoming'ombe na Iwela. Kuna wakati wanaambiwa watatakiwa wahame katika ardhi ile kupisha uwekezaji wa masuala ya mchuchuma na liganga na hivyo kupelekea uibuaji wa miradi kama ya *TASAF*, majosho na miradi mingine kama Zahanati ya kudumu muda mrefu kusitishwa kwa sababu kuna uwezekano wa kuhama na wakati mwingine wamekuwa wakipata tamko kwamba msiwe na wasiwasi muendelee kuishi, haina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kupata tamko kutoka Wizarani: Je, eneo hili ambapo chini yake kuna raslimali na madini la Wilaya ya Ludewa, Tarafa ya Liganga, wananchi waendelee kuishi, kuwekeza au kutakuwa na utaratibu wa kuhama?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunafuata taratibu kati yetu na wenzetu katika Sekta ya Madini kwamba katika hali hii, sasa pale kama mipango yao ni kwamba wangependa wananchi watoke kwenye eneo hilo, bado haijatufikia. Labda niseme tu kwamba hili tutalifanyia kazi kati ya sisi na Sekta ya Madini ili kusudi wananchi wajue mustakabali wao ni nini.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa vile katika maelezo yangu nilizungumzia juu ya mgogoro wa ardhi kwa wananchi wa shamba lililokuwa la *NAFCO* Kapunga na wananchi wa pale kwamba ardhi ile alipewa mwekezaji pamoja na maeneo yao. Nikazungumzia eneo la Igomelo kwamba ardhi ile nayo iko mashakani, ipo tu kwa kauli ya Waziri. Nikazungumzia juu ya *NARCO* ambayo wamepewa watu na wananchi wanahangaika, lakini wanaambiwa wakodi mle. Nikazungumzia mambo mengi Kijiji cha Luhanga kwamba kuna wajanja wameingia pale wanataka kuchukua ardhi yao, lakini nikawa nimemwambia wananchi wale wamesema nisirudi kama majibu hayo hayapo na Waziri hajanijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibiwe na kama sijajibiwa, hiyo shilingi nabaki nayo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama nilivyosema kwamba majibu yamepatikana, siyo kwamba arudi mikono mitupu, nimetangaza kwamba enzi za kukodisha ardhi, Bunge hili Tukufu ndio lina uwezo huo wa kuyaondoa hayo. Kwa hiyo, nilitaka kusema kwamba wale wenye matatizo, jibu hapa limetoka. Hiyo shilingi yangu usininyime kwa sababu jibu unaondoka nalo, siyo kwamba huna cha kuwaambia wananchi migogoro ya ardhi ya mashamba watu ambao wana mashamba hawalimi, kazi yao kukodisha wananchi kwa gharama hiyo, nadhani naweza kusema imefikiwa tamati. Lakini lazima nikiri kwamba nguvu hiyo lazima mpaka turudi Bungeni, Serikali ikishajipanga. *(Makofi)*

**MHE. ROSE KAMILI SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchango wa Mheshimiwa Waziri, ingawa hakunijibu, lakini nataka kuweka imani kwake kama hatafungwa *speed governor*. Katika maelezo yangu nilizungumzia ugawaji holela wa viwanja Mjini Katesh na Basutu na Endasak, lakini naomba nielezee suala la ugawaji holela kwa maana kwamba maeneo yaliyotengwa kwa ajili matumizi ya watumishi wa Serikali yanagawanywa ovyo Wilaya ya Hanang kwa ajili ya watu binasi au kwa ajili ya Wakuu wa Idara bila kutumia vikao halali. Sasa hayo majibu sikuyapata kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Pia nilieleza suala la ugawaji au matumizi ya fedha zaidi ya Shilingi milioni 100 zilizotumika kwa ajili ya ugawaji wa ardhi ya Wareti na ardhi hiyo bado haikukamilika na fedha hizo wananchi wa pale hawakupata hata hati miliki moja. Je, anatujibu nini kwa ubadhilifu huo wa fedha, Shilingi milioni 100 na Shilingi milioni mbili kwa ajili ya kupewa viongozi wa CCM Mkoa? Nataka majibu hayo. Mheshimiwa Waziri atatusaidiaje? Au yeye mwenyewe ajiandae kwenda Wilayani Hanang tukamweleze wazi kinagaubaga ili atambue ubadhirifu huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rose Kamili kwa swali hili na taarifa ambayo ametupatia. Tunaloweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tumepokea taarifa hii na Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara husika tutafuatilia na kuhakikisha kwamba hatua za kisheria zimechukuliwa pale ambapo itabainika kwamba kuna ubadhirifu uliofanyika.

Kuhusu kutembelea Wilaya ya Hanang, napenda kumthibitishia kwamba tutafika Hanang na kushirikiana pamoja naye na Mbunge wa Jimbo hilo ili kuweza kupata ufumbuzi wa matatizo ya ardhi pamoja na mipango miji katika Halmashauri hiyo.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kikao cha faragha na Waziri Mkuu na kukubaliana na kwa kauli yake aliyotoa hapa Bungeni na kusema kuwa sasa atakutana na Wabunge wa Dar es Salaam kwenye mambo mbalimbali ambayo yanahusu Mkoa wa Dar es Salaam kwa maana ya Kigamboni, Kurasini na Bonde la Msimbazi, kwanza nichukue nafasi hii

kumshukuru kwa namna alivyoona umuhimu wake. Lakini pili, niwahakikishie wananchi wa maeneo haya yanayohusika kuwa Wabunge wenu tunalifanyia kazi, tulieni, pumzikeni acheni hofu, Serikali hii ni sikivu na iko tayari kutusikiliza na kupata muafaka wa maendeleo ya nchi yetu. Kwa maana hiyo sasa jana sikuunga mkono hoja, lakini leo sasa kwa maneno mazuri ya Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NGUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Nami niungane na Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Dar es Saalam kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuliona hili suala la Kigamboni kwamba ni suala kubwa na linagusa maisha ya watu wengi, watu ambao kwa muda takribani miaka mitatu wamekuwa kifungoni na kukubaliana kwa msingi kabisa kwamba tutakutana baada ya Bunge kukaa na kujadili suala hili kwa kina. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hii mikakati yao ambayo watataka kuiweka ili basi itakapofika tarehe 30 Juni, 2012, Serikali ije na mipango thabiti inayoeleza kwa kina, kitu gani ambacho kitaendelea Kigamboni. Baada ya kusema hayo machache na mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza bayana migogoro ya ardhi iliyopo katika Kata kubwa nne.

Pamoja na majibu ya Waziri kwamba muda hautoshi, lakini tu kwa faida ya wapigakura wangu, waelewe Serikali inatoa tamko gani katika mgogoro wa ardhi katika vijiji vya Manza na Vitongoji vya Kinyenze. Lakini pia nimeongelea suala mgogoro wa ardhi kwa wafugaji wa asili ekari 5,000 ambazo wamepewa vigogo ambao wanatambulika kama *Katenda Group* na Elisa Mollel. Lakini pia nimeongelea mgogoro wa ardhi wa muda mrefu ambapo Rais pia aliahidi kutatua kuhusu shamba linalojulikana la Sumaye pale Mvomero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeongelea suala la mgogoro wa ardhi kati ya Vijiji vinavyozunguka Kiwanda cha Mtibwa na hasa eneo la *New Land* ambalo kiwanda kimepora eneo hili. Sasa kwa kuwa Rais anao uwezo wakati wowote kubadilisha umiliki wa ardhi wa maeneo haya, Serikali inatoa kauli gani ili kuwatendea haki wananchi wa Jimbo la Mvomero katika kata hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kupitia Bunge lako Tukufu, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Amos Makala - Mbunge wa Mvomero kwa namna anavyofuatilia na kushughulikia kero za wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea taarifa hii na sisi tutafanyia kazi kwa kufuatilia na kujua taratibu zilizotumika kugawa ardhi hiyo na pale ambapo tutabaini kwamba sheria haikuzingatiwa, Rais atashauriwa ipasavyo ili wale waliomilikishishwa bila kuzingatia sheria hatua ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Waziri Mkuu kwa hotuba aliyoitoa hapa, imeniingia akilini na hotuba aliyoitoa Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu Waziri imenifanya niishukuru sana Serikali kwamba wametuelekeza vizuri. Ombi langu, nilikuwa naomba tu Mheshimiwa Waziri kwamba tukimaliza huu mjadala twende naye mpaka Mkoa wa Tanga akaangalie ile misitu ya Mamlaka ya Mkonge jinsi ilivyokua ili wananchi wa Mkoa wa Tanga wagawiwe ardhi ambayo sasa hivi wanapata shida sana.

Kwa kuzingatia kwamba kuna kijiji kule Makulasi, wananchi walipewa na Serikali baada ya kupatwa na mafuriko, lakini mamlaka ya Mkonge imeingia kati na kuwataka kuwatoa kwa nguvu ili wawape watu binafsi. Naomba ikiwezekana, Mheshimiwa Waziri na sisi Wabunge wa Mkoa wa Tanga twende mpaka kwenye mashamba ya mkonge akaone dhuluma inayopatikana kule. Sina haja ya kutoa shilingi ila nashukuru sana kwa hotuba yako nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli namshukuru Mheshimiwa Mbunge na nasema safari ya Tanga imekamilika. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea hali halisi ya viwanja vya ufukweni jinsi gani ambavyo havijatolea utaratibu na kwamba vingi vinamilikishwa kwa wageni na nilisema kwamba kuna hatari ikiwa tunaendelea na utaratibu huu wa kumiliki viwanja vya ufukweni hasa kwa Wasomali tukifahamu hali halisi kwamba ni watu ambao ni haramia na walikuwa wanafanya matukio mengi ya uhalifu katika bahari zetu. Je, kama tutawapa viwanja, wakajenga hoteli au nyumba, hatuoni kwamba zitakuwa ni maficho kwa ajili kuendeleza uhalifu katika bahari zetu? Naomba Serikali itolee majibu suala hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelipokea suala hilo, tutafanya *audit* na kuchukua hatua stahili.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu kwa sasa linakabiliwa na tatizo kubwa sana la bomoa bomoa ya makazi ya watu. Bomoa bomoa hii kwa sehemu kubwa inatekelezwa kwa mujibu wa sheria kama ambavyo tunaelezwa na Wizara ya Ujenzi. Lakini kwa bahati mbaya sana kwamba pia waliojenga katika maeneo husika ni watu ambao walifuata taratibu zote chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nilikuwa nahitaji kauli ya Serikali kupitia Waziri kwamba Serikali haioni kwamba ni muda muafaka Serikali ianze kulipa fidia hata kwa watu ambao walijenga ndani ya Hifadhi ya Barabara ilimradi tu wana vielelezo vyote vya Wizara kwamba walistahili kujenga pale? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya barabara viwango vyake vilikuwa vinafahamika na pale ambapo barabara imewafuata watu sharti fidia itolewe. Lakini pale ambapo watu wameifuata barabara hapo kuna mjadala. Kwa hiyo, nilitaka kusema kwamba labda nichukue nafasi kumpongeza Waziri Magufuli, tayari sasa ameshaweka *demarcation* za barabara zake, kwa hiyo, nadhani sasa hivi Tanzania hakuna mtu yeyote ambaye yuko kwenye hifadhi ya barabara ambayo hana habari hiyo.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema kwamba kama mtu ameifuata barabara, fidia inaweza kuwa ngumu kupatikana. Lakini pia kama mtu ameifuata barabara kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, ana hati na nyaraka halali ambazo zimepatikana kihalali na siyo kwa ujanja na ikaonekana kwamba hapo barabara itakuwa imemfuata, niseme kimsingi hapa kwamba kama barabara imekufuata ni haki yako kupata fidia. Labda nifafanue tu kwamba fidia inatolewa na Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, Wizara ya Ujenzi haiamui fidia. Fidia inaamuliwa na Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, nataka hili lieleweke, kama kuna utata, sisi tunakuja pale kufanya kazi yetu na kutoa uamuzi.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Katika Hotuba ya Waziri, katika ukurasa wa 17 napenda kusema kwamba nimefurahi sana kwamba Mji wa Katoro na Buselesele, tayari ramani zimekamilika. Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba Serikali inajipanga vipi kuhakikisha kwamba mpango wa kupanga mji huu kwa sababu Mji wa Katoro na Buselesele inakua kwa kasi sana? Kwa hiyo, nitaka nifahamu ni lini sasa Serikali itaanza kupanga miji hii na kuweza kupima viwanja na kuhakikisha kwamba viwanja vinagaiwa kwa wananchi ili mji huu uwe safi kabisa? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge wa Busanda kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, itashughulikia mpango huo na yeye akiwa ni Diwani, tunaamini kwamba atahimiza Halmashauri ya Wilaya ili kwamba ilete ombi kwetu tuweze kutoa watalaam katika upangaji wa mji huo na utekelezaji wa mpango huo. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. KAILA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inasifika kwa amani, lakini kule kwangu Ngorongoro nina migogoro ya mipaka, migogoro ya mashamba na maeneo ya malisho ya mifugo kati ya Watanzania wa jamii ya Kimasai na Wabateni au Wasonjo na Mheshimiwa Chiligati alipokuwa Waziri wa Ardhi alisaidia sana kuleta hela ya kupima mipaka hiyo ili kuweza kuondoa hiyo migogoro. Sasa nilikuwa nataka tu ufafanuzi kutoka kwa Waziri ili ionekane kwamba

kuna *continuity* ya Serikali katika masuala haya: Je, Profesa anaweza akaniahidi kwamba hiyo kazi nzuri ambayo ilikuwa imeanzishwa na Mheshimiwa Chiligati ataiendeleza? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo kazi ambayo nimeirithi inaendelea na hata katika hotuba nimekiri kwamba hakuna kilichobadilika, tunaendelea na yale mazuri ambayo nimeyapokea. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba na *apartment* ambazo zinapangishwa na wawekezaji zinatozwa kodi kuanzia Dola 1,500 kwa chumba kimoja kodi ambayo Watanzania wengi hawawezi ku-*afford* wakiwemo na Wabunge. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri: Je, hizo nyumba zilizojengwa na Wawekezaji, walijengewa akina nani? Hii hali itaendelea mpaka lini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi juu ya suala la Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme kwamba kodi ya nyumba hupangwa kisayansi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa. Thamani ya nyumba ni kigezo namba moja kinachotumika kupanga kodi ya nyumba na kigezo cha pili ni mahali nyumba ilipo *(strategic location)* ya nyumba, kwa mfano nyumba iliyoko ufukweni kodi yake haiwezi ikawa sawa na nyumba iliyoko Kariakoo. Lazima itatofautiana. Kwa hiyo, ziko *factors* kama hizi ambazo zinatumika kupanga nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la nyumba bado ni huria, Serikali haidhibiti. Tulikuwa na Sheria ya *Land Restriction* ya mwaka 1984. Kwa sasa hivi hatudhibiti kodi za nyumba. Kwa hiyo, tunachoweza kusema ni kwamba Shirika letu la Nyumba tutalihimiza liendelee kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kama ambavyo mmeshuhudia hapa Dodoma kwamba imeanza ili wananchi wote waweze kupata nyumba za kodi nafuu. Nashukuru sana.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Waziri Mkuu kusema kwamba tulikuwa gizani Kigoma. Ni kweli tumepata mwanga juzi juzi, lakini kipindi hicho ambacho tupo gizani, hawa matapeli wa ardhi hawakuja, tumepata neema, hizi siku mbili ndiyo wameanza kuja. Kuna mgogoro, wamekuja mafisadi vigogo na wake zao wanashirikiana na Afisa Mipango Miji, wamepora ardhi yetu, wanawanyang'anya wakazi maeneo ya Burega yanayoangalia Ziwa Tanganyika. Sasa wananchi wa Kigoma wanataka kujua: Je, uko tayari kuunda Tume itakayoshirikiana na Kamati ya Mipango Miji kutatua tatizo hili ama wasubiri washike mapanga kama wanavyokatana Tarime na maeneo mengine? Naomba majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hapana, hatuko tayari kabisa wananchi washike mapanga na wala hakuna sababu, tuko kazini. Kwa hiyo, nimesikia na tutachunguza.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa niaba yako na kwa niaba ya watu wa Kilole na kupitia ujumbe uliopokea mwenyewe, naomba niusome. "Bajeti hiyo wananchi wa Kilole, Korogwe tuna hasira, mashamba yetu yamepimwa, viwanja vimeuzwa, vinajengwa, sisi wenye mashamba hatujalipwa chochote. Sasa basi: Je, huo ndiyo utawala bora?" Namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie nini msimamo wa Wizara yake sasa kwa wale wote waliopima mashamba ya watu na hatimaye wakauza viwanja wakashindwa kuwalipa wenye mashamba na adhabu gani atawapa? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Nassir kwamba ujumbe tumeupokea, kama nilivyosema kazi yetu inakwenda kwa sheria na taratibu, tutachunguza na ole wake atakayebainika kwamba alifanya makosa.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 47 anaonyesha idadi ya vyeti vilivyotolewa katika Halmashauri mbalimbali na hati miliki. Kilindi inaonekana imetolewa vyeti 42 na hati miliki 42, hiyo sio sahihi kabisa. Vyeti vilivyotolewa ni sita tu na hati miliki tatu, nyingine tano ndiyo zinashughulikiwa. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameeleza katika hotuba yake kwamba katika mwaka huu wa fedha wanakusudia kufanya upimaji wa viwanja 35,000 na mashamba 800 na kwa sababu sisi hatuna hati miliki ambayo ni haki ya kimsingi ya wananchi na kwa sababu tuna migogoro mingi ambayo imepelekea kumwaga damu: Je, atakubaliana nami kwamba tutapewa kipaumbele Wilaya ya Kilindi kwa sababu ni makazi mapya?

La pili, kwa kuwa Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa Wilaya ambazo siyo mpya sana lakini ina karibu miaka nane, lakini watumishi wengi wanakimbia kwa kukosa makazi, kwa sababu *national housing* wanafanya kazi nzuri kwa kupitia Mkurugenzi wao Mchechu: Je, inawezekana akatujengea hata nyumba 50 ili tuweze ku-*retain* watumishi na sisi tuwe na watumishi wenye sifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Beatrice lijibiwe la kwanza au la pili? Ni moja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yote au hata moja, la kwanza.

**SPIKA:** La kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, ningemwomba Mheshimiwa Beatrice Shellukindo akiwa ni Diwani namba moja wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kwamba tutashirikiana na Halmashauri yake katika kuwasaidia wananchi wake kupima viwanja hivyo. Kwa maana hiyo ni kwamba Halmashauri pamoja na wananchi washirikiane nasi kwa hali na mali ili kuweza kutekeleza kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu…

**SPIKA:** Hapana. Mheshimiwa Anna Malaki.

**MHE. ANNA M. J. MALAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilipenda kufahamu kwamba Serikali inatoa sheria gani kwa Mabwana Ardhi ambao wanagawa viwanja kwa wananchi na vinachukua muda mrefu bila kujengwa na kusababisha mapori katikati ya mji huku wananchi wengine wanahangaika mahali pa kujenga?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimjibu Mheshimiwa kwamba katika *audit* ambayo tutazifanya mojawapo itakuwa ni hiyo hiyo ya viwanja ambavyo navyo kimsingi vimetelekezwa. Kwa hiyo, kuna mashamba yaliyotelekezwa, lakini pia kuna viwanja ambavyo vimetelekezwa, maana yake sheria iko wazi, baada ya miaka mitatu kama hakuna dalili ya maendelezo, hapo tuna haki ya kutoa kiwanja.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kwamba kwa kuwa Serikali inapohitaji kutumia ardhi katika eneo ambalo wananchi wamewekeza kwa kujenga aidha kwa kilimo, Serikali huwa ina utaratibu wa kufanya tathmini kwa lengo la kulipa fidia wanaohusika, lakini tatizo linapatikana kwamba tathmini inafanywa leo, lakini fidia au malipo yanafanywa baada ya mwaka mmoja, miwili au mitatu. Hili ni tatizo hasa ukilinganisha kwamba thamani za bidhaa na hata ardhi inakuwa inapanda siku hadi siku, mwaka hadi mwaka. Naomba ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri unawaeleza nini wananchi juu ya tatizo hili? Ahsante.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa kwamba fidia kuchelewa katika bajeti hii utaona kwamba tunajitahidi, sasa tuko mbioni kuanzisha *compensation fund* ambayo itatuondolea tatizo hili ambalo kusema kweli ni kero katika sehemu nyingi. Lakini hapo hapo nitoe rai tu katika kufafanua kwamba wenye miradi ile sasa hususan katika mipango miji, wenye miradi ni Halmashauri husika, kwamba itabidi sasa waonyeshe kwamba kweli wanafidia kabla hawajaanza kuwasumbua wananchi. Hili tumejifunza,

imekuwa ni chanzo cha migogoro na tutalirekebisha. Kwa hiyo, wale ambao fidia zao zimecheleweshwa, wana haki ya kudai asilimia sita kwa kuchelewa. Sheria inatamka wazi wazi.

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nimehoji Serikali ni lini itafika Shinyanga kusuluhisha mgogoro mkubwa katika Kata za Ndembezi, Kitangiri, Ndala na Masekelo. Nataka kusikia *commitment* ya Serikali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Maselle kwamba kwanza mwaliko wake tulishaupata na tunajiandaa kusudi sasa safari yetu iwe na tija. Kwa hiyo, safari hii ni Jimboni kwa Mheshimiwa Maselle na yenyewe ni kama inakamilika hivi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kama nilivyokuwa nimechangia, ni kwamba vijana ni bomu linalokuja na ukizingatia vijana wamekosa fursa katika sekta nyingine kwa ajili ya kujikwamua na umasikini na tatizo la ajira linalowakabili. Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijasikia akizungumzia mikakati yoyote ya kumkomboa kijana wa Kitanzania kupitia ardhi yake. Je, Mheshimiwa Waziri anawaeleza nini vijana wa Tanzania kuhusiana na ardhi yao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ardhi kwa vijana na wanawake tunahitaji tuangalie kwa ukaribu zaidi. Sasa katika hili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na wasiwasi, nitashughulika kama mwanaharakati. Kwa hiyo, hawajasahaulika, ni sekta mtambuka inapokuja kwa wanawake na vijana kupata ardhi kusudi na sisi tupigane na umasikini.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa majibu mazuri sana kwa siku ya leo. Mimi ni ombi tu. Katika Mkoa wa Mwanza, hatuna Afisa Mteule anaye-*sign deed plan* ambayo ni nyaraka muhimu sana. Serikali inasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Ndassa kwa jitihada za kutetea wapigakura wake wa Jimbo la Sumve na Mkoa wa Mwanza kwa ujumla. Napenda kueleza kwamba Mheshimiwa Mbunge atusaidie kwa kusaidiana na uongozi wa Jiji la Mwanza ili wapendekeze Afisa atakayeteuliwa kushika wadhifa huo.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliulizia juu ya mgogoro wa ardhi ulipo katika kijiji cha Kabage kuporwa ardhi yao na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda wa kiongozwa na watumishi ndani ya Idara ya Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Kakoso kwamba taarifa hiyo tumeipokea. Kama kuna watumishi, maafisa ardhi ambao wataonekana kwamba wamejihusisha na kitendo kama hicho kuwapora wananchi ardhi zao kwa vyovyote vile tutawashughulikia. Kwa hiyo, tunaomba taarifa, tumeipokea, tutaishughulikia.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi naomba ufafanuzi mfupi tu, Wizara hii ya Ardhi ni pamoja na Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa kuwa umasikini wa nchi pia unapimwa kwa vigezo na nyumba na makazi ya watu wake jinsi wanavyoishi, lakini kwenye bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri sehemu kubwa, asilimia kubwa ya bajeti imeelekezwa kwenye suala la ardhi, lakini bado nchi yetu ina tatizo kubwa la makazi ya watu hasa wale ambao bado wanaishi kwenye nyumba za nyasi na udongo na wengine ambao hawana makazi kabisa kama kule Mkoani kwetu Manyara, wale wa Hadzabe na wengineo. Sasa bajeti hii ndogo, itajielekeza vipi katika kutatua tatizo hili la makazi ya watu hasa kuondokana na nyumba duni kama za udongo na nyasi?

**SPIKA:** Kuondokana na nyumba za matembe, *Proffessor*. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Martha kwamba bajeti hii haina mahali popote Sekta ya Nyumba, kwa sababu Sekta ya Nyumba nimeifafanua kwamba bajeti yake iko kwenye Shirika letu la Nyumba. Kwa hiyo, shirika la *National Housing Cooperation* ambayo nadhani imeelezewa katika *budjet speech* takribani Shilingi bilioni 311 na nusu, kwa hiyo, unakuta kwamba ni bajeti kubwa sana, lakini iko nje ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nifafanue kwamba bajeti ya Serikali haiwezi kubeba bajeti ya nyumba kwa sababu Serikali yetu haina uwezo ya kuwajengea wananchi nyumba. Nyumba ziko katika sekta binafsi na ndiyo maana shirika letu linawawezesha wananchi kupata nyumba, lakini kimsingi kwa kupitia sekta binafsi. Ahsante.

**MHE.DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii, lakini pia niseme kwamba Wilaya ya Ngara inakabiliwa na tatizo kubwa la mgogoro wa ardhi kati ya wananchi au wakulima na wahamiaji haramu kutoka nchi za jirani ambao wameingia katika Wilaya yetu na mang'ombe mengi na wanachunga katika ardhi yetu na wameanza kuwauwa wananchi. Sasa nianze kwa kuishukuru Wizara kwa kupima vijiji 68 kati ya vijiji 73. Ombi la wananchi wa Ngara ni kupatiwa hati za vijiji hivyo na pia tukamilishe matumizi bora ya ardhi ili kwanza tufaidike kwanza na mradi wa MKURABITA lakini pia hati hizo itakuwa kinga dhidi ya wahamiaji haramu hawa kwa sababu Idara ya Uhamiaji imeshindwa kutusaidia.

Sasa nimalizie kwa kusema naomba *political support* ya Waziri na Naibu Waziri kwa Katibu Mkuu – Ndugu Patrick Rutabanzibwa kama Katibu Mkuu msataafu wa Utumishi, namfahamu sana Ndugu Patrick kama Katibu Mkuu mzuri, muadilifu, mzalendo na ataweza kuisafisha Wizara hiyo kama atapata *support* ya Mawaziri. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ntukamazina kwamba suala la matatizo ya wahamiaji Ngara, tunalifahamu na tunalifanyia kazi na mimi nilishasema na nasema tena kwamba kazi ambayo ameifanya Rutabanzibwa ni kubwa sana na astahili kila pongezi na kwamba mimi mwenyewe namtegemea sana, maana yake, lazima nikiri kwamba hii ni *team work.* Bila *team work* hatutafika popote.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 46 ameonyesha vijiji katika Wilaya mbalimbali ambavyo vimebainishwa kwa wawekezaji kwenda kuwekeza, na katika mchango wangu nimeulizia kama wananchi wa vijiji hivyo ambavyo tayari wako kule wanaendesha maisha yao ya kila siku. Je, hao wawekezaji au hao wananchi wameshirikishwa kukaa pamoja ili na wao wafaidike katika huo uwekezaji unaokwenda badala yao kuwa ni wafanyakazi na wapagazi katika eneo lao? La mwisho: Je, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako tayari kwenda kuona hali halisi ya huko ikoje?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Zaynabu Vullu - Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani na kumjulisha kwamba tuko tayari kwenda kuona eneo hilo na kwamba katika kutoa ardhi kwa wawekezaji, Serikali itahakikisha kwamba wananchi wanakuwa wabia katika miradi hiyo.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa upungufu mkubwa wa wataalam wa ardhi umekuwa ukisababisha migogoro ya ardhi katika maeneo mengi na katika mchango wa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Wizara itawasilisha ombi Serikalini kupata kibali cha kuajiri wahitimu moja kwa moja. Sasa naomba kauli ya Serikali kuwa suala hili litakamilika lini? Kwa sababu Halmashauri zimetenga fedha, lakini haziwezi kuajiri kwa kuwa hazina kibali cha kufanya hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Zabein Mhita kwa swali lake na napenda kumjulisha kwamba Wizara yangu itawasilisha ombi hili Menejimenti ya Utumishi wa

Umma ili Serikali iweze kufikiria na kutoa kibali kwa ajili ya nafasi zilizo wazi katika Halmashauri na Wizara kuweza kujazwa mapema iwezekanavyo.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mkoa wa Morogoro unaitwa shamba la bibi kwa kuwa watu wengi wamekuwa wakija wakivamia ardhi ya wananchi. Karibu Wilaya zote Mkoani Morogoro wana matatizo ya migogoro ya ardhi na mimeshtushwa sana baada ya kuja kusikia mpaka vigogo wa nchi waliowahi kuwa viongozi nchi hii wanamiliki ardhi katika Mkoa wa Morogoro. Nilikuwa nina ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba Morogoro ipewe *special attention,* watu wote ambao wataonekana wanamiliki ardhi ambao sio wazawa wa Mkoa wa Morogoro warudi makwao.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu niseme kwamba Wizara yangu inaongozwa na sheria. Kama kuna watu wowote ambao wako Morogoro, nadhani ni ruksa kwa kila Mtanzania kutafuta ardhi Morogoro ilimradi alime. Kwa hiyo, tatizo hapa kama mtu akihodhi ardhi Morogoro, hapo kuna matatizo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa sera ya watu wa Morogoro na sisi wa Dodoma tunasema watu wote msiokuwa wa Dodoma, rudini kwenu.*(Kicheko)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mikoa ya Mtwara na Lindi ina matatizo makubwa sana ya kupata huduma za hati za kumiliki ardhi na hivyo kulazimika kwenda Dar es Salaam na pia huchukua muda mrefu sana kwenye zoezi hili la kupata hati hizi za ardhi. Mwaka jana Mheshimiwa *Comrade* Chiligati akiwa Waziri wa Wizara hii, aliahidi Bungeni hapa kwamba kungeanza utaratibu wa kusajili hati pale Mtwara, lakini hadi leo hakuna Msajili wala Kamishna Msaidi kwa ajili ya utoaji wa hizo hati. Wako wafanyakazi pale wenye sifa, kwa nini Wizara isiwape hadhi hiyo wale wafanyakazi walioko pale ili kumaliza tatizo hili la kwenda Dar es Salaam na kukaa muda mrefu kupata hati, bila sababu ya maana? Ahsante.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue kwamba, tayari Wizara imeshamteua Kamishna Msaidizi kwa ajili ya Kanda ya Mtwara. Kwa hiyo, tatizo limeshashughulikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ambao mliomba kuzungumza katika nafasi hii mlikuwa 75. Waliopata nafasi ya kuweza kuitumia ni 25. Kwa hiyo, Wabunge 50 hamjapata nafasi. Kwa hiyo, kila mmoja ambaye hajaguswa, naomba tuchukuliane kwa upendo. Tunaendelea.

Kif.1002 - *Finance and Accounts…….…….. Tshs.682,593,000/=*
Kif.1003 - *Policy and Planning …………... Tshs.2,879,639,840/=*
Kif.1004 - *Management Information System……... Tshs. 904,373,680/=*
Kif.1005 - *Internal Audit ………………………Tshs. 278,270,520/=*
Kif.1006 - *Procurement Management Unit…….........Tshs. 320,306,080/=*
Kif.2001 - *Land Administration Division....................... Tshs. 1,669,390,120/=*
Kif.2002 - *Surveys and Mapping Division.... Tshs. 2,989,562,470/=*
Kif.2003 - *Registration of Titles Unit................Tshs. 761,863,360/=*
Kif.2004 - *Valuation Unit .........................Tshs. 660,135,190/=*
Kif.3001 - *Physical and Planning Division.......................Tshs.3,727,465,640/=*
Kif.3002 - *Housing Division ......................... Tshs. 2,076,415,860/=*
Kif.3003 - *District Land and Housing Tribunal Unit..……Tshs. 3,568,978,640/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif.1001 - *Administration and General.........................................  Tshs. 1,200,000,000/=*
Kif.1003 - *Policy and Planning .................. Tshs. 0/=*
Kif.2001 - *Land Administration Division...... Tshs. 16,217,932,000/=*
Kif.2002 - *Surveys and Mapping Division..... Tshs. 1,579,705,000/=*
Kif.2003 - *Registration of Titles Unit ............ Tshs. 0/=*
Kif.3001 - *Physical Planning Division ............Tshs. 3,012,800,000/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2011/2012, kifungu kwa kifungu na kupitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFRIKA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012, yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Tunawatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu, Viongozi wote wa Wizara hiyo, tunawatakia kazi njema. Watanzania wana matumaini makubwa sana nanyi. Kwa kuwa, ninyi ndio msingi wa maendeleo yetu, tuna matumaini makubwa kwamba tukikutana mwakani kutakuwa na mabadiliko makubwa katika maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasemea kwa niaba ya Waheshimiwa wananchi. Tunawashukuru mno na kila la heri.

Waheshimiwa Wabunge, juzi tulikuwa na Waandishi wa Habari, wanaoandika habari za Bunge, na baadhi yao wakauliza kwamba, hivi ni kwanini Mheshimiwa Spika, Naibu Spika au Wenyeviti tunapohoji wanaosema ndio, waseme ndio! Wanaosema sio, waseme sio! Halafu tunasema ‘nafikiri’ wa upande fulani, kutegemeana na wanaoshinda wameshinda. Wakawa wanauliza ni kwa nini lile neno ‘nafikiri’, ina maana hamna uhakika? Sasa huenda linawasumbua Watanzania wengi na huenda pia baadhi ya Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, inasemwa hivyo kama utamaduni wa Kibunge. Kwa sababu katika Kanuni zetu, huwa kuna fursa ya Mbunge ambaye anaona kama kura hizi huenda upande wake umeshinda ila Spika, kwa namna moja au nyingine hakusikia vizuri au amelalia upande mwingine, kusimama mahali pake na kuomba kura zihesabiwe.

Kwa hiyo, Spika akisema upande huu wameshinda moja kwa moja, ina maana amefunga. Lakini akisema nafikiri, inampa nafasi ya kusahihishwa. Niliona niseme hilo ili sote tushee uzoefu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kesho tutaendelea na Wizara ambayo leo imeweka Randama yake Mezani, ambayo ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Ambapo katika orodha, walioomba kwa leo, waliochangia mara moja ni watano, waliochangia mara mbili ni 35, wanakuwa 40; waliochangia mara tatu ni 17, kwa hiyo, inakuwa 57 na waliochangia mara moja ni mmoja, inakuwa 58. Kwa vyovyote vile hatuwezi kupata hata nusu ya hawa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli ambazo zimepangwa katika *Order Paper* au orodha ya shughuli za leo ya Mkutano wa Nne, Kikao cha 48, zimekamilika. Naomba nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge, hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.27 jioni, Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 17 Agosti, 2011, Saa 3.00 Asubuhi)*